Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA MBILI**

**Kikao cha Kumi na Tano - Tarehe 1 Julai, 2003**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 140

**Ubovu wa Barabara ya Manawa-Mbarika**

**MHE. STEPHEN M. KAZI (k.n.y. MHE. JACOB D. SHIBILITI)** aliuliza:-

Kwa kuwa katika Mkutano wa Bajeti wa mwaka 2002/2003 nilieleza ukubwa wa tatizo la ubovu wa barabara ya Manawa-Nduha, Kasololo hadi Mbarika yenye urefu wa kilomita 42; na kwa kuwa nilielezea pia kuwa makalvati yaliyoandaliwa ili yawekwe katika Mto Nyakahumbo eneo la Nduha hayakutengenezwa kwa ubora unaotakiwa kuhimili uzito wa magari:-

(a) Je, Serikali imelitembelea eneo hilo kama nilivyoomba na wameona nini?

(b) Kwa kuwa ubovu wa barabara hiyo bado umebakia vile vile, na unazidi kuwatenga wananchi wa maeneo ya Nduha, Kasololo Igonjwa na Mbarika katika kupata huduma muhimu za kijamii? Je, Serikali itawasaidiaje wananchi wa maeneo hayo ili waondokane na kero hiyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mbunge wa Misungwi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, barabara hiyo mwanzoni ilikuwa inahudumiwa na Mhandisi wa Mkoa na ilikuwa imesajiliwa kimkoa na kupewa Namba *R. 165*. Baada ya kuanzishwa kwa Wakala wa Barabara *(TANROADS)* mwaka 2000, barabara hiyo iliondolewa kwenye orodha ya barabara zitakazohudumiwa na Wakala huyo. Kutokana na hali hiyo barabara hiyo sasa imebidi kuhudumiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia uongozi wa Mkoa umetembelea barabara hiyo kama Mheshimiwa Mbunge alivyokuwa ameomba. Mhandisi wa Sekretarieti wa Mkoa wa Mwanza alitembelea barabara hiyo kati ya tarehe 6 na 7 Juni, 2001 na kujionea hali halisi ilivyo. Alishauri Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi kuiweka kwenye Bajeti ya mwaka 2002/2003 na kuendelea ili iweze kufanyiwa matengenezo angalau madogo madogo ili kuwapunguzia wananchi kero wakati ufumbuzi wa kudumu

unatafutwa. Kiasi shilingi 18,000,000/= zilitengwa, lakini kutokana na ufinyu wa Bajeti kiasi hicho hakikuweza kutolewa.

(b) Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi inafanya upembuzi yakinifu ili kubaini gharama halisi za ukarabati na baadaye iweze kuomba fedha hizo *(Special Fund)* kutoka Mfuko wa Barabara au kutoka kwa baadhi ya wafadhili ili iweze kutengenezwa.

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Nashukuru Mheshimiwa Spika, kwa kuwa barabara hii mpaka sasa makalvati bado yako pale Nduha na Serikali haijafanya utaratibu wowote wa kuweza kuyaondoa yale Makalvati na inavyoonekana wafanyakazi wa Nduha, Mbarika mpaka Kialambogo wana matatizo hayo. Je, Serikali ina utaratibu gani na si wa kutegemea Halmashauri ili kuweza kuwaondolea tatizo hilo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema barabara hii gharama zake za kutengeneza ni kubwa katika makisio ya mwanzo inakisiwa kwamba inaweza ikagharimu karibu shilingi milioni 365 kuitengeneza. Kwa hiyo, tulichoshauriana moja ni kuiomba Halmashauri ijaribu kutenga fedha kidogo kidogo. Kwa sababu ni lazima muda wote ijaribu kupitika. Ndiyo juhudi za kwanza.

Lakini pili, ni kufanya *through study* ambayo ndiyo itatupatia kihalisi fedha inayohitajika. Ni kweli kwamba kulitengenezwa makalvati ambayo yapo mpaka sasa katika barabara hiyo. Lakini yalikuwa ni kwa lengo la kujaribu kutengeneza yale maeneo madogo madogo ili kuweza kuwezesha barabara hiyo kupitika. Kwa hiyo, juhudi zinaendelea na mimi nina hakika tunapokwenda huenda tukafanikiwa.

Na. 141

**Kunyang'anywa Mali Wafanyabiashara Ndogo Ndogo**

**MHE. MOHAMED RAJAB SOUD** aliuliza:-

Kwa kuwa wafanyabiashara ndogo ndogo walio wengi hapa nchini husumbuliwa na Manispaa zao kwa kufukuzwa kila mara kwenye maeneo wanayofanyia biashara:-

(a) Je, kuna uhalali gani wa kunyang'anywa bidhaa zao?

(b) Kwa kuwa vibanda vyao vingi huvunjwa usiku bila ya wao wenyewe kuwepo; je, ni uhalali gani uliohalalisha hivyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Rajab Soud, Mbunge wa Jang'ombe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, biashara ndogondogo zimeshamiri katika maeneo mbalimbali ya Miji yetu. Biashara hizi hufanyika katika vituo vya mabasi, barabarani pamoja na maeneo mengine ambayo si rasmi na kinyume cha Sheria. Biashara hizi nyingi ni za mikononi na hutembezwa barabarani katika maeneo yenye msongamano wa watu. Hali hii husababisha usumbufu mkubwa kwa watembeao kwa miguu na hata wanaotumia vyombo vya usafiri. Kutokana na hali hii Halmashauri zimejitahidi kuandaa maeneo rasmi ya kufanyia biashara za aina hii kwa kufuata utaratibu.

Hata hivyo, wafanyabiashara wengi hawapendi kufanya biashara zao katika maeneo haya. Hivyo ili kuwaondoa wafanyabiashara wasiozingatia sheria Halmashauri zimekuwa zikiwatumia Polisi na wakati mwingine Mgambo ili kuwaondoa katika maeneo yasiyo rasmi. Uamuzi huu huchukuliwa kwa lengo la kuimarisha usalama wa watu, mali zao pamoja na kuhifadhi mazingira pamoja na usafi wa miji. Ni wazi

kwamba katika zoezi zima la kuwakamata wale wanaofanya biashara ndogo ndogo kinyume cha Sheria, upotevu na uharibifu wa mali wakati mwingine hutokea.

(b) Mheshimiwa Spika, Halmashauri hutumia utaratibu wakati wa kuvunja vibanda ambavyo vimejengwa bila kufuata taratibu za mipango miji kama ilivyoainishwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, tarehe 1 Julai, 2003. Taarifa za kubomoa vibanda hutolewa na mara nyingi ubomoaji hufanywa na wafanyabiashara wenyewe. Ni mara chache ambapo Halmashauri zimelazimika kutumia askari pale wahusika wanapogoma kufanya hivyo kama ilivyotokea katika eneo la Manzese hivi karibuni na zoezi lilifanyika mchana.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge watakubaliana nami kwamba kero ambayo wananchi walikuwa wanaipata katika maeneo yaliyokuwa yanatumiwa na wafanyabiashara kama vile mitaa ya Kariakoo sasa zimepungua kwa kiwango kikubwa baada ya wafanyabiashara kuondolewa. Naendelea kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge na Viongozi wengine hasa Madiwani kuzisaidia Halmashauri zetu kwa kuweka mazingira mazuri ya kufanyia biashara pamoja na kuwaelimisha wafanya biashara ndogo ndogo ili wazingatie matakwa ya Sheria.

**MHE. MOHAMED RAJAB SOUD:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri. Lakini bado nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa katika mitaa wengi wanaonyang'anywa vitu vyao huchukuliwa vitu vyao na wakaondoka navyo ndani ya magari. Swali, je, mtindo huu wanaotumia kuchukua vitu vyao bila wao kuwepo na kuwanyang'anya si kuwarejesha nyuma katika biashara zao ndogo ndogo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema suala la ku-*deal* na wafanyabiashara wadogo wadogo kidogo najua ni *delegate,* inawezekana likaleta tafsiri mbalimbali. Lakini tunachotazama hapa ni kwamba maadam tumeshakupa taarifa ya kuondoa vibanda au shughuli zako mahali panapotakiwa, ni wajibu wako basi kutekeleza kama tulivyotoa tangazo na inapotokea sasa kwamba hilo halikutekelezwa ndipo unapoona wakati mwingine sukumanasukumana inajitokeza na hata bidhaa kuchukuliwa kwenye malori kwa sababu umeshakuwa mhalifu kwa maana ya utekelezaji kwa agizo lililotolewa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, bado nazidi kusisitiza tusaidiane. Kwa sababu najua tusiposaidiana katika eneo hili huenda zoezi hili likawa gumu sana.

**MHE. REMIDIUS E. KISSASSI:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa kuniona. Kwa kuwa Serikali yetu ya Muungano inayoongozwa na CCM ni ya kiungwana; je, haoni ni busara zaidi kutumia mpango shirikishi, kwa kuwashirikisha wafanyabiashara wale katika kuamua maeneo ya kufanyia biashara kuliko kuwasukuma namna hii? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, muda wote utaratibu huo umekuwa unafanyika, kujaribu kushirikisha wafanya biashara wadogo wadogo hata pale wanapokuwa na vyama, umoja wa namna moja au nyingine umetumika na kwa kweli katika maeneo iliyofanyika hivyo imefanikiwa vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, matatizo tunayapata zaidi ni kwa Jiji la Dar es Salaam ambapo unakuta kidogo tuna matatizo na wafanyabiashara wadogo wadogo na juzi tulikuwa tunawatolea viongozi wa Halmashauri kujaribu kuwaomba wawe na vyama vya namna moja au nyingine ili kupitia vyama hivi viweze pengine kuzungumza nao na tukaelewana vizuri zaidi badala ya purukushani ambavyo hivi sasa imejitokeza katika maeneo ya Jiji la Dar es Salaam.

Na. 142

**Wafanyakazi wa *Liparamba Game Reserve***

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA** aliuliza:-

Kwa kuwa wataalam na wafanyakazi wengine wamekwama sana katika shughuli za kuhudumia *Liparamba Game Reserve* kutokana na ukosefu wa vifaa muhimu ikiwemo gari:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha hayo?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga, Mbunge wa Mbinga Magharibi, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Pori la Akiba la Liparamba *(Liparamba Game Reserve),* lilipata hadhi ya kuwa Pori la Akiba baada ya kuandikishwa kwenye Gazeti la Serikali Namba 289 la tarehe 18 Agosti, 2000. Mbali ya kuwa Pori la Akiba, eneo la Liparamba ambalo lipo katika Wilaya ya Mbinga ni eneo la mwinuko lenye miti mingi ya aina mbalimbali. Kuwepo kwa miti na majani ya aina mbalimbali kunafanya eneo hili kuwa makazi muhimu ya wanyamapori wa aina mbalimbali kama vile pofu, mbarapi *(Sable Antelope),* pongo, ngiri, ngedere, nsya *(Common Dulker)* na ndege wa aina mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga, Mbunge wa Mbinga Magharibi, kama ifuatavyo:-

Pamoja na kwamba Wizara yangu ndiyo msimamizi mkuu wa mapori yote ya akiba likiwemo la Liparamba, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara yangu inaendelea kushirikiana na uongozi wa Mkoa wa Ruvuma kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga, kusimamia shughuli mbalimbali zinazohusiana na uendeshaji wa pori la akiba la Liparamba.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la wafanyakazi, Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga, imetoa wafanyakazi watano kwa ajili ya kuhudumia pori hilo. Aidha, Wizara yangu kwa kutumia Kikosi Dhidi ya Ujangili Kanda ya Kusini, chenye makao yake mjini Songea imeendelea kuhudumia pori la Liparamba katika ulinzi na uendelezaji wa rasilimali zilizomo.

Katika mwaka wa fedha wa 2002/2003, Wizara imepeleka shilingi 10,000,000/= kwa ajili ya uendeshaji wa doria, ufyekaji wa mipaka na matengenezo ya barabara katika pori hilo.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itaendelea kulihudumia pori hilo huku ikifanya kila njia kupunguza tatizo la ukosefu wa vifaa muhimu vya kazi. Kwa sasa, Wizara imekamilisha taratibuza kulisimamia pori hilo moja kwa moja kupitia Idara ya Wanyamapori badala ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga. Aidha, Wizara imetenga gharama za kusimamia pori hilo katika Bajeti yake ya mwaka 2003/2004 inayotarajiwa kuwasilishwa katika Bunge lako tukufu ikiwa ni pamoja na gharama za ujenzi wa Ofisi, ununuzi wa gari na vifaa vya Ofisi. Vile vile, Wizara itamteua Meneja Mradi atakayesimamia shughuli za uhifadhi katika pori hilo.

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwanza, natoa shukrani kwa mipango mizuri ya Wizara kwa kuitambua *Game Reserve* hiyo na kuiwekea Bajeti. Kwa kuwa *master plan* ya kupanua programu ya utalii nchini imeorodhesha vituo vyote hapa nchini. Je, *Game Reserve* ya Liparamba imo katika hiyo *master plan* na kama haipo itaorodheshwa lini katika *master plan* ya utalii nchini? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, *master plan* ya utalii inaainisha maeneo yote nchini Tanzania na katika hali mbalimbali na katika upande wa wanyapori, katika fukwe, katika utamaduni na kadhalika. Kwa hiyo, pori hili nalo limeainishwa. Lakini utaratibu wa kufikia maeneo haya yote kwa kweli hatuwezi kuyafikia kwa mara moja.

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa pori la Liparamba linapakana na nchi ya Msumbiji na kwa kuwa wanyama kama tembo, samahani ni ndovu huwa wanahama kutoka nchi moja kwenda nchi nyingine na kuwa inavyofahamika kwamba upande wa pili wa Msumbiji hakuna utaratibu unaoeleweka wa kuhifadhi wanyama. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba wanyama wanapohama kutoka Liparamba na kwenda upande wa pili wanakuwa salama? *(Kicheko/Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, siku zote tumekuwa tunasema kwamba wanyama hawana Utaifa maalum na wanyama wanazunguka. Kwa hiyo, wanyama wale wakiwa Msumbiji wanakuwa Wanamsumbiji, wanyama wakiwa Tanzania wanakuwa Watanzania, kwa maana hiyo. Sasa labda niseme kwamba kwa sababu Tanzania pia ni mwanachama wa nchi za Kusini za *SADC*.

Kwa hiyo, kuna programu ambazo zinashughulikia hiyo. Lakini pia sisi tumesaini mkataba ambao unaitwa *Lusaka Agreement,* makubaliano ya Lusaka ambayo inaangalia masuala yote ambayo yanahusu wanyamapori.

Na. 143

**Zana za Kilimo - Wilaya ya Kilwa**

**MHE. OMAR M. MWENDA** aliuliza:-

Kwa kuwa kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi wa Taifa letu na kwa kuwa wakuima wengi hawana zana bora za kilimo hasa kwa Wilaya ya Kilwa.

Je, Serikali itakubaliana nami kuwa sasa ni wakati muafaka kwa Serikali kununua zana bora za kilimo kama matrekta na kuyaweka Wilayani ili wakulima wayakodishe kwa ajili ya shughuli za kilimo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Omar Mwenda, Mbunge wa Kilwa Kusini, kama ifuatavyo:-

Nakubaliana na Mheshimiwa Omar Mwenda, kuwa wakulima wengi katika Wilaya ya Kilwa hawana zana bora za kilimo. Takwimu zinaonyesha kuwa miaka kumi iliyopita Wilaya ya Kilwa ilikuwa na matrekta kumi na tatu.

Kwa sasa hivi Wilaya hiyo ina matrekta mawili tu yanayofanya kazi vizuri. Wakati wa msimu wa kilimo, wakulima wachache wenye uwezo wa fedha hukodisha matrekta kutoka Wilaya ya Rufiji na kutoka Misheni ya Kilangala katika Wilaya ya Lindi.

Kutokana na mabadiliko ya Sera za uchumi, Serikali imejitoa katika shughuli za moja kwa moja za uzalishaji na kibiashara. Serikali kwa hiyo, haina mpango wa kununua matrekta na kuyaweka Wilayani kwa ajili ya kuyakodisha wakulima. Hata hivyo, Serikali imebuni njia mbadala ya kuhamasisha Sekta binafsi kuanzisha vituo vya kukodisha zana za kilimo.

Katika mwaka wa 2003/2004, Serikali inakusudia kuanzisha utaratibu wa kuwapatia wakulima mikopo nafuu ya kununua matrekta mapya na kukarabati matrekta mabovu kutoka kwenye Mfuko wa Pembejeo wa Taifa na Taasisi za fedha za hapa nchini. Kiasi cha shilingi bilioni moja, zimetengwa chini ya Mfuko wa Pembejeo wa Taifa zitakazotumika kutoa mikopo hiyo. Aidha, Wizara ya Kilimo na Chakula, itatoa ushauri wa kiufundi kwa wananchi, vikundi na taasisi zitakazoanzisha vituo vya kukodisha zana za kilimo.

**MHE. OMAR M. MWENDA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu yake mazuri Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kumwuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa mikopo hiyo wanaiwekea masharti ni lazima mtu awe na dhamana ya hati ya nyumba au hati ya shamba. Je, kwa mkulima wa kawaida ataipata hiyo hati ya shamba au ya nyumba, anaweza kukopeshwa pia hati hiyo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, haikuwekwa kwa ajili ya kuwasumbua wakulima. Imeweka kulinda mali zetu dhidi ya wale wanaoweza kuzembea kulima. Hata hivyo, si lazima uweke nyumba tu, unaweza kupitia kikundi cha wakulima, mfano chama cha ushirika au *SACCOS* fulani na kupitia *SACCOS* ukadhaminiwa upate mkopo huo. Hii ni sharti la kulinda fedha hizi kusudi mzunguko wake usije ukaharibika.

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, miaka 15 iliyopita Wamisionari wa Benedictine, waliweka kituo cha ukodishaji wa matrekta kwa wananchi kwa lengo la kusaidia kilimo na kwa kuwa kituo hicho kilikuwa kinakodisha kwa wananchi, Serikali ikaona wanafanya biashara na hivyo kuwatoza kodi. Baada ya kuombwa hivyo, Wamisionari wakaomba msamaha ili waweze kusaidia kilimo, lakini Serikali haikuweza kusaidia.

Je, Naibu Waziri anatoa tamko gani katika kusaidia Wamisionari na watu wengine wa aina hiyo wanaopenda kusaidia kuweka vituo lakini wanashindwa kwa sababu ya kodi katika nchi nzima? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, sina uhakika sana kuhusu kodi hiyo ilikuwa ya namna gani. Lakini ninavyojua kwa sasa hivi watakaopenda kuanzisha vituo hivi tunawapa ushauri na kwa hiyo, matatizo yao ya aina hiyo yakajadiliwa. Ninavyojua sasa hivi Askofu Mkuu wa Songea anataka kuanzisha Kituo kingine. Kwa hiyo, tutasubiri wakiwa tayari tutajadiliana.

**MHE. WILLIAM J. KUSILA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa matumizi ya dhana bora ya kilimo kama swali la msingi lilivyouliza ndiyo utakaotuwezesha kufanya mapinduzi ya kilimo katika nchi hii na kwa kuwa ili wananchi wengi waweze kuzimudu zana hizo za kilimo ni lazima waboreshe kilimo chao cha sasa cha kutumia zana duni kwa kuzingatia kanuni zote za kilimo bora ili kiongezeke na kuwezesha kumudu zana hizi bora.

Je, ni kwa kiasi gani wananchi wetu hivi sasa wanazingatia Kanuni bora za kilimo na kama mpaka sasa wengi hawazingatii kanuni bora za kilimo na je, Wizara itakubali kuwajibisha wote wanaohusika na huduma za ugani kwa kushindwa kufanya kazi yao? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli matumizi ya zana bora za kilimo ni muhimu katika kukifanya kilimo kiboreke. Watumishi wa ugani wapo katika Wilaya hapa nchini na kwa bahati nzuri sisi Waheshimiwa Wabunge ni Wajumbe wa Kamati na Halmashauri mbalimbali katika Halmashauri zetu. Hivyo nawaomba kwamba kabla hatujawachukulia hatua, kwamba tuwasimamie vizuri hawa watumishi wa ugani ambao wapo kila Wilaya kusudi tusifike huko unakosema kuwawajibisha.

Na. 144

**Matatizo ya Maji Vijiji vya Olchorovus na Oloitushula**

**MHE. FELIX C. MREMA (k.n.y. MHE. ELISA D. MOLLEL)** aliuliza:-

Kwa kuwa vijiji vya Olchorovus na Oloitushula vimekuwa na matatizo makubwa ya maji na kwa kuwa vyanzo vya maji vilivyoko katika kijiji cha Mlimani na Shamba la *Monduli Coffee Estate,* Wilayani Monduli vina maji ya kutosheleza mahitaji ya wanavijiji wa Mlimani na Shamba la *Monduli Coffee Estate* wakishirikiana na wananchi wa vijiji vya Olchorovus na Oloitushula:-

Je, Serikali inatoa tamko gani kwa wananchi wa Arumeru ambao hapo awali walikuwa wanatumia maji haya?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Elisa Mollel, Mbunge wa Arumeru Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na shida ya maji kwa wananchi wa eneo alilolitaja Mheshimiwa Mbunge la kihistoria. Mwaka 1934 mmiliki wa shamba la *Monduli Coffee Estate* alipewa hati ya kutumia maji yote ya vyanzo vya Mussa *(Mussa Springs)* kwa hati Na. 983 ya mwaka 1934. Baada ya wananchi kulalamika Mahakama ilimwagiza mmiliki wa *Monduli Coffee Estate* kuweka bomba la inchi 2 kuelekea kijiji cha Oloitushula na kujenga birika la kunywesha mifugo ya kijiji hicho.

Mwaka 1955 mmiliki wa shamba la *Rasharasha Coffee Estate* alipewa hati ya kumiliki maji kutoka chanzo cha maji cha Larash kwa hati Na. 3008 ya mwaka 1955. *Rasharasha Coffee Estate* nayo iliagizwa na Mahakama kutenga kiasi cha lita 0.79 kwa sekunde kwenda kijiji cha Mlimani, kwa njia ya bomba. Mwaka 1976, tatizo liliongezeka baada ya matumizi ya maji kupanuliwa ili kukidhi mahitaji ya Mji wa Monduli kwa kuongezea bomba la *Rasharasha Coffee Estate* la inchi 2 hadi mji wa Monduli.

Matumizi ya maji yameendelea kuongezeka na uharibifu wa mazingira kuongezeka kwenye vyanzo vya maji na kusababisha upungufu wa maji. Kwa ajili hiyo, kumekuwepo na migongano ya jamii katika kugombea maji, hususan Kata ya Musa katika Wilaya ya Arumeru na Engutoto katika Wilaya ya Monduli.

Mheshimiwa Spika, Serikali imefuatilia kwa makini suala hili ikiwa ni pamoja na kuitisha vikao vya wadau wote kuhusu hali halisi ya maji na vyanzo vilivyoko kwenye Mlima wa Monduli. Sambamba na mikutano hiyo ya wadau pia Wizara yangu imeendelea na zoezi la kupata taarifa zitakazowezesha kulipatia ufumbuzi wa kudumu.

Taarifa hizo ni pamoja na takwimu za wingi wa maji katika vyanzo kwa vipindi tofauti vya mwaka, kupata maoni ya viongozi na wadau wote kwa njia shirikishi ili kubaini matatizo na kiini cha upungufu wa maji katika maeneo hayo. Wizara imekusudia pia kufanya warsha mwezi Septemba, 2003 itakayojumuisha Wadau wote ili kupata mapendekezo ya jinsi ya kugawa maji yaliyopo kulingana na matumizi ya sasa kwa shughuli mbalimbali zinazofahamika.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumshauri Mheshimiwa Mbunge, kuwahamasisha wananchi wa maeneo husika ili waimarishe na kuendelea kuchangia mifuko yao maji kwa lengo la kujenga malambo mapya ya mifugo na kukarabati miradi ya maji iliyopo. Ujenzi wa malambo utasaidia kuongeza kiasi cha maji na kupunguza mahitaji ya maji kwa ajili ya mifugo na binadamu.

**MHE. FELIX C. MREMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ningependa kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa inaonekana itachukua muda mrefu kulipatia tatizo hili sugu ufumbuzi; je, Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza kuungana na sisi katika Wilaya hiyo ya Arumeru pamoja na Arusha Kata za Musa, Kisongo, Madebesi na pia katika Manispaa ya Arusha, kutuongezea nguvu katika jitihada zetu za kutatua matatizo sugu ya maji katika Kata hizo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, maeneo ya Kata alizozitaja za Kisongo, Mussa na Madebesi, ziko kwenye maeneo ambayo yanaweza kufikika na mtandao wa maji ya Mamlaka ya Maji Mjini Arusha. Hivyo, kulingana na mipango ya Mamlaka hii ya Maji ya Mji wa Arusha, nina hakika siyo muda mrefu utapita maeneo hayo yatafikiwa au kwa kutumia vyanzo vilivyopo au kwa kuviendeleza vyanzo vingine ambavyo viko karibu zaidi na maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, pili, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, maeneo mengine ambayo yametajwa, ikiwa wananchi watachangia pamoja na Halmashauri husika kuchangia, Serikali iko tayari kutoa msaada ili wachimbe malambo ambayo ndiyo *more property* kwa ajili ya mifugo ili kupunguza *pressure* ya mahitaji ya maji kwenye maeneo hayo.

Na. 145

**Majosho ya Mbwa**

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa uogeshaji wa wanyama mara kwa mara pamoja na kuchanja ni jambo jema ambalo huwasaidia wanyama hao kuepukana na magonjwa mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuepusha kichaa cha mbwa:-

(a) Je, Serikali ina habari kuwa sehemu nyingi hasa Mijini zilizokuwa na majosho ya wanyama hao hapo awali kuwa sasa hazina majosho hayo na kama yapo hayafanyi kazi?

(b) Je, Serikali ina habari kwamba hapa Dodoma pia hakuna majosho kama hayo na vile vile kama yapo hayafanyi kazi kama siku zilizopita ambapo ilikuwa ikitengwa siku moja kwa juma kwa ajili ya kupeleka wanyama hao kwenye josho?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli kuwa utaratibu wa kuogesha wanyama mara kwa mara na kuchanja ni utaratibu unaokubalika kitaalam kuwakinga na magonjwa yanayoenezwa na kupe. Hata hivyo kuogesha hakuepushi ugonjwa wa kichaa cha mbwa ila ugonjwa huu unaweza kuepukwa kwa chanjo inayofanyika mara kwa mara kila mwaka kwa mbwa na paka. Mara nyingi wataalam wa mifugo wanautumia mkusanyiko huo wa mbwa kwenye majosho kutoa huduma nyingine ikiwa ni pamoja na chanjo.

Mheshimiwa Spika, Serikali ina habari kuwa sehemu nyingi za nchi yetu zilizokuwa na majosho zinaendelea kutoa huduma ya uogeshaji kwa kiwango kisichoridhisha. Majosho ya mbwa yapo katika Miji mbalimbali, baadhi yanafanyakazi na yaliyo mengi hayafanyikazi kutokana na ukosefu wa waendeshaji, usimamizi duni toka kwa watendaji wa Halmashauri husika na kutokuwepo Sheria ndogo ndogo za Halmashauri husika za kuwabana wenye mbwa Mijini kuwaogesha mbwa wao.

Idadi ya majosho ya mbwa katika baadhi ya Mikoa ni Iringa 5, yote yanafanya kazi, Pwani 2, moja linafanya kazi, Kagera 2, yote hayafanyi kazi, Kilimanjaro 2, yote yanafanya kazi, Mara 1, linafanya kazi, Mtwara 3), yote hayafanyi kazi, Ruvuma 1, linafanya kazi, Tabora 2, yote yanafanya kazi, Arusha 1, linafanya kazi na Dodoma 2, yote hayafanyi kazi.

(b) Mkoa wa Dodoma una majosho mawili ya kuogeshea mbwa yaliyopo katika Miji ya Mpwapwa na Manispaa ya Dodoma. Josho la Manispaa lilifungwa kuepusha usumbufu kwa vile josho lilikuwa limejengwa karibu sana na Ofisi hiyo ya Manispaa ikaamuru lijengwe sehemu nyingine. Mipango ya kujenga josho hilo sehemu nyingine inaendelea chini ya sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaandaa mkakati wa kufufua shughuli za uogeshaji ikishirikiana na Halmashauri zote na sekta binafsi. Mkakati huu utazingatia mbinu zitakazowashirikisha wadau mbalimbali ili majosho yaweze kuendeshwa na sekta binafsi na tayari maelekezo hayo yameanza kutolewa kwa baadhi ya Miji kama Mji wa Mbeya au Manispaa ya Mbeya.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, naomba niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imekwishathibitisha mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba majosho mengine hayafanyi kazi kwa asilimia kubwa; je, Serikali itatuambia nini hivi sasa na lini itafanya

marekebisho hayo haraka sana ili hayo majosho yaweze kufanya kazi kwa kuzuia hayo maradhi tuliyokuwa tumeuliza? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwenye jibu la msingi, kuna majosho mengi ya kuogesha mbwa hayafanyi kazi, hii inatokana na utendaji usioridhisha unaotokea kwenye Halmashauri zetu za Miji kwa sababu wanaona majosho ya mbwa siyo kitu cha msingi kwa uelewa wao. Hivyo Serikali inakumbushia tu kwa sababu shughuli ya uogeshaji na uwekaji wa majosho ya mbwa Mijini na maeneo niliyoyataja, ni shughuli ambayo inatakiwa kufanyika au kufanywa na Halmashauri na usimamizi wake wote unatakiwa kufanywa na Halmashauri.

Hivyo basi, Serikali Kuu tutaendelea kuhimiza Halmashauri zikumbuke kwamba ni wajibu wake na pia Sekta binafsi inakaribishwa kwa sababu ni kitu kinachoweza kuleta *income* na kuhamasisha uogeshaji na uchanjaji wa mifugo kama vile mbwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nawatafuta watu wa Iringa, Mheshimiwa William Lukuvi, hana swali. *(Kicheko)*

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri ameutamka Mkoa wa Dodoma kwamba hauna josho la aina yoyote na akijua ya kwamba Dodoma ni Makao Makuu ya Chama na Serikali; je, kama ugonjwa huu wa kichaa cha mbwa utalipuka, Watanzania tutanusurika tukiwa hapa Dodoma?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, kwanza, kama nilivyoeleza kwenye jibu la msingi kwamba Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma yenyewe iliamua kulifunga josho lililokuwepo. Kwa hiyo, moja kwa moja wajibu wa kujenga josho lingine ni wa Manispaa ya Dodoma.

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge lako Tukufu naomba na kuiagiza Halmashauri hii ya Manispaa ya Dodoma, wajenge josho hilo na Serikali itasaidia mahala ambapo utaalam utahitajika. *(Makofi)*

Na. 146

**Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya Mwaka 1999**

**MHE. JAMES P. MUSALIKA** aliuliza:-

Kwa kuwa Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya mwaka 1999 kifungu cha 5 kinahalalisha ugawaji wa ardhi, eneo au shamba uliofanywa kimila katika *operation* Vijiji au vinginevyo kati ya tarehe 1 Januari, 1970 na 31 Desemba, 1977; na kwa kuwa kifungu Na. 16 cha Sheria hiyo kinachohamasisha ugawaji huo uliofanyika tangu tarehe 1 Januari, 1978 hadi sasa kama umefanywa na Serikali ya Vijiji chini ya Sheria ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1982; na kwa kuwa hadi sasa kesi nyingi za ardhi au mashamba zinapelekwa moja kwa moja kwa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo bila kupitia Serikali za Vijiji kama Sheria inavyoelekeza:-

(a) Je, ni Mahakimu wangapi wa Mahakama za Wilaya wamepata nakala ya Sheria hiyo na ni wangapi wamezipeleka hadi kwa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo?

(b) Je, ni lini Mahakama za Ardhi za Kata zitaanza kufanya kazi na kama zinafanya kazi ni Wilaya ngapi zina Mahakama hizo na kwa nini Wilaya nyingine hazina?

(c) Je, ni nani mwenye mamlaka ya kusikiliza mashauri ya ardhi baina ya Mahakama za Mwanzo, Mahakama za Ardhi za Kata na Mabaraza ya Kata?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika!! *(Kicheko/Makofi)*

Nawashukuru kwa kushangilia, lakini nilikwishaachia ngazi siku nyingi. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa James Musalika, Mbunge wa Nyang'hwale, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, hadi sasa Sheria ya Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi na Nyumba Na. 2 ya mwaka 2002 *(The Lands Disputes Courts Act No. 2 of 2002)* haijaanza kutumika kutokana na maandalizi muhimu yanayohitajika kufanyika. Maandalizi hayo ni pamoja na uchapishaji wa Sheria yenyewe, uandaaji wa Kanuni, uanzishwaji wa Ofisi, kupata Mahakimu wa kusikiliza mashauri hayo na uteuzi wa Wajumbe. Sheria hii itakapoanza kutumika Mahakama ya Ardhi za Kata na nyingine zitaanza kufanya kazi. Kwa hivi sasa kazi za uchapishaji wa nyaraka mbalimbali na ukarabati wa majengo kwa ajili ya Ofisi zinaendelea. Mara Sheria itakapoanza kutumika, mashauri yatafunguliwa na kusikilizwa kwa kufuata mfumo mpya na mashauri ya zamani yataendelea kushughulikiwa na Mabaraza ya Ardhi na Mabaraza ya Nyumba yaliyopo sasa katika kipindi cha mpito cha miaka miwili.

(b) Mheshimiwa Spika, hakuna Hakimu katika ngazi za Wilaya na ngazi nyingine aliyepata Nakala ya Sheria ya Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi na Nyumba Na. 2 ya mwaka 2002. Nakala zitaanza kusambazwa mara baada ya kukamilisha uchapishaji wa Sheria hiyo unaoendelea hivi sasa na kukamilika kanuni zake na taratibu nyingine zinazohitajika ikiwa ni pamoja na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. Usambazaji huo utaenda sambamba na utoaji wa elimu kwa umma.

(c) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria mpya ya Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi itakapoanza kutumika, mashauri kuhusu ardhi yataanza kusikilizwa na Baraza la Ardhi la Kijiji. Mwananchi ambaye hataridhika na uamuzi wa Baraza la Ardhi la Kijiji atakuwa na fursa ya kukata rufaa katika Baraza la Kata na atafuata ngazi za Mahakama ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya kisha Mahakama Kuu Idara ya Ardhi hadi Mahakama ya Rufaa. Katika mfumo huu, Mahakama za Mwanzo hazihusiki na utatuzi wa migogoro hiyo.

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, napenda kuuliza swali la nyongeza moja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mwaka 2002 Halmashauri nyingi zilianzisha Mabaraza ya Kata ili kusaidia kupunguza msongamano wa kesi katika Mahakama za Mwanzo zikiwemo zile kesi za ardhi; na kwa kuwa Mabaraza mengi katika Halmashauri nyingi hazijaanza kufanya kazi; je, Serikali inatoa tamko gani kuhusu Mabaraza ya Kata ambayo hayajaanza kufanya kazi?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kama Mabaraza ya Kata yameanza kufanya kazi, yanafanya kazi kinyume na taratibu ambapo Sheria bado haijaanza kufanya kazi.

Kwa hiyo, ningewashauri waendelee na mfumo ule ule kwa sababu walikwishapewa muda wa miaka miwili kumalizia kesi zote ambazo zilikuwa zinashughulikiwa na Mahakama ya Mwanzo. Sasa kama wataanzisha Mabaraza ya Kata wenyewe wanavijiji kinyume na utaratibu watakuwa wamekiuka Sheria.

Mheshimiwa Spika, ningeomba wafanye subira, waendelee kuyaamini Mabaraza yale ambayo yalikuwa yanafanya kazi mwanzo kupitia Mahakama za Mwanzo, kesi zote ziendelee kufanyika hivyo. Napenda kuwaomba wananchi wafanye subira maandalizi karibu yatakamilika na mara Sheria hiyo itaanza kutumika kwa mujibu wa Sheria tuliyoipitisha hapa Bungeni.

**MHE. PROF. DAIMON M. MWAGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa utaratibu aliouzungumzia Mheshimiwa Naibu Waziri wa kushughulikia masuala ya ardhi haujaanza na Sheria hii imetungwa mwaka 1999 sasa takriban ni miaka minne; je, ni lini utaratibu huu utaanza?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, Sheria haikuanza mwaka 1999, ni Sheria ya Ardhi Na. 4 na Na. 5 ndiyo zilianza mwaka huo lakini Sheria ya *The Lands Disputes Courts Act* tumeipitisha hapa mwaka 2002.

Kwa hiyo, bado hatujachelewa na nawaomba muendelee kuvuta subira ili Mahakama hizo zifanye kazi kwa utaratibu wa Sheria tuliyopitisha wenyewe mwaka 2002.
Na. 147

**Mabadiliko Mengi ya Sheria za Ardhi**

**MHE. HAROUB SAID MASOUD (k.n.y. MHE. FATMA SAID ALI)** aliuliza:-

Kwa kuwa Wizara imefanya mabadiliko mengi ya Kisheria kuhusu Mipango Miji, kufutwa kwa Hatimiki za Mashamba makubwa, ubinafsishaji wa Nyumba za Serikali na Wanawake kumiliki ardhi:-

Je, Serikali haioni kwamba upo umuhimu wa kutoa elimu ya mabadiliko hayo yote kwa Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote wa Tanzania Bara?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fatma Said Ali, Mbunge wa Mlandege, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inatambua umuhimu wa kutoa elimu kuhusu Sera na Sheria za Sekta ya Ardhi na Makazi. Nguvu nyingi zimeelekezwa kutekeleza jukumu hili. Hata hivyo, kutokana na ukubwa wa nchi yetu na ufinyu wa Bajeti ya Serikali, kazi hii imekuwa ikitekelezwa kwa awamu kupitia vipindi vya redio, *television,* makala maalum kwenye magazeti na kuandaa semina na warsha kwa Watendaji na wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza jukumu hili kikamilifu Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imetoa mafunzo kuhusu Sheria Mpya za Ardhi kwa Watendaji wa Kata wa Mikoa kumi na moja ya Tanzania Bara ambayo ni Mikoa ya Tanga, Arusha, Manyara, Mara, Shinyanga, Dodoma, Iringa, Morogoro, Mbeya, Mtwara na Ruvuma. Utoaji wa elimu ulienda sambamba na usambazaji wa nakala za sheria za ardhi pamoja na kanuni zake.

Mheshimiwa Spika, katika Mikoa tuliyoifikia, nakala za sheria za ardhi zipatazo 3,464, kanuni zake nakala 2,681 na kitabu cha mwongozo cha mafunzo ya sheria ya ardhi ya Vijiji nakala 7,876 zilisambazwa. Aidha, kwa kushirikiana na wadau wengine, Wizara yangu imetayarisha mkakati wa Kitaifa wa kuelimisha umma juu ya Sheria za Ardhi utakaoanza kutekelezwa mwaka wa fedha 2003/2004. Utekelezaji wa mkakati huu utashirikisha wadau wengi na utaongeza kasi na wigo wa utoaji wa elimu hiyo nchini.

Mheshimiwa Spika, napenda kukiri kuwa Wizara yangu haijaandaa mafunzo au semina maalum juu ya Sera na Sheria za Ardhi kwa Waheshimiwa Wabunge. Hata hivyo, kwa kuwa nakala za Sera na Sheria za Ardhi na kanuni zake zilikwishagaiwa kwa Waheshimiwa Wabunge wote, napenda kutumia fursa hii kuwaomba muendelee kuzisoma nakala hizo na tutaendelea kuelimishana kwa kutumia mbinu mbalimbali ikiwa ni pamoja na semina maalum kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la ubinafsishaji wa nyumba za Serikali linashughulikiwa na Wizara ya Ujenzi.

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Spika, baada ya majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ningeomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mkoa wa Pwani na Mkoa wa Dar es Salaam sasa hivi kuna wananchi wengi ambao mashamba yao yamechukuliwa na Serikali na kugaiwa viwanja tofauti, kuna manung'uniko makubwa kwamba baadhi yao hawatendewi haki.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba ni bora katika Mikoa mingine ambapo shamba lolote linapochukuliwa na Serikali na wananchi kugawiwa viwanja, *priority* ya mwanzo apewe yule mwenye shamba baadaye vile vile wanawe ambao wamefikisha umri wa miaka 18, kupewa viwanja bila ya gharama yoyote ile?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, nakataa kusema kwamba viwanja 20,000 tulivyovipima Dar es Salaam waliokuwa wanakaa pale wamechukuliwa viwanja vyao kwa uonevu, watu wamepewa kihalali viwanja na fidia ambayo wamepewa imewaongezea kipato chao na kama kuna gharama kidogo waliyoambiwa watoe ni kwa ajili ya kuboresha miundombinu ambayo imewekwa na Serikali, kwa mfano barabara, kuvuta maji na umeme, ni gharama hizo tu ndiyo wanazolipia, lakini wamepewa nafasi ya kwanza katika maeneo waliyokuwa wanakaa kupewa kiwanja kimoja au viwanja viwili.

Mheshimiwa Spika, kusema kwamba wapewe mpaka watoto wa umri wa miaka 18. Hatufanyi himaya ya ukoo kwa sababu eneo lile anaweza akagawiwa mtu mwingine yeyote yule na kama kuna nafasi mahali pengine watapewa kutokana na kuomba lakini kwa himaya Serikali haifanyi iwe himaya ya ukoo katika maeneo haya. Sambamba na Mikoani kama jambo hili litafanyika, tutaendelea kutafuta viwanja, kupima na kugawa kwa mujibu wa taratibu ambazo tumejiwekea lakini hakuna viwanja vya himaya au vya ukoo.

Na. 148

**Walimu Jimbo la Buchosa**

**MHE. SAMWEL M. CHITALILO** aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wa Buchosa wanakwenda na wakati kwa kutaka watoto wao wasome na wapate elimu bora kama ilivyo kwa wananchi wengine waliopo kwenye sehemu nyingine mbalimbali:-

(a) Je, ni lini Serikali itapeleka walimu wa kutosha katika Shule za Kome, Nyahunge na nyingine nyingi zilizopo pamoja na Shule za Msingi na kuandaa walimu zaidi kwa shule zinazojengwa kwa nguvu za wananchi na Serikali kama vile Shule ya Sekondari Migukulama, Mwangika, Nyakarilo na Kakobe?

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (k.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Samwel Chitalilo, Mbunge wa Buchosa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2001/2002 Wizara yangu ilizipangia Shule za Sekondari za Kome na Nyahunge walimu watatu kila moja na mwaka 2002/2003 shule hizo zimepangiwa mwalimu mmoja kila moja. Juhudi zinaendelea za kuwahamasisha walimu kutoka shule nyingine za sekondari kwenda Kome na Nyahunge.

Kwa mujibu wa taarifa tulizonazo Wizarani, Shule za Sekondari za Migukulama, Mwangika, Nyakarilo na Kakobe bado zinajengwa. Kwa hiyo pindi zikikamilika Wizara itazipangia walimu wa kuziwezesha kufunguliwa. Wizara yangu itaendelea kuwapanga walimu katika shule hizo kadri Serikali inapopata uwezo wa kuajiri walimu wapya.

Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara imeshaelekeza Mikoa katika Waraka wa Elimu Na. 3 wa mwaka 2002, kuwa maombi ya kufungua shule za sekondari mpya yaletwe Wizarani mwezi Januari kila mwaka kwa ajili ya kufungua shule za sekondari Januari mwaka unaofuata. Hii itaisaidia Serikali kuweka mipango halisi ya walimu na vifaa vya kujifunzia na kufundishia.

Aidha, Halmashauri ya Sengerema ambako ndiko Jimbo la Buchosa la Mheshimiwa Mbunge, uwiano wa mwalimu kwa wanafunzi katika shule za msingi kabla ya ajira ya mwaka 2003 ulikuwa mwalimu 1:69. Halmashauri ya Sengerema ilipewa nafasi za kuajiri walimu 272 mwaka 2003.

Mheshimiwa Spika, ningeomba nifafanue kwamba Wilaya ya Sengerema ilipewa idadi kubwa kabisa ikizidiwa tu na Wilaya ya Geita ambayo ilipewa walimu 437 Kitaifa. Kwa hiyo, Kitaifa Wilaya ya Sengerema ilikuwa ni Wilaya ya pili.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, inategemewa baada ya ajira mpya mwaka 2003 Halmashauri ya Sengerema kutakuwa na uwiano wa mwalimu 1:59 juu kidogo tu ya uwiano wa Kitaifa wa mwalimu 1:52. Aidha, Wizara yangu ilishatoa maelekezo ya kuwapanga upya walimu *(Deployment of Teachers)* katika shule za msingi zote nchini pamoja na Halmashauri ya Sengerema. Hata hivyo naomba Waheshimiwa Wabunge kufuatilia kwa Maafisa Elimu wa Wilaya na Halmashauri kuhusu utekelezaji wa maagizo ya Serikali likiwemo Jimbo la Buchosa.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashauri Waheshimiwa Wabunge, Halmashauri na wananchi, kuwa sambamba na ujenzi wa shule pia tuwajengee walimu hawa nyumba nzuri za kuishi ili wabaki katika shule za sekondari na za msingi wanazopangiwa. Walimu wengi wameondoka kutoka shule walizopangiwa kwa kukosa mahali panapofaa pa kukaa na kufanyia kazi zao muhimu.

**MHE. SAMWEL M. CHITALILO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amesema kwamba walimu waliopelekwa kule inatokana na idadi ndogo labda ya walimu waliopo; je, kwa kuwa walimu hawa hawatoshi kabisa katika shule hizi za Kome na Nyahunge, ni lini sasa atafanya bidii ya kuwapeleka walimu wa kutosha kabisa katika shule hizi mbili?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa uimarishaji wa elimu ni pamoja na kuwajengea mazingira mazuri walimu; je, sasa ni lini walimu hawa watajengewa nyumba bora ili waweze kuishi katika sehemu hizi ambazo wanakimbia kwa sababu nyumba bora hazipo?

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (k.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI):** Mheshimiwa Spika, lini Serikali itaajiri walimu wa kutosha? Nilipokuwa nikijibu swali la msingi nilisema, Serikali itaendelea kuwaajiri walimu kutokana na uwezo wa kiuchumi unavyozidi kuongezeka na kwa hiyo kuongeza idadi ya walimu.

Hata hivyo, juhudi zinaonyesha kwamba Serikali imeanza kujitahidi kupambana na tatizo hilo. Kwa mfano, mwaka 2001/2002 walimu wa sekondari wapya 1,700 waliajiriwa, mwaka 2002/2003 walimu wa sekondari wapya 2,125 waliajiriwa na mwaka huu wa fedha tunakusudia kuajiri walimu wapya 1,700. Kwa hiyo, juhudi tayari zimekwishaanza.

Mheshimiwa Spika, lini walimu watajengewa nyumba mpya? Nimesema nilipokuwa nikijibu swali la msingi kwamba ninawaomba Waheshimiwa Wabunge tukisaidiana na Halmashauri na wananchi, kuhamasishana ili tujenge nyumba za kutosha kwa walimu hao kwa sababu tukiisubiri Serikali kuja kujenga nyumba za walimu itachukua muda mrefu sana. Tuiache Serikali ipambane kwanza na matatizo yale mazito ya kutafuta vifaa vya kufundishia na vya kujifunzia na kuajiri walimu.

Na. 149

**Mikopo kwa Walimu**

**MHE. DR. AISHA O. KIGODA** aliuliza:-

Kwa kuwa Walimu kama watumishi wengine wanaruhusiwa kujiunga na Ushirika wa Vyama vya Akiba na Kukopa ili waweze kukopa na kupunguza makali ya maisha; na kwa kuwa makato ya fedha kwa

ajili ya mikopo wanayokopa hukatwa moja kwa moja kupitia Halmashauri na Kurugenzi zao baada ya kupokea idadi ya waliokopa na kuwakilisha kwenye Idara ya mishahara; na kwa kuwa utaratibu wa makato ni kwamba yasizidi asilimia 50 ya mishahara yao.

(a) Je, ni chombo gani kinawalinda Walimu hao ili kuona kwamba huduma hiyo inawasaidia kuboresha maisha yao badala ya kuwakandamiza?

(b) Je, ni sababu zipi za Msingi zinazozifanya baadhi ya Halmashauri na Kurugenzi kutumia makato ya mishahara hiyo ya walimu kwa shughuli nyingine na kuchelewesha mawasilisho ili walimu hao waweze aidha kukopeshwa au kurejesha mikopo kwa wakati unaotakiwa?

(c) Kwa kuwa kuna Taasisi nyingine na hata watu binafsi ambao hupeleka maombi katika baadhi ya Halmashauri za Wilaya kama *Tunakopesha Limited, Bondeni Investment* na kadhalika kama kule Wilaya ya Handeni ili waweze kuwakopesha wafanyakazi wakiwemo Walimu kwa riba kubwa inayokaribia 50% ikilinganishwa na asilimia 5 wanayotoza Ushirika wa Walimu wa Akiba na Kukopa, matokeo yake Walimu hushindwa kumudu kulipa mikopo hiyo na deni hujilimbikiza kila mwezi; je, ni nini agizo la Serikali kwa Kurugenzi hizo ili kuwanusuru Walimu hao?

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (k.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, Mbunge Viti Maalum, swali lake lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, Mbunge Viti Maalum, kuwa walimu kama watumishi wengine wanaruhusiwa kujiunga na ushirika wa vyama vya akiba na kukopa ili kuweza kukopa na kupunguza makali ya maisha. Ili kuhakikisha kuwa mwalimu huyu anarejesha makato hayo bila kuathirika kimaisha zipo sheria ambazo zimewekwa na nchi ili kumlinda mtumishi yeyote anayekatwa mkopo usizidi zaidi ya 1/3 ya mshahara wake. Kwa mujibu wa kifungu Na. 4 na Na. 8, vifungu vidogo (a) na (b) cha kanuni za kudumu za utumishi yaani *Standing Orders* za mwaka 1984 kinatoa ufafanuzi wa namna mtumishi wa Serikali anavyotakiwa kurejesha mkopo huo.

(b) Mheshimiwa Spika, Halmashauri na Kurugenzi yoyote inayotumia fedha za makato ya mishahara ya walimu kwa shughuli nyingine na kuchelewesha mawasilisho ili walimu hawa waweze aidha kukopeshwa au kurejesha mikopo kwa wakati unaostahili zinakwenda kinyume na Sheria za fedha. Hivyo basi, Wizara yangu kwa kushirikiana na TAMISEMI kwa pamoja zimekuwa zikikemea na kuchukua hatua pale inapothibitika kuwa Halmashauri na Kurugenzi zimetumia makato ya mishahara ya walimu kwa shughuli nyingine na kuamriwa kurejesha fedha hizo mara moja.

(c) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa kuna mashirika mengi ambayo yameingia mkataba na watumishi wa Serikali kama yalivyoainishwa na Mheshimiwa Mbunge kama vile *Bondeni Investment, Tunakopesha Limited* na kadhalika. Kimsingi ni vyema mwalimu au mtumishi yeyote kuelewa vizuri masharti yaliyomo kwenye mikataba ya ukopeshaji yaliyowekwa na mashirika hayo kabla ya kuingia kwenye mkataba wa kukopa.

Mheshimiwa Spika, kwa kufanya hivyo, mtumishi ataepuka athari anazoweza kupata endapo atachukua mkopo huo. Aidha, Halmashauri na Kurugenzi yoyote inatakiwa kufanya uchunguzi wa kina kuhusu mashirika mbalimbali yanayojihusisha na ukopeshaji ili kuweza kushauri watumishi wao kuhusiana na mikopo inayotolewa na mashirika hayo.

**MHE. DR. AISHA O. KIGODA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Kwa vile katika *pay slip* za baadhi ya Walimu inaonekana kwamba wale watu ambao wamependekezwa kuwa wanakopesha majina yao yanajitokeza mara mbili au mara tatu kwa mfano kama *Tunakopesha Limited,* unakuta inajitokeza mara tatu katika *pay slip* kwa wakati mmoja na kusababisha

mshahara wa Mwalimu kubakia sifuri ni kwa nini basi Halmashauri hizi zisifuatilie ili kuhakikisha kwamba majina ya hawa wakopeshaji hayatokei mara mbili?

(ii) Kwa vile wanaohusika na kupeleka makato ya Walimu hawa ambao wamekopeshwa katika Idara ya Mishahara ni Mkurugenzi kwa nini basi inajitokeza hivi haoni kwamba ikijitokeza mara mbili au tatu inaashiria kuna hali ya rushwa au mianya rushwa inayotokea hivyo kuongeza malalamiko kwa Walimu?

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (k.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI):** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kama kweli kwenye *pay slip* ya Mwalimu, kampuni moja imejitokeza mara mbili au tatu na una hakika Mwalimu yule hakukopa, hayo ni makosa. Tunachoomba ni kwamba Mwalimu huyo basi awasiliane na Halmashauri ili waweze kurekebisha kosa hilo.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, tunaomba kama unazo taarifa zinazoashiria kwamba kuna rushwa tuletee Wizarani tutawashughulikia wahusika mara moja.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha. Kabla hatujaendelea, kuna matangazo ya vikao viwili vya Kamati kwa leo. Kamati ya kwanza, Kamati ya Uwekezaji na Biashara, Mheshimiwa William Shellukindo, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, anaomba kikao kifanyike leo Jumanne tarehe 1 Julai, 2003 mara baada ya kipindi cha maswali na majibu chumba cha Kamati namba 54.

Kamati ya pili itakayokutana leo ni Kamati ya Hesabu za Serikali *(PAC),* hii inahitaji maelezo, ni kwamba kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kamati ya *PAC* Mwenyekiti wake anatokana na Kambi ya Upinzani. Sasa tulishafanya maelewano ya siku nyingi kwamba Spika anashauriana na Kiongozi wa Upinzani Bungeni wangependa nani awe Mwenyekiti wa Kamati hiyo wakishakubaliana jina la huyo basi Spika anamteua na kumweka kwenye Kamati ya *PAC* ili aweze kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti.

Kwa msimamo huo, nimeshauriana na Kiongozi wa Upinzani Bungeni na amenishauri kwamba wanapendekeza Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, awe Mwenyekiti wa Kamati hiyo. Kwa hiyo, jana nilimteua kumwingiza kwenye Kamati hiyo, leo naitisha kikao cha Kamati ili kifanye uchaguzi rasmi wa Mwenyekiti wao kulingana na Kanuni za Bunge. Kwa hiyo, majira ya saa tano mkutane kwenye vyumba vya Kamati. *(Makofi)*

Baada ya hapo, napenda kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge jambo lifuatalo kwamba kwa ajili ya ugeni wa Marais wawili kesho, Spika amewaalika kwenye chakula cha mchana hapa kwenye kantini yetu. Baada ya shughuli za kuhutubia Bunge, wageni watakula chakula hapa. Kwa ajili hiyo basi, kesho tangu asubuhi kantini itafungwa hakuna chai ili iwekwe katika hali ya kupokea ugeni wa namna hiyo. Kwa hiyo, mipango ya chai kwa kesho, naomba ifanywe sehemu nyingine sio kwenye kantini yetu.

Mwisho wa matangazo, tunaendelea na *Order Paper.*

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2003/2004**
**Wizara ya Kilimo na Chakula**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami nichangie machache juu ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula.

Mheshimiwa Spika, awali kabisa, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula, kwa kutoa ufafanuzi mzuri kabisa katika hotuba yake, kwa kina kabisa na mambo yake yameeleweka vizuri, nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia naomba nichukue nafasi hii rasmi niwapongeze wanawake wote wa hapa nchini hasa wale wanaotoka katika Mikoa inayozalisha chakula kwa wingi kwa mfano Mbeya, Iringa, Rukwa pamoja na Ruvuma wanafanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unapozungumzia suala la Mikoa kuzalisha ziada ya chakula na hasa kwa wakulima wadogo wadogo kule vijijini ni lazima uelewe kwamba kazi hiyo kwa kiasi kikubwa sana imefanywa na wanawake. Hiyo sio siri ni suala la ukweli na uwazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo basi, ni vizuri wanawake wasaidiwe katika suala zima la uzalishaji wa chakula. Unawezaje kuwasaidia? Ni kama ilivyoainishwa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwamba wapewe unafuu wa bei za mbolea, pembejeo na kadhalika. Kwa hiyo, naunga mkono 100% kwa Serikali kutoa unafuu au ruzuku ya mbolea kwa Mikoa ile minne ambayo inazalisha chakula kwa wingi. Naamini hilo litatusaidia sana hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina mfano wa Mkoa wa Mbeya ambao nimeuzoea sana na ni mwakilishi wa wanawake wa Mkoa ule, katika miaka ya 1980, 1990 Mkoa wa Mbeya kwa kutumia wakulima wadogo wadogo walikuwa wanaweza kuzalisha mahindi ekari moja magunia 25-30 hayo ni mambo ya ukweli kabisa lakini hapa katikati wakati tumepata matatizo kidogo ya kuwa na bei kubwa sana ya mbolea basi uzalishaji ulishuka kidogo. Lakini naamini katika mpango huu, tumetoa maamuzi ambayo ni ya busara kabisa na ni lazima tuyaunge mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ni lazima tuwasaidie hawa wanawake kwa sababu ni wazalishaji wakubwa wa mazao mbalimbali ni kuwasaidia mitaji wanapokuwa wakianzisha viwanda. Wanawake ni mafundi sana katika uanzishaji wa viwanda vidogo vidogo vya usindikaji wa mazao. Kwa hiyo, ni lazima tujitahidi kuwapa mikopo midogo midogo ili waweze kusindika mazao mbalimbali. Mimi nina ushahidi kazi hiyo wanaiweza kule Mkoa Mbeya nimeona wanafanya kazi nzuri sana, Kilimanjaro nimeona wanafanya kazi nzuri sana kupitia vikundi vyao vya uzalishaji. Hapo naona ni lazima tuwaunge mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kidogo suala la mazao ya biashara kwangu mimi suala la zao la kahawa linanigusa sana kwa sababu linanihusu huko Mkoani Mbeya na vile vile katika Mkoa wa Kilimanjaro. Kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula ni kweli kabisa kwamba uzalishaji wa mazao yetu makuu sio tu umeshuka kiuzalishaji lakini vile vile hata bei zake zimeshuka. Sasa sio sahihi ninavyoona mimi na ni vigumu kabisa kuzungumzia kutupilia mbali uzalishaji wa zao la kahawa. Mimi sitakuwa mmoja wa wale ambao wanakubaliana na wazo hilo dawa kubwa ni kujizatiti katika ubora wa zao la kahawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ni shahidi kabisa kwamba ukijizatiti katika kuboresha kahawa ni kweli kabisa unapata bei nzuri. Pale Moshi niko katika soko la kahawa la *(TCB),* najionea mwenyewe kwamba kwa wakulima hasa wale wanaopitia vikundi vya uzalishaji wa kahawa na sasa hivi ni vingi tu na Vyama vya Ushirika vya Msingi wale ambao wameamua kukusanya nguvu zao pamoja na kufuata taratibu na kanuni nzuri za kilimo ili waweze kupata ubora wa kahawa, wanapata bei nzuri.

Kwa hiyo, ni sahihi kabisa na nakubaliana na wazo la Wizara au Serikali la kutaka kila Mkoa uchague zao moja ili waweze kujiimarisha hapo waweze kuzalisha zao ambalo ni zuri na litakuwa bora litapata fedha nyingi. Kwa hiyo kwa Kilimanjaro, Mbeya, Kagera, Iringa, Ruvuma Mikoa yote ambayo inazalisha kahawa, nawashauri wachukue zao la kahawa kama ndio zao watakalolisimamia kufa na kupona tusiivunje historia ya nchi hii kwa kulitupilia mbali zao la kahawa. Kwa wengi hasa katika Mikoa hii niliyoitaja wamelelewa na zao la kahawa kwa hiyo siyo busara kabisa kulitupa na itakuwa ni makosa. Ili kufikia kiwango hicho ni lazima Serikali iunge mkono na njia ya kuunga mkono ni hiyo ambayo Serikali imefanya kwa kipindi hiki kwa kujaribu kusaidia uzalishaji wa zao la kahawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza wenzetu wa *EU* kwa kuunga mkono juhudi zetu Watanzania katika kuliendeleza zao la kahawa. Tumesikia jinsi ambavyo Serikali itaweza kusaidia kupitia fedha ya *STABEX. STABEX* ni fedha ya *EU* kwa hiyo, *EU* iko mstari wa mbele katika kutusaidia. Lakini vile vile inatusaidia katika kufanya utafiti wa zao la kahawa kupitia Taasisi

ya Utafiti wa Kahawa Kituo ya Lyamungo. Wameamua katika kipindi cha miaka mitatu watatusaidia katika suala zima la utafiti na kuanzia mwaka 2004 wako tayari kutoa *Euro 90 millions* ili kusaidia taasisi hii iweze kufanya utafiti wa kina kuhusu uzalishaji wa mbegu nzuri ambayo inastahimili magonjwa ya kahawa na kwa faida ya sisi Watanzania. Ndio maana narudia kusema kwamba tusifanye makosa kuacha zao la kahawa likiwa linapata matatizo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba hivi sasa kuna haja kuangalia na mazao mengine ambayo yatatusaidia. Kuna baadhi ya Wabunge nafikiri jana wametaja moja ya zao ambalo na mimi naunga mkono ni zao la maua. Ni wazi kwamba umefika wakati sasa tuangalie namna gani zao la maua linaweza kutusaidia. Imejionyesha wazi kwamba zao la maua ni zao ambalo linaweza kutusaidia sana kiuchumi. Hivi sasa Kenya wanazalisha hekta 1,000, Zambia hekta 240, Uganda hekta 210 sisi Tanzania hekta 70 tu bado bado tuko nyuma hata wale walioanza nyuma yetu katika uzalishaji wa maua kwa mfano Zambia na Uganda wako mbele kutokana na takwimu nilizozitaja.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nashauri kama Wizara ilivyojizatiti ielekeze nguvu yake katika kuwasaidia wakulima wa maua hasa wale wakulima wanaotoka Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Mikoa mingine kama Mbeya na Iringa inafaa kuzalisha maua ambapo wangeweza kujipatia fedha nyingi. Maeneo haya yana mazingira mazuri kabisa katika uzalishaji wa maua ingawa kwa Mkoa wa Mbeya labda tutakwama kidogo kwa sababu kiwanja cha ndege hakijawa tayari na kwa nafasi hii pengine kwa sababu sitapata nafasi ya kuchangia Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi basi tukipe *priority* kiwanja hiki kwa sababu kina manufaa yake, tutoe fedha za kutosha ili tuweze kusaidia wananchi wa Mikoa ile na wao waweze kupata nafasi ya kusafirisha maua kwa sababu watapenda vile vile kuzalisha maua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, faida nyingine ni kwamba ni sekta inayoajiri watu wengi. Asilimia 70% ya watu ambao wanaweza kuajiriwa katika hekta moja ni wanawake na 30% ni wanaume. Kwa hiyo, kwa ajira ni zao ambalo linaweza kutusaidia kabisa. Lakini vile vile linakomaa haraka miezi sita tu unaweza kupata mavuno yako na vile vile linaweza kusaidia kabisa uchumi wetu kwa maana hiyo niliyoieleza.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nakubaliana kabisa na maelezo yaliyotolewa na Serikali kuanzishwa kwa Mfuko wa *Export Credit Guarantee Scheme* uweze kusaidia wakulima wa maua. Naamini Mheshimiwa Waziri atapenda kutufafanulia vizuri jinsi gani wakulima wa maua wataweza kufaidika chini ya mfuko huu. Vile vile nashauri wakulima wadogo na wakubwa waweze kusaidiwa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba nitofautiane kidogo na mtizamo wa Kamati ya Kilimo na Ardhi wa kushauri kwamba *extension* au wataalam wa kilimo warudi kusimamiwa na Wizara. Naomba nishauri kwamba waendelee kubaki chini ya Halmashauri za Wilaya, cha kufanya labda ni kuongeza idadi ya *extension staff* kwa sababu hivi sasa tunazungumzia mazao mengi sana, ya viungo, matunda na yale ya asili kwa hiyo tunahitaji kuongeza *extension staff* lakini wawepo Wilayani chini ya Madiwani yaani Halmashauri za Wilaya na kwa kutumia mbinu shirikishi jamii hawa watu tunawahitaji wawe pale pale katika Halmashauri za Wilaya na sio vinginevyo.

Tukirudi tena nyuma katika mtizamo wa zamani ambao tuliubadilisha nafikiri katika miaka ya hivi karibuni, ninavyoona mimi ni makosa. Kwa hiyo, waendelee kubaki katika Halmashauri ya Wilaya kwa maoni yangu mimi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niliona nichangie hayo machache kwa sababu tunayo kazi kubwa kitabu hiki kimeainisha mambo mengi sana. Nafikiri ni wakati ambao hata Waheshimiwa Wabunge tushirikiane kuwashawishi wakulima warudi kazini wafanye kazi badala ya starehe, watu wamezidisha mno starehe, wanatoa vipaumbele kwenye starehe zaidi kuliko kazi lakini tukifanya kazi tutafanikiwa tu lisiwe jukumu la mtu mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Felix Mrema, kabla hujaanza namwita Mheshimiwa Naibu Spika, aje kuongoza Bunge ili mimi niendelee na maandalizi ya ugeni wetu.

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti*

**MHE. FELIX C. MREMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Pia najiunga na wenzangu kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote waliochaguliwa katika chaguzi zilizofanyika tarehe 18 Mei, 2003, karibuni sana hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula na safu yake yote ya uongozi kwa hotuba yao nzuri ya Bajeti aliyowasilisha jana. Nimtoe wasiwasi, naunga mkono hoja yake kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hiyo kwa sababu ukiiunganisha hotuba hiyo aliyotoa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula, Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, zinadhihirisha wazi kwamba safari hii Serikali sasa ni *serious* katika kuwalenga wakulima wa nchi hii. Hii *seriousness* iko wazi kabisa katika hotuba ya Waziri wa Fedha na Waziri huyu wa Kilimo na Chakula kwamba wanachukua hatua za kuongeza uwekezaji katika sekta hii muhimu ya kilimo ili kukifanya kikue kwa haraka zaidi. Ametueleza kwamba mwaka huu kimekua kwa 5% na tunahitaji kufikia 10% ili kuondoa umaskini na kuchangia katika Pato la Taifa. Sasa bado safari ni ndefu lakini mwanzo huu unaashiria kwamba tutaweza kufika kwa haraka zaidi kuliko ilivyokuwa huko nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huko nyuma kwa muda mrefu tumekuwa watu wa maneno mengi sana, msamiati wa kila aina tumekwishautoa, siasa ni kilimo, kilimo cha kufa na kupona, mambo mengi tumeyasema kwa muda mrefu sana mpaka imefika wakati tunaanza kufananishwa na kama wenzetu wa Argentina walivyokuwa wanajifananisha. Wao wana ardhi nzuri sana ekari karibu 100 milioni ya ardhi ambayo *the best in the world, supper fertile.* Wakawa wanasema Malaika wakamuuliza Mwenyezi Mungu mbona umependelea nchi hii ya Argentina namna hiyo ukawapa ardhi nzuri namna hii? Akajibu akasema hebu ngojeni tu muone nitaweka watu wa namna gani katika nchi hiyo hamtawaonea wivu kwamba wamependelewa. *(Kicheko)*

Sasa sisi tulikuwa tunaanza kusogeleasogelea huko huko lakini pengine Malaika wangeuliza mbona umewapendelea Watanzania kwa kuwapa ardhi nzuri namna hiyo maana tuna karibu milioni 40 ya ardhi ambayo wanasema ni nzuri sana kwa kilimo lakini tunayolima haizidi ekari 8 milioni, sasa Mwenyezi Mungu angesema hebu ngoja uangalie nitawapa viongozi wa namna gani katika nchi hiyo ya Tanzania tuangalie kama wanaweza kutumia raslimali yao ile kujiendeleza. Lakini sasa tunaona kweli tuna uongozi ambao unaelewa *potential* iliyoko katika nchi hii na una mikakati thabiti ambayo inawalenga wakulima wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema tatizo letu ni sisi viongozi sio wakulima. Wakulima wetu wameshuhudia jinsi sisi tulivyowageuza wao kuwa kama chombo cha majaribio ya nadharia zetu za *social engineering.* Tumefanya hivi badala ya kutambua kwamba raslimali kubwa tuliyonayo ni *brain power* ya wakulima wetu. Hawa wakulima *they have survived against all odds,* ikija ukame mzigo wanaubeba wenyewe wanaelewa jinsi ya kujihami mpaka mvua ije, viwavijeshi wanaelewa jinsi ya kujihami mpaka msimu mwingine, bei mbaya ya mazao yao wanaelewa jinsi ya kujihami mpaka bei itakapopanda tena, njaa ikija sisi Dar es Salaam tunashughulika jinsi ya kupata mchele wa Japan wa kwenda kuwauzia wakulima je, tunaelewa jinsi Mjapan anavyomlinda, kumtetea na kumpendelea mkulima wake?

Serikali ya Japan kwa makusudi kabisa na kwa muda mrefu bei anayolipwa mkulima wa mpunga kule Japan ni mara kumi ile ya *world market price* na wanahakikisha kwamba mchele kutoka nje hauingii Japan mpaka upewe *quota. WTO* ikaamua kuwaambia bwana hizi *quota* zenu mziondoe wakaziondoa lakini Wajapan wanahakikisha *duty* ya kuingiza mchele Japan mpaka leo hii ni maradufu inaifanya bei ya mchele Japan kutoka nje iwe ni ghali zaidi kuliko huko ilikotoka kwa makusudi kabisa kumlinda na kumtetea mkulima wake.

Sasa sisi tunatakiwa pia kufanya hivyo na nashukuru Serikali sasa inatambua umuhimu wa kumsaidia huyu mkulima wetu nayo imekuja na mipango ya ruzuku na hatuonei aibu ruzuku. Wenzetu

*Europe* hawaoni aibu kumsaidia mkulima wao kwa kumpa ruzuku. *Europe* na Marekani wanabishana kiwango cha ruzuku anayopewa mkulima na juzi tu wamekubaliana kwenye *EU* kwamba mkulima badala ya *subsidy* ile iwe *pegged to production* sasa inakuwa *pegged* kwa kulinda mazingira lakini *subsidy* bado inatolewa wameipa jina lingine tu la kulinda mazingira lakini *subsidy* inatolewa na Ufaransa wamehakikisha wanabakiza ya kwao iwe *pegged to production* sasa sisi hapa tunaona aibu kupeana ruzuku, kwa nini tunaona aibu kutoa ruzuku kwa mkulima wetu huyu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru Ndugu yangu Cynthia Ngoye, kazungumzia sekta ya maua ambayo mimi nashiriki ilikuwa inanitia aibu saba. Hekta 70, ardhi tunayo nzuri sana wenzetu Kenya wana hekta 1,000 na sisi maua yetu tunayapeleka Kenya kwa sababu hatuwezi kuyapeleka *Europe* kupitia *Kilimanjaro International Airport* kwa sababu ni ghali zaidi tunayapeleka Kenya halafu Kenya wanaweka kama ndio *export* za Kenya hizo. Nikasema jamani nchi yetu hii, *we have to be serious* katika sekta hii ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kuna hii programu inaitwa *ASDP* inatia moyo sana kwamba sasa tunalenga kwa mkulima na wanasema 75% ya mradi mzima unakwenda kwa wakulima. Mimi nasema *Alhamdulillah* kama kweli ndivyo ilivyo nashukuru Mungu kwamba, *World Bank* na wahisani wote hawa wanakubali kutoa fedha zitakazomlenga mkulima moja kwa moja. Lakini nilipoangalia ndani ya mradi wenyewe nina wasiwasi huko ndani Kamati zimezidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hebu ni-r*un down list* za Kamati ambazo zimeundwa katika hii *ASDP.* Kuna Kamati ya Kitaifa ya Uongozi wa Mpango *(National Steering Committee)* hiyo ni ya Makatibu Wakuu na watu wengine wote. Kuna Kamati ya Pamoja ya Serikali na Sekta Binafsi *(Agricultural Sector Advisory Committee - ASAC) Chairman* wake anatoka kwenye sekta binafsi lakini wengine wote ni hao hao. Kuna Kamati ya Pamoja ya Serikali na Wahisani inaitwa *Food and Agricultural Sector Working Group (FASWG).* Pia kuna Kamati ya Usimamizi na Uratibu wa Mpango*(Inter-ministerial Coordination Committee),* Kamati ya Kitaifa ya Uongozi *(National Sector Committee)* ambayo inatakiwa kuwa na mkutano mara moja kwa mwaka na katika mkutano huo Rais anatakiwa awe Mwenyekiti.

Halafu kuna sektarieti ya Mipango ya Mkoa na kwenye Wilaya kuanzia kwenye Kijiji, kwenye Kata mpaka kwenye *Full Council* kuna Kamati za Ushauri. Halafu unaendelea tena kuna *Task Forces* wanaita Kamati za Kusimamia Uandaaji na Utekelezaji wa Mpango katika maeneo makuu ya mpango. Halafu kuna *working group* zinaitwa timu za wataalam. Nikasema kwa mkao huu tutafika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu nikaenda nikachunguza sasa ule mgawanyo wa fedha kwa miaka mitano tunaambiwa kwamba ni dola 617 milioni za mradi mzima, za *development* ni milioni 383, basi hiyo ndiyo ambayo inakwenda moja kwa moja katika *development.* Mishahara ni dola milioni 73 kwa miaka mitano hiyo na *Other Charges (OC)* ni milioni 144. Jumla ya mishahara na *OC* ni milioni 217.

Sasa jamani Mheshimiwa Waziri naomba aliangalie tena hilo. Mkazo wa hizi uende zaidi kwenye mambo muhimu na yatakayomlenga mkulima na mambo muhimu yapo na yanajulikana *we don't need to invent the wheel,* tunajua nini kinachohitajika kwa ajili ya kuinua kilimo katika nchi yetu, bila mtaji hatutafika. Kwa hiyo, ni lazima kuunda chombo kama alivyosema Mheshimiwa Waziri, *Agricultural Finance Cooperation,* Kenya wanayo hii na hivi sasa wametenga karibu dola milioni 143 kwa mwaka huu wa fedha kwa ajili ya kutoa mitaji kwa wakulima na wanatoa mikopo ya muda mrefu na ya riba nafuu ya asilimia tano. Sasa tupange kitu cha namna hiyo hapa kwa ajili ya kusaidia sekta yetu ya kilimo, bila hivyo tutakuwa tunazungumza tu maneno yatakayokuwa yanaendelea tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unajua wanasema kama hutaki kitu kifanyike unda Kamati, hakitafanyika. Sasa mimi naomba tusiwe hivyo, tuziangalie hizi Kamati zetu na kama kuna umuhimu wa kuwa na hizi Kamati zote au kama kuna njia tunaweza tukazi-*streamline* tufanye hivyo ili tuwe na chache zitakazofanya kazi. Unajua badala ya Kamati mpe mtu kazi ya kufanya ili akaifanye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa wakulima wetu ni wajanja, wanaelewa bwana, tusiwadharau, wame-*survive* na mpaka sasa hivi wana-*survive* wakati hatujawapa ruzuku na wala akipata matatizo hatuko pale kumsaidia. Ukitokea ukame Marekani, Bush anakwenda *Congress* kutafuta pesa ya

kuwasaidia wakulima. Sisi hapa hatuna mpango wa namna hiyo, anabaki mwenyewe tu. Sasa tunachotaka ni kumtengenezea mazingira mazuri ya yeye kuweza kutumia brain power yake na uzoefu wake ili kuweza kuzalisha kile ambacho tunataka kizalishwe ili kuinua uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala la soko. Mimi nilikuwa nafikiri kwamba tunaweza tukaitumia *strategic drain reserve* kama chombo sasa cha kumpa mkulima bei ambayo inaoana na matumizi yake pamoja na faida ambayo anategemea kuipata katika sekta ya kilimo na sisi tuitumie ile *SGR* kwa kutafuta masoko ndani au nje ya nchi. Tunaweza tukawa kabisa hapa ni *bread basket* katika ukanda huu wote wa Afrika. Hakuna mwingine mwenye ardhi nzuri na kubwa kama yetu sisi. *South Africa* ambao wanatulisha sisi sasa hivi ardhi yao ni jangwa kwa kiwango kikubwa kabisa, lakini wameweza kutumia hicho kidogo walichonacho kitaalam kuhakikisha kwamba wanazalisha ziada ambayo inatulisha sisi katika ukanda huu.

Kwa hiyo basi na sisi tugeuze kilimo chetu kwa kutumia hii ardhi nzuri na inayolimika ambayo Mungu ametuzawadia, pamoja na amani hii tuliyonayo, tuje na mipango ya kuitumia ardhi hii. Hatuna sababu kwa nini hatuwezi kukigeuza kilimo chetu tukafikia hiyo asilimia kumi ambayo tunataka ifikie ya kukua ili kuondoa umaskini katika nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MATHEW T. OLE-TIMAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyo mbele yetu. Aidha, nimpongeze Mheshimiwa Waziri pamoja na safu yake yote kwa kazi nzuri na hotuba nzuri ambayo wameiandaa na kuiwasilisha hapa, hivyo ninaunga hoja mkono kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa Yesu wananchi wa nyakati zile walilima kwa kutumia jembe la mkono pamoja na jembe la kukokotwa kwa kutumia wanyama kazi. Miaka 2003 baadaye, bado sisi Watanzania tunalima kwa kutumia jembe la mkono na jembe la kukokotwa na wanyamakazi hasa watu wa Kijijini na bahati mbaya haya majembe ya mkono pamoja na haya ya kukokotwa wala hatuwezi kujitosheleza kwa kuyatengeneza, bado tunahitaji kuyaagiza nje.

Mimi nafikiri ni aibu na kwa utaratibu kama huu mimi naogopa kwamba hatutaweza kujitegemea kwa chakula. Tutaendelea kuwa tegemezi na ombaomba ambapo nafikiri ni aibu kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naishauri Serikali na Wizara, ndiyo nimeona kwenye kitabu hiki kwamba wameagiza matrekta makubwa 274 kipindi kilichopita na matrekta madogo 75 na mimi nasema kwamba hayo hayatoshi. Naomba tuyaagize zaidi kwa sababu tunahitaji kubadilisha utaratibu wetu wa kilimo. Badala ya kulima kwa kutegemea jembe la mkono tulime kwa kutegemea trekta ndogo na kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, naomba nizungumzie kidogo kilimo cha umwagiliaji. Nafikiri sote tunakubali kabisa kuwa kilimo cha uhakika ni kilimo cha umwagiliaji na kwa bahati nzuri kama Waziri alivyoonyesha kwenye kitabu chake nchi yetu tuna sehemu au maeneo makubwa ambayo tunaweza kuyatumia kwa shughuli za umwagiliaji. Hayo anayazungumzia kwenye ukurasa wa 26 aya ya 52.

Aidha, wananchi wetu kwa muda mrefu wanafahamu kilimo cha umwagiliaji. Mfano mzuri nichukue wananchi Wilayani Ngorongoro wa kabila la Wasonjo kwenye Vijiji vya Samunge, Digodigo, Kisangiro, Oldonyosambu na Sale, wamekuwa wakitumia kilimo cha umwagiliaji miaka nenda rudi tangu enzi za mababu. Kwa hiyo, kinachohitajika ni kwa Serikali yetu kuwasaidia wananchi hao kuwapa uwezo na utaalam wa kisasa ili waweze kuboresha na kuimarisha kilimo cha umwagiliaji. Bila kufanya hivyo tutaendelea kuwa tegemezi kwa chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu ambalo nataka kuchangia ni kuhusu Mfuko wa pembejeo. Lengo la Mfuko huo ni zuri kwa sababu lengo lake ni kusambaza pembejeo za kilimo na mifugo kwa wananchi wetu Vijijini. Nitoe mfano, mwaka 2002 Wilayani Ngorongoro tulivuna mahindi mengi sana kuliko kawaida. Lakini kwa bahati mbaya yakashambuliwa na dumuzi, tukatafuta dawa, hatujaipata, tuliyoipata ni aina fulani ya dawa kutoka Kenya ambayo walisema kwamba ni *fake.* Tulishindwa kupata

dawa hiyo pamoja na kuwepo kwa Mfuko huu wa pembejeo. Kwa hiyo, Mfuko huu wa pembejeo kwa maoni yangu umeshindwa kufikia malengo yake yaliyotarajiwa. Kwa nini Mfuko huu umeshindwa kufikia malengo yake?

Kwanza, utaratibu wa kuwataka wakulima na wafugaji wadogo wadogo kuwa na dhamana isiyohamishika na yenye hati unajiuliza watapata wapi? *(Makofi)*

Pili, ni masharti ya Mfuko wa pembejeo ambayo ni ya Kibenki. Hivyo wakulima na wafugaji wadogo wadogo hawataweza kutimiza masharti hayo hata kidogo na hayo mabenki mara kwa mara huwa yako mbali.

Kwa hiyo, Mfuko huu unakuwa ni kwa watu wanaoishi Mijini na kwa watu ambao wana uwezo wa kifedha lakini hauwafikii walengwa walioko Vijijini yaani wakulima na wafugaji. Kwa hiyo, mimi namshauri Mheshimiwa Waziri pamoja na Serikali kwa ujumla kwamba tutafute njia ya kulegeza utaratibu na masharti hayo ili Mfuko huu uweze kuwafikia wananchi wakulima na wafugaji wadogo wadogo huko Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. BENITO W. MALANGALILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nikushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula na nianze kwa kumpongeza kwa hotuba nzuri.

Hotuba hii ni nzuri, imeandikwa vizuri kabisa, ni bahati mbaya tu na naomba nimpe pole kwamba anaendesha Wizara hii katika kipindi kigumu kabisa. Kipindi ambacho Taifa letu lina matatizo hasa ya chakula na niseme tu kwa ufupi kwamba mwaka 2000 Mheshimiwa Rais aliigawa Wizara ya Kilimo na Ushirika kuwa Wizara mbili, Wizara ya Kilimo na Chakula na Wizara ya Ushirika na Masoko. Ni wazi kwamba yalikuwa ni matarajio ya Watanzania wengi kwamba Wizara hizi mbili zitafanya kazi nzuri kwa kujaribu kupunguza matatizo ya wakulima katika nchi. Kwa hiyo, najaribu kuiona kama hii ni changamoto kwa Wizara hizi mbili kuona kwamba angalau zinafanya vizuri katika jukumu hili ambalo walipewa na Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mchango wangu mimi kwanza kabisa nianze na zao la pareto. Mimi Wilaya yangu ya Mufindi na Mikoa ile ya Kusini Nyanda za Juu ni Mikoa ambayo kwa sehemu kubwa sana inalima zao la Pareto na uhai wa zao hili kwa sehemu kubwa ulikuwa unategemea kiwanda kile kilichopo pale Mafinga cha Kusindika Pareto. Kiwanda hiki kwa miaka mingi kimekuwa na matatizo mpaka kilipofikia kubinafsishwa akapewa mwekezaji mmoja pale Mafinga. Lakini alifanya kazi nzuri kwa kipindi kifupi sana baadaye kiwanda kile kimeanza kutokufanya kazi nzuri na kwa kweli hakuna maelezo yanayoeleweka ambayo yanatolewa na Serikali juu ya kusuasua kwa ufanyaji kazi wa Kiwanda kile. Mimi nadhani ni wakati muafaka sasa kuiuliza Serikali matatizo ya Kiwanda cha Kusindika Pareto pale Mafinga yakoje na ni yapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri amesema Serikali itatoa fedha kwa ajili ya kununua pareto waliyonayo wakulima hivi sasa. Sasa mimi nauliza je, utaratibu huu ni wa kudumu? Ni vizuri tukajiridhisha, tukawa na majibu ambayo sisi kama wawakilishi wa wananchi tutakwenda kuwaambia wananchi kwamba hivi sasa pareto yote itaendelea kununuliwa na Serikali.

Kwa hiyo, ni vizuri tukawa tunajua kwa sababu kuna kigugumizi kikubwa sana juu ya kuendelea kuwaambia wakulima walime pareto ambayo wamekaa nayo ndani ya nyumba zao kwa muda mrefu. Kwa hiyo, nadhani tunahitaji maelezo ya kina ya Serikali juu ya maendeleo ya ukulima wa pareto ndani ya nchi yetu ili na sisi tupate nguvu ya kuwaambiwa wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, zao la pili ambalo pia ningependa kulizungumzia ni zao la chai. Kwanza kabisa, ningependa kuipongeza sana Bodi ya Chai kwa kufanya kazi nzuri sana ya kuwatetea wakulima wa zao hili. Sina hakika na Bodi nyingine lakini moja ya kazi nzuri ambazo zimefanywa na

Bodi ya Chai ni kuhakikisha kwamba inawawekea wakulima bei ya chini ya zao lao la chai. Mara nyingi tunapoiambia Serikali iziruhusu Bodi za Chai kupanga bei ya chini ya mazao ya wakulima Serikali imekuwa ikipata kigugumizi juu ya jambo hili.

Mimi nafikiri Bodi ya Chai imeonyesha mfano, bei ya chini kabisa ambayo mwekezaji mwenye kiwanda anayotakiwa kununua kwa mkulima ni shilingi 65/= kwa bei ya sasa. Jambo hili limewafurahisha sana wakulima, kwa hiyo nilikuwa nadhani ni vizuri Serikali ikabadilisha sheria yake kwamba Bodi za Mazao pia ziwe na uwezo wa kupanga bei ya chini ya mazao ya wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia moja ya mambo ambayo ningependa kuishauri Serikali yamekuwepo maoni ya muda mrefu kwamba katika zao la chai kuna Bodi mbili, kuna Bodi ya Chai na kuna Bodi ya Wakala Wanaosimamia Wakulima Wadogo. Sasa *cess* ambayo inatozwa kwa ajili ya kuendesha Bodi hizi mbili ni asilimia moja ya mauzo yote ya chai ndani ya nchi. Sasa yapo mapendekezo ya muda mrefu kwamba gharama za kuendesha Bodi hizi mbili ni kubwa na ni vizuri Bodi hizi mbili zingeunganishwa ikawa Bodi moja. Nilikuwa nafikiri ni vizuri Serikali au Wizara hii ikaona namna ya kutekeleza ushauri huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nilikuwa nafikiri Serikali ni vizuri ikawa inazisikiliza sana Bodi hizi. Mimi najua hivi sasa kuna nguvu kubwa kabisa inayotaka kulazimisha kwamba zao la chai liruhusiwe kuingia kutoka nchi za nje. Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake hapa ameeleza kwamba zao la chai bado lina matatizo mengi.

Mimi nafikiri huu si wakati muafaka wa kuruhusu chai kutoka nje iuzwe ndani ya nchi. Sisi wenyewe kwa mwaka tunazalisha chai kama tani 25,000, lakini matumizi yetu ni tani 5,000. Kwa hiyo, tuna ziada ya tani 20,000, ambazo inabidi tutafute soko la nje. Nilikuwa nafikiri ni vizuri tukashirikiana na wenzetu hasa katika Afrika Mashariki kwa pamoja tukatafuta soko la nje ya Afrika Mashariki badala ya kufungua milango ndani ya nchi yetu na kuuana sisi wenyewe. Sisi uzalishaji wetu bado ni mdogo, bado tuna viwanda ambavyo havijawa imara kwa sababu viwanda vingi ndiyo hivi sasa vimebinafsishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu ambalo ningependa kulizungumzia pia ni hali ya chakula nchini. Tumeelezwa hivi juzi kwamba hivi sasa Wilaya 52 zimesharipoti kwamba zina njaa. Sasa Wilaya 52 ni nusu ya nchi na wakati huu ni wakati wa mavuno. Kwa hiyo, ni dhahiri kwamba nchi yetu ina njaa. Sasa ningeshauri katika jambo hili tusione aibu kulizungumza na wala tusipate kigugumizi kutangaza kwamba nchi yetu ina njaa. Maana yake huu ni mwezi wa Saba lakini *already* Wilaya 52 hazina chakula. Sasa hili ni tatizo kubwa, hapa ni lazima tuwe wakweli na tulizungumze bila kuona haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda tujiulize tulikosea wapi? Moja ya mambo ambayo lazima tukubali, tulitii mno masharti kutoka nje. Ondoa ruzuku, tukaondoa, msipange bei ya mbolea tukaondoa upangaji wa bei ya mbolea na tukaruhusu ununuzi holela wa mazao ya wakulima. Mimi natoka katika Mkoa ambao unalima mahindi, hivi sasa kule kuna watu wamefilisika na ni maskini kutokana na kujiingiza katika kilimo cha mahindi. Hapo ndipo kosa lilipotokea, sasa tufanye nini? Kabla sijashauri tufanye nini, labda nieleze kidogo tulikotoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 1992 kule Songea ulifanyika Mkutano wa Wakuu wa Mikoa minne ya kule Nyanda za Juu Kusini. Wakuu hawa wa Mikoa walikutana kujadili namna gani watumie mahindi katika kulisha wanyama katika nchi, nchi hii ilishafika huko. Tulikuwa na mahindi ambayo tulishindwa kuyala sisi wenyewe, tukayauza nje lakini yakawa bado yapo, tukawa tumefikiria ni namnna gani sasa tutumie mahindi hayo kulishia wanyama, tulikwishafika hapo. Leo nusu ya nchi tunazungumzia njaa na tunasema kwamba njaa hii ni kwa sababu ya mvua. Wakati mwingine tunasingizia tu mvua lakini ukweli ni kwamba tunayo matatizo ya msingi katika kilimo.

Katika hili nianze kwanza kuipongeza Serikali kwa kurudisha ruzuku katika mbolea na jambo hili limezungumzwa sana na mimi kimsingi sioni aibu kumpongeza Waziri wa Fedha, *he is a courageous, a daring,* mtu anayeweza kujaribu. Mimi nasema hii ni hatua ya kwanza ya kujaribu jambo jema. Kurudisha ruzuku kwa wakulima ni hatua nzuri na ni hatua ambayo kwa kweli inatakiwa kupongezwa. Hata hivyo bado ruzuku hii haitoshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbolea kutoka mwaka 1992 mpaka sasa bei yake imepanda mara thelathini katika kipindi cha miaka kumi. Pamoja na ruzuku iliyowekwa bado haitoshi na mimi ningeshauri mambo yafuatayo:-

Kwanza, ningependekeza kabisa Kamati ya Kilimo na Ardhi ifanye tathmini juu ya bei ya kweli ya mbolea. Nasema Kamati kwa sababu tukiiachia Wizara peke yake mimi naamini inawezekana mambo yasiwe kama tunavyoyatarajia. Kamati hii ifanye tathmini ya kweli juu ya bei ya mbolea na bei ya mbolea ijulikane kila Mkoa kwamba angalau gharama ya kufikisha Mbolea Iringa ni shilingi kadhaa kwa mfuko wa kilo hamsini. Nafikiri itakuwa ni kazi nzuri badala ya kuacha mbolea kuwa biashara holela. Kimsingi kilimo kimevurugika na ni vizuri kuanza upya, kwa hiyo, tukae tutafakari.

Katika kutafakari jambo hili ni vizuri tukawashirikisha wakulima wenyewe, ni *wrong assumption* kufikiri kwamba wakulima hawajui kitu, si kweli, vitabu vingi sana vimeandikwa na Wizara ya Kilimo na Chakula, lakini bado hatuendi mbele katika kilimo. Mimi nadhani ni vizuri tukawashirikisha wakulima wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ambalo nilitaka kushauri ni kuhusu mbolea ya msaada tunayopata kutoka nje. Mimi nadhani ni vizuri badala ya kuwa katika *Counterpart Fund* sasa ikaenda katika Mfuko wa Pembejeo wa Taifa. Naamini mbolea ikiwa huko, kwanza naamini ni kiasi kikubwa na kitautunisha Mfuko huu na Mfuko huu utafanya kazi nzuri zaidi badala ya utaratibu wa sasa kwamba mbolea ya msaada inayokuja katika nchi hii kwanza hata hatujui ni kiasi gani na hakuna mahali ambapo inakuwa *reported.* Lakini ikiingia katika Mfuko wa Pembejeo wa Taifa ninaamini kwamba taarifa zake zitapatikana katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri na tutaijadili na pia Mfuko huu kwa sababu utapata mbolea ya msaada kutoka nje naamini utakuwa na uwezo wa kutoa mikopo mingi zaidi si katika mbolea tu lakini pia katika viwanda vidogo vya kusindika mazao ya wakulima. Naamini huo pia utakuwa ni ufumbuzi wa namna ya kuwasaidia wakulima ili waweze kuongeza uzalishaji katika maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo pia ningependa niliseme kwa ufupi kabisa ni juu ya *SGR*. Mimi nadhani utaratibu wa sasa wa kununua mazao ya wakulima na kuyahifadhi mpaka wakati wa njaa ni utaratibu ambao siyo mzuri.

Mimi nafikiri *SGR* ifanye kazi kama ilivyokuwa inafanya *National Milling Corporation,* ifanye biashara, ikinunua mahindi kutoka kwa wakulima ikiwa nayo mengi inauza halafu inanunua tena, iwe na *rotation* badala ya kusema kwamba utahifadhi chakula.

Mimi nadhani *SGR* ifanye biashara ya nafaka katika nchi, naamini hiyo itaongeza sana uwezo wa *SGR* yenyewe kuwa na fedha za kutosha za kununua mazao ya wananchi na itaboresha bei kama walivyoshauri wasemaji wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, *SGR* ifanye kazi za *National Milling* na mara nyingi nimeshauri yale maghala ambayo zamani yalikuwa yanatumika na *National Milling* kuhifadhia nafaka ni vizuri yakaanza kufanya kazi ya kuhifadhi mahindi, lakini pia ikipata soko la nje mahindi hayo iyauze na kununua mengine kutoka kwa wakulima. *SGR* ifanye biashara, isisubiri tu mpaka eneo lipate njaa. Nafikiri huu ni utaratibu ambao kwa kweli hautatusaidia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na nisingependa nigongewe kengele nyingine na hivyo naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula. *(Makofi)*

**MHE. OMARI MJAKA ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza sina budi kukushukuru kwa kunipatia nafasi hii. Baada ya shukrani zangu hizo nataka nimpongeze sana Waziri wa Kilimo na Chakula, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara hii kwa ajili ya hotuba yao nzuri waliyoifikisha katika Bunge hili Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kweli hotuba hii ikifanyiwa kazi nataka nilithibitishie Bunge lako kwa mtazamo wangu niliouona, kwa kweli Taifa letu katika eneo hili tutapiga hatua moja kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hili la kilimo ni muhimu sana kwa Taifa letu la Tanzania. Sasa hivi kuna malalamiko ya upungufu wa chakula, lakini kubwa ni kwa vijana wetu kukimbilia Mjini na kukosa ajira. Sasa eneo hili kubwa ndilo tunaambiwa linaajiri Watanzania kama asilimia 80 na siamini kama itakuwa asilimia 80, inawezekana ikawa 82 mpaka 85 hasa kutokana na watu wengi ambao wamestaafu kazi na ajira nyingi zipo katika ajira binafsi pengine wengine baada ya kustaafu wamerudi Vijijini kuendeleza katika kujiajiri katika kazi za kilimo.

Kwa hiyo, kama hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri itafanyiwa kazi ya dhati kabisa nataka kusema kwamba malalamiko haya, mapungufu ambayo tunayo katika mwaka 2003 tuna uhakika kwamba mwaka 2004 na kuendelea Taifa letu litaweza kuondokana na matatizo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maeneo ambayo mimi yamenifanya nichangie hotuba hii na kwa kweli nataka nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwamba ni mchapa kazi sana. Kama atapata ushirikiano wetu sisi Bunge, wananchi na maeneo mengine ambayo yanashughulika na eneo hili, tuna uhakika kwamba anaweza akafanikisha lengo hili muhimu la Serikali yetu na wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nataka kwenda moja kwa moja kwenye ukurasa wa 24 ambao unazungumzia kilimo cha umwagiliaji maji mashambani. Hapa Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake amesema jumla ya hekta 8,995 ziliendelezwa kwa kilimo cha umwagiliaji maji kwenye mwaka wa 2001/02. Kwa hiyo, takwimu hii ambayo malengo ya Serikali yalikuwa ni hekta 191,900 na tukafikia 200,895 tukapata ongezeko la hekta hizi 8,995 na ndiyo maana nikasema kwamba yapo matumaini makubwa ya kuweza kufanikisha mpango huu kama tutasimamia vizuri kwenye masuala haya ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo kubwa la nchi yetu maji tuna maji mengi. Tukiangalia kuna baadhi ya Mikoa kuna maji yanapotea katika mitiririko mbalimbali na vile vile tunayo Maziwa makubwa sana. Kwa hiyo, malengo haya ambayo tumeyaweka katika kitabu hiki cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri tuyafanyie kazi siyo maneno tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa huo huo wa 26 Mheshimiwa Waziri amezungumza kwamba: "Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo na Chakula, kwa kushirikiana na Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Japan *(JICA),* imekamilisha maandalizi ya sehemu ya kwanza ya Mpango kamambe wa Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani." Nimenukuu hapo kwa sababu Shirika alilotaja ni la Japan na wenzetu ni wakweli sana na Mheshimiwa Waziri kutokana na juhudi zake alipokuwa Meya katika Jiji la Dar es Salaam na Japan ndiyo waliotu-*support* katika kutengeneza zile barabara, kama atafanya nao kazi vizuri katika eneo hili tunaweza tukafanikiwa vizuri na tukalibadilisha Taifa letu hili kwa mafanikio makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni matumaini yangu kwamba kwa sababu kigezo cha mwanzo kama kweli Japan watashiriki kutusaidia kujenga uchumi wa nchi yetu kwa kweli eneo kubwa tufanye kazi vijijini na mashambani kwa ajili ya kuunganisha wakulima wetu na kuwasaidia. Kwa kweli hapa nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na namtakia mafanikio na usimamizi mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa 26 huo huo, anasema: "Mpango huu umeonyesha kwamba kuna hekta milioni 2.3 zenye uwezekano mkubwa wa kuendelezwa high *development potential."* Kama hekta milioni 2.3 kutoka kule kwenye 200,000 tukazifanikisha hizi, mimi naamini kwa muda unavyokwenda tutafika mahali pazuri sana. Halafu amesema kwamba kuna hekta milioni 22.3 zenye uwezekano mdogo wa kuendelezwa *low development potential,* kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri tujitahidi na hizi milioni 22.3 zije ziwe katika uhakika kwenye hizi milioni 2.3.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri amesema kwa ujumla Taifa lina hekta milioni 29.4 zinazofaa kuendelezwa kwa kilimo cha umwagiliaji maji mashambani. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula na takwimu hii aliyotupa tunataka mwaka 2004 ionekana kwamba imeanza matunda. Sisi kuanzia leo tunachukua hii takwimu, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri mwenyewe na watendaji na Wizara yake na wananchi lazima tuweke nguvu za pamoja kuleta mabadiliko

ya uchumi. Haya mambo madogo madogo yanatokea sasa hivi kwamba ooh, kuna njaa, ni kwa sababu huu mfumo tulikuwa hatuna.

Kwa hiyo, kama tunamiliki hekta 29.4 tunaweza tukafika mbali katika Sekta ya Kilimo. Kwa hiyo, zinahitajika nguvu za pamoja Waheshimiwa Wabunge, Serikali na Mahakama, vyombo hivi vitatu viungane pamoja. Kwa sababu kuna maeneo mengine wananchi wanavunjika moyo tu kutokana na mashitaka madogo madogo wanakosa haki zao Mahakamani kwa ajili ya kugombania ardhi, kuharibiwa mazao yao. Kwa hiyo, tuunganishe nguvu za pamoja tuweze kuwasaidia wananchi wetu tufikie malengo haya kwa ajili ya faida ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile katika ukurasa wa 30 Mheshimiwa Waziri anazungumza kwamba Mradi wa Ushirikishi wa Maendeleo ya Kilimo na Uwezeshaji *(Participatory and Agricultural Development and Employment Project), project* hii kwa kweli ni muhimu. Kama tulivyosema kwamba inaajiri asilimia 80 ya Watanzania, lakini inawezekana ni zaidi ya asilimia 80 kutokana na sekta binafsi inavyofanya kazi, na sasa hivi sekta binafsi inaajiri wataalam kutoka nje, inawezekana asilimia 100 ya watu wetu, ile asilimia 20 hatuipati.

Kwa hiyo, hapa itufanyie kazi na wakijenga mazingira mazuri katika vijiji na mashambani itatupunguzia idadi kubwa ya vijana wetu kukimbilia mijini, kwa sababu kutakuwa na uzalishaji wa kutosha, wananchi watakuwa wanapata maslahi yao na watakuwa wanapata mitaji mizuri hapa kwa kweli Mheshimiwa Waziri tunataka utufanyie kazi. Ndicho kilichonisababisha mimi kuunga mkono hoja yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikimnukuu tena Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake ukurasa wa 30 anasema: “Mheshimiwa Spika, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa Mradi Shirikishi wa Maendeleo ya Kilimo na Uwezeshaji umeanza kutekelezwa rasmi kuanzia mwezi Mei, 2003.” Umeanza tunataka tuone matokeo yake. Hatutaki hesabu ya miezi miwili iliyopita, kwa sababu umeanza mwezi Mei, tumemaliza mwezi Juni na sasa hivi tuko mwezi Julai, lakini tunataka mwaka 2004 atupe matokeo sahihi ili kuondoa matatizo kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri amezungumza mradi unalenga kuongeza uzalishaji na tija ya kilimo na hivyo kupunguza umaskini, hapa ndiyo lengo la Taifa letu. Lengo kubwa la Taifa letu ni kupambana na umaskini kwa wananchi wake. Kwa hiyo, kama sehemu kubwa ya asilimia 80 au na zaidi kama Wizara ya Kilimo na Chakula itaifanyia kazi tunaweza tukayafikia yale malengo ambayo tumeyakusudia.

Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, kitabu chake cha hotuba kwa kweli ni kizuri sana, tutakuja kumsuta hapa mwaka 2004, kwa hiyo, haya ndiyo masisitizo yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa huo wa 30 katika kitabu cha hotuba yake amesema: “Mradi huu utatekelezwa katika Wilaya 28 za Tanzania Bara na Tanzania Visiwani.” Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri. Zanzibar ni sehemu ya Tanzania na kama Mradi huu wa umwagiliaji sisi Zanzibar tuna maji mengi sana kule, kama tutachimba visima vya kutosha kwa kweli tuna maji mengi sana.

Kwa hiyo, tusije kusutana hapa mwaka 2004, tunataka Mradi huu uende sambamba baina ya Tanzania Bara na Tanzania Visiwani ili kuwaondoa wananchi wetu katika matatizo makubwa, ambapo kwa kweli wanaweza wakapata maslahi mazuri na maisha mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa 34 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri kuhusu Zana za kilimo. Tuko karne ya 21 na kwa kweli wakulima wetu wengi sana wanatumia zana duni kama katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ilivyobainisha. Kwa hiyo, tuweke msukumo wa haraka sana ili tuweze kwenda sambamba na karne hii ili wananchi wetu waweze kuwezeshwa kuwatoa katika zana duni ambazo wamezizoea za majembe yale ya kutumia mikono na twende kwenye teknolojia ya kisasa ili tuweze kufanikisha katika uzalishaji mali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa 35 kwenye kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri, amezungumzia kuhusu matumizi ya ardhi bora. Sehemu kubwa ya nchi yetu inakabiliwa na

mmomonyoko wa udongo unaosababishwa na kuondolewa kwa uoto wa asili na kilimo kisichohifadhi ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikimnukuu Mheshimiwa Edson Halinga, jana alilalamika kwamba Jimboni kwetu wataalam waliokuwepo zaidi siyo wale wa kilimo ni wa mifugo. Kwa hiyo, malalamiko kama yale tunaiomba Wizara ikafanye utafiti kama ni kweli yaweze kufanyiwa mabadiliko na kuweza kupeleka wataalam husika. Kwa sababu kama leo tutapeleka wataalam wa kilimo wanaweza kwenda na elimu ambapo watajua hali ya ardhi yetu iko vipi na tukaepukana na mmomonyoko huu wa ardhi ili tupate ardhi yenye rutuba na kupata faida. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri malalamiko haya na maelekezo ya Waheshimiwa Wabunge tunaomba uyachukulie kwa uwazi na uyafanyie kazi ili kuleta faida kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa 43 kuhusu Mafunzo kwa Wataalam na Wakulima. Nikimnukuu Mheshimiwa Waziri amesema kwamba: "Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2002/2003, Wizara iliendelea kutoa mafunzo na kujenga uwezo wa Taasisi na watalaam wake kwa kutoa mafunzo yenye lengo la kuwawezesha wataalam na wakulima kuendesha kilimo cha biashara." Mheshimiwa Waziri nakupongeza sana. Hapa wananchi wakiweza kumiliki kilimo cha biashara kwa kweli tutakuwa tumewapatia ajira iliyokuwa ni muhimu sana kwa ajili yao na kwa ajili ya Taifa letu. Kwa hiyo, suala hili liende sambamba na uwezeshwaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu nilipoingia Bungeni mwaka 2000 kuna malalamiko madogo madogo, Serikali inatoa baadhi ya mikopo kwa wakulima. Lakini mara nyingi sana mikopo ile inafikia pengine kwa Waheshimiwa Wabunge na kwa watendaji wengine wa Serikali ambao wana uwezo wa kuweza kukopa katika maeneo mengine, tunawaacha wananchi wa vijijini ambao ni maskini.

Kwa hiyo, hili nalo tuliangalie sana, ile mikopo ya Serikali iwe inawafikia wakulima. Kuna wakulima fulani wanatakiwa wapatie mikopo kwa ajili ya kuimarisha kilimo, hiyo mikopo isikimbiliwe na Waheshimiwa Wabunge na watendaji wengine wa Serikali ambao wana uwezo wa kuweza kukopa katika maeneo mengine. Tuwawezeshe wananchi ili waweze kuendesha kilimo kwa faida yao na maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hili ni muhimu sana na Mheshimiwa Waziri tunamtegemea ili kujenga mfumo ambao utaweza kutoa ajira na kuleta mazao ya biashara katika nchi yetu, na vilevile Mheshimiwa Waziri uweze kushirikiana na Wizara ya Ushirika na Masoko na Serikali Kuu kwa jumla kuweza kutafuta masoko ya uhakika ili kusaidia uzalishaji huu utapozalishwa wananchi wajue wapi wanauza mazao yao. Lakini kama tutawaacha tu wananchi wanazalisha mazao ya kutosha lakini hawajui wapi wayauze tutakuwa tunafanya nini hatutafika mahali tulipokusudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo haya ambayo nimeyanukuu nataka nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwamba yamenisababisha niweze kuchangia hoja hii na nimtakie mafanikio, kwa kweli kama Taifa tunamtegemea. Nchi hii tuna eneo kubwa ambalo lina maji mengi sana na inawezekana kutokana na mifumo ya huko nyuma ilitufikisha hapa, kwa hiyo kwa kuwa tunaanza naamini tutafika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naomba niongee moja, ningeomba wataalam walioko katika Wizara ya Kilimo na Chakula wawe ni wataalam. Nalizungumza hili kwa sababu juzi nilishtuka sana siku ya Ijumaa wakati naenda Dar es Salaam, ilibidi wanipe elimu katika basi, kuna kijana mmoja mpaka nilimuuliza una umri wa miaka ngapi, akasema nilizaliwa mwaka 1967, nikamwambia basi nyamaza na Mheshimiwa Issa Mohammed Suleiman, ni shahidi huyu hapa. Yule kijana ni mtumishi wa Serikali, lakini kumbe hafahamu hata Dira hii ya 2020-2025 na yuko kwenye Wizara nyeti.

Mimi niliona atanisumbua na nashukuru baadhi ya wasafiri katika lile basi, waliniunga mkono na walimshangaa yule kijana, ni mfanyakazi katika Serikali lakini hafahamu ile Dira mwisho wake inafikia wapi. Lakini mimi nikawambia wewe ufahamu kama nchi hii baada ya kujikomboa tulilikomboa Bara la Afrika.

Je, hukumbuki kama kuanzia mwaka 2000 tumeanza kuinua uchumi wa nchi hii, hajui. Umezaliwa mwaka gani, ananiambia nimezaliwa mwaka 1967, nikamwambia basi wewe unyamaze, nililazima kusema hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wataalam wetu ni lazima wawe wanafahamu hali halisi ya mwenendo na mfumo wa mzima wa Serikali kuhusu masuala ya uchumi. Msituweke tu vijana ambao hawafahamu kitu. Amemaliza Chuo Kikuu lakini mfumo mzima wa Serikali haufahamu na Mheshimiwa Issa Mohammed Suleimani ni shahidi huyu hapa.

Nashukuru waliokuwemo kwenye basi nao waliniunga mkono. Nililazima kusema kwa muda mrefu sana karibu nusu saa nzima natoa elimu ile. Nikamwambia nchi haikuwa hivyo kijana, lakini wewe unakumbuka. Kwa hiyo, tunapowaandaa wataalam wetu lazima wafahamu na sera zetu za nchi, ili kuleta maendeleo ya kweli lakini vinginevyo tutakuwa tunagongana hatufiki mahali.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nataka nirudie kwamba naunga mkono hotuba hii asilimia mia moja. Nimtakie mafanikio Mheshimiwa Waziri katika kutekeleza majukumu yake. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia katika hotuba hii ya Waziri wa Kilimo na Chakula. Kwa hiyo, naomba nitumie nafasi hii ya awali kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri ambayo kwa kweli imeweka mambo yote ambayo yanahitajika. Vile vile nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na wataalam wote waliomsaidia katika kuandaa hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mengi yamesemwa kwa hiyo, nitajitahidi kukwepa ili nisirudie sana yale yaliyokwishakusemwa au nitatoa tu mifano michache katika kuboresha hoja hii katika maeneo fulani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri ametwambia katika hotuba yake kwamba Sekta ya Kilimo imeanza kuonyesha dalili ya kukua na akatoa mifano, mwaka 1999 ilikua kwa asilimia 4.1, mwaka 2000 kwa asilimia 3.4, mwaka 2001 kwa asilimia 5.5 na mwaka 2002 ilikua kwa asilimia 5.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo lilikuwa ni kufikia asilimia 6 na vile vile ametueleza kwamba haikuweza kufikiwa kwa sababu ya bei ya mazao hasa ya biashara kama kahawa, pamba pamoja na chai kwa sababu yalishuka bei. Vile vile ametueleza kwamba ili uchumi ukue, unaonekane kwamba unakua unatakiwa ufike kwenye asilimia 10 ili tuweze kupambana vizuri na umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nataka changamoto ni kwamba tutafika vipi kwenye hiyo asilimia 10. Je, tunao mpango wa kutufikisha kwenye asilimia 10, mpango ambao umeandaliwa vizuri na umefikiriwa vizuri. Tunao mpango ambao kwa kweli unatuweka mahali ambapo tunakuwa na *strategic thinking* na *long term planning,* tunao mpango wa aina hii kweli! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi watu wanajiuliza tumejiwekea kwenye Dira ya Taifa ya 2020-2025 kwamba *per capital income* ya mwananchi tuipandishe kutoka dola 210 hadi 3,420. Tunaulizwa na wananchi hivi tunafikaje hapo na ili kufika hapo ni lazima tuwe na mpango unaonyesha mwaka hadi mwaka kwamba tunakwenda namna gani. Jambo hili ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya kilimo inakabiliwa na matatizo mengi sana. Kwa hiyo, inahitaji sana kwa kweli kuwekewa mpango. Kwa mfano, matatizo ya ukame, mlipuko wa wadudu, magonjwa, mafuriko, matumizi ya teknolojia na mambo haya ya bei ya kupanda na kushuka. Kwa hiyo, sekta hii inahitaji mikakati ya mpango ambao kwa kweli utatuwezesha kuhakikisha kwamba tunafikia hiyo asilimia 10 ambayo kwa kweli Mheshmiwa Waziri ameitaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini zipo kauli ambazo mara nyingi Serikali inatoa na inaonyesha kwamba kwa kweli pengine basi hatuna mpango sawasawa au hatufikiri vizuri katika mpango wetu. Kwa mfano, mara nyingi utasikia Serikali ikitokea matatizo kidogo ya njaa na nini inahimiza limeni maeneo yote yanayowezekana, kilimo cha kufa na kupona, tumieni maji ya mvua, viongozi fuatilieni sana, kila Mkoa andaa mpango wa maalum, kamati za njaa zikae, hivi Kamati za shibe ziko wapi! Ni wakati wa njaa tu tunakuwa na kamati za njaa, wakati wa shibe hatuna kamati. Sasa kila mtu aweke akiba, Serikali haina mpango wa kuwaletea chakula, limeni mazao yanayostahimili ukame, yanayokomaa haraka, uuza mifugo na viongozi wawajibike kuanzia sasa. *(Makofi)*

Mimi nataka kusema haya maneno ya kuanzia sasa ambayo Mheshimiwa Waziri ameyatumia katika ukurasa wa 13 na naomba niyanukuu amesema hivi: "Kuanzia sasa, viongozi watakaozembea katika kuwahimiza wananchi walime mazao yanayostawi katika mazingira yao, watawajibishwa kwa kosa la kuhatarisha maisha ya wananchi wa maeneo yao."

Je, Mheshimiwa Waziri ana mpango wa kuwawajibisha hawa na uko wapi? Au ni maneno tu ambayo yatakuwa yameandikwa hapa. Tunataka mpango basi wa kuwawajibisha, ili tukija hapa mwakani atueleze hatutaki tena aeleze hayo. Tutataka aeleze amewawajibisha viongozi wangapi na lazima uwe na mpango.

Kama hakuna mpango tukubaliane kwamba ni katika zile zile taratibu za kawaida, lakini basi tuone kwamba wanawajibishwa taarifa tuipate. Ni lazima tuhame kutoka kwenye maneno twende kwenye vitendo. Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani hilo Mheshimiwa Waziri atalizingatia ili mwakani tuweze kujua hili, vinginevyo nadhani Mheshimiwa Charles Keenja, hajaonja kushikiwa shilingi, inawezekana akafikia huko. Kwa sababu *statement* hii ni kubwa, na tunataka kuona kabisa kwamba kweli viongozi wanawajibishwa katika hili, ili lisiwe maneno tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumze jambo la pili, ambalo ni Mpango kamambe wa kilimo cha umwagiliaji maji mashambani. Mheshimiwa Mbunge aliyemaliza sasa hivi amezungumzia habari ya hekta milioni 29. 4 zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji maji mashambani. Kwa kweli kama utapiga mahesabu kwa hekta karibu milioni 29.4 unao uwezekano kama kila heka kwa mfano ya nafaka kama mahindi ukapata gunia kama 20, unaweza ukapata karibu tani milioni 145 kwa hesabu zangu hizi za haraka haraka. Sasa tunao mpango kweli hasa wa kutumia hizi hekta milioni 29.4, na tunao mkakati kabisa wa kutekeleza au ni mikakati hii ya muda mfupi ambayo ipo hapa, sijui kama itatufikisha huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka basi nigusie katika huo mpango wake mzima ambao ni Mpango shirikishi wa kilimo cha umwagiliaji maji mashambani. Huu ni mradi ambao upo chini ya *PEDP,* nafahamu Mradi huu uko kwenye Mikoa 6 na Wilaya 12 na mimi kama mwakilishi wa wakulima nimepata nafasi ya kupita na kuona mradi huu katika maeneo haya ambao kwa kweli unajaribu kutaka kuendeleza kutufikisha kwenye hekta 7,200 mwisho wa mpango huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika kupita kwenye maeneo haya mradi huu. Nimegundua mambo machache na haya ndiyo ambayo naona kwamba ni vizuri kwa kweli Mheshimiwa Waziri ayachukue na kuyafanyia kazi. Moja nimegundua kwamba wadau wote wa mradi huu au wadau wengi wao katika maeneo hayo hawafahamu kama fedha zinazotolewa asilimia kubwa ni mkopo ambao Watanzania wote tutaulipa.

Kwa hiyo, tuwe wazi kwa wananchi na wajue kwamba fedha hizi zinazopita kwenye miradi hii ni mkopo na mkopo ukipelekwa kwenye Wilaya fulani ijulikane kabisa kwamba watakaolipa ni Watanzania wote. Katika Mradi huu asilimia 80 inatolewa na *IFAD,* Serikali ya Ireland inatoa kama *grant* ya asilimia 4 na *WFP* inatoa vile vile *grant* kwa njia ya chakula kama asilimia 6 na Serikali ya Tanzania inachangia karibu asilimia 9 na wadau wamepewa kuchangia asilimia 1. Sasa ni vizuri maana wananchi au wadau katika haya maeneo wengi wao wanadhani ule ni msaada tu.

Kwa hiyo, katika mpango huu kabambe wa umwagiliaji maji ni vyema wananchi wafahamu kwamba kwa kweli fedha tunazopata ni mkopo, na kwa hiyo watu kwenye maeneo hayo wanayo dhamana kwa niaba ya Watanzania wote kuhakikisha kwamba mkopo unatumika vizuri na wao wanashirikishwa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango huu ukifeli maana yake kwa kweli itakuwa mzigo mkubwa sana kwa Watanzania wengine. Kwa hiyo, nataka nimshauri Mheshimiwa Waziri kwamba viongozi katika ngazi zote nao wafahamu hili kuanzia watendaji wa vijiji, watendaji wa kata na watendaji wa Tarafa wajue mradi hata kama una walengwa ambao wanautekeleza, lakini mradi huu kwa sehemu kubwa unapaswa kusimamiwa na Serikali kwa hiyo ni mradi wa Serikali. Kwa sababu unahusu mkopo kwa ajili ya Watanzania wote. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili, ambalo nimeliona kwenye zile *schemes* za mpunga katika Mikoa hii sita au katika Wilaya 12. Nimeona kwamba *schemes* nyingi zimekamilisha taratibu za kuomba hati miliki ya maji. Lakini hizi hati miliki za maji zimekwama huko Wizarani. Sasa Wizara inayohusika kama Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo au Wizara gani basi tujue kwamba kwa kweli hizi hati miliki ni muhimu sana kwa ajili ya kumiliki maji katika maeneo hayo ya *schemes.* Kwa hiyo, ni vizuri sana kwa kweli lifuatiliwe jambo hili kwa makini sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu ni suala la ununuzi wa mitambo pamoja na magari na vifaa, wafadhili wanatushangaa. Kwa kweli ukiangalia katika Mradi huu unakuta magari kwa mfano, nimeona tumetumia karibu mwaka mmoja na nusu tukihangaika na taratibu za kununua gari na wakati mwingine tunasingizia hii sheria mpya ya *Procurement Act,* Sheria ile ilitungwa kwa ajili ya kuziba mianya mimi ninavyofahamu, sasa tatizo pengine si Sheria, tatizo pengine ni watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku hizi si gari unaenda *Toyota* pale zipo unanunua tu, sasa taratibu zinachukua muda mrefu karibu mwaka moja na nusu Mradi unacheleweshwa katika hali hii. Naomba Mheshimiwa Waziri alichukulie hili kwa sababu hata wafadhili nadhani wa Mradi huo wanashangaa wakati fedha wameishatoa. Lakini vifaa havipatikani kwa sababu ya mlolongo mrefu ambao kwa kweli mara nyingine tunasingizia tu sheria ya *Procurement Act.* Lakini sidhani kama hilo, mimi nadhani tatizo ni watu wanaohusika na taratibu hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la nne, ni suala la matumizi ya mkopo wenyewe. Katika matumizi ya mkopo huu wenyewe tunajenga vibanio vya maji na *structures* kwa ajili ya maeneo ya umwagiliaji maji. Lakini liko sharti la kutumia Wakandarasi ambao kwa kweli wengi wana gharama kubwa sana.

Sasa kila inapowezekana mimi nadhani ni vizuri *negotiations* nazo zikafanyika ili kwa kweli kuona na wale wakandarasi wa ndani ambao wanaweza wakafanya kazi nzuri nao wanaweza wakapewa kazi hiyo. Mbona mimi nimepita kwenye ofisi ya Waziri nataka nimpongeze hapa nimeona akijenga ofisi yake hapa Dodoma kwa kutumia wataalam wake, nimepita pale mimi bila ya yeye kujua. Lakini nimeona ofisi inajengwa vizuri na kwa kutumia kabisa wataalam na Wahandisi walioko katika Wizara yake. Ni jambo nzuri sana hili. Sasa na kwenye hii miradi tuangalie vile vile gharama kwa sababu huu ni mkopo lazima tuutumie vizuri mkopo huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naomba nishukuru kwamba kuna vijiji vyangu vitatu, ziko *schemes* tatu, kuna *schemes* ya Matufa na Maimairo, Gijameda na Kashi ambazo kwa kweli zipo katika mpango huu na namuahidi Mheshimiwa Waziri nitafuatilia vizuri sana na tutashirikiana naye katika kuhakikisha kwamba Mradi huu unafanikiwa vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme moja tu kuhusu zao la pamba pamoja na zao la mbaazi, Babati. Katika maeneo hayo kwa kweli Babati kuna eneo ambalo linafaa sana kwa pamba ambapo ni eneo nzuri sana hasa katika Tarafa ya Mbungwe. Lakini Bodi ya pamba haijatilia mkazo katika jambo hili.

Sasa sijui tunapanuaje kilimo kama hatuwezi kuona maeneo mapya yanayofaa kwa ajili ya uzalishaji wa mazao muhimu kama ya biashara hatuwezi kuyashughulikia sana. Zao la mbaazi ni zao linalohitaji sana kutafutiwa soko kwa sababu kwa kweli lina soko kubwa kwenye nchi ya India kule na katika maeneo mengine. Sasa katika mpango huu mzima wa kuimarisha kilimo tunahitaji kwa kweli kuimarisha eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nakubaliana na wenzangu wote waliosema kuhusu Mfuko wa Pembejeo. Mimi nakubali utaratibu sasa umefungua kidogo maana mambo yanaanzia kwenye Halmashauri. Lakini je, tunatumia muda gani toka mtu aombe kupitia Halmashauri na kwenye Vikao na Mkurugenzi wa Mfuko naye ana vikao halafu uende *Exim Bank* na nini. Hivi ni muda gani, miezi mingapi na gharama zote hizi za mtu kufuatilia mambo yote haya. Tujue kwamba tunatumia muda gani. Tutumie muda mfupi iwezekanavyo kama ni mkopo basi watu wapewe ili kwa kweli shughuli za kilimo au za kufikisha pembejeo kwa wananchi ziweze kwa kweli kufika kwa haraka, tusitumie muda mrefu katika vikao. Mkurugenzi sijui atakaa lini na Halmashauri ya Wilaya, mpaka Mkurugenzi wa Mfuko, halafu kule *Bank* utaratibu mzima unatumia pengine muda mrefu sana.

Tunaomba muda huu ufupishwe sana na mimi nawahakikisheni kwamba Babati kule sisi tunatumia zaidi matrekta. Hapa leo asubuhi kulikuwa na swali, kuna Wilaya ina trekta mbili, kule kwangu kijiji kimoja cha juu sana ambacho ndicho kina trekta nyingi ni matreka 51 kijiji kimoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. PAUL E. NTWINA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia katika hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula. Lakini leo nitakwenda moja kwa moja. Naanza na ukurasa wa 67 ambao unasema: "Mheshimiwa Spika, mwaka 1999 Serikali ilizuia kilimo cha pamba katika Mikoa ya Kusini ili kukidhi kuenea kwa funza mwekundu wa pamba katika maeneo mengine nchini. Ili kutafakari zaidi suala hili, tarehe 7 Juni, 2003 Wizara iliandaa warsha iliyohudhuriwa na Waheshimiwa Wabunge wanaotoka katika maeneo yanayozalisha pamba na wataalam wa zao la pamba. Warsha ilipendekeza kuendelea kuwepo kwa karantini ya funza mwekundu nchini. Aidha, wajumbe wa warsha hiyo kwa pamoja walitoa changamoto kwa watafiti kuendelea kutafuta mbinu mbadala ya kumdhibiti mdudu huyo. Wizara itashirikiana na Taasisi za Utafiti za Kimataifa kutafuta mbinu za kumdhibiti mdudu huyo." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulialikwa kwenye warsha hiyo kwa barua Kumb. *IB/19/133/1* ya tarehe 26 Mei, 2003 inayotoka Wizara ya Kilimo na Chakula, Idara ya Utawala na ilikuwa imesainiwa na Ndugu R. S. Kipande, Katibu Mkuu. Nayo kidogo tu ningeweza kuinukuu inasema kuwa: "Kuwepo kwa mjadala wa siku nyingi nje na ndani ya Bunge la Tanzania kuhusu kuzuiwa kwa kilimo cha pamba katika Mikoa ya Kusini mwa Tanzania. Inafahamika kwamba kilimo cha zao hili katika Mikoa ya Mtwara, Lindi, Ruvuma, Mbeya na sehemu za Mikoa ya Rukwa na Iringa kimezuiwa kisheria kutokana na kuwepo katika Mikoa hiyo mdudu hatari wa pamba maarufu kwa jina la funza mwekundu. Wanasema tunayofuraha kukufahamisha kwamba Wizara ya Kilimo na Chakula imeandaa warsha ya siku moja ambayo pamoja na mambo mengine itazingatia suala nzima la kilimo cha pamba katika Mikoa hiyo."

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi baada ya kupata barua hii nilijua sasa Waziri wa Kilimo na Chakula, atakwenda kutuambia haswa mambo ambayo yanatufanya tuzuiwe kulima pamba katika mikoa ile. Nilitegemea kuwa kungekuwepo na Wabunge kutoka Mtwara, Lindi, Ruvuma, Mbeya, Rukwa na Iringa, lakini kinyume chake ni kwamba tulikuwa Wabunge wanne, wawili wa Bodi, mimi na Mheshimiwa Njelu Kasaka.

Sasa maamuzi haya ambayo yameandikwa kwenye kitabu hiki sijui tuna-*represent* na Wabunge wenzetu wa mikoa mingine. Lakini ninachotaka kusema ni kwamba bado msukumo mkubwa haujafanyika katika kutatua tatizo hili la wakulima la kulima pamba katika mikoa ile. Zipo sababu za msingi kabisa ambazo tumekuwa tukizieleza katika mikutano hii, lakini Serikali haitaki kusikia. Kitu kikubwa zaidi ni kwamba hali ya wananchi wa maeneo ambayo walikuwa wanalima hususan maeneo yangu ya jimbo la Songwe ni kwamba wananchi wamekuwa ni maskini mno na nilitarajia kuwa pengine kwa sababu aliahidi mwaka jana, suala hili lingeweza kutatuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu mwaka 2002 tumeambiwa hapa kama walivyozungumza wenzangu kuwa Wabunge wa maeneo haya watahusishwa na wataalamu waweze kutembelea nchi zile ambazo zinapakana na nchi yetu ili waweze kuangalia zao hili linalimwaje. Inashangaza kuona kuwa nchi nyingi zilikuwa zina mdudu huyu na Serikali inajua lakini wenzetu wanalima pamba. Hata wale ambao bado hawajajua jinsi gani ya ku-*tackle* tatizo la mdudu huyu wanalima bado katika hali ya kama tunavyolima sisi na bado wanapata zao hili na wanazidi hata zile sababu ambazo tunapewa za kimsingi hapa. Ni kweli huyu mdudu kama kweli angekuwepo kule Kusini huko Msumbiji na maeneo mengine angeshafika maeneo ya juu ambayo tunayasema pamoja na sababu nyingi ambazo tunaambiwa kuwa pengine hawezi kuvuka mito na vigezo vingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili kwa kweli halileti sura nzuri katika uwakilishi wetu kwa wananchi tunakotoka. Ni suala ambalo naiomba sana Serikali ingejaribu kuliangalia upya kwa sababu katika ya 21 unazuia mdudu inakuwa kama Ukimwi hata Ukimwi, watu hawauogopi. Halafu tunazungumzia *AGOA,* tunazungumza mambo mengi na tunajirudisha nyuma katika maeneo mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pale kwenye kikao tulishauri na tukawahoji kwa mfano tuliuliza huyu mdudu jinsi alivyopatikana katika maeneo yetu alionekana na mkulima gani, kiongozi gani alimwona. Ni majibu ambayo yanaleta utata mpaka leo kwa wananchi wetu. Ukiwauliza viongozi watakujibu tu haraka haraka alionekana akaenda Wilayani akaenda Mkoani na wakawadanganya hata hawa viongozi wa mkoa wengine kutokujua kweli alionekana huyu mdudu au vipi.

Sasa haya mambo ni ya utaalamu kama yanapatikana kimsingi kule kijijini inapaswa uangalie na uwaeleze wanaohusika kuwa hapa kuna tatizo hili na hili. Sasa wananchi wanahoji kuna pamba pori kule twendeni sasa hivi tukaangalie kama huyo mdudu yupo, kama pambapori yule tutamkuta na yule mdudu itadhihirisha kuwa kweli mlimkuta yule mdudu kule.

Lingine hata gazeti lile gazeti lililosimamisha wananchi wasilime kule hata siku ile tumelihoji pale lilikuwa halina namba ya gazeti. Sasa nilitarajia tu kwa kuwa walijua kuwa tulikuwepo pale na tulihoji tungeweza kuletewa lile gazeti namba yake kuwa ilikuwa namba hii na ndiyo lililosimamisha. Halafu hili nililolisema la Wabunge tuelimisheni Wabunge wote kwa sababu lina maeneo yote haya kutoka Lindi na kadhalika, lakini kwa Mkoa wa Mbeya ni tatizo kubwa. Sio tatizo kubwa katika jimbo la Songwe tu na vijiji vyake. Lakini ukienda hata mkoani vitu vimesimama, kuna viwanda vimesimama pale ajira hakuna. Watu wetu wanapata matatizo makubwa.

Katika jimbo la Songwe watu wanashindwa kusomesha watoto, wanashindwa kujenga nyumba bora na ukiangalia hali ilivyokuwa wakati wa zao hili la pamba wakati lipo maendeleo yalikuwa yanakwenda kasi sana, wananchi walikuwa wanamudu kusomesha watoto na kujenga nyumba nzuri na maisha kwa ujumla yalikuwa ni bora. Lakini sasa baada ya kuondoka hilo hakuna zao mbadala tumebabaishwa kwa kuletewa ufuta, ambao ufuta kule jimboni kwangu tumelima miaka mingi ya nyuma nao una magonjwa yake. Halafu sijui labda kwa kuwa hotuba za mwaka zimesema kuwa tutafute zao mbadala. Hivi katika maeneo kweli Wizara haijui pamba inastawi vizuri zaidi kwa mvua ile na *climate* ile ya kule ambao ni zao ambalo lilitakiwa wananchi waweze kupata maslahi yake. Wizara inajua, mvua ya kule sio kubwa sana ambayo inaweza kukidhi mazao mengine. Tunapata mahindi na ndio zao tunaona siku hizi ndiyo kidogo linatuletea fedha kidogo katika kuboresha maisha ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninalotaka kusema ni kwamba ebu Wizara ikae na sisi tuangalie upya hivi watafiti wetu hawa hawa ambao siku hiyo walikuwa wengi kweli, maana sisi tulikuwa wanne wenyewe walikuwa zaidi ya 20 wanashindwaje kutafiti huyu mdudu na kuweza kuangalia jibu lake linakuwaje na kwa nini kuwe na tafiti basi mngevunja hizo tafiti zote tujue moja. Kwa sababu kama tunashindwa mdudu ambaye nimesema kuna magonjwa ambayo yametafutiwa na yameweza kupata ufumbuzi. Hata tunaambiwa siko *sure* kuwa ni kweli. Tunaambiwa nchi jirani kuna *genetic seeds* ambazo zinalimwa. Kuna mbegu nyingine ambayo zimetengenezwa kwa ubora wake ambayo mdudu yule akila hawezi kudhuru lile zao, sasa kwa nini haya Mheshimiwa Waziri tutakuja kila mwaka hapa tunaelezana juu ya hili.

Mimi naomba Serikali ingekaa kwa kweli Waziri kila siku tutakufuata fuata kwa jambo hili la pamba halafu inakuwa sio eneo zuri ambalo sisi tungependa kulijadili mara kwa mara. Nasisitiza mimi tuweko Wabunge wote wa eneo la Kusini sio mmoja mmoja ili tuweze kulijadili hata tuusishe na wananchi wetu ambao ni wanaohusika kwa wadau kwa asilimia kubwa zaidi kuliko sisi kama wawakilishi, mnaona wawakilishi wawili ambao labda tunakuleteeni kero kila siku kulizungumza hapa halafu hata posho sikupata haikuwepo.

Mimi naomba kwa kweli hili suala la pamba ungeliangalia upya. Kwa kweli limeharibu hotuba yako katika maelezo haya ambayo umeeleza kuwa tulikubaliana. Hatuwezi kukubaliana na sisi wanne kwa watendaji ishirini. *Obvious* watendaji watatuzidi nguvu na wataandika wanachotaka kama walivyokuandikia kwenye kitabu katika hotuba yako. Natarajia mwaka ujao au tutakapokutana katika majibu yako utatujibu mambo ambayo yanaelekeweka juu ya suala hili la pamba na hasa la mdudu huyu kama kweli hawezikani basi twambieni moja kwa moja kuwa hiyo haiwezekani kuliko kutuita kwenye semina na kujadiliana vitu ambavyo tunafikiri havina mwisho wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia hoja hii ya Waziri wa Kilimo na Chakula. Sisi tunaozungumza mara ya mwisho mwisho hapa mambo mengi yatakuwa yameshazungumzwa na nitajaribu sana nisirudie lakini najaribu kuangalia mambo ya msingi ambayo ninafikiri kuna haja ya kushauri ili tuweze kuelewa kwamba tunafanya nini. Nianze kwanza kwa sababu baadaye si unajua nitapata matatizo, kwa hiyo bora nianze kutamka kabisa mimi hoja hii naiunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitaka kusoma hii *document* halafu umemaliza ukasema kwamba itakuwa na matatizo hatutakuelewa. Labda kama tungekuwa na utaratibu wa kusema kwamba twende tukatekeleze halafu urudi ndiyo tupitishe hapo ndiyo ungembana. Nchi yetu ya Tanzania hii ni nchi ambayo kwa programu haina matatizo kabisa. Ukisema Utawala Bora atakuletea Mheshimiwa Wilson Masilingi, hapa programu nzuri, safi na *first class.* Ukisema habari ya misitu, barabara wewe utapata mipango ya kina Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, watakuja hapa watakupa mipango *first class.* Hupati matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nenda kwa Waziri Mkuu, kwa Mheshimiwa William Lukuvi, pale atakuambia hapa mafuriko yametokea, ukame utaratibu huu safi, hupati matatizo. Kwa hiyo, *problem* yetu ni *implementation* yake.

Mimi nimewahi kukaa na Warundi walikuwa wanasema hivi wewe jambo lolote hata kama ni simu, maji, bahari, *name it* shule, nenda Tanzania utaupata mpango mzuri wewe katekeleze kule *first class.* Tatizo letu sisi liko kwenye utekelezaji, hakuna jipya ambalo limesemwa hapa ambalo halikuwahi kusemwa katika nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo letu liko kwenye mkakati. Unasema kilimo unaweza ukakigawanya mara mbili, unaweza ukasema kilimo kikubwa kile cha akina *Lord Onasis* ambacho ni *mechanised agriculture* ukakiweka pembeni hapa. Ukasema mimi hawa nitawapelekea *combine harvesters,* nitawapelekea matrekta ni kilimo kikubwa, mtaji na vingine utapeleka pale. Kilimo kingine unachokizungumza ni kilimo kidogo kidogo cha wakulima wadogo wadogo ndio tunawaita *peasants.*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nchi hii ukisoma programu zetu zote tunazungumzia 87% ya wananchi wa Tanzania ndio wakulima wadogo wadogo. Uka-t*race historically background* yake na ukawachukua akina Frederick Engeles, yule alikuwa sio lofa alikuwa tajiri kwa maana yake watu ukitaja majina haya wanaogopa wanafikiri unataja majina gani. Yule ali-*characterise,* watu wengine wanayo ile ya kutoka kwenye ujima kuja kwenye utumwa, kuja kwenye ukabaila kwenda mpaka kwenye ubepari mpaka kwenye ujamaa. Ile *characterisation* watu wanafikiri ni akina Max, sio Max. Max alizungumzia zile za *mode of production. Germanic mode of production model of production* hizo ndizo *Asiatic* alizozungumzia. Aliyeweka ile *characterisation* ya kutoka kwenye ujima mpaka uko juu alikuwa ni Frederick Engels.

Engels alikuwa ana mawazo ya kijamaa ni tajiri mkubwa. Lofa pale alikuwa ni Max. Lakini anakwambia mkulima mdogo mdogo ame-*exist* katika *epoc* zote hizo mpaka tano. Na ndiyo maana nakubaliana na ile ya Mheshimiwa Felix Mrema, alinifurahisha sana aliposema wakati wa ukame wamo, wamo. Mtumwa ameondoka kwa sababu yeye amepata matatizo hayo na *revolution* imekuja pale ameondoka. Nokoa ameondoka. Anaye *exist* ni mkulima mdogo mdogo. Kwa nini ana *exist,* ana *exist* kwa sababu kuu mbili tatu. Moja yeye mwenyewe ni mmilikaji wa ardhi kwa vile anamiliki ardhi ni *very conservative,* ukigusa habari ya *revolution* anaogopa kwamba hii ardhi itakwenda na mimi nitakosa.

Pili anajilimia chakula chake yeye mwenyewe na haya maneno nataka niyaelekeze kwa Waziri wa Kilimo na niyaelekeze pia kwa Waziri wa Fedha Mzee Basil Mramba.Unapompa mkulima mdogo mdogo unataka kumsaidia ukamwambia kwamba alime kilimo achague mazao mawili huyu mkulima mdogo modogo haelewi kwa sababu analo tatizo la mtaji. Yeye anachofanya anafanya *probability* anajaribu kubashiri tu kwamba ni mahali gani atapata na ni mahali gani atakosa na ndiyo maana ukienda mahali kama Kilimanjaro ana-*spread over* mtaji wake mdogo katika mazao mbalimbali ni kama mtu anayecheza bahati nasibu.

Kwa hiyo, ule mtaji anaugawanya anaupeleka anau-*spread over* katika maeneo mbalimbali, akikosa maharage apate muhogo, akikosa muhogo apate mahindi na kadhalika. Ukim-*convince* ukamwambia nenda kwenye mazao mawili anaogopa. Kwa sababu hana hakika na hali ya hewa itakavyokwenda hana hakika na *behaviour* kwa ujumla ya *economy.* Moja mimi nilisema juzi na leo narudia. Ningekuwa mimi naambiwa fanya uamuzi sasa ningesema hivi mbolea kwa ajili ya wakulima wangu mimi nita-*subsidies 25 percent* peleka mahali popote katika nchi hii, lakini mimi nitakuletea ruzuku pale ya 25% itakwenda. Kwa hiyo, mimi nabana hapo, anayepeleka Kagera, Mwanza, Dar es Salaam, Mbeya, Mtwara na popote apelike lakini *percentage* yangu mimi ya mbolea ni hii, kwisha.

Unasema Wilaya 28, Prof. Jumanne Maghembe, amezungumza hapa na fedha zitakazokwenda pale hatuelewi kwa sababu sisi hatuishi hapa duniani milele, sisi tunaishi hapa kwa muda mfupi tu siku zako ni 70 Mungu akipenda ni 80 na hivi mmeingia matatizo makubwa haya ya kisasa huna hakika na kuishi. *Juice* kama tunakunywa, *juice* tunywe leo, kama tunakula kabichi tule leo. Huwezi kuzungumza habari ya Wilaya 28 halafu na nyingine zisubiri, *it does't make any sense.* Hakuelewi kabisa. Aliyekuwa Mpanda, Rombo anataka sasa. Sasa ndiyo tunataka kupanda sasa. Unasubiri unasema miaka mitano tutaangalia Tabora na ndiyo mimi nakubaliana na Mheshimiwa Rais, jana alipozungumza kuhusu *TASAF* mwelekeo wake ni kwamba Wilaya zote zifuate ule mpango wa *TASAF.* Kwa sababu kama ni barabara nzuri huwezi ku-*postpone* kunywa chai ya maziwa, kula nyama ukasema mimi nataka nijibane sitakula nyama ili nile baadaye lini, *package* yote nzima ni sasa unatakiwa uendelee na uende nayo.

Kwa hiyo, mimi nataka kuishauri hapa na hili ninalileta katika suala zima la *STABEX.* Hii *STABEX* tumezungumza hapa. Mheshimiwa Waziri Charles Keenja jambo hili napigiwa kelele maamuzi ya kusema fedha iingie kwenye mfuko wa mtu kwa maana ya fedha zote zilizotolewa Serikali imesema haiwezekani kwa sababu maelekezo yaliyotoka *European Union* yanasema kwamba iende kwa ajili ya kusaidia.

Mimi jana asubuhi nimeleta hapa habari ya barabara yangu ilijibiwa. Mimi nimeitaja makusudi kwa sababu najua unaweza tukazungumza hapa baadaye ukaambiwa hakuna cha barabara, hakuna cha watu wamepewa na hakuna cha pembejeo. Lakini na hii Mzee Basil Mramba, Mchaga yule wa kweli kweli anayeijua pesa, anasema pesa ni ile inayopita hapo kwenye mkono wake. Isipopita hapo kwenye mkono wake hiyo pesa haielewi.

Sasa Mzee Charles Keenja, anasema hivi hawa ukiwapa hiyo fedha wanakwenda kupiga kitochi, hapana. Mkulima *responsible* hawezi kwenda kupiga mbege akaacha kahawa inaanguka pale, huwezi ukaweka *welfare* ya watoto wako na familia yako na wewe mwenyewe chini ya kitochi haiwezekani. Atachukua ile fedha sehemu kubwa atakwenda kununua solo ile ya kupigia dawa, atakwenda kununulia mkasi, magunia na chekecheke. Hii ya barabara ndiyo fedha pekee ambayo ikitumika huwezi kui-*trace.* Lakini hii ya kuwalipa wakulima ikienda kwao pale utawaambia mimi nataka niwaambie hata kwenda kwa *karamazoo big contradiction* iliyotokea pale ilikuwa ni nini eti kwa sababu imeingia soko huria. Soko huria *was way back in 1995.* Sisi tuliuza katika ushirika kutoka mwaka 1993, 1994 na 1995 na rekodi hizi ziko kwenye ushirika mwuliza Sir George Kahama anazo, kwa nini usirudi nyuma mpaka pale kwenye hicho kipindi cha l993, 1994 na 1995 ukasema hii ndiyo nitakayotumia kama *criteria* ya kuwalipa wakulima kwa sababu wote waliuza katika vyama vya msingi, vyama vya ushirika, inaleta matatizo hapa. Nataka niseme kitu kimoja bado tunaweza tukafanya hivyo kama Serikali inavyosema lakini iko haja ya kuwaangalia hawa wakulima. Sehemu fulani itoke ya hiyo senti iliyokuja ipelekewe wakulima hata kama *for psychological purposes. (Makofi)*

Juzi tumefuta hapa kodi ya maendeleo. *Two, three years ago* ungesema kitu cha namna hiyo watu wangekushangaa sana. Lazima tufanye tamaa za kisiasa. Ujasiri walikuwa wanazungumza wanajeshi walikuwa Wajerumani, Waingereza na Wamerikani. Mjerumani wa kwanza akawaambia wenzake nataka niwaonyeshe maana ya ujasiri. Akamwambia utachukua hizi silaha ambazo zinalipuka, kimbia juu ya hii reli anguka chini, simama halafu rudi hapa akafanya akaenda akarudi akapiga saluti. Mjerumani akasema *that's what I mean by saying he is courageous.* Akakimbia Muingereza akafanya hivyo hivyo. Akarudi akapiga saluti akasema hii ndiyo maana ya ujasiri ninayoizungumzia. Akaja Mmarekani akaambiwa beba

haya masilaha yanayolipuka nenda juu ya reli jizunguushe anguka anguka halafu rudi hapa. Yule Mmarekani akasema, *what? You must be crazy man, what are you talking about?*

Mimi nitakufa nikienda hivyo mnavyosema. Mmarekani akapiga saluti akasema hiyo ndiyo maana ya ujasiri. Ujasiri ni uwezo wa kusema hapana. Serikali yetu ifike mahali iseme hivi *EU, World Bank, IMF no way* ni lazima tumsaidie mkulima wetu sisi Watanzania. Lazima tumwekee ruzuku akina George Bush wanakataa, wakina Shark wanakata sisi Tanzania tunasema hivi ni sawa hatutamsaidia. Mimi naiomba Serikali iangalie. *(Makofi)*

Mwisho, wenzangu wamezungumzia habari ya *alternative crop.* Wamezungumzia sana suala la maua. Maua yanafanya mambo makubwa ni miezi sita, miezi sita ikashafika unapeleka Ulaya. Ndani yake watu wanapata ajira, kabichi, nyanya na mboga mboga za aina mbalimbali. Soma historia yake. Arusha wame-*practice* pale mimi nilikuwa Mkuu wa Wilaya niliiona. Mimi naishauri Serikali na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula, nashauri kwamba tuangalie hili eneo la kilimo kwa umakini zaidi na tuweke nguvu yetu zaidi pale. Maneno haya yaliyozungumzwa hapa nimemsikia hata Mkuu wangu wa Mkoa wa Kilimanjaro akizungumza jambo hili ni jambo la msingi ni jambo muhimu litatusaidia.

Kwa kufanya hivyo hata wakulima hao wadogo wadogo ambao tumewazungumzia hapa waku-*create* ile *industry* wanaweza wakazalisha kwa *supervision* na kwa *standards* watakazoelekezwa wakapeleka pale kwenye yale mashamba makubwa makubwa tukapata mauzo ya nje mazuri na hali ya maisha ikawa ni nzuri. *Industry* hii moja ya *contradiction* ambayo inakusaidia ku-*solve* ni suala la ajira. Wanakuwa mpaka 3,000 au 4,000. Hawa akina Mheshimiwa Felix Mrema, wanafahamu pale Arusha. Kwa hiyo, mimi naiomba Serikali ilitazame kwa karibu sana iangalie jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *irrigation,* mimi nimezungumza habari ya Mfongo wa Mzungu kule kwangu kuna mifereji ambayo walileta wazungu tunaita Mfongo wa Mzungu. Mheshimiwa Charles Keenja, ukitaka watu wakuheshimu barabara nzima kama ilivyokuwa Dar es Salaam hapa angalia maeneo mawili, angalia suala la *irrigation* na *extension services fool stop*. Ukisambaa sehemu kubwa *management* ya kitu kikubwa ni ngumu sana. mtu ana-*manage* kitu vizuri anapoji-*confine* katika eneo dogo. Habari ya mvua Mungu ataleta, habari ya namna gani tutakwenda itakwenda, lakini *confine yourself* katika kilimo cha umwagiliaji. *I am glad,* kwamba hii imetamka kwamba kuna *Department* ya kilimo cha umwagiliaji kimeanzishwa mahsusi kabisa kwa hilo.

Sasa tuelekee kwenye suala la umwagiliaji, sasa tuelekee katika huduma za ugani, hili ni tatizo kwangu Kijiji cha Nnao-Kisangara wameniandika kwenye magazeti hujatusaidia kwenye mifugo na kilimo. Hatuna wataalam, watu wanalalamika pale wanasema sisi tunataka mtu wa kutuonyesha namna ya kupalilia na kusimamia kahawa. Hili tuliwekee mkazo. Ukiakaa halafu ukalisimamia vizuri huko kwingine kote unaweza ukaacha. Ukasema mimi huku siwezi kwa sababu mvua kama itanyesha, itanyesha kama haitanyesha, haitanyesha, kama ni misitu watapanda akina Mheshimiwa Arcado Ntagazwa na Mama Zakia Meghji, watafanya kazi hiyo. Kilimo kiji-*confine.* Peleka plau *every amount of money* umeipata ipele katika *production unit.* Irudishe pale ifanye kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kawaida unafikiri kuna ugomvi hapo? Hakuna ugomvi. Mimi narudia kuunga mkono hoja hii nai-*support,* nashukuru kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**MHE. CHRISTOPHER S. WEGGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi na mimi nichangie kidogo Wizara ya Kilimo na Chakula. Nianze kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na wataalamu wote wa Wizara ya Kilimo na Chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, kelele zote unazozisikia hapa mimi nadhani zina uhakika ndani ya Wabunge. Lakini msingi mzima tuzungumze ule ukweli. Nchi hii kama haitakubali kutoa fedha kwenye kilimo haiwezi kufika mahali popote.

Mimi nimeingia Bunge hili mwaka 1995 ushauri wangu mkubwa nilikuwa nikisema wapeni watu wa kilimo fedha tufanye kazi, haya mambo mengine tunayoyajaza humu hayana maana hata kidogo. Suala hapa ni kilimo. Suala la kusema sijui tunafanya utafiti, sijui kuna mafunzo, Mheshimiwa Waziri, wakulima ni wajuzi sawa sawa. Hakuna mkulima ambaye unaweza ukamfundisha sasa hivi hayupo.

Mimi kila siku nasema mfano mzuri nendeni Kilombero. Wale watu pale sisi hatujawapeleka chuo. Tulichofanya tumewezeshana kukaa, kuzungumza na mwekezaji mliotuletea pale Bwana *Europe,* tukasema kwamba Serikali haina fedha tupe wewe fedha. Hivyo ndiyo maana tuwe tunakwenda *Europe* kila siku kuwaambia Serikali haina fedha tupe wewe fedha. *Europe* anasema mimi nawapa fedha, mashamba yako wapi. Tukasema haya hapa nitawalimia, nitawapa mbegu tutakutana kwenye kuvuna, kwisha, hakuna hadithi nyingine. Sasa ndiyo haya tunasema mazao yote kama tunataka kulima kuwe na mfumo huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niombe sana hivi tunaposema tunao Mabwana shamba kweli tunao Mabwana shamba. Nani anapokwenda kijijini anaona Mabwana shamba Mheshimiwa Waziri ulinitembelea shamba Mabwana shamba uliwaona kule. Mwaka 1996 nilikuambia naomba wavae *uniform* wale watu waonekane kama ma-*traffic* tunawaona barabarani humu. Sasa unamkuta Bwana shamba saa tatu amekwishakunywa hana *uniform,* yuko hoi wapeni uwezo hawa. Wapeni pikipiki ndiyo haya tunayozungumza sio kuwapeleka vyuoni sio utafiti na kadhalika.

Sasa bwana shamba kama hata *uniform* hana, unamwambia Kijiji hapa bwana shamba yuko wapi, ndizo kazi tunazowafanya Wabunge. Wanakwambia bwana shamba ngoja tukutafutie bwana shamba alikuwa hapa hapa. Lakini zamani kazi hii ya kilimo ilikuwa na utaratibu Mabwanashamba walikuwa na unifomu na tunawaona yule. Kama ametoroka kazini utamwona na tunaomba sasa kama mtawashonea kwa kweli yasiwe makhaki magumu kama yale ya zamani. Sasa washoneeni nguo nzuri, suti tuwaone wale wenzetu wanafanya nini. Sisi kusimamia tunatosha. Akilewa tutakuletea tunamwondoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la viwanda vya sukari leo sitaki kusema sana. Kwa sababu wewe umeshanijua kwamba umekuwa nikipiga kelele humu ndani suala la viwanda vya sukari. Matunda sasa unayaona. Hatuna tatizo la sukari Tanzania. Katika hesabu ile uliyotoa tani 284 zitasagwa mwaka huu kwa kima tunachotumia tani 300 kuna shida tena ya sukari hapa. Kuna mtu ana matatizo ya viwanda vya sukari. Sasa tuna tatizo na Serikali, sio viwanda tena. Tuna tatizo na Serikali tunaomba mlinde viwanda hivi. Huwezi ukamsumbua mtu ameweka fedha yake katika nchi yako halafu unambabaisha babaisha hivi unamzungusha zungusha hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa badala ya kuwalinda mimi naomba waiteni mkae nao wapeni viwanda vya kutengeneza *industry sugar* ili tumalize tatizo la *industry sugar.* Zungumzeni nao kwamba hawa wamefikia tani hizi leo watashindwa kutengeneza *industry sugar,* wataweza. Kaeni nao bwana hili tatizo linalofanya kuingiza sukari nyingi hapa mpaka mnashindwa kuuza ya kwenu *industry sugar,* sawa, tengenezeni, leteni kiwanda kingine kiwe *special for industry sugar.*

Mheshimiwa Naibu Spika, huu mchezo kuna sukari wa njia za panya, *Bagamoyo route,* sijui Zambia inaingia nyingi utakwishia hapa. Iko lugha inasema kama una wasi wasi na mchawi mpe mwanao alee mchawi. Sasa wapeni na kiwanda cha *industry sugar* mmalize hilo tatizo, kelele zangu zitaishia hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, amekuja kutembelea jimboni kwangu. Nimefurahi tumekaa naye siku mbili nimemwonyeshs mashamba yote. Ninachotaka kuzungumza hapa ni kwamba, yale mashamba sugu niliyomwonyesha Mheshimiwa Waziri ni ya mwekezaji asiye na adabu! Yeye anaitwa mwekezaji, lakini ni mhuni!

Tulimwomba Mheshimiwa Waziri awafukuze, atupe yale mashamba, mbona hata sioni majibu katika hotuba yake? Kwa historia mashamba yale siyo ya Serikali, Serikali iliyachukua kwa Wananchi wakalima mkonge, mengine yakalimwa miwa pale Luhembe. Mpaka leo mashamba yale hayajafufuliwa, mfano katika lile shamba la Zombo, tumekuta mtu anang'oa mataruma na nguzo anauza, Mheshimiwa Waziri akakamata nguzo moja akaondoka nayo, kesi ile imefikia wapi? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba lile shamba la Miombo ili tulime pamba. Shamba lenyewe ni hekta 3,000 tu, hivi hizo nazo mtatafuta mwekezaji? Katika shamba la Ulaya tulifika tukakuta mtu ameng'oa *engines* na *bearings* zote, nikamwambia Waziri niandikie barua kama ya kujidai tu kwamba, Mheshimiwa Christopher Wegga, nimekupa shamba hili uwape watu wako walime pamba, hilo tu! Katika Majimbo yaliyozungukwa na mikonge hakuna mashamba zaidi ya mikonge, tutaingiana na

tutabanana mle mle kwenye mashamba yale, hatuachii nafasi. Tunaomba mtupe mashamba ya Ulaya, Miombo na Luhembe. Namshukuru sana Mheshimiwa Charles Keenja, na niseme namshukuru zaidi kwa sababu ana miaka sita na kesi moja ya shamba la Luhembe, unapocheleweshewa kesi unashukuru. Pia, *Attorney General* nakushukuru sana kwa kuchelewesha kesi ile ya Luhembe, lakini naomba chonde chonde shamba lile kesi yake imalizike ili tuendeleze kilimo la miwa pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la mikopo ni kwamba, mikopo iliyozungumzwa ni mizuri, lakini ninachotaka kuzungumza hapa na hata waliotangulia kuzungumza wamesema kwamba, hutapata mkulima ambaye ana nyumba yenye hati Dar es Salaam, si rahisi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri atakumbuka nilikwenda nyumbani kwake na tukapata chakula cha mchana, namshukuru sana, lakini jambo kubwa nililomwambia ni kwamba, siwezi kuchukua mkopo wa shilingi milioni 20, kwa sababu nimeteuliwa kusambaza pembejeo katika zile Tarafa tatu za Mikumi, Masanze na ndizo ambazo zinazolima pamba, pamoja na umwagiliaji katika Tarafa ya Malolo. Eti ananipa shilingi milioni 20, nikasema, chukua hizo, kaa nazo mwenyewe.

Tarafa ya Mikumi peke yake, kwa maana ya Kata ya Kidodi na Luhembe ni shilingi bilioni 4.0. Kwa miezi sita tumeuza miwa kwa shilingi bilioni 4.0. Nimewekwa *centre* ya kusambaza pembejeo, eti napewa shilingi milioni 20, sasa kuna hesabu inakuja hapo, yaani Mheshimiwa Waziri haniamini hata mimi Mbunge! Akishindwa kumwamini Mbunge, atamuamini nani? Lakini nashukuru aliniambia nitakufikiria baadaye, nadhani baadaye yenyewe ndiyo hii sasa. *(Kicheko/Makofi)*

Kuhusu Vyuo vya Sukari, hakuna Chuo cha Sukari kama kile cha Kidatu, Kilombero. Tuna tatizo katika Chuo hiki, tunaomba Serikali itusaidie na tunashukuru mpaka pale tulipofikia, lakini tunaomba msaada zaidi kwenye ukarabati. Walio-*invest* katika Chuo kile ni Waholanzi kwa zaidi ya shilingi bilioni 5.0 sasa hivi kina matatizo ya ukarabati, tunaomba shilingi milioni 600 tu. Kama kweli Serikali inahitaji kuongeza Vyuo vya Kilimo ni pamoja na Chuo hicho kukarabatiwa. Si Chuo kinachozungumzia masuala ya sukari tu, hata hawa *big four,* kutoka Iringa, Mbeya na kadhalika, watakuja kwa ajili ya masuala ya mahindi pale. Pia, tunao watu kutoka Uganda, Kenya na Zimbabwe.

Kwa hiyo, naomba sana tufikiriwe kwenye Chuo kile, kwani kwa kweli kina hali mbaya. Ruzuku inayotolewa pale nashukuru inatosha kwa mishahara na viwanda navyo vinatoa ruzuku ya kuendeshea, lakini naomba kikarabatiwe ili kiwe na hadhi ya Chuo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza sana Mkurugenzi wa *SUDECO,* Ndugu yangu Frank, kwa kazi nzuri anayoifanya pale Kibonde. Tulikuwa na matatizo ya kifedha, wakati wa kulipana mishahara ilifikia mahali tunawaambia watu, subirini kidogo bado tunatafuta mishahara, lakini mahusiano yaliyojengwa kati ya Serikali na Chuo kile yamekuwa mazuri. Tunaomba tumalizie kwenye kukikarabati ili kifanane na wanafunzi kinaowapokea, tunajaza wanafunzi kama kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu masoko, huko zamani tulikotoka si kwamba wakulima walikuwa hawataki kulima, bali walikaa na pamba yao majumbani na ukitaka ushahidi pale Masanza mpaka leo watu wana pamba za zamani. Tunasema kwamba, tunarudi kwenye kulima na tunaitikia wito wa kulima, lakini tunaomba mtupe msimamo wa malipo. Tunataka soko likianza tunapima pamba na kulipwa hapo hapo, mtu asiondoke na risiti, zile risiti ndiyo tatizo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Wizara ya Ushirika na Masoko, ishirikiane na Wizara ya Kilimo na Chakula, kwa sababu kazi yao ni moja, Wizara ya Ushirika na Masoko, ni kwa ajili ya masoko ya mazao na Wizara ya Kilimo na Chakula ni kwa ajili ya mazao. Wakae wazungumze na waelewane, hizo fedha wasizikimbize huku na huko zikaleta matatizo. Waziri wa Ushirika na Masoko azungumzie kuhusu wakulima ili tupate kulipwa, tatizo ni kulipwa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la mashamba ya umwagiliaji, shamba na Kilangali, Malolo nimeona hata katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri amelisahau kabisa, pamoja na kwamba yeye mwenyewe alikwenda kuliangalia. Lumuma nimeiona, ni kwa nini Malolo ameiacha?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, kabla sijagongewa kengele, kwenye Jimbo langu naomba trekta 10 tu basi na tutalipa, trekta 2 Malolo na 3 Kilombero pale kwenye shilingi bilioni 4.0. Kwenye shamba lile la Kilangali Mheshimiwa Waziri alikuta *caterpillar* imekufa kabisa haina hata hamu akasema ataifufua, naomba asifufue lile trekta la zamani, anipe trekta mpya. Achana na mambo ya kufufua fufua matrekta ya zamani utagombana na watu bure! Trekta ya zamani leo ukifunga tairi ya mbele, linachomoka la nyuma, utagombana na watu bure, lete trekta mpya.

Jimboni kwangu nataka matrekta 10 tu niweke hizo *extension* mnazosema, mbili nitaweka Ulaya, tatu nitamalizia Zombo na nyingine mbili napeleka Uleling'ombe tumemaliza, nitalisha Tanzania hii! Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula, aje pamoja na Mheshimiwa Waziri wa Ushirika na Masoko, kwani ushirika tumeshaunda. Tunapoongea tunaomba Serikali ifahamu kwamba tumechukia kwa sababu katika suala la kilimo mmetuacha nyuma. Leo wanazungumza watu hapa kwamba kuna mazao yamekauka tu, kwa mfano mazao ya kahawa haya hata hayatamaniki! Ndugu zangu pale wanapiga kelele, Moshi ya zamani siyo tuliyonayo sasa, Tukuyu ya zamani siyo ile na Mbozi siyo ile, ndiyo maana unaona akina Mheshimiwa Edson Halinga, sasa wamelewa pale! Tunaposema kilimo, hakuna haja ya kufundishana, watu wanajua kulima! Leteni hizo pesa tufanye kazi ya kulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga hoja mkono. *(Makofi)*

**MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. NJELU E. M. KASAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia hoja ya Wizara ya Kilimo na Chakula, kama ilivyowasilishwa na Mheshimiwa Charles Keenja, naanza kwa kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuunga mkono hoja, ninapenda kuzungumzia mambo yafuatayo:-

(i) Kwanza, kuhusu kilimo cha tumbaku. Zao hili ni la wakulima wadogo wadogo ambao hawasaidiwi na shirika lolote isipokuwa makampuni yanayonunua tumbaku. Kwa hali hiyo, ilitazamiwa kuwa Serikali ndiyo ingekuwa mstari wa mbele kuwasaidia wakulima hawa. Lakini mambo sivyo. Huduma za ugani katika maeneo ya tumbaku ni kdigo sana. Wakulima hawapati mafunzo au maelekezo toka kwa Maafisa Kilimo. Wakulima hawatembelewi na wataalam wa zao hilo kwa vile hawatoshi au ni wachache mno. Baya zaidi katika baadhi ya maeneo Maafisa kilimo siyo wanataaluma ya kilimo. Mtaalam wa mifugo hufanya kazi katika eneo la mazao na hivyo kushindwa kuwashauri wakulima ipasavyo. Kwa mfano, Wilaya ya Chunya ina Maafisa Kilimo watatu walifunzwa tumbaku tu na katika hao ni mmoja tu ndiye aliyeko mashambani (kijiji cha Mamba), mmoja amepewa kazi tofauti na kilimo na aliyebaki yupo kwenye Ofisi ya Kilimo Wilayani.

Kwa hiyo, wakulima wanalima bila ya utaalam wowote. Lakimi mahitaji halisi ya Wilaya ni Maafisa Kilimo Tumbaku 42 na kufanya upungufu kuwa 39. Katika Wilaya ya Manyoni ambayo huzalisha tumbaku kidogo kuliko Chunya ina Maafisa Kilimo watano kati ya tisa wanaohitajika. Iringa ambayo uzalishaji wake umeshuka sana miaka ya karibuni ina wataalam wa tumbaku tisa kati ya mahitaji ya wataalam 12. Serikali inashindwa nini kuainisha mahitaji ya wataalam na uzalishaji? Hali ni mbaya sana katika Wilaya ya Urambo ambayo ndiyo mzalishaji mkubwa wa tumbaku. Mahitaji ya Wilaya hiyo ni wataalam 98, lakini waliopo ni tisa tu na wasio na taalum ya tumbaku ni wawili.

Katika mazingira kama haya utapataje zao lenye ubora wa Kimataifa? Utaongezaje uzalishaji kwa hekta bila ya utaalam? Wakulima waliopewa mafunzo miaka ya sitini na sabini sasa hawapo waliopo ni wapya ambao wanahitaji utaalam. Katika uchunguzi wangu, nimegundua kuwa kwa nchi nzima kuna wataalam wa tumbaku 138 tu kati ya 395 wanaohitajika. Naiomba Wizara ipeleke wataalam wa kutosha kwenye maeneo ya tumbaku pia ianze kufundisha wataalam zaidi wa zao la tumbaku.

(ii) Kituo cha Utafiti Tumbaku Tumbi. Kama ambavyo ugani umeshuka katika zao la tumbaku vivyo hivyo ambavyo utafiti umekufa. Kituo cha Tumbi na vituo vidogo vya Mtanila na Sitandole

havijafanya kazi kwa muda mrefu. Uzalishaji bila ya utafiti hauwezi kuwa na tija. Kuna taarifa kuwa Serikali imekabidhi utafiti wa tumbaku kwa wanunuzi na wakulima.

Kwa taarifa ya Waziri, wanunuzi wamekataa kugharamia utafiti. Kwa hiyo, wamebaki wakulima wadogo peke yao kupitia *Tobacco Apex.* Serikali kutazamia utafiti wa tumbaku kufanywa na wakulima wadogo ni kujidanganya kwa sababu hawana uwezo kifedha, kiutaalam na kimenejementi. Naishauri Serikali masuala ya utafiti yafanywe na Serikali na iachane na wazo la sasa. Chai ina wakulima wakubwa na ni wao waliomba waachiwe suala la utafiti na wanafanya vizuri. Tusichanganye mambo haya Serikali ichukue utafiti wa tumbaku.

(iii) Ugani na usimamizi wa kilimo kwa ujumla umezorota sana. Kuzorota huko kwa kiwango kikubwa kunatokana na mabadiliko ya mfumo wa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa. Wizara kutokuwa na usimamizi wa moja kwa moja wa wataalam wake katika Mkoa na Wilaya kumechangia sana matatizo ya sasa. Sheria Na. 6 ya mwaka 1999 iliyozifanya Serikali za Mitaa kutosimamiwa moja kwa moja na Wakuu wa Wilaya na Mikoa imekuwa na matokeo mabaya.

Hadi sasa kwa hali halisi *DC* anafanya ya kwake na *DED* anafanya ya kwake. Kilimo hupata msukumo zaidi pale ambapo *DED* ana mwelekeo wa kilimo kama hana mwelekeo basi kazi za kilimo hukosa msukumo. Lakini kubwa zaidi ni kwamba *DED* si mhamasishaji ambapo *DC* anatakiwa kwa mujibu wa kazi yake kuwa mhamasishaji. Ili kuleta maendeleo ya haraka kwenye Wilaya na Kata, viongozi hawa wawili wanapaswa kuunganishwa kwa sheria na siyo kwa agizo tu la Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, usimamizi wa *DC* kwa *DED* kwa agizo la Rais bila sheria kumesababisha kutoelewana kwa viongozi hao na kufanya kazi za maendeleo ikiwa ni pamoja na kilimo kuzorota. Kuna haja ya kuutazama upya mfumo wa sasa wa kusimamia kilimo na pia Sheria Na.6 ya mwaka 1999 inayowaondoa ma-*DC* na ma-*RC* kuwa wahimili wasaidizi na wahimili wa Halmashauri. Kwa msimamo wa sheria hiyo, *DC* huonekana kama mtu anayeingilia shughuli za Halmashauri.

(iv) Kuhusu kilimo cha umwagiliaji, Chunya. Naishukuru Wizara kwa kuipatia Wilaya ya Chunya fedha zipatazo shilingi milioni 22 kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji katika kijiji cha Ifumbo. Eneo hilo ni zuri sana kwa kilimo hicho lakini limekosa uwekezaji ili kuweza kuzalisha kwa uwezo wake. Fedha hizo zimekuja wakati muafaka kwa vile eneo hili lina shida ya mvua mara kwa mara na mwaka huu limeathirika. Ninaomba fedha zaidi zipatikane ili kuwezesha eneo kubwa kulimwa kwa njia ya umwagiliaji. Maji ya eneo hili hutoka kwenye milima ya Mbeya kwa *gravity.* Aidha, Mto Wombo ambao una maji mwaka mzima ungejengwa Bwawa na hivyo kuwa na uhakika wa maji ya kumwagilia.

Nakuomba Mheshimiwa Waziri upeleke wataalam wakaangalie uwezekano wa kujenga Bwawa kwenye Mto Wombo. Tukitaka kuimarisha kilimo cha umwagiliaji, Serikali iwe tayari kujenga mabwawa katika maeneo yanayofaa kama Ifumbo ambapo maji yatatolewa kwa *gravity* tu. Ardhi ya eneo la Ifumbo lina rutuba ya asili na halihitaji mbolea ya chumvi chumvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia kwa kuunga mkono hoja na kuwatakia mafanikio.

**MHE. KHALID S. SURU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kutakuwa na mkakati wa kilimo kupitia programu mbalimbali ikiwemo ya umwagiliaji, nimeshangaa kuona Bonde kubwa la Mto Bubu kule Kondoa halikuingizwa katika *Master Plan* maalum ya kilimo cha kumwagilia maji mashamba. Bonde hilo ni kubwa na lina rutuba na ni muhimu sana. Likitumiwa vizuri litaleta ajira na kuondoa umaskini Kondoa. Waziri wa Kilimo na Chakula, Mheshimiwa Charles Keenja na Naibu Waziri wa Kilimo na Chakula, Mheshimiwa Pius Mbawala, wanalifahamu kwani mwaka 2002 walilitembelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, chini ni Kata, watu na idadi ya hekta zilizopo ambazo zikitumika kupitia programu hii ufanisi utapatikana sana na wakulima wataondokana na njaa pia umaskini. Ni kandokando ya Mto Bubu huko Kondoa.

| Kata | Idadi ya Watu | Hekta |
|---|---|---|

| | | |
|---|---|---|
| Kikilo | 9,447 | 125 |
| Thawi | 10,364 | 65 |
| Changaa | 13,987 | 3,020 |
| Suruke | 11,711 | 1,612 |
| Kingale | 10,525 | 15 |
| Kondoa mjini | 21,878 | 20 |
| Jumla | 77,912 | 4,837 |

Mheshimiwa Naibu Spika, bonde hilo ni muhimu sana linafaa kuingizwa kwenye mpango kamambe wa kilimo cha umwagiliaji maji mashambani. Namwomba Mheshimiwa Waziri, aingize Bonde hilo, nchi itanufaika. Nasubiri jibu wakati wa majumuisho yake na ni matumaini yangu kwamba ushauri wangu utazingatiwa kwa manufaa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, naunga mkono hoja.

**MHE. ARIDI M. ULEDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nachukua nafasi hii kukushukuru kwa kupata nafasi hii ili nichangie hoja ya Waziri wa Kilimo na Chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza mchango wangu kwa kujielekeza kwenye zao la korosho ambalo hulimwa kwa wingi katika Mikoa zaidi ya sita hapa nchini. Zao la korosho ndilo zao kuu la biashara katika Wilaya yangu ya Masasi ambayo inakadiriwa kuwa na mikorosho zaidi ya milioni tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzoefu unaonyesha kuwa mkorosho mmoja ambao unatunzwa vizuri kwa kupaliliwa kwa wakati, kupuliziwa dawa na *sulphur* kwa wakati na wingi unaotakiwa hutoa korosho si chini ya kilo 50 kwa mwaka. Kwa Wilaya kama Masasi ambapo kuna mikorosho zaidi ya milioni tano uzalishaji wa korosho ungezidi kilo 250,000,000. Lakini kwa kukosa palizi nzuri za mikorosho, wananchi kukosa dawa za kupulizia mikorosho yao kwa wingi wa dawa unaohitajika, Masasi huambulia kuzalisha korosho kiasi cha kilo 18,000,000 tu kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nini kifanyike kwa wakulima wa zao la korosho? Kwanza, kufanyike sensa ya wakulima wa zao la korosho na idadi ya mikorosho kwa kila mkulima. Pili, kwa kufuata ukubwa wa mashamba ya mikorosho kuwepo na mipango ya kupeleka matrekta hadi ngazi ya Tarafa, Kata na hata vijiji kulingana na mahitaji kwa ajili ya wakulima kukodi ili kupalilia mashamba ya mikorosho. Kwa wakulima ambao hawana fedha za kukodi matrekta basi wakopeshwe ili wakati wa mauzo ya korosho wakatwe fedha kufidia mikopo yao. Kwa njia hii tutahakikisha mikorosho yote inapaliliwa kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza kuwepo na *Farm Centres* katika Wilaya, Tarafa, Kata ambazo zitakuwa na wataalam wa ugani wa kuelekeza juu ya kilimo bora. *Farm Centres* hizi ziwe na pembejeo na dawa kwa ajili ya mazao kama korosho ili wananchi wenye fedha waweze kununua na wale ambao hawana fedha wakopeshwe na wakati wa mauzo ya mazao yao wakatwe fedha kufidia mikopo yao. Nina hakika kwa njia hii uzalishaji wa mazao kama korosho utapanda juu haraka sana kwani ili uzalishaji wa korosho uongezeke twahitaji mambo manne nayo ni watu, mikorosho, palizi na pembejeo. Watu tunao tele, mikorosho ya kutosha tunayo lakini tunakosa palizi na pembejeo. Kwa hiyo, naomba Serikali ikafanikisha wakulima wa korosho kwa palizi na pembejeo ili uzalishaji wa korosho uongezeke kwa haraka sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na kuongeza uzalishaji wa korosho, suala la kubangua korosho ni la muhimu sana. Pamoja na Serikali kukazania kubinafsishwa au kukodishwa kwa viwanda 12 vya kubangua korosho, naomba vile vile ukazanie kuwasaidia wakulima kuwezeshwa kupata mikopo ya kununulia mashine za kubangulia korosho ili kuongeza thamani ya zao la korosho.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti tayari unaonesha kuwa sehemu zingine za mikorosho zinaweza kutoa faida kubwa. Mabibo, utonvu, maganda ya korosho na mkorosho wenyewe ni baadhi tu ya vitu vinavyoweza kuongeza pato la mkulima wa korosho. Naomba Serikali kwa kutumia tafiti ambazo zimefanyika na zile zitakazofanyika imsaidie mkulima wa korosho kuongeza kipato kutokana na zao hilo kwa kutumia tafiti hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wakulima wa korosho, tunaona korosho ndiyo ufunguo wa kila kitu. Kwa kuboresha uzalishaji wa korosho, tutapiga vita umaskini wa kipato, adui njaa, ujinga, maradhi, hivyo kuboresha hali ya maisha ya wananchi kwa kujihakikishia kuwa wanapata nyumba nzuri za kuishi, mavazi mazuri ya kuvaa, chakula kizuri na usafiri mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Masasi ni miongoni mwa Wilaya ambazo zimekumbwa na njaa mwaka huu. Sababu za kuwepo njaa Wilayani Masasi ni ukame ambao umesababisha mazao kukauka na kushindwa kukomaa na wanayama waharibifu ambao hushambulia mazao hasa katika maeneo ambayo yanazunguka na kupakana na Hifadhi ya Lukwika - Lumesule na kwenye njia ya wanyama wanaohama kutoka Hifadhi ya Selone upande wa Kaskazini kwenda Hifadhi ya Lukwika - Lumesule upande wa Kusini. Hii inatokana na udhibiti mdogo wa wanyama hao kulinganisha na ukubwa wa eneo ambalo limeathirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, usimamizi mzuri wakati wa kusambaza chakula cha msaada ni muhimu sana kwani huko nyuma kumekuwepo malalamiko mengi juu ya ugawaji mbovu wa chakula cha msaada. Wale ambao hupewa jukumu la kusimamia ugawaji wa chakula cha msaada wanashindwa kugawa kwa haki hivyo kusababisha manung’uniko mengi kutoka kwa wananchi. Ni matumaini yangu kuwa Serikali itahakikisha kuwa chakula cha msaada kinakwenda kwa walengwa tu na si vinginevyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuchangia haya, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja na nashukuru kwa kupata nafasi hii ya kuchangia.

**MHE. JOHN L. MWAKIPESILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Waziri wa Kilimo na Chakula ni nzuri sana na inatoa matumaini mapya kwa wananchi vijijini. Kilimo ni sayansi na teknolojia na kinahitaji ujenzi na maarifa. Kilimo cha jembe la mkono ambacho ndicho kinatawala katika nchi yetu haikiwezi kukuza uchumi wa kisasa na kupunguza umaskini ambao unatusumbua Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mikopo ya fedha za kununulia matrekta mapya na kutengenezea matrekta ya zamani ni suala la msingi na linaweza kuleta mapinduzi makubwa katika kilimo na kukuza Pato la Taifa. Kwa kiasi kikubwa, Wizara ibuni utaratibu mzuri zaidi wa kukopesha matrekta kuliko wa hivi sasa kupitia Mfuko wa Pembejeo na *Exim Bank.*

Mtu ambaye hana Hati miliki kama dhamana ya mkopo aruhusiwe kukopa ili mradi analo shamba na makazi yanayoeleweka na Serikali ya kijiji inamtambua. Waheshimiwa Wabunge waruhusiwe kukopa matrekta kama wajibu ili waonyeshe mfano katika mapinduzi haya ya kilimo. Wizara ya Kilimo na Chakula, iweke utaratibu wa kumdhamini mkopaji wa trekta kwa masharti yanayoeleweka na kutekelezeka. Mpango huu utakuwa na faida kubwa kwa nchi:-

(a) Kilimo kitapanuka na kukua;
(b) Mauzo ya nje yataongezeka;
(c) Thamani ya shilingi itapanda na kupunguza gharama/bei ya bidhaa tunazonunua toka nje;
(d) Akiba ya fedha za kigeni Benki Kuu ya Tanzania itaongezeka na hatimaye kupunguza utegemezi wa bajeti ya Serikali kutoka mikopo na misaada kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kilimo cha umwagiliaji ni suala la msingi na kiini cha mafanikio katika kilimo cha kisasa. Lakini nimeshtuka kuona kwamba Wilaya ya Kyela haimo kabisa katika mpango wa kilimo cha umwagiliaji. Wilaya ya Kyela inayo mabonde makubwa ambayo yanafaa kabisa kwa kilimo cha umwagiliaji kwa zao la mpunga. Mpunga wa Kyela unaa sifa ya pekee katika soko la ulimwengu na unauzwa kwa bei ya juu kuliko mpunga unaolimwa sehemu nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kyela ina Mito isiyokauka zaidi ya sita na wakazi wa Wilaya hii ni wakulima stadi wa mpunga kwa zaidi ya miaka 80 hivi sasa. Wizara ina maelezo gani kutoweka Kyela katika mpango wa kilimo cha umwagiliaji? Kuna sifa gani ambazo Kyela haina? Ni uzembe wa wataalam wa Wizara ya Kilimo na Chakula Mkoni Mbeya na Wilayani Kyela? *What is it?* Au Mbunge wa Kyela lazima apige magoti kwa Waziri?

Mara nyingi nimezungumza na Mheshimiwa Profesa Pius Mbawala, Naibu Waziri wa Kilimo na Chakula, juu ya suala la kilimo cha umwagiliaji na akanipa maelekezo nini *DED* wa Kyela afanye. *DED* alitekeleza maelekezo hayo. Wananchi wa Kyela hawataki kuachwa nyuma katika mapinduzi haya ya kilimo na ningependa Waziri anijibu nini kimetokea Wizarani kwake kwa kuiacha Wilaya ya Kyela katika mpango huu wa kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti ni muhimu sana katika nyanja zote za maisha na maendeleo ya binadamu. Utafiti ndio msingi wa maendeleo na mafanikio. Lakini utafiti hauna faida kama haumpunguzii matatizo mkulima. Wakulima wa mpunga Wilayani Kyela wameingiliwa na gonjwa linalokausha mpunga ukifikia umri wa miaka miwili au mitatu. Tumetoa taarifa za ugonjwa huu Serikalini. Utafiti umegundua kuwa ugonjwa huu unaletwa au kusababishwa na vidudu vya aina ya virusi na hauna dawa. Lakini sasa *what next?*

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri gani Serikali inatoa kwa wakulima wa mpunga wa Wilaya ya Kyela? Mwaka 2003 asilimia 20 ya zao la mpunga limeharibika kutokana na ugonjwa huu hasa Kata za Malewale, Lusungo, Mwaya, Buyonde na Songwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Waziri wa Kilimo na Chakula.

**MHE. ALHAJ SHAWEJ ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia kwa maandishi hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Kilimo na Chakula ya mwaka 2003/2004 kama ilivyotolewa na Mheshimiwa Charles Keenja, Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama cha Mapinduzi na Waziri wa Kilimo na Chakula kama ifuatavyo:-

(i) Kwanza ni kuhusu matumizi ya ardhi *(Land use).* Zamani matumizi ya ardhi yalikuwa yamepangwa katika viwango tisa *(Land Classification Classes I-IX).* Kitengo hiki cha matumizi ya ardhi umuhimu wake unapatikana kwa kuhusiana na Hifadhi ya Ardhi na Upimaji. Hiki ndicho Kitengo kinachosimamia ujenzi wa matuta ili kuhifadhi ardhi sehemu za miinuko, kuhifadhi unyevunyevu na hata *survey* ya udongo. Kwa ajili ya umuhimu wa matumizi ya ardhi, nashauri kuwa ipo haja kubwa ya kurudia utaalamu huu ili maeneo ya ardhi yapate kuainishwa kufuatana na *Land Classification Class.*

Kwa hiyo, napendekeza Wizara ya Kilimo na Chakula, ipanue Chuo chake cha Igurusi ili kipate uwezo wa kufundisha wataalamu wengi zaidi wa fani hii kwa sababu elimu ya fani hii ndiyo inayopelekea kuwezesha kujua viwango vya *Farm Production* na kuwezesha Wizara ya Kilimo na Chakula kutoa kipaumbele cha mazao katika maeneo. Kukosa kuwa na *Land Classification Classes* kwa maoni yangu ndiyo kunakosababisha mashamba kulimwa kwenye miinuko, mabonde mazuri ya mazao kujengwa nyumba, maeneo yanayofaa kilimo kuchungiwa na kadhalika.

(ii) Kuhusu *Farm Production,* baada ya kujua *Land Classes* inafuatia kujua viwango vya *Farm Production. Land classes* zikishafahamika ndipo kipaumbele cha mazao katika maeneo kinapotolewa. Kwa ajili hii, nashauri badala ya maamuzi ya uzalishaji kubaki kwa wakulima, Wizara ya Kilimo na Chakula itoe *priority crops* za kila eneo au Wilaya au Kanda. Baada ya hapo nguvu zote za Wizara zilekezwe kule na kwa kuwa maeneo mengine yanaweza kuendelea kuzalisha mazao mengine lakini *resources* nyingi za Taifa zielekezwe kwenye kipaumbele. Utaratibu huu ufanywe kwa mazao yote yawe ya biashara au chakula.

(iii) Kuhusu *Farm inputs,* Wizara itakapochagua *priority crops* ndipo itakapojua mahitaji ya pembejeo ambazo ni muhimu zipelekwe huko kwenye *priority crops.* Lakini napendekeza Wizara itoe kipaumbele kwenye *farm power and mechanization.* Mimi sizungumzii matrekta mapya wala majembe na *harrow* mpya, nazungumzia Bajeti ya ukarabati wa mashine tulizonazo. Kwa kuwa *inputs* nyingine kama vile mbolea na dawa za kilimo tayari zimechukuliwa na *private dealer*s au *stockiest,* napendekeza Bajeti ielekezwe kwenye *Agriculture Machinery Rehabilitation and Repair.* Napendekeza pia Wizara ibuni namna ya kuanzisha vituo vya *Farm Power Service Centres.*

(iv) Kuhusu *other charges* ya Wizara iendayo Wilayani, nashauri Bajeti ya *other charges (OC)* itumwe Wilayani kwa vigezo. Kwa mfano Wizara inaweza kuweka vigezo vya Idara ya Kilimo, Idara ya Mifugo, ukubwa wa eneo linalolimwa, wingi wa mifugo, ukubwa wa eneo linalomwagiliwa na kadhalika.

Ni vizuri Wizara ikatambua fedha za *OC* ndizo zinazowezesha Idara kufanya kazi Wilayani kwa sababu fedha za miradi ya wafadhili zinaambatana na masharti yake. *DALDO* hawezi akalipa umeme, simu na stampu kwa fedha za miradi ya wafadhili. Pia hawawezi wakashirikisha viongozi katika kampeni za kilimo na mifugo kwa fedha za miradi ya wafadhili. Nashauri Wizara isiwe inachelewa kupeleka Wilayani fungu hili la *other charges* kwa sababu Wizara inapochelewa kupeleka *OC* itambue inakwamisha utekelezaji wa mipango ya kilimo Wilayani.

(v) Kuhusu kilimo cha umwagiliaji. Kwa kuwa *scheme* ya umwagiliaji kwa sasa inatoa kipaumbele katika mambo makubwa matatu kama ifuatavyo:-

1. (a) *Presence of Traditional Irrigation;*
   (b) *Canals;* na
   (c) *Weirs* (mabanio)

2. *Dependency of Farmers on Irrigation and Scarcity of Rain.*

3. *Adequacy of Irrigation water.*

Naomba kushauri Wizara ya Kilimo na Chakula, ikubali katika programu yake ya *scheme* ya umwagiliaji kujumlisha vijiji vya Mwasa, Magulu/Kikundi na Rudewa Gongoni, Kata ya Rudewa Wilaya ya Kilosa na Kata ya Kidete.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji hivi vina sifa zote zinazohitajika katika *scheme programme* ya umwagiliaji. Vijiji vyote vina *traditional irrigation canals, weirs,* vina uhaba wa mvua na wakulima wake wanategemea kilimo cha umwagiliaji. Vijiji vyote vina *very high adequate irrigation water* na vina mabonde ya maeneo yenye ekari nyingi. Jambo zuri na linalovutia zaidi ni umwagiliaji wake unaotumia *gravity* na sio *pumps* kama ilivyo sehemu nyingine.

Nashauri Wizara ya Kilimo na Chakula, ikubali kujumlisha vijiji katika *scheme programme* ya umwagiliaji katika Bajeti ya mwaka 2003/2004 kwa sababu *all basic irrigation functions like economic functions, financial function and social function have already been started to be used.*

(vi) Kuhusu matumizi ya fedha za *STABEX* kuendeleza kilimo cha kahawa. Kwa kuwa matumizi ya fedha za *STABEX* katika mpango wa kuendeleza zao la kahawa umetenga shilingi bilioni 10 kwa ajili ya matengenezo ya barabara za Mikoa na za vijiji, naomba kushauri Wizara ya Kilimo na Chakula ikubali mpango huo wa matengenezo ya barabara za Mikoa na vijiji kwa maeneo yanayolima kahawa ujumlishe pia Mkoa wa Morogoro kwa sababu Mkoa wa Morogoro zao la kahawa linalimwa katika Wilaya zote kwa mfano Wilaya ya Kilosa zao la kahawa linalimwa kijiji cha Uponela, kijiji cha Mwisini, Kata ya Mamboya, kijiji cha Idete kata ya Chanjuru, kijiji cha Lumbiji Kata ya Lumbiji, Tarafa yote ya Nongwe na kijiji cha Luwemba Kata ya Kidete na Kijiji cha Mohwe Kata ya Msowero. Naomba Wizara ya Kilimo na Chakula isiwe na ubaguzi wa kuchagua maeneo kwa sababu nia ya mpango huu wa *STABEX* ni kukuza na kupanua kilimo cha kahawa katika nchi yetu.

(vii) Uendelezaji wa kilimo cha zao la mkonge. Ingawa ubinafsishaji ulibahatika kupata wawekezaji muhimu katika *Sisal Industry* Duniani kama vile *Wiggles Worth & Co. Ltd,* hii ni kampuni ya siku nyingi ya Kiingereza ina uzoefu mkubwa wa uuzaji wa mkonge na bidhaa zake na biashara nyingine kwa kipindi cha miaka 105 sasa na pia wamewekeza katika kilimo cha mkonge Kenya na pia wana hisa katika mashamba ya Amboni.

Mwekezaji mwingine aliyepatikana ilikuwa *DELOWE GmbH.* Kampuni hii inahusika na biashara ya utengenezaji wa mazulia kwa kipindi cha miaka 120. Hii ni kampuni ya Kijerumani, ni wasambazaji wakubwa wa *Sisal Carpets* nchi za *North America, Europe,* Japan na Asia pia wapo na ushirika na India, Romania na *Portugal* katika uzalishaji wa *natural fibre carpets* na *Geo-textiles production.*

Mwekezaji mwingine alikuwa *Grecian Investments (UK) Ltd.* Hii ni *British Company* wawekezaji hawa tarehe 13 Februari, 1998 walitia hisa 999,999 kati ya Hisa 1,000,000. Serikali ilibaki na *One Golden Share.* Pia walilipa malipo ya awali kama mkataba wao ulivyoelekeza. Baada ya kukaa kwa miezi 22 bila

kupata hati miliki wawekezaji hawa walijitoa. Jambo linalonishangaza mpaka sasa imepita miezi 64 bado hati miliki hazijatolewa na Serikali na hivyo kwa kipindi chote hicho bado hati miliki hazijapatikana.

Kwa kuwa sekta ya kilimo cha mkonge ni endelevu katika Pato la Uchumi wa Taifa letu na zao la mkonge ni *environmental friendly,* uchimbaji wa madini una ukomo pale madini yanapomalizika, Pato lake nalo linakwisha na kuacha uharibifu wa mazingira.

Kwa kuwa Serikali inatambua kuwa wawekezaji katika sekta ya kilimo cha mkonge walishindwa kusubiri kuwekeza katika sekta ya mkonge kwa sababu ya kukataliwa kupewa hati miliki, Serikali inaweza kueleza ni sababu zipi na vigezo gani walivyotumia kukataa kutoa hati miliki kwa wawekezaji katika sekta ya kilimo cha mkonge wakati Serikali hiyo imetoa hati miliki kwa wawekezaji katika sekta ya madini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hali ilivyo sasa inakuwa vigumu sana kuliendeleza zao la mkonge kwa mfumo wa zamani. Nchi kama Brazil, Mexico na China ambazo kwa sasa ndizo zinazozalisha mkonge kwa wingi duniani, zinatumia mfumo wa kushirikisha wakulima wadogo wadogo kulima mkonge. Kwa ajili hii, sisi kuendelea kubaki na uendelezaji mkonge kwa mfumo wa zamani bila kushirikisha wakulima wadogo wadogo tusipochukua hatua za tahadhari, zao la mkonge litakufa kabisa katika orodha ya mazao yetu ya biashara. Kwa ajili hii, naomba kupendekeza Wizara ya Kilimo na Chakula, iweke fungu na kuwa na mikakati ya kuhamasisha wakulima wadogo wadogo kushiriki katika kilimo cha zao la mkonge.

**MHE. PAUL E. NTWINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Kilimo na Chakula, kwa hotuba nzuri, nami nitaiboresha tu maeneo machache.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo ambalo nitamhoji Waziri ni lile la kusitishwa kwa zao la pamba Mkoani Mbeya hususani katika Wilaya ya Chunya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bajeti ya mwaka 2002 suala hili lilijitokeza na Waziri akatoa ahadi kuwa angepeleka Wabunge na watendaji waende wakaone nchi jirani wanafanya nini juu ya huyu mdudu *Red boll worm.* Napenda kupata majibu kwa nini Mheshimiwa Waziri, hajatekeleza ahadi hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa karne hii ya 21, mdudu huyu ambaye alikuwa tatizo hata *American, South Africa,* Zimbabwe, Malawi sio tatizo tena. Zipo mbegu *ginned seeds* na *genetic seeds* zilizotengenezwa mahsusi kuzuia mdudu huyu ndizo zinazopandwa kwa sasa na nchi hizo na hivyo kuondokana na tatizo la mdudu huyu. Sasa swali lini tutaruhusiwa kuanza kulima zao la pamba? Je, kuna tatizo gani la msingi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini kusiwe na maeneo mawili ya pamba ya kawaida na eneo lingine tulime zile mbegu za *genetic seed* au *ginned cotton seeds* tuangalie gharama zake? Bado sielewi kigugumizi kipo wapi? Je, Waziri huoni anawapa mateso ya bure wananchi kwa kuwakosesha fedha kwa kilimo hiki cha pamba? Wananchi wanangojea maamuzi ya Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri angeangalia upya tatizo hili na kulipatia ufumbuzi wa kudumu na hasa ukijua karibu miaka kumi imepita kwa wananchi kukatazwa kutolima zao hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kuhusu kilimo cha umwagiliaji. Jimbo la Songwe, tulipendekeza maeneo mbalimbali ya bonde la Songwe, eneo la Mbuyuni, Mwambani, Totowe na Itekenya yana mabonde mazuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tunalo Ziwa la Magadi pale kati ya Kanga, naomba sana Serikali ijaribu kutusaidia tulime mwani kule pia kama tunaweza kuwezeshwa kulima zao la michikichi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waziri akumbuke yeye na Wizara yake kuwa Jimbo la Songwe, wananchi wanalima kahawa eneo la *Ngwaza Mines.* Lakini barabara za eneo hilo ni mbovu sana toka Kapalala-Kininga kwenda Kininga. Naiomba Serikali ijaribu kutengeneza barabara kuelekea huko inakolimwa kahawa. Tuna imani fedha zilizotengwa kuboresha zao hilo zitaletwa Jimbo la Songwe Wilaya ya Chunya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiunga mkono hoja hii na bila shaka nitajibiwa swali la kulima pamba kule Chunya na Mbeya kwa ujumla.

**MHE. REMIDIUS E. KISSASSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kusema kuwa ninaunga mkono hoja hii na ni matumaini yangu kuwa sasa ni mwanzo mzuri wa kuleta mapinduzi katika kilimo. Hata hivyo naomba kuchangia machache kama ifuavyo:-

(i) Sielewi vigezo vilivyotumika kuwapa *Exim Bank* kuratibu fedha za Mfuko wa Pembejeo wakati kuna benki zenye mtandao mkubwa zaidi nchi nzima. Naomba maelezo.

(ii) Nashauri Serikali iagize kwa makusudi kuwa Benki zetu nchini zianze kutenga fedha maalum kuwekeza katika masuala ya kuendeleza kilimo na wafugaji. Hii itasaidia sana kushajiisha uwekezaji na kutoa mafunzo na ufanisi katika sekta hizi muhimu.

(iii) Wizara ya Kilimo za Tanzania na ile ya Zanzibar zishirikiane kwa karibu sana hasa katika kuhakikisha Maafisa Ugani wanapewa nyenzo (motisha na usafiri) ili waweze kufanya kazi zao vizuri zaidi. Pia napendekeza upandishwaji vyeo kwao uwe kwa kigezo cha ubora wao wa kutoa huduma kwa wakulima na wafugaji wao.

**MHE PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpongeza Mheshimiwa Charles Keenja, Waziri wa Kilimo na Chakula pamoja na Naibu wake, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara kwa maandalizi mazuri ya hotuba ya bajeti na kwa ufafanuzi wa kina wa hali ya chakula na maendeleo ya mipango ya kufufua kilimo nchini. Naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Serikali kwa uamuzi wake wa kuwapunguzia mzigo wa bei ya mbolea wakulima wa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini. Hatua hii itarejesha heshima ya awali ya *The Big Four* kwa uzalishaji wa chakula na hasa mahindi. Lakini bado naiomba Serikali itizame upya gharama na kodi/*VAT* ambazo zinasababisha bei ya mbolea kuwa juu sana. Hivi ni kwa nini mbole mfano Urea iuzwe hadi kufikia shilingi 18,000/= kwa mfuko wa kilo 50 wakati bei halisi mbolea ikifika bandarini huwa ni *USD* 155 kwa tani sawa na shilingi 8,060 kwa mfuko. Bila shaka zipo kodi na gharama nyingi ambazo zinaongeza hadi kufikia shilingi 18,000 au sehemu nyingine shilingi 19,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri, Mheshimiwa Waziri akachunguza hilo na kushauri Serikali iondoe baadhi ya kodi/*VAT* kwa mbolea ikiwa ni pamoja na *VAT* ya usafirishaji, vifungashio, gharama za *port handling, clearing and forwarding* na kadhalika. Nitaomba Mheshimiwa Waziri aeleze kwa undani hali halisi ilivyo na anavyolishughulikia tatizo hili. Tukitatua tu tatizo hili kutakuwa hakuna umuhimu wa kuomba ruzuku bali kupunguza mzigo wa kodi/*VAT* mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula, atusaidie wana Rukwa kwa kuendelea kupeleka fedha za kununulia mahindi ya *SGR*. Uamuzi huu una faida zifuatazo:-

(i) Kichocheo kwa wanunuzi binafsi kuongeza bei kwa mazao ya wakulima;

(ii) Kuimarisha *stocks* kwa ajili ya dharura toka Mikoa yaTabora, Shinyanga, Singida hadi Mwanza. Usafiri kwa njia ya treni ni rahisi kupitia Mpanda;

(iii) Kujiandaa wakati wowote Mkoa wetu ukiwa na njaa isiwe lazima kuleta chakula toka Makambaku/Dar es Salaam;

(iv) Kukifanya kitengo hiki kiwe na *Revolving Stock;* na

(v) Mwaka huu hali ya chakula kwa majirani zetu siyo mbaya kama mwaka jana hivyo kasi ya ununuzi siyo ya ushindani mkubwa kama ilivyokuwa msimu uliopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, tungeshauri pia Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula, aone uwezekano wa kuwahamasisha wafanyabiashara binafsi waanzishe vitengo vyao vya hifadhi ya chakula kinaposalia katika msimu mmoja hadi mwingine. Ni vizuri pia Serikali ikawawekea masharti nafuu ili wasije wakajikuta wanaingia gharama kubwa za kuhifadhi kwa ajili ya kodi/*VAT.* Pia ipo hoja ya kuimarisha *storage facilities* zilizopo katika maghala ya vijijini ili nayo wakati wa neema, wanahifadhi hata kidogo kwa maandalizi ya msimu wa baadaye. Vihenge kwa kila familia vipewe umuhimu wa pekee kwa hifadhi ya chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshauri Mheshimiwa Waziri aanze kufufua moyo wa watumishi wastaafu na vijana wa mijini kupenda kilimo kwa kuwatafutia maeneo ya kulima, sehemu zilizo karibu na Jiji la Dar es Salaam.

Naelewa mipango mizuri ya wananchi wenyewe bila kulazimishwa na Serikali kwenda kulima inaweza kupata msaada wa *UNDP, ILO, HABITATI, UNESCO, NIGP, FAO* na wengineo. Mfano wa mpango ulioanzishwa katika vijiji vya Kidunda; Nyani kwenye Wilaya ya Kisarawe *(along Uhuru Corridor)* kandokando ya Reli ya *TAZARA* ingeweza kujibu baadhi ya matarajio yetu ya kuendelea na upanuzi wa washiriki wa kilimo nchini. Wataalamu nao wasio na kazi wapewe baadhi ya maeneo ya mashamba wakaonyeshe utaalam wao kwa kuwasaidia nyenzo za kuanzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mashamba ya zao la zabibu kwa ajili ya wakulima wadogo wadogo Dodoma, inaonekana kuwa zao hili litakufa kutokana na ukosefu wa huduma muhimu za maji. Maji ya bomba hayawezi kutumika kwa umwagiliaji hivyo ni budi jitihada za makusudi zifanyike ili visima virefu na vifupi vichimbwe kila sehemu na wakulima waandaliwe utaratibu wa kuchangia gharama zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ni vizuri Mheshimiwa Waziri, akaendelea na juhudi zake za kuboresha hali na maslahi ya wataalam wote wa Wizara ili wachape kazi bila kinyongo. Mpango mzuri ulioandaliwa na Wizara hauwezi kutekelezwa bila ya maandalizi mazuri ya wahusika kuusimamia vizuri. Binadamu kila wakati anaweza kufanya mazuri zaidi na zaidi akipewa motisha ya kufanya hayo unayotaka afanye.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii na kuitakia kheri, fanaka na utekelezaji mwema wa dira yetu mpya ya kilimo kufikia 2025.

**MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wapigakura wa Jimbo la Jang'ombe, napenda kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Mkurugenzi pamoja na wataalamu wao wote kwa pamoja kwa kuweza kuandaa Bajeti yao hii inayoonyesha matumaini kwa wakulima wetu ambao wengi wao ni watu wanaotumia nguvu zao zaidi kuliko kutumia mashine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo ni uti wa mgongo kwa Taifa letu na ni kisaidizi cha hali ya juu kwa wananchi wetu kwa kuendesha maisha yao na kuweza kupata chakula chao, lakini bado Serikali juu ya jitihada zake za kukuza kilimo hatujafikia kiwango cha kusema sasa tunaweza kukidhi haja zetu kwa kutumia kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Serikali kwa kutoa uamuzi wa makusudi wa kusogeza pembejeo karibu na wananchi wetu kwani kusogezwa kwa pembejeo hizi ni njia moja na hatua thabiti zinazoonyesha kuwa sasa Serikali imeamua kweli kweli sio ile ya zamani kusema tu kuwa kilimo ni tegmeo letu lakini kuongeza nguvu za pembejeo ni ushahidi tosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, shida kubwa kwa wakulima wetu ni upatikanaji wa mikopo kwa wakulima lakini nashukuru kwa kupitia hotuba ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri inazungumzia kupatikana kwa Benki ya Wakulima, mimi nawapongeza na naomba Mwenyezi Mungu azma hiyo ifanikiwe kwani hiyo ndio njia moja ya kujikomboa.

Kuhusu utafiti, nashukuru Mheshimiwa Waziri katika Bajeti hii ametoa maelezo mazuri tu kuhusu utafiti na upatikanaji wa mbegu bora ambazo zitakuwa na uwezo wa kutoa mazao mengi na yenye ubora kuliko hizi zilizopo hii sasa inaonyesha wazi kuwa madhumuni ya kukuza kilimo kweli yamepewa umuhimu zaidi kuliko huko nyuma tulikotoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo machache, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Charles Keenja, Waziri wa Kilimo na Chakula, kwa hotuba yake nzuri sana inayoeleweka vizuri na yenye takwimu muhimu.

Aidha, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Profesa Pius Mbawala, Naibu Waziri wa Kilimo na Chakula, pamoja na Katibu Mkuu na watendaji wengine katika Wizara hiyo na mashirika yake kwa kumsaidia Waziri kwa ufanisi na kuijengea Wizara hiyo heshima kubwa humu Bungeni na naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, ninalo ombi moja, nalo linahusu Taasisi ya Utafiti wa Zao la Chai kwamba sasa waangalie wakulima wa eneo la chai la *West Usambara* ambalo bado kunufaika na utafiti kama ilivyo kwa wenzao wa Rungwe na Njombe.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, natoa shukrani zangu za dhati kwa kusaidia Morogoro Vijijini hususani Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki, kijiji cha Matuli, kwa kilimo cha umwagiliaji. Vikundi vimeshaanzishwa, mafunzo yamekamilika, bado uchimbaji wa bwawa Mto Matuli. Fedha iliyotolewa ya bwawa haitoshi, tunaomba iongezwe ili bwawa lichimbwe. Vikundi vyote vya Matuli na Kikondeni vina *Accounts* Benki nimewachangia 100,000 ni vikundi vitatu kila kikundi 47,600 tunasubiri sana hatua ya uchimbaji wa hilo Bwawa, naomba Katibu aje Matuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya njaa, Morogoro Vijiji, naomba msaada kujua bei ya mahindi ya hifadhi kwa gunia moja la kilo 100. Mimi nimeomba kibali cha tani 50 ili wanyabiashara wa Jimbo langu wafike kununua chakula na kuuza kwa bei nafuu eneo la njaa - Kidugallo, Tununguo Mkulazi, Mikese na Ngerengere.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya Mfuko wa Pembejeo, ninapongeza hatua ambazo mfuko huu umefikia na kuanza kutoa mikopo. Kama inavyoelezwa utaratibu wake hauko wazi sana. Ninaomba sana wajumbe wapya iwe kazi ya kwanza kuuweka mfuko huo uwe wazi kwa wote mfumo giza ulioko ndani ya mfuko huu upatiwe kandili ili wote tuwe na imani na mfuko huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukuwaji wa kilimo, kwa mtindo huu kilimo kamwe hakiwezi kukua kama Wizara hii haitakubali kubadilika kifikra, maoni, msimamo na mwelekeo. Tuige mfano wa Indonesia ambapo Serikali imeteua zao la biashara na kulisimamia Kitaifa siyo wazo lililotolewa la kuwa kilaWilaya kuteua zigizaga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kasheshe za mazao yaliokopwa na ushirika yamezua matokeo yafuatayo. Pamba sasa inapambanisha wakulima na viongozi wao na ufuta unawafuta wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, mashamba ya mkonge, ninaomba Waziri atoe tamko kwamba yale mashamba yaliyobinafsishwa tangu miaka ya tisini sasa waachie wananchi walime na agiza kesho kwa ma-*DC* wa maeneo hayo wagawe.

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama ya kulima, wanavijiji wanashindwa kulima kutokana na gharama ya matrekta kila heka moja kati ya 17,000 hadi 20,000. Hii bei ni ghali sana. Mafuta mbona yanapungua bei na matrekta yamepunguzwa bei, Idara ya Kilimo kila Wilaya iangalie bei za kilimo cha trekta kwa heka moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, shamba la mfano la Wizara ya Kilimo na Chakula liko Mkoa gani? Nasubiri majibu.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami naomba kuchangia mawazo katika lengo la kuboresha hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Kilimo na Chakula, 2003/2004 kwa njia ya maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwanza kutamka kwamba naunga mkono hoja. Aidha, nampongeza mtoa hoja, Mheshimiwa Charles Keenja, Waziri wa Kilimo na Chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo ni baba wa nguvukazi hapa nchini kwani zaidi ya 80% wanapata ajira na Watanzania wote wanaoishi mijini na vijijini wanategemea mazao ya kilimo kwa maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo hiki kinachogusa maisha ya Watanzania wote, kimsingi kinaboreshwa ipasavyo kinadharia tatizo liko katika utekelezaji wa matendo. Ninalisema hili nikizingatia Ibara za 10-11 ukurasa wa tano wa hotuba ya Waziri anasema: "Ukuaji wa kilimo mwaka 2002 haukufikia lengo la asilimia sita kutokana na kushuka kwa bei ya mazao makuu ya biashara hususani kahawa, pamba na chai..... Aidha, ili kilimo kichangie ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini kwa kasi ya kuridhisha, inabidi kikue kwa zaidi ya 10% kwa mwaka."

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba imeendelea kusema kwamba: "Hali hii mbaya inasababishwa kwa kiasi kikubwa na hali mbaya ya hewa hususani ukame, uwekezaji mdogo katika sekta ya kilimo... na matumzi madogo ya teknolojia."

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na Ibara hizo mbili, ninashauri Wizara iachane na mazoea ya kutuletea taarifa za matatizo bali tuelezwe juhudi zilizofanyika na matatizo waliyokumbana nayo na jinsi wavyojaribu kuyatatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Kagera ni wakulima wazuri na wachangiaji wa Pato la Taifa. Kwa miaka mingi, tangu bei ya zao la kahawa na chai ianguke, wananchi wa Kagera wamegubikwa na lindi la umaskini na kushindwa hata kuendesha maisha yao ipasavyo na kujiletea maendeleo. Nashauri kama inawezekana Kagera sasa tulime zao jipya la *Vanilla* ambalo soko lake ni kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ukame, nashauri Wizara itilie nguvu katika kilimo cha umwagiliaji mazao ya mboga mboga na matunda kwa kuwa yanakomaa kwa muda mfupi na yanalipa. Mkoa wa Kagera una maeneo mengi sana na mazuri ya kilimo yanayozunguka Mto maarufu Mkoani unaojulikana kama Mto Ngono una maji mwaka mzima. Bonde la Mto Kagera pia lifanyiwe uchunguzi, nashauri yaanze kufanyiwa kazi wakulima wako tayari.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna kilimo bora bila huduma za ugani, nashauri Wizara isomeshe wataalam wake na iwapeleke kule waliko wakulima na wafanye kazi kwa malengo yanayopimika. Huduma za ugani kwa wakulima hazipo. Aidha, wale wachache waliopo hawana malengo kwa hiyo, wapo wapo tu. Pia wataalam hawa wapewe zana za usafiri, teknolojia itatumikaje kwa mtu asiyeweza kufikia walengwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, mazao yetu sasa yasindikwe. Serikali na wale wakulima hawawezi kuongeza Pato la Taifa wala kupata faida na ndoto ya ziada kufikiwa pasipo kuuza mazao yetu yakiwa yamesindikwa, mazao ghafi hayana faida na huharibika haraka.

Mwisho, naupongeza Mkoa wa Kagera kwa kuwa miongoni mwa Mikoa inayojitosheleza kwa chakula mwaka 2003/2004, Wilaya zote za Muleba, Biharamulo, Ngara, Karagwe na Bukoba, zina chakula cha kutosha, napongeza viongozi na Mungu awatie nguvu.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia kusema kwamba naunga mkono hoja.

**MHE. FRANK M. MUSSATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Kasulu Mashariki, Mkoani Kigoma, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Aidha, napenda kutoa hongera kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wafanyakazi wote wa Wizara kwa kazi nzuri waliyoifanya katika mwaka 2002/2003.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba yafuatayo yazingatiwe ili Wizara yako iongeze tija katika mwaka 2003/2004, nayo ni:-

Kwanza, ni kuhusu usambazaji wa zana za kisasa za kilimo. Wakulima hapa nchini bado wanatumia jembe la mkono kwa kulimia. Serikali lazima ichukue hatua za makusudi kuwakopesha na hivyo kuwawezesha wananchi kupata matrekta yenye bei nafuu hata yale ya kusukumwa kwa mikono. Hatua hii ichukuliwe hasa kwa Mikoa kama Kigoma na Tabora ambayo ardhi ya kilimo ipo ya kutosha na haihitaji mbolea na hali ya mvua bado inaridhisha.

Pili, uanzishaji wa Benki ya Kilimo, Serikali inashauriwa kuanzisha hivi sasa Benki ya Kuhudumia Wakulima ili waweze kukopa fedha kwa ajili ya kununulia zana za kisasa kama matrekta na pembejeo za kilimo. Benki zilizopo haziwasaidii wakulima kwani zinawalenga wafanyabiashara. Kwa sababu *NMB* ina mtandao mkubwa nchini kote basi itakuwa vyema kama Benki hii itapewa jukumu la kushughulikia masuala ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu ni kuhusu usindikaji wa mazao ya kilimo, Wizara isimamie usindikaji wa mazao ili kuyaongezea thamani. Katika maeneo mengi ya nchi matunda kama machungwa, maembe na mapapai yanaoza kwa kukosa soko na namna ya kuyasindika. Wizara inawasaidiaje wakulima wa Kasulu ambao wana miwa mingi isiyokuwa na mnunuzi? Ihimize uanzishaji na uendelezaji wa viwanda vidogo vidogo chini ya *SUDECO* vya kutengeneza sukari. Aidha, mazao kama nyanya, vitunguu na tangawizi ambayo yanazalishwa kwa wingi Wilayani Kasulu yasindikwe na viwanda vidogo vidogo vya wakulima wadogo.

Mhehsimiwa Naibu Spika, nne, huduma za ugani. Hivi sasa huduma hizi ni duni sana au katika maeneo mengi hazipo kabisa. Wizara lazima ihakikishe huduma hizi zinaboreshwa na matokeo ya tafiti mbalimbali yanawafikia wakulima ili waweze kuongeza uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, masoko ya mazao. Wizara yako inatakiwa ishirikiane na Wizara ya Ushirika na Masoko kuwatafutia wakulima masoko ya mazao yao vinginevyo wakulima wakikosa soko hukata tamaa na kuacha kuzalisha zao ambalo halinunuliwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. MOHAMED A. ABDULAZIZ:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

1. Serikali ionyeshe nia ya kweli ya kukifanya kilimo chetu kiwe cha kisasa.

2. Hali ya wakulima wetu ni mbaya, hawana mikopo hawapati pembejeo kwa wakati na zikipatikana bei zipo juu sana. Hivyo wakulima hawapati tija nzuri.

3. Huduma za ugani ni dhaifu. Wizara isaidie zana za usafiri kwa Maafisa wa Ugani katika Vijiji vyote.

4. Hali ya hewa ya mwaka huu haikuwa nzuri. Hivyo katika maeneo mengi mavuno hayakuwa mazuri.

Katika jimbo langu la Lindi Mjini hali ni mbaya. Maeneo ya Vijijini Kingeng’ene, Mtange, Tulieni, Kitumbi Kwela, Hyato, Kitunda, Mayani na Mitwero hali si nzuri. Zipo dalili zote kwamba watahitaji msaada wa chakula cha kazi katika kipindi kifupi kijacho. Naishauri Serikali kufanya maandalizi ya mapema.

Mwisho, naomba masharti ya mfuko wa pembejeo yatazamwe upya ili kuwarahisisha wakulima kupata mikopo hiyo kwani hivi sasa mikopo hiyo inatolewa kwa kufuata masharti ya biashara na inawawia vigumu wakulima kupata mikopo hiyo.

**MHE. LEPHY B. GEMBE:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula kwa hotuba yake, na nianze kwa kuunga mkono hoja mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mimi ninatoka Mkoa wa Rukwa hususan Jimbo la Mpanda Kati; nimefarijiwa sana na Bajeti ya mwaka huu kwa sababu imegusa, tatizo sugu ambalo wananchi wengi wamekuwa wakilipigia kelele. Suala zima la kilimo; zana na pembejeo za kilimo.

Mheshimiwa Spika, ni kwa muda mrefu hii imekuwa kero, kwamba Serikali ingetakiwa iwawezeshe wakulima na hasa wakulima wadogo kwa punguzo la bei ya zana pamoja na pembejeo za kilimo.

Mheshimiwa Spika, rai yangu ni kuwa Serikali imefanya vizuri kupunguza bei na kutoa ruzuku kwa baadhi ya mikoa, Rukwa ukiwa mmojawapo. Ombi langu kwa Serikali ni kwamba naomba uwekwe utaratibu mahsusi, namna gani mbolea hiyo itakavyomfikia na bei gani, na mkulima aelewe kuwa Serikali imemsaidia nini. Hapa nina maana ile margin ieleweke na iwe wazi; na mbolea hiyo imfikie mkulima huyu mapema kabla ya msimu kuanza.

Katika suala la mkoa kuchagua zao la biashara na zao la chakula, hili nalo ni jambo jema, lakini niiombe Serikali kuwa ifanye utaratibu wa kuwataka Mabwanashamba walioko Vijijini kuwa kila siku wafanye kazi yao, kwa sababu vinginevyo itakuwa si rahisi kutekeleza hili, kwa sababu wakulima wetu wamezoea kilimo kile kwanza kuchelewa kupanda, kupalilia, kuvuna na kadhalika. Hivyo Maafisa kilimo wakifanya kazi sambamba na wakulima kwa kuzingatia. Misingi ya kilimo bora itasaidia kuvuna zaidi na hatimaye kumuondoa mkulima huyu kwenye umaskini.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali, iangalie upya suala la matumizi ya fedha, fedha nyingi zinatumika kwa ajili ya gharama za uendeshaji wa Ofisi, nadhani kutoka huko tuelekee kumlenga mkulima, kwa sababu fedha nyingi zimetumika kwa ajili, semina, magari ya kifahari, posho ya kujikimu na kadhalika. Unakuta fedha karibuni asilimia 85 imetumika kwa shughuli za uendeshaji kinachokwenda kwa mlengwa ni sawa na hakuna. Hivyo naomba Serikali ibadilike itoe kipa umbele kwa mkulima kuliko hivyo ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, nadhani yakizingatiwa haya yatabadilisha hali ya uchumi wa nchi yetu. Ahsante sana.

**MHE. JOHN E. SINGO:** Mheshimiwa Spika, kwanza naunga hoja mkono na kumpongeza Mheshimiwa Waziri, ndugu yetu Charles Keenja - Waziri wa Kilimo na Chakula. Pamoja na pongezi hizo ninao mgogoro mkubwa na Wizara hii kwa jinsi ambavyo imeshindwa kushiriki maendeleo ya kilimo Wilayani Same. Kila mara nimeliongea hili Bungeni mwaka wa fedha 2001/2002 na 2002/2003 bila mafanikio yoyote. Pembeni na kuliongea Bungeni nilimwandikia Mheshimiwa Waziri mara mbili kuhusu kero hii na namshukuru Waziri kwa uamuzi wake wa kuja kutembelea Wilaya ya Same japo kwa muda mfupi sana wa siku moja. Hii ni kwa sababu Wilaya ya Same ni kubwa mno kwa kutembelea maendeleo ya kilimo kwa siku moja. Wilaya ya Same ndiyo Wilaya kubwa sana Mkoani Kilimanjaro. Mgogoro wa pili na Bajeti hii ni uamuzi wa Wizara kuitenga Wilaya yote kama Wilaya kame inayostahili kilimo cha ukame pekee! Ni kweli yapo maeneo kame kama Same, Njoro, Makanya, Mwembe na Hedaru. Lakini sio kweli kuwa maeneo haya hayafai kilimo, Wizara iyasaidie maeneo haya na kuwawezesha wananchi kulima kilimo cha mazao yanayostahili ukame kwa njia za kisasa za kuvuna maji ya mvua katika mabonde ya maeneo haya niliyoyataja.

Mgogoro wa tatu ni Wizara kukataa kutambua kuwa Wilaya ya Same inayo maeneo mengi ya kilimo cha umwagiliaji kwa kutegemea mito ya kudumu ya Pangani, Nakombo, Yangoma, Saseni na Hingilili. Mito hii ina maji mengi ya kilimo cha umwagiliaji katika kata za Ruvu, Makanya, Hedaru (Mto Pangani), Kisiwani (Mto Nakombo) Gonja (Mto Yongoma) na Ndungu (Mto Hingilili), Kihurio na Bendera (Mto Saseni). Ni kwa sababu gani Bajeti ya Wizara ya Kilimo haikutenga hata mradi mmoja wa kilimo cha umwagiliaji Wilayani Same? Katika ukanda wa milimani *(Highlands of Same District)* yapo maeneo mazuri ya kilimo cha umwagiliaji kwa kuvuna maji ya mito midogo midogo na chemichemi za msituni kwa "Ndiva". Kilimo cha "Ndiva" au *"Traditional small water dams"* ndicho kilimo cha

umwagiliaji katika milima ya Same. Tunaomba Wizara ikitupie macho na kutoa msaada kwa kuwawezesha wananchi ili wakilime kwa teknolojia ya kisasa.

Mwisho, nihitimishe mgogoro wangu na Wizara ya Kilimo kwa kumwomba Mheshimiwa Waziri wa Kilimo atumie ukakamavu na ujasiri wake wa kuinusuru Wilaya ya Same ili isiharibikiwe kiuchumi, kwa kuwa na maendeleo duni katika sekta ya kilimo. Kwa maana nyingine namwomba Mheshimiwa Waziri atupatie walau miradi miwili ya kilimo cha umwagiliaji kule katika Bonde la Makanya na Kisiwani alipopatembelea hivi karibuni. Namwomba pia atume wataalamu wake katika bonde la umwagiliaji la Mto Pangani (maeneo ya Kata za Ruvu, Makanya na Hedaru); Mto Makombo (Kisiwani), Mto Yongoma (Gonja) na Bendera). Hatimaye namwomba apange ziara nyingine ya siku 2 au 3 ili aweze kuona maeneo ya kilimo cha umwagiliaji nilichokitaja. Pasipo kuendeleza kilimo cha umwagiliaji Same, wananchi wa Same watakosa imani ya Serikali yao ya CCM walioichagua bila kuwa na "Chuya" hata moja. Hivyo naiomba Serikali iliangalie hili kwa makini na kudumisha imani ya wananchi wa Same kwa Serikali yao ya CCM.

Mheshimiwa Spika, namalizia tena kwa kuunga hoja mkono kwa matumaini kuwa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo ataufanyia kazi ushauri nilioutoa hapa na hivyo kuepuka mgogoro wa kukataa hoja ya Wizara yake siku zijazo.

**MHE. COL. FETEH SAAD MGENI:** Ninampongeza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula, Naibu wake, Katibu Mkuu pamoja na watendaji na wataalamu wake wote kwa kazi nzuri ya hotuba yenye mipango mizuri ilioelekezwa kwa manufaa ya wananchi. Ninaanzia kuchangia kwenye kifungu cha upungufu wa chakula. Kwanza ninakubaliana na Mheshimiwa Waziri katika hatua ambazo amezipanga kuchukua katika taarifa yake ukurasa Na. 13 kuanzia kifungu (a) hadi (c).

Mheshimiwa Spika, ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri asilionee aibu kabisa suala hilo kwani Taifa kuwa na njaa ni aibu sana, suala la ombaomba ni fedheha hasa kwa Taifa kama hili kubwa. Njaa kwa nchi kama hii ni aibu kubwa, imani kwa wananchi wetu haitakuwepo hata kidogo na maana yake Taifa tunalipoteza, hivyo kwanza tuondoe njaa na wananchi washibe ndio imani inakuwepo.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni kilimo cha biashara lazima tuwe wakali katika kusimamia kilimo cha biashara na kwani hali ya uchumi wetu uko kwenye kilimo ndio maisha yetu. Kilimo ndio njia kuu ya uchumi wa Taifa letu. Pamoja na juhudi, hizo ambazo tuna nia ya kutaka kuyafanya kwa bidii lakini lazima tuyaangalie sana mambo yafuatayo:-

1. Lazima tuhakikishe kwamba tunakwenda na hali ya kitaalamu kabisa na sio kubahatisha;

2. Lazima tuhakikishe kwamba tumepata zana za kisasa za kilimo tuondoke kwenye jembe la mkono na la mkokoteni wa ng'ombe;

3. Tuhakikisha pembejeo zimefika kwa wakati kwa wakulima na itumiwe kitaalamu kabisa;

4. Tuhakikishe mbegu zetu ni nzuri na zenye uhakika wa kuleta mazao mazuri na yenye ushindani katika masoko;

5. Lazima wataalam wetu wabakie vijijini na wawasaidie vya kutosha wakulima wetu, wakubali kwamba wataalam hao ni sehemu ya wanavijiji;
6. Lazima wataalamu wetu wapatiwe vifaa vya usafiri na zana zinazostahili kwa kuboresha kazi zao.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango wangu huo ninaomba kusema kwamba ninaunga mkono hoja ya Waziri wa Kilimo na Chakula asilimia kwa mia. Ahsante sana.

**MHE. KARIM SAID OTHMAN:** Mheshimiwa Spika, napenda nami kushiriki katika kuchangia hotuba ya Waziri wa Kilimo na Chakula.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula aanze utaratibu wa kusafirisha matunda kupeleka nchi za Falme za Kiarabu, kwa yale matunda ambayo tunayo nchini petu kwa wingi, na kwa sababu hivi sasa sio rahisi kuanzisha viwanda vya kusindikia matunda hayo, kwa sababu ya ukata wa nchi yetu. Mimi binafsi nilikwenda kutembelea nchi tano za Falme za Kiarabu na nikapata nafasi ya kuona masoko ya nchi hizo, nilichogunuda ni kwamba baadhi ya matunda kwa mfano machungwa, mananasi na maembe yamefanana na ya kwetu Tanzania, lakini yamefungwa vizuri kwenye maboksi maalum ambayo yanaonyesha nembo ya bidhaa kutoka Kenya.

Nilipata nafasi ya kumwuliza kijana mmoja ambaye ni ajenti wa upokeaji wa matunda aliniambia kwamba baadhi ya embe ni kutoka Unguja na Pemba (Embe muyuni na boribo), mananasi ni kutoka Kibaha na machungwa ni kutoka Muheza Tanga. Matunda haya ya Tanzania wafanya biashara wadogo wadogo huyasafirisha na kuyapeleka Kenya. Wafanyabiashara wakubwa wa Kenya huyasafirisha katika nchi za Falme za Kiarabu kama ni bidhaa kutoka Kenya. Naiomba Serikali ifanye utafiti wa hili ili kuwapatia soko wakulima wetu pili kuondoa aibu ya nchi nyingine kunufaika kwa uchumi wetu. Pia naiomba Serikali ifanye kila mpango baada ya miaka miwili iwe imepata angalau viwanda vitatu vya kisasa vya kusindika matunda, kimoja kijengwe (Kipatimu Kilwa), (Muheza Tanga) na kingine (Morogoro)

Ni aibu Watanzania kunywa juisi ya embe (Maaza) inayoagizwa kutoka Oman, wakati embe za kutengenezea juisi hiyo zinatoka Tanzania. Namwomba Mheshimiwa Waziri atembelee Kipatimu, Muheza, Kibaha ajionee jinsi matunda yanavyopotea ovyo kwenye miti na namna ambavyo wakulima wanavyopata hasara. Machungwa ambayo kwa wastani yauzwe moja shs. 30/= basi huuzwa kwa mapakacha kwa bei ya kutupa.

Mheshimiwa Spika, wazo langu lingine ni kuhusu ukulima, kilimo ni uti wa mgongo wa Tanzania nchi yetu, lakini Serikali haijatoa mkazo wa kutosha katika kilimo. Kwa sababu uwezo wetu wa kiuchumi ni mdogo basi ningeiomba Serikali ikatilia mkazo zaidi katika kilimo cha wakulima wadogo wadogo. Serikali iwekeze kwa wakulima kwa kuwapatia mambo yafuatayo bure. Mbegu, mbolea, matrekta, maplau, maksai, wataalam madawa; mambo haya yote kuyatoa bure ni gharama kubwa lakini ni kuwekeza wataalamu wakishirikiana vizuri na wakulima basi mambo matatu yatatokea (a) mwenye uwezo wa kulima ekari mbili chini ya mpango huu atalima kumi, (b) mkulima atapata chakula cha mwaka mzima na ziada ya asilimia themanini (80%) atauza atapata fedha. (c) Serikali itapata faida ya kuwa wananchi wake hawana njaa wana fedha za kutosha za matumizi, mkulima, atachangia bila kulazimishwa maendeleo ya elimu, afya, maji, umeme na kila kitu cha maendeleo bila bughudha wala manung'uniko kwa sababu Serikali imemwezesha. Huu ndio uwekezaji kwa wakulima, utaratibu huu ndio unaofuatwa na nchi kama China, Japan kwa wakulima wadogo, ingawa ni mpango unaohitaji fedha nyingi lakini tujaribu japo mkoa mmoja kwanza Mungu atatuwezesha.

Mheshimiwa Spika, Wachina wanalima kwenye miamba ya mawe, wanavunja mawe, wanachukua udongo kwa magari kutoka sehemu nyingine ya nchi na kufikia miamba, hulima na mazao wakapata. Wajapani wanalima kwenye milima mikubwa, wanaikata milima hiyo kwa ukulima unaoitwa *(tiresing)* wanalima na wanapata mazao. Wachina na Wajapani ni marafiki zetu kwa nini tusiwaombe wataalamu hawa wakatusaidia kulima ardhi yetu ambayo si ya miamba wala milima ni ardhi yenye rutuba ya kutosha. Tuwaombeni wawekeze kwenye mashamba badala ya kutupa msaada wa shilingi tano za kijungu jiko!. Wizara hii ni kubwa ingestahiki iwe na Manaibu angalau wawili. Ahsante.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia kwa mia. Kwanza kabisa niwapongeze Mawaziri wote wawili kwa hotuba nzuri, pia na wataalam wote walioshiriki kuandaa.
Baada ya kumpongeza naomba nichangie, sehemu ndogo katika hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Utafiti, vyuo vilivyopo tangu zamani ningeshauri vipewe fedha nyingi ili viweze kuimarika na kutoa mafunzo mazuri kama vile Chuo cha Utafiti Tumbi - Tabora, Chuo cha Utafiti Uyole - Mbeya ni mfano wa kuigwa.

Mheshimiwa Spika, ukarabati wa vyuo hivyo ni muhimu ili kuweka mazingira mazuri kuna wanachuo na walimu wao na kupata mvuto kwa wanafunzi wanaomaliza masomo ya Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Spika, ushauri/ombi kwa kuwa Mkoa wa Tabora una uzoefu wa muda mrefu kwa kilimo cha Mpunga Wilaya ya Igunga nilikuwa niiombe Wizara iangalie uwezekano wa kuwakopesha Wanawake na kuendeleza kilimo hicho.

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Hata hivyo napenda kuongezea jambo moja la ziada baada ya kuwasilisha ya awali.

Kilimo cha Umwagiliaji: pamoja na kuwa jimbo langu lipo mjini, bado kilimo cha umwagiliaji ndiyo nguzo kubwa ya kulisha watu zaidi ya 300,000 ya wakazi wa jiji la Mbeya.

Zipo hekta 200, bonde la Uyole, ambalo linamilikiwa na wana ushirika wa Umwagiliaji bonde la Uyole, na tayari wamemiliki eneo hili kwa ajili ya Kilimo. Naomba sana Wizara isaidie kuimarisha Kilimo cha Umwagiliaji Mbeya Mjini hususan Bonde la Uyole. Wakulima wasaidiwe mikopo na ujuzi wa kuyatega maji ili yafaaye zaidi. Naunga mkono hoja.

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii mia kwa mia. Naipongeza hotuba hii ya Waziri wa Kilimo na Chakula. Natoa ushauri ufuatao :-

1. Kuchimba mabwawa kwenye maeneo ambayo yana mvua zisizo na mvua za kuaminika ili wananchi wayatumie kwa kilimo cha kumwagilia hasa katika Mkoa wa Dodoma.

2. Maji ya Mzakwe kwa sasa ni mengi ila nashauri yafanyiwe utafiti na uwezekano wa kupunguza gharama ili yatumike hata kwa kumwagilia

3. Kitengo cha kuzalisha mbegu bora kingerudishwa ili tupate mbegu bora kwa manufaa kwa wananchi. Naunga mkono hoja.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri nakupongeza wewe, Naibu Waziri wa Kilimo na Chakula, Katibu Mkuu na Watendaji wengine wote kwa kweli hotuba yako ni nzuri na yote yaliyoandikwa yakitekelezwa tutakuwa tumejikomboa upande wa kilimo.

Mheshimiwa Waziri tatizo lililopo sasa hivi ni njaa. Nakuomba sana chakula cha kutosha cha kununua kipelekwe kwenye maeneo husika ikiwepo Wilaya ya Iramba na hasa Iramba Mashariki.

Mheshimiwa Waziri napongesa sana *IFAD* kwa kazi nzuri inayofanya kwa kuanzisha miradi ya umwagiliaji Maji. Wananchi wa Iramba Mashariki - kata ya Mwangeza wamefurahi sana kupatiwa mradi wa umwagiliaji maji. Vile vile tunaomba miradi kama hiyo ianzishwe maeneo mengine ya Iramba Mashariki ili uweze kuwakomboa wananchi wetu. Naunga mkono hoja hii mia kwa mia.

**MHE. DAMAS P. NAKEI:** Mheshimiwa Spika, Naipongeza Serikali kwa mikakati mbalimbali ya kukabiliana na tatizo la ukame. Ni vizuri maagizo/maelekezo ya Mheshimiwa Rais wa Nchi yakatekelezwa ipasavyo kama yalivyoainishwa katika ibara ya 18.

Katika ibara ndogo ya (3) kuhusu kuvuna maji ya mvua na kuyatumia kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji maji, mimi ninaamini eneo hili linahitaji *input* kubwa kutoka Serikalini. Ningependa naishauri Serikali ianze operesheni maalum ya kuchimba mabwawa na/au malambo makubwa na madogo kwenye mito na mabonde yenye *Catchment Area* kubwa ya kutosha. Kazi hii inahitaji *machinery* mitambo mikubwa. Serikali ituambie kwa nini operesheni hii isiwezekane katika mpango wa muda mfupi na muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, sambamba na jitihada za kilimo cha umwagiliaji naishauri Serikali itoe elimu ya kutosha kwa wakulima wadogo na wakubwa kuhusu kilimo cha Nyanda kame - *Conservation Tillage* - kilimo cha tindo ambapo hardpan ya ardhi inavunjwa na maji kupenya na kukaa ardhini kwa muda mrefu zaidi. Kwa wale wachache walio - *adopt* kilimo hiki Wilayani kwangu Babati kumekuwa na mafanikio makubwa. Ningependa kufahamu mafanikio ya kilimo hiki kwingineko nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kahawa, napenda kuipongeza Serikali kwa azma yake ya kusimamia na kuendeleza mazao makuu ya biashara. Napenda kutoa dukuduku langu na la wananchi, wapiga kura wangu wa jimbo la Babati Magharibi kuhusu zao hili la kahawa kama ilivyoelezwa katika aya ya 136. Serikali inasema: "Juhudi zitaelekezwa katika kufufua ushirika, husuan vyama vya msingi, na kusisitiza usimamizi ili kuepusha upotevu wa fedha na raslimali za wanachama."

Sasa mimi nataka kufahamu; na wakulima wa kahawa wa Mlimani *Farmers Co-operative Society* wanataka kufahamu - wamenituma, nini hatima ya migogoro wao na *M/S Balton Tanzania Limited.* Mgogoro wa muda mrefu tangu mwaka 1998/99 unaohusu dawa ya *"Pyrnex 48 EC"* - dawa iliyoua kahawa yao.

Mheshimiwa Spika, utafiti/uchunguzi ulikwishafanyika na kuthibitisha kuwa dawa hiyo ilihusika kuua kahawa yao wakati. Wanachotaka ni fidia tu - ni haki yao. Naomba Serikali itufahamishe nini hatima ya hili - haki ya wanaushirika hawa kulipwa fidia - tupate ufafanuzi - ni muda mrefu sasa, hali inakatisha tamaa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Pareto, wakulima wa zao hili katika jimbo langu wamejikuta wanaingia kwenye matatizo ya kukatwa fedha zao wakati wanauza Pareto yao. Makato ya mauzo pareto yao yanafanywa na Bodi ya Pareto. Wakulima wanaona Bodi hii ya Pareto imedandia katika suala zima la soko la zao hili katika Kanda ya Kaskazini. Wakati wakulima wa Wilaya za Babati (Tarafa ya Bashanet) na Mbulu na kwingineko Kanda ya Kaskazini walipokuwa wanafufua zao la Pareto Bodi ya Pareto haijawahi kuonekana huko kusaidia ufufuaji wa zao hili, kwa namna yoyote.

Mheshimiwa Spika, lakini leo baada ya wakulima hawa kuhangaika wenyewe na kujipatia soko lao dogo - kwa mnunuzi binafsi aliyeko mjini Arusha, Bodi inawahi pale kuwakata fedha, zao - kama shs. 30/= kwa kilo bila ridhaa yao!. Ibara (para) ya 138 inadhihirisha kuwa bodi hii ya Pareto ni ya huko Kusini Wilaya ya Makete, na kadhalika. Naomba maelezo kuhusu Bodi hii, uhusiano wake na wakulima wa Pareto wa Bashanet - Babati, Mbulu na kadhalika na hususan kukatwa fedha zao, wakulima, bila ridhaa yao.

Mheshimiwa Spika, mwisho naunga mkono hoja hii asilimia mia moja nikiamini Serikali/Wizara itatoe maelezo kwa ajili ya wakulima wa maeneo yangu ya uwakilishi.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri na Naibu Waziri wa Kilimo na Chakula, Katibu Mkuu na watumishi wa Wizara kwa kuja na Hotuba nzuri. Naiunga mkono na kupendekeza yafuatayo ili kuboresha.

Kukosekana kwa matumizi madogo ya teknolojia ndio kunako didimiza kilimo Tanzania. Hata tukafanya nini, kilimo cha jembe la mkono hakitatufikisha mbali. Napendekeza Serikali iwe na mpango maalum wa kuwa na vituo vya matrekta, power tillers na kadhalika ili kuwezeshwa wananchi wakodi na kulimia katika mashamba yao. Kukodisha huko kuwe na malipo ya awali *(advance)* ili kuhakikisha huduma hiyo inalipiwa. Katika kituo hicho kuwe na gereji ya kuhudumia vifaa hivyo vya kilimo na kufundisha wakulima juu ya utunzaji wa vifaa vya kilimo. Mafunzo hayo hatimaye yawezeshe wakulima kununua vifaa hivyo wenyewe na kuvitumia.

Maafisa Ugani *(Extension officers)* mafunzo yao yaende na wakati. Hivi sasa ipo haja ya kuwafundisha zaidi matumizi madogo ya teknolojia ili wanapokwenda vijijini waweze kufundisha wakulima juu ya teknolojia hiyo. Maafisa Ugani wetu hawatusaidii kuleta Mapinduzi ya kilimo, wao bado wanaendeleza kilimo kile kile cha zamani ambacho ni lazima tukibadili tukitaka mabadiliko. Vijijini Maafisa Ugani wao wenyewe wawe ni mfano bora wa kilimo cha kisasa kupitia mashamba yao. Maafisa toka Wilayani wawe wanakagua mashamba ya binafsi ya Maafisa/Ugani vijijini kama sehemu ya kazi yao na kuitolea ripoti.

Kuhusu upungufu wa chakula, Wilaya ya Masasi ni mojawapo iliyoathirika na ukame hivyo kuna upungufu mkubwa wa chakula. Kitengo cha Maafa cha Waziri Mkuu kimetenga tani 1,407 toka mwaka jana lakini mpaka leo chakula hiki hakijapelekwa Masasi. Kisingizio ni kuwa hakuna fedha za kulipia

usafiri kupelekea chakula hicho. Mheshimiwa Waziri masuala ya umangimeza namna hii yataongeza hali ya njaa nchini pamoja na uwezekano wa chakula hicho kuoza katika maghala yenu wakati watu wanakufa njaa. Nalileta suala hili kwako ili muwasiliane Kiwizara ili kuondoa matatizo ya aina hii kabla njaa haijaanza kwa nguvu.

Suala la umwagiliaji maji kama lilivyo katika hotuba yako siridhiki nalo. Sioni jitihada za makusudi kushirikisha eneo kubwa la Mikoa ya Kusini ambayo lina maeneo makubwa ya kumwagilia toka Mto Rufiji, bonde la Mto Matandu, Mbwemkuru, bonde la Mto Lukuleti (Masasi + Lindi Vijijini) na Ruvuma. Kama kuna misaada ambayo Wizara inapata toka kwa wafadhili, ya kufanyia upembuzi yakinifu mbona katika miaka hii 40 ya uhuru sijaona makusudio ya kutumia maji haya mengi yanavyopotea kwenda baharini. Kwa nini miradi yenu inajigubika zaidi katika vianzo vya maji vidogo vidogo na kuacha maeneo yanayoweza kulisha Tanzania yote.

Kuhusu uhamasishaji wa sekta binafsi kuendeleza viwanda vya kusindika mazao ya kilimo, pia naona hakuna msukumo toka Wizara yako kuendeleza teknolojia rahisi ya kubangua korosho, ambayo inaweza kuwahusu mamilioni ya watu wa Mikoa ya Kusini. Mbona India kuna vijiji vingi vinabangua korosho kwa kutumia viwanda vidogo vidogo na teknolojia na hivyo kubangua kiasi kikubwa cha korosho. Kwa nini Tanzania haifuati mifano hii na badala yake kutumia fedha nyingi kukarabati viwanda vya zamani. Kwa taarifa, Kiwanda cha Masasi na Kibaha ingawaje vimekarabatiwa kwa mamilioni ya fedha, hakuna uzalishaji wa korosho wa maana uliofanyika. Yamejaa matatizo kibao. Kwa hali ilivyo Waziri Hatuwezi kufika. Anzisheni viwanda vidogo vidogo, na kwa upande wa Masasi wananchi tumewaandaa lakini msukumo wa kuwasaidia toka Wizara yako haupo. Waziri umesema maeneo yote yaliyolimwa muhogo hayana upungufu wa chakula. Kwa ukame wa mwaka huu uliotokea Masasi usemi huo sio sahihi. Nimeona mwenyewe mihogo imekauka mashambani na mihogo mingine ina mizizi tu bila kuwa na Nyama ambayo ndiyo ingekuwa chakula kwa binadamu. Kwa hiyo muhogo nao ukishambuliwa na ukame wa kuzidi hauwezi kusaidia upungufu wa chakula.

Mheshimiwa Waziri, mwisho, naunga mkono hoja bali nitashukuru endapo katika utekelezaji mtazingatia mawaidha haya kidogo niliyowaletea kwa maaandishi.

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hotuba ya Waziri wa Kilimo na Chakula Mheshimiwa Keenja asilimia mia moja. Ninampongeza Waziri kwa hotuba nzuri. Pia nampongeza Naibu Waziri Mheshimiwa Prof. Mbawala pamoja na wataalam husika waliokamilisha hotuba hiyo.

Pamoja na mipango mizuri iliopo katika Bajeti ya kilimo kwa mwaka 2003/2004 napenda kumtahadharisha Mheshimiwa Waziri kwamba kwa baadhi ya maeneo yetu kufanikiwa kwa kilimo kunahitajika mikakati ya namna ya kudhibiti wanyamapori ambao ni tishio kwa usalama wa wakulima pamoja na mazao wanayolima. Pia wanyamapori ni tishio hata kwa wataalam wa kilimo kama hawatapata usafiri wa uhakika katika kufuatilia utekelezaji vijijini. Napenda kutoa mfano wa jimbo langu la Liwale lenye eneo la 39,000 *kms.* ambalo asilimia 53 ni *Selous Game Reserve* lenye wanyamapori wengi mno kama vile tembo, simba, chui, nyani, ngedere, nguruwe na kadhalika.

Hivyo kilimo katika jimbo langu la Liwale kinaathirika sana karibu asilimia 50 ya mazao mbalimbali yanayolimwa huharibiwa na wanyamapori hao kila mwaka. Wakulima wengi ama hupoteza maisha/hujeruhiwa kila mwaka na wanyamapori. Kwa mfano kati ya 1996/99 wakulima 43 waliuawa na wanyamapori na 43 walijeruhiwa. Kati ya 2000/2003 wakulima 11 waliuawa na 10 walijeruhiwa na kati ya 2002/2003 Aprili wakulima 13 waliuawa na wengine wapatao 6 wamejeruhiwa.
Kutokana na hali hiyo nadhani ni wakati muafaka kwa Wizara ya Kilimo kushirikiana na Wizara ya Maliasili kubuni mbinu za kuwasaidia wakulima waishio katika maeneo yanayozungukwa na wanyamapori kama ilivyo Liwale. Liwale ina *Game Scouts 11* tu wakati vijiji vinavyokumbwa na matatizo ya wanyamapori ni 42. Ili kuboresha kilimo Wilaya ya Liwale lazima kila kijiji kiwe na *Game Scout* mmoja na urasimu upunguzwe katika kupata askari pori. Pawe na *Crash Programme* ya ajira vinginevyo maandalizi ya Wizara ya Kilimo kuboresha kilimo kila Wilaya kwa Liwale itakuwa ndog *(Angalia Appendix A):-*

(i) Pamoja na maelezo hayo naomba mfuko wa pembejeo mikopo itolewe na *NMB* ambayo ipo Wilayani karibu na walengwa.

(ii) Wataalam wa kilimo waboreshwe hali zao kwa kupata *promo tions* kwa wakati, vitendea kazi kwa Liwale wataalam waliopo ni 19 ambapo idadi inayotakiwa ni 65. Naomba pengo hilo lizibwe haraka.

(iii) Wataalam wa Kilimo Liwale wanahitaji usafiri wa uhakika *Hardtop* na Pikipiki kuwawezesha kwenda vijijini kwa salama.

(iv) Napendekeza Mheshimwa Waziri awe na utaratibu wa kufanya *Crop Inpsection* kila mwaka nchini kote ikiwa kama njia mojawapo ya kuhimiza matarajio yako katika kilimo.

Ninamalizia kwa kuunga mkono hoja hii tena kwa asilimia mia moja.

*Appendix "A"*

***MOVE TO PROTECT PEOPLE, CROPS AROUND SELOUS***
***(From Lucas Liganga in Dodoma)***

*The Minister for Natural Resources and Tourism, Mrs. Zakia Meghji, said yesterday her ministry has trained village game scouts in areas flanking the Selous Game Reserve in a move intended to protect people against wild animals.*

*The Minister told the Daily News in an interview here that the training of village scouts was done because the Selous Game Reserve had a small number of game scouts to do the job without help.*

*Mrs. Meghji said her ministry has also asked district councils, which are close to the game reserve to train own scouts, adding that her ministry normally responds fast after receiving reports of animals invading villages or farms. She was reacting to remarks by a legislator that efforts to increase agricultural production in Liwale District, Lindi Region, were being frustrated by destructive animals from the Selous Game reserve.*

*Mr. Hassan Chande Kigwalilo (Liwale-CCM) said 53 per cent of the district's 39,000 square kilometres was occupied by the game reserve, sheltering elephants, lions, buffaloes, monkeys, zebra, just to mention but a few.*

*Mrs. Meghji added: "It is true that the animals sometimes destroy farms but we normally act very fast by deploying armed game scouts to control such situations". She said since the government succeeded in controlling poaching, the number of animals such as elephants has increased tremendously, adding that most of them moved to villages in search of pasture and water during dry season.*

*The Liwale legislator told the Daily News over the weekend that elephants were roaming in the district's 42 villages, wreaking havoc to people and farms. "It is a disaster that calls for the government's urgent attention. The government should provide the district with a game scout for each village otherwise villagers' efforts to increase agricultural production will not succeed,' said Mr. Kigwalilo. The Liwale legislator added that apart from destroying farms, the wild animals from the Selous Game Reserve were also killing people who have no means to defend themselves from the animals, chiefly elephants and lions. For example, Mr. Kigwalilo said between 1996 and 1999 the animals killed 43 people and injured 40 others. "Surprisingly, elephants have now started eating cashewnuts, our only cash crop", he lamented, adding that a community conservation services project established by the game reserve was more focused on the protection of the animals than the welfare of communities living around the reserve.*

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Ninapenda sana kumpongeza Mheshimiwa Waziri Keenja, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalam wote wa Wizara hii kwa kuandaa hotuba nzuri sana. Pia juhudi kubwa za kimapinduzi za kuendeleza kilimo katika nchi hii. Lazima sasa tukubali kwamba yapo matumaini makubwa sana ya kuimarisha hali ya maisha ya wananchi wote kwa kuboresha kilimo ambacho ndio Ajira pekee inayotegemewa na asilimia kubwa ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu au ufumbuzi ni Kilimo cha Umwagiliaji. Ninaomba nipongeze Wizara hii kwa kutunza ahadi yake ya kufanya kazi nzuri anayofanya ya kuendeleza miradi ya kilimo cha umwagiliaji katika bonde la Mto Pangani hasa katika miradi ya Kwamgumi, Mahenge, Kwemazandu.

Ninashukuru sana kwa niaba ya wananchi wa Korogwe hususan jimbo langu la Korogwe Mashariki kwa kutupatia wataalam watatu toka Misri wa umwagiliaji. Ninapenda kukuhakikisha kwamba mimi mwenyewe nikiwa Mbunge wa eneo hilo nimeonana nao na nimewakaribisha na kuwahakikishia ushirikiano.

Ninaomba sana mradi huo ukamilishwe katika Vijiji vya Kerenge, Lusanga, Makorora, Magoma ambapo tayari wananchi katika vijiji hivyo wanaendelea na umwagiliaji wa kiasili. Zipo ahadi na mara nyingi wataalam wengi wametembelea wananchi Skimu kuanzishwa katika vijiji hivyo lakini hakuna utekelezaji. Ningependa kufahamu ni kwa nini katika vijiji nilivyovitaja mradi huo hauanzi. Ninapata taabu sana kujibu wananchi wa maeneo hayo.

Kuhusu zao la Mkonge ninaomba nipatiwe jibu la namna ya kuondokana na tatizo la wawekezaji walioshindwa kuendeleza mashamba ya Mkonge na hatimaye uzalishaji kushuka sana. Pia tutawaambia nini wananchi wenye nia ya kuyalima mapori yaliyoachwa na wawekezaji walishindwa kuyaendeleza mashamba. Mheshimiwa Waziri suala hili ni la muda mrefu sana. Serikali kushindwa kulitafutia ufumbuzi maana yake ni kwamba nayo Serikali haina nia nzuri ya kuliendeleza zao la Mkonge.

*Katani Ltd.* ni lazima kama kweli wana nia nzuri ya kuendeleza Mkonge basi washauriwe wabakie na mashamba mawili au moja tu ambalo watakuwa na uwezo wa kuliendeleza ipasavyo. Mashamba mengine Serikali iwapatie watu wenye uwezo wa kujiendeleza kama ilivyo shamba la Gomba. Kuhusu wakulima wadogo wadogo wa Mkonge ni mbinu ya *Katani Ltd.* Wasinyang'anywe mashamba. Wapo wakulima wadogo wadogo ambao Mkonge umekomaa lakini hawajui watamuuzia nani na hata hawajui utaratibu wowote wa namna ya kupata maslahi yao. Korona hakuna matrekta ya kubebea mkonge hayupo.

Ombi au ushauri wangu kwa Mheshimiwa Waziri, ardhi ya zao mbadala litakalowakomboa wananchi badala ya hali ilivyo sasa. Kuendelea kukaa na mapori yasiondelezwa ni kuhujumu uchumi wa nchi. Hivi watu hawa wachache kusaliti nchi Serikali haioni. Watu wa Mkoa wa Tanga ni maskini wakutupa kwa sababu ya eneo lao kubwa kuwa pori.

Kuhusu matunda, haiwezekani katika miaka yote hii Mkoa wa Tanga kukosa Kiwanda cha Kusindika Matunda. Kwa sababu ya ukosefu wa Kiwanda wakulima wengi wa matunda wanakata sana tamaa ya kupanda michungwa, migomba mi-*passion* na kadhalika. Kiwanda cha *TANGOLD* kilipokuwa kinafanya kazi umaskini kwa wananchi wetu wa Korogwe na Mkoa wa Tanga ulipungua sana. Wananchi wengi walikuwa na maisha bora.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kwamba juhudi za Serikali zinahitajika kutafuta mwekezaji wa kufufua Kiwanda cha Kusindika Matunda cha *TANGOLD.*

Pia wananchi wameniomba kama itashindikana kupata mwekezaji wananchi wenyewe hasa wakulima wa matunda wakiwemo Wabunge wao wanaomba wapewe Kiwanda cha *TANGOLD.* Ninaomba jibu.

Mheshimiwa Spika, mwisho ninaunga mkono hotuba hii nzuri kwa asilimia mia moja.

**MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote natanguliza shukrani kwako kwa kunipatia fursa ya kuchangia hoja ya Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, ili kupata maendeleo endelevu katika kilimo na kuhakikisha upatikanaji wa chakula wakati wote, Wizara ya Kilimo lazima iweke mbele *Research and development.* Utafiti lazima uendelee kwa fani zote, mazao, ardhi/udongo, wadudu na maradhi ya mimea, na njia bora ya kuyahifadhi mazao na *processing.* Weka muda mrefu sasa utafiti haujapewa kipaumbele kinachofaa.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu pia matokeo ya utafiti yapelekwe kwa wakulima na yasibakie kwenye makabati ya watafiti tu. Hivyo elimu ya ugani ni muhimu sana. Utafiti lazima ulenge wakulima wa aina zote wakubwa na wadogo. Ni muhimu utafiti na elimu ya ugani vikatengewa fedha za kutosha.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine muhimu ni upanuaji wa mashamba ya umwagiliaji maji kwa kutumia utaalam wa kisasa wa kilimo cha umwagiliaji. Nchi za Asia wakulima wadogo wadogo ndiyo wanaolisha nchi zao na kuuza ziada nchi za nje. Kufuzu kwao kunatokana na matumizi bora ya ardhi kwa umwagiliaji na kutumia mashine ndogo ndogo kwa shughuli mbalimbali. Hivyo kuna haja ya kuingiza utaalam huo hapa nchini ili wakulima wadogo wadogo waweze kulima ardhi kubwa zaidi na kuzalisha zaidi kwa kila eneo. Ili wakulima waweze kumiliki pembejeo na mashine na vifaa mbalimbali vya kilimo ni muhimu kuwe na fursa za mikopo ya kilimo na walipe baada ya mavuno.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Waziri wa Kilimo na Chakula.

**MHE. ESTHER NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii nawapongeze Waziri Mheshimiwa Charles Keenja, Naibu Waziri Mheshimiwa Profesa Pius Mbawala na Kaimu Katibu Mkuu kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, kilimo ndiyo uti wa mgongo kwa Taifa letu la Tanzania. Nashukuru bajeti ya mwaka 2003/04 imeanza vizuri kuona Watanzania asilimia 80 wanategemea kilimo

Mheshimiwa Spika, kama kweli tukisimamia vizuri mabonde mengi tuliyonayo hapa Tanzania, hatutakuwa na njaa. Tanzania ni nchi iliyobarikiwa kwa kila kitu, ardhi ipo nzuri, mito, mabwawa yapo na mabonde mengi. Lakini watalam hakuna wanaokwenda kule kuwaelimisha wananchi kutumia maeneo hayo. Nashukuru sasa Serikali imetenga fedha kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, kutegemea mvua tu toka kwa Mungu hatutafika popote. Hivyo napendekeza mambo yafuatayo:-

* Wataalam sasa warudi katika maeneo ya shamba kwa kazi maalum ya kuelekeza wananchi kilimo cha kisasa.

* Mabonde yote yaanze kulimwa sasa.

* Mashindano yawekwe Kimkoa tuone ni Mkoa upi unatekeleza agizo hili la kutumia ardhi katika maeneo yao.

* Mbegu, mbolea na zana za kilimo zifikishwe kwa wananchi kwa mkopo au kuwauzia kwa bei ndogo ili waweze kununua.

* Vyuo vya Kilimo viimarishwe katika kutoa mafunzo zaidi kwa vijana wetu ili wataalam wawe wengi waende Vijijini na ajira iongezeke katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, Serikali mwaka 2003/04 imetenga fedha ambazo zitapelekwa moja kwa moja kwa Wakuu wa Wilaya. Ninaomba mambo yafuatayo:-

* Fedha hizi zitumike kwa kilimo si vinginevyo.

* Fedha hizi zitolewe taarifa zake hadharani kwenye vikao vya maendeleo ya Vijiji na Kata ili wananchi waelewe kuwa fedha zao za kodi zinarudi kwa maendeleo yao.

* Mkuu wa Wilaya yeyote atakayekiuka matumizi ya fedha hizi awajibishwe na atangazwe ili iwe fundisho kwa wengine.

* Wananchi waelekezwe kilimo cha kisasa na aelezwe fedha hizi ni za mkopo si mgao wa bure.

Mheshimiwa Spika, narudia tena kuwapongeza Waziri na Naibu Waziri wa Wizara ya Kilimo na Chakula kwa hotuba yao nzuri , sasa ina matumaini. Naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia, wapewe fedha zote walizoomba kwa mwaka 2003/04.

**BEATUS R. MAGAYANE:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wake kwa hotuba nzuri na yenye matumaini. Naiunga mkono.

Hata hivyo naomba ufafanuzi kwa yafuatayo:-

Moja kuna mbolea nyingi sana katika maghala ya Dar es Salaam ambayo yameisha muda wake. Nini mipango thabiti ya kutekeleza bila kuathiri mazingira? Kwa nini ilitelekezwa bila kufikishwa kwa wakulima?

Pili, je, kuna mipango yoyote ya kufufua Kiwanda cha Mbolea cha Tanga ili kizalishe hapa hapa nchini bila kutegemea huruma ya wafanyabiashara kuleta mbolea nchini?

Tatu, nini Serikali inafanya kuhakikisha pembejeo zinazofika ni zenye ubora unaotakiwa kwa wakati muafaka na kwa bei nafuu ili tatizo kama la mbegu zisizoota lisijitokeze tena na kuleta hasara kwa mkulima?

Nne, naipongeza Serikali kwa kutilia mkazo uteuzi wa zao la biashara na chakula kila Wilaya ambalo litapata ufadhili wa Serikali. Tatizo ni pale ambapo kutokana na *topography* na hali ya hewa, kunakuwako na mazao mawili tofauti hata katika Tarafa moja, achilia mbali Wilaya. Kahawa hulimwa sehemu za mlimani na pamba au michikichi hustawi vizuri maeneo ya chini katika Tarafa ya Kakonko. Sasa zao lipi litachaguliwa?

Tano, kwa nini vituo vya zana na pembejeo za kilimo *(agricultural implements and inputs centres)* zisianzishwe jirani na wakulima ili hata wale wasiokuwa na uwezo wa kununua basi angalau waweze kukodisha zana toka vituo hivyo? Hii itasaidia sana.

Sita, siku za nyuma tulikuwa na Mabwana Shamba waliokuwa wanashughulikia mazao ya biashara yaliyokuwa chini ya Bodi kwa kila kata-kahawa, pamba na tumbaku katika Jimbo la Buyungu. Leo hii hata Afisa Ugani *(General)* hakuna na hivi uzalishaji na ubora wa mazao vinashuka sana. Je, Wizara kupitia Bodi za Mazao husika, haiwezi kurudisha utaratibu huo?

Mwisho, naishukuru Wizara kwa kuanzisha miradi ya mabonde ya Muhwazi na Ruhwiti. Hata hivyo nashauri skimu kama hizo zielekezwe mto Mwiruzi na Mto Mugembezi ambapo *potential* ni kubwa sana. Maji ya Mto Mwiruzi hutumiwa vizuri sana na majirani wa Burundi, ni vema na sisi tuanzishe matumizi ya maji ambayo eneo lake la mafuriko ni kubwa sana.

**MHE. DR. BATILDA S. BURIAN:** Mheshimiwa Spika, naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na chakula pamoja na timu yake kwa hotuba hii nzuri ya Bajeti.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizi naomba kuchangia hoja hii katika sehemu chache kama ifuatavyo:-

Kwanza, kuhusu hali ya chakula. Kutokana na utafiti uliofanywa na Benki ya Dunia (2002) katika kutathmini mafanikio yaliyopatikana na nchi maskini katika kufikia *Millenium Development Goals (MDGs)* zilizowekwa, kwa upande wa Tanzania, utafiti unaonyesha kuwa lengo la kuondoa umaskini kwa

nusu ifikapo 2015 pamoja na kupunguza asilimia ya wakazi wanaoishi bila mlo wa kutosha na wenye caloric values zinazohitajika kwa mahitaji ya binadamu halitafikiwa kwani mpaka sasa kwa Tanzania asilimia 49 wana umaskini wa chakula.

Mheshimiwa Spika, hivyo ni matumaini yangu kwamba, Wizara hii ingeweka mikakati thabiti kukabiliana na upungufu huu wa chakula. Kwanza, katika *Macro level* na pia katika *Micro level* kwa kushirikiana na sekta zingine kama vile Ofisi ya Makamu wa Rais - masuala ya umaskini, Tawala za Mikoa pamoja na Wizara ya Afya. Kwa mfano, katika ngazi ya familia *(micro level)* kwa vile wakulima wengi hapa nchini ni wakulima wadogo wadogo, basi hata utatuzi wa upungufu wa chakula uonyeshe kuelewa hilo. Kwa hiyo, hakuna budi kuwe na utaratibu wa usimamizi mzuri wa mavuno. Kwa mfano, sheria zingewekwa kuzuia kabisa matumizi ya nafaka kwa ajili ya pombe. Pia uvunaji wa nafaka kwa mfano mahindi mabichi kwa kipindi cha upungufu wa chakula, ungezuiliwa kabisa. Pia utaratibu wa kukagua maghala ya nafaka ufanywe kama vile tunavyokagua vyoo huko Vijijini.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni Wizara hii ione jinsi gani tunaweza kushirikiana na Mashirika kama *UNIDO,* ili kusaidia wakulima wadogo wadogo kupitia vikundi vyao waweze kusindika vyakula wanavyozalisha utaratibu huu utasaidia kuongeza mapato na hivyo kuwafanya hawa wakulima wakawa na additional income. Hivyo kupunguza utegemezi wa kilimo katika kipindi ambacho si cha mavuno.

Mheshimiwa Spika, tatu, umuhimu wa takwimu na taarifa sahihi. Nimefurahi kuona takwimu mbalimbali zimetumika, hata hivyo kuna takwimu zilizotumika zimepitwa na wakati au ni za nyuma. Kwa mfano, Jedwali Na. 2 Ukurasa wa 16, uzalishaji wa mazao ya biashara. Jedwali hili linaonyesha taarifa za mazao ya korosho, kahawa, pamba, sukari, chai, tumbaku, mkonge, pareto na uzalishaji wake kati ya mwaka 2000/2001, 2001/02 na 2002/03. Tatizo nililoliona ni kwa zao la tumbaku.

Jedwali linaonyesha kwamba katika kipindi cha mwaka 2002/03 inatarajiwa kwamba tumbaku itakayozalishwa itakuwa ni tani 32,693.62. Cha kushangaza ni kwamba tumbaku ya mwaka huu tayari imeshauzwa. Je, kwa nini bado takwimu zinaonyesha matarajio? Pia katika ukurasa wa 57 hotuba inasema kuna jitihada za kusambaza teknolojia za kudhibiti upotevu wa mazao baada ya mavuno. Hata hivyo hotuba hii haifafanui kabisa, teknolojia hizo ni zipi.

Mheshimiwa Spika, nne, zana za kilimo, Mheshimiwa Waziri mwaka jana katika bajeti yake aliahidi kuanzishwa kwa agencies zitakazokodisha matrekta. Hata hivyo sijaona katika hotuba hii chombo chochote au taarifa yoyote kuhusu ukodishwaji wa matrekta ili kusaidia wakulima wadogo wadogo ambao hawawezi kununua matrekta yao binafsi.

Mheshimiwa Spika, ni mategemeo yangu kwamba hayo niliyoyapendekeza yataangaliwa.

Mwisho, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. MAJOR JESSE J. MAKUNDI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia hotuba hii japo kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kuwepo Mfuko wa Pamoja wa Msaada wa Chakula kati ya Tanzania na Japan *(Tanzania -Japan Food Aid Conterpart Fund FACF)* kugharamia miradi midogo ya maendeleo ya sekta ya kilimo hasa ukarabati wa skimu za kilimo cha umwagiliaji wa shilingi 795 milioni likiwemo shamba la Ghona lenye hekta 450. Eneo hili ni la tambarare na mara kwa mara eneo hili linakumbwa na njaa. Hakika njia hii ndiyo ya kukomboa wananchi hawa kutokana na baa la njaa. Napendekeza eneo hili liendelezwe na liwe la mfano kwa wananchi watakaotembelea eneo hilo. Ahsante Japan.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kahaa (uk. 63) utafiti uendelezwe na miche isambazwe kwa wakulima wakati wa msimu wa kupanda miche ya kahawa. Kuhusu viwanda vya kupukuchua kahawa *Central Pulparies* ziendelezwe kila Kijiji kilimacho kahawa, ndiyo njia pake yake ya kuwa na kahawa bora kuliko wakulima kupukuchulia nyumbani, kusafisha kahawa hiyo na majitaka na kuanika kahawa hiyo kwenye mavumbi na hivyo kahawa kunuka vumbi, ngozi ya ng’ombe na uchafu mwingi.

Mheshimiwa Spika, kama Wizara hii itazingatia *Hansard* ya hotuba hizi na maoni ya wachangiaji, hakika Wizara hii itawezesha Taifa letu kukua kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. FATMA SAID ALI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa kuwasilisha hoja hii.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Utafiti Minazi Mikocheni, naomba watafiti wa kituo hiki wakatembelee *Far East na Caribbeans* vipi nazi zinavyotumika kwenye vinywaji *liquir* na kadhalika. Pia mashine za kukamulia mafuta ya NAZI ziagizwe nyingi ili wakulima wa minazi wafaidike na kilimo cha minazi.

Mheshmiwa Spika, mikopo kwa ajili ya wanawake wakulima iwepo kwa ajili yao kwa makusudi ili waweze kupanua kilimo kwenye mashamba yao madogo madogo.

Mheshimiwa Spika, naomba mafunzo maalum kwa viongozi wa Wanawake hasa wa UWT kama tulivyofanya hapa Bungeni.

**MHE. PHILLIP S. MARMO:** Mheshimiwa Spika, kwanza, kuhusu hifadhi katika ngazi ya kaya. Wilaya ya Mbulu ingekuwa inajitosheleza kwa chakula kwa kiasi kikubwa iwapo madawa ya uhakika ya kuhifadhi chakula yangekuwepo. Yaonekana mdudu Dumuzi *(Scania)* kwa Mbulu na Wilaya za jirani amekuwa sugu kwa madawa. Taarifa zimeletwa Wizarani kupitia Mkoa wa Manyara. Tani nyingi za mahindi ya miaka ya 2000/01 na 2001/2002 yameharibiwa na dumuzi. Hatua gani Wizara inachukua kutatua tatizo hili?

Pili, Mheshimiwa Spika, kutokana na Bajeti hii kiasi cha fedha kitafikishwa Wilayani. Wizara zingine zina taratibu za kufuatilia kuhakikisha fedha zinazopelekwa Wilayani zinatumika ipasavyo. Wizara ya Kilimo inaandaa utaratibu gani wa kufuatilia fedha zake?

Mheshimiwa Spika, tatu ni kuhusu zao la pareto. Wizara inatelekeza wakulima wa pareto wa Kanda ya Kaskazini Meru, Babati na Mbulu. Kiwanda cha zamani cha pareto Arusha, mali ya Bodi ya Pareto ikiwa ni pamoja na majengo yanatelekezwa.

Mwekezaji anayehamasisha wakulima na kununua pareto anakatishwa tamaa kiasi cha kutaka kuhamia Kenya. Yaonekana katika Bodi ya Pareto *(regulator)* Kanda ya Kaskazini haina mwakilishi wa matatizo ya wakulima na hayafahamiki ipasavyo. Waziri angeangalia matatizo haya uwezekano wa uzalishaji wa pareto Mbulu na Meru ni mkubwa sana. Katika miaka ya 60 na 70 maeneo haya yalikuwa yakizalisha asilimia themanini ya pareto yote ya Tanzania.

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, malengo na makusudio ya Wizara hii yanaleta matumaini makubwa. Naamini yakitekelezwa yataelekeza nchi katika mafanikio.

Mheshimiwa Spika, mikakati iliyowekwa ni mizuri, hata hivyo nashauri tathmini ya kampeni mbalimbali za kilimo zilizopita kama vile kilimo ni uhai, kilimo cha kufa na kupona, Azimio la Iringa na kadhalika ifanyike. Mambo mazuri yaliyofanyika katika kampeni hizo yaendelezwe. Mikakati ya makusudi na mahsusi iwekwe ili kuvutia wawekezaji katika kilimo cha mashamba makubwa *(large scale farming)* hapa nchini hasa baada ya mashirika ya Serikali ya sekta ya kilimo kubinafsishwa na *NAFCO.*

Mheshimiwa Spika, pili, ruzuku ya moja kwa moja *(direct subsidy)* kwa wakulima wadogo wadogo ni muhimu katika kukuza kilimo. Serikali itafute njia ya kulipa ruzuku ya moja kwa moja kwa wakulima katika vikundi *(co-operatives)* ili kukuza kilimo.

Mheshimiwa Spika, tatu, bado lipo tatizo la huduma za ugani kwa wakulima. Wataalam wa kilimo waliopo sasa wengi wao wanaonekana kuchoka na hawana ari kabisa ya kazi hiyo. Serikali ichukue hatua za makusudi kuwapiga msasa *(re-training)* wale wanaoonekana hawawezi kubadilika waachishwe kazi na waajiriwe watumishi wapya wenye ari ili wasaidie wakulima. Hili tusilionee aibu ili kuinua kilimo.

Mheshimiwa Spika, nne pawepo na mahusiano bayana ya kweli kati ya Wizara ya Kilimo na TAMISEMI ili kufanikisha utekelezaji na malengo kufikiwa.

**MHE. LEONARD N. DEREFA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na nawatakia utekelezaji mwema wa bajeti ya 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Wizara isaidie Jimbo langu la Shinyanga Mjini kuhusu miradi mitatu ya umwagiliaji katika Kata za Vijijini

Mheshimiwa Spika miradi hiyo ni kuziba vijito vidogo ambavyo vinaingiza maji Mto wa Manonga. Miradi hiyo midogo inaungwa mkono na Manispaa na wananchi wako tayari kushirikiana na Serikali kwa kutoa nguvu zao kwa hali na mali.

Mheshimiwa Spika, miradi hii ikitekelezwa itapunguza umaskini na njaa kwa wananchi. Miradi hiyo nimeiwakilisha kwako kwa barua Kumb. *BGT/GEN/214/VOL. 14* ya tarehe 5/5/2003. Miradi ni kama ifuatavyo:-

(a) Mwagala/Bugweto upo katika Kata ya Ibadakuli na makisio yake ni shilingi 41,246,205/=.

(b) Mradi wa Kolandoto/Ibadakuli upo katika Kata ya Kolandoto/Ibadakuli makisio yake ni shilingi 46,163,775/=

(c) Mradi wa Seseko/Ndembezi upo katika Kata ya Mwamatili/Ngokolo na makisio yake ni shilingi 50,171,730/=. Jumla ya miradi yote ni shilingi 137,581,710/=.

Mheshimiwa Spika, miradi hii inaweza kutekeleza kwa kupitia Manispaa yetu ambayo inao watekelezaji wenye ujuzi wa miradi ya umwagiliaji maji.

Mheshimiwa Spika, natanguliza shukrani zangu kwa msaada wa Wizara yako. Tunayo matatizo mengi lakini tukisaidiwa miradi hii mitatu itakuwa hatua kubwa ya maendeleo kwetu.

Mheshimiwa Spika, narudia kusema kuwa naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na kuwatakia utekelezaji mwema wa bajeti ya Wizara ya Kilimo na Chakula na maandalizi ya njaa mwaka 2004 kama ulivyotoa historia ya njaa ili kunusuru watu wetu.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru Serikali imeanza kuona umuhimu wa kuelekeza angalau kiasi kikubwa cha fungu la fedha kwenye sekta ya kilimo. Pamoja na jitihada hizo nzuri yafuatayo pia yanapaswa kupewa kipaumbele:-

Kwanza, Wizara ya Ushirika na Masoko inapaswa ifanye shughuli zake kwa karibu na Wizara hii. Aidha, mpango mahsusi uandaliwe na kutekelezwa kwa kutafuta na kuanzisha mtandao unaoaminika wa masoko ndani na nje ya nchi. Wakulima waanzishiwe vituo vya upashanaji habari za masoko.

Pili, Serikali kama mwangalizi na msimamizi mkuu wa mwenendo wa kiuchumi inapaswa kuchukua hatua za makusudi za ku-*promote* masoko ya ndani na kuyalinda. Viwanda vinavyosindika mazao ya wakulima na matunda, mboga na kadhalika viwanda hivyo inabidi vilindwe kwa nguvu zote kwa ku- *discourage* uingizaji bidhaa zinazotoka nje. Hii itasaidia upatikanaji wa masoko ya bidhaa zinazozalishwa.

Pia watu wataongeza utashi wa kupenda kutumia vitu tunavyozalisha hapa hapa nchini kwa vile ndivyo vilivyopo. Kwa njia hiyo soko la ndani litakua, viwanda vitazalisha zaidi, mazao ya wakulima yatanunulika kwa wingi na kuongeza mapato. Serikali kama mlipaji mkuu wa mambo mbalimbali iagize

Idara zake kununua bidhaa zinazozalishwa na viwanda vyetu vyenye kutumia mazao ya wakulima wetu, mfano, juice, kahawa, vyakula vya makopo na kadhalika. Vitu hivyo ndivyo vitumiwe kwenye makongamano, semina, warsha na kadhalika.

Tatu, wataalam wetu ambao wanafuzu mafunzo katika vyuo mbalimbali vya kilimo na wakaonyesha uwezo na umahiri wa kupenda kuingia kwenye shughuli ya kilimo wapewe mikopo inayojitosheleza kwa njia ya nyenzo za kufanyia kazi ili waingie kwenye kilimo kikubwa na cha kisasa. Mikopo hiyo itarejeshwa kwa kuwakata sehemu ya mapato yao. Waingie Mikataba maalum na Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. JUMA S. KIDUNDA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Naibu wake, Mheshimiwa Keenja na Mheshimiwa Mbawala pamoja na timu yao ya wataalam wakiongozwa na Katibu Mkuu kwa kazi nzuri sana wanayoifanya, hongera sana.

Mheshimiwa Spika, ombil langu ni kuwa, kwa kuwa Wilaya mpya ya Kilindi ina mabonde makubwa na yenye mito ya kudumu mingi lakini kwa kuwa uongozi wa Handeni ya zamani haukuainisha maeneo haya mazuri kwa umwagiliaji, naomba apeleke timu ya wataalam au aagize Mkuu wa Wilaya mpya amletee taarifa za kina za mabonde ya Kilindi ili ayaingize katika orodha ya maeneo ya mpango mkuu wa umwagiliaji nchini. Wilaya ya Kilindi ni tofauti sana kijiografia na ile ya Handeni.

Maafisa Ugani wapewe mbinu za ugani shirikishi ili ushauri wao uwe wa manufaa endelevu. Maafisa Ugani wapewe vitendea kazi muhimu kama vile *simple spirit level* na kadhalika kwa ajili ya kupimia makinga maji ambayo ni muhimu kwa kuzuia mmomonyoko wa ardhi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ni vema Serikali ikaangalia upya maslahi ya Mabwana Shamba pamoja na utaratibu wa mafunzo ya kujiimarisha au kunolewa kitaaluma mara kwa mara ili kwenda na wakati wa mabadiliko kwenye Vituo vya Utafiti.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Wizara ya Kilimo moja kwa moja ili wapewe fedha za kutekelezea azma nzuri na yenye matumaini makubwa kwa Taifa.

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba wataalam wa umwagiliaji waende Ismani (Tarafani) wakasaidie kuandaa michoro ya kujenga mabwawa angalau matatu ya umwagiliaji kwa mwaka huu na hatimaye maombi yapelekwe *FACF* ili fedha zipatikane. Ismani ni eneo muhimu kwa kilimo cha mahindi, lakini hakuna mito wala vyanzo vyovyote vya maji. Hivyo uchimbaji wa mabwawa ndiyo suluhisho.

**MHE. PROF. JUMA M. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iweke miundo mbinu katika maeneo yote yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji na kuwakopesha wakulima wadogo wadogo nyenzo mbalimbali na pembejeo ili waje kulipa wanapovuna mazao yao.

Naomba Wizara ya Kilimo na Chakula kupeleka wataalam wa umwagiliaji katika eneo la Ziwa Zimbwini lililoko Kibiti ili eneo hilo litumike kwa umwagiliaji. Kilimo cha umwagiliaji katika eneo la Segeni (Ikwiriri) kipanuliwe hadi kufikia hekta 5000. Naomba maeneo mengine ya bonde la Mto Rufiji yatumike kuanzisha kilimo cha umwagiliaji.

Kuhusu zao la korosho, ukurasa wa 64 mpaka 65. Ili zao la korosho liongezeke kutoka tani 90,000 mwaka 2002/2003 hadi kufikia tani 125,000 au zaidi kwa mwaka 2003/2004, napendekeza mambo yafuatayo:-

* Huduma za ugani ziongezwe.
* Mfuko wa uendelezaji zao la korosho au chombo kingine kianzishwe.
* Mbolea ya sulfur ipelekwe kwa wakulima mapema iwezekanavyo.

* Soko la uhakika lipatikane.
* Viwanda vidogo vidogo vya ubanguaji vianzishwe na kusambazwa.
* Miche mipya ya mbegu bora iboreshwe na kuandaliwa haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara ya Kilimo na Chakula kukubali kuanzisha kilimo cha pamba Wilaya ya Rufiji kwani pamba ya huko ni bora ile ya *long fibre.*

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iongeze Bajeti ya Wizara ya Kilimo ili iwezeshwe katika kilimo cha umwagiliaji.

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika hotuba, ukurasa wa sita kwa mwaka 2002/03 Wilaya ya Karatu haikuorodheshwa katika Wilaya zilizokumbwa na njaa. Mwaka 2003/2004 pia haikuorodheshwa. Je, tatizo ni nini hasa? Wananchi wa Karatu waliokolewa na chakula kilichotolewa na Jimbo Katoliki la Mbulu na *Caritas Tanzania.* Mwaka huu pia Jimbo Katoliki na *Caritas Tanzania* tayari wamefanya tathmini na kuona katika Kata 13, Kata sita zitakuwa na upungufu mkubwa wa chakula. Lakini hotuba ya Waziri haikuweka Wilaya ya Karatu kama Wilaya zilizoathirika. Naomba maelezo ya kina. Nategemea pia Waziri atawapongeza Jimbo Katoliki la Mbulu na *Caritas Tanzania* kwa kutoa mchango mkubwa katika kuokoa maisha ya watu wetu, wengi ambao hata kununua hawakuweza kutokana na hali ya ukame ambayo imetukumba karibu kwa mwaka wa nne mfuulizo.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atoe ufafanuzi wa kina jinsi shilingi bilioni 10 kwa ajili ya barabara zitakavyogawanywa. Wilaya ya Karatu inayo mashamba makubwa 45 ya kahawa na wakulima wadogo wadogo. Mara ya mwisho fedha ziligawanywa karibu shilingi bilioni 1.5 kwa maeneo ya kahawa, Wilaya ya Karatu haikupata mgawo wowote. Waziri afafanue kwa kina vigezo vinavyotumika katika kugawa fedha hizi na Wilaya ya Karatu imetengewa kiasi gani katika mgawo wa shilingi bilioni kumi. Kwa kweli nisipopata maelezo ya kina sitaunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, tatu ni kuhusu *Tanzania-Japan Food Aid Counterpart Fund,* Mfuko huo umetolewa na Serikali ya Japan kusaidia maendeleo ya nchi yetu na wakati huo huo kupunguza matatizo ya njaa. Kuna taarifa na imethibitisha na taarifa ya *CAG* kuwa toka 1995 hadi 2002 wafanyabiashara kadhaa wamechukua chakula bila kulipa *Counterpart Fund* jambo ambalo linawanyima Watanzania manufaa ya Mfuko huu. Naomba Waziri afafanue kwa kina:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, ni wafanyabiashara au Makampuni mangapi yanadaiwa *Counterpart Fund* na ni kiasi gani wanadaiwa kati ya 1995 hadi 2002?

Pili, makampuni na wafanyabiashara sugu hao wamechukuliwa hatua gani za kisheria, ikiwa ni pamoja na maofisa waliosababisha kwa uzembe au makusudi chakula hicho kuchukuliwa bila kwanza kulipia Counterpart Fund?

Mheshimiwa Spika, kuhusu ubinafsishaji wa Mashirika ya Kilimo. Naomba ufafanuzi wa kina kuhusu ubinafsishaji wa mashamba ya *NAFCO,* Hanang. Kwa zaidi ya miaka kumi sasa mashamba hayo hayazalishi na mengine yamegeuka kuwa pori isipokuwa maeneo kidogo yaliyokodishwa kwa wawekezaji wachache au kwa wananchi na wafanyakazi. Kutokana na kuyaacha mashamba hayo wafanyakazi wengi hawajalipwa sasa kwa zaidi ya mwaka na mashamba mengine zaidi ya miaka miwili. Matokeo yake mali nyingi zikiwemo matrekta zimehujumiwa na wafanyakazi wenye kutafuta uhai wao kwa kuuza spea.

* Je, Serikali inachukua hatua gani kuokoa angalau mali zilizoko zisiendelee kuangamia?

* Pili, kusaidia wafanyakazi wengi waaminifu ambao bila makosa yao wamekumbwa na hali ya kutolipwa mishahara na mafao yao?

Mheshimiwa Spika, iwapo sitapata maelezo ya kina, Mheshimiwa Waziri ajiandae wakati wa kujadili mafungu.

Kuhusu kilimo cha umwagiliaji. Nashauri wakati sasa umefika wa kuingia katika kilimo cha kisayansi. Nchi zote zilizoendelea duniani, zimefanikiwa kwa kuingia katika kilimo cha kitaalam, kisichotegemea wingu la Mungu. Isitoshe, wote hulenga kupunguza asilimia ya wakulima na kuweka mazingira ya watu walio wengi kuingia katika *Tertiary Sector* na *industry.* Wastani wa wakulima ni kati ya asilimia tatu hadi kumi. Tanzania wakulima ni karibu ya asilimia 85 hivyo:-

* Badala ya kutawanya sana fedha chache zilizoko na nyingi ni kopo ambayo *return* yake haina uhakika kwa kutegemea wingu tuwekeze kwenye mabonde yaliyoko na pia kutumia kwa makusudi Maziwa yetu kama Victoria na kufikisha maji hadi Dodoma. Ukipeleka maji, ukatoa pembejeo, mbegu, hatuhitaji kutumia fedha nyingi kwenye *coordination, Capacity Building* na kadhalika. Wakulima wanajua kabisa wanachotaka, kwa hiyo wawezeshe tu kwa kujengewa mazingira kwa maana ya infrastructure.

Mheshimiwa Spika, ningependa Waziri afafanue kasma gani ametumia kupitishia fedha zinazopelekwa Wilayani kwa zao la biashara na zao la chakula. Waziri aeleze ni kiasi gani kwa kila Wilaya zimetengwa na ametumia vigezo gani kutoa mgawo huo. Mheshimiwa Spika, natanguliza shukrani za dhati.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakupongeza kwa hotuba nzuri yenye uchambuzi wa kina kuhusu Wizara yako hususan sekta ya kilimo. Pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Pamoja na kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja napenda kuchangia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Vituo vya Utafiti wa Kilimo ni muhimu sana na hasa utafiti wa mbegu bora. Mkoa wetu wa Dodoma una vituo vya utafiti vya Hombolo (mazao), Makutupora (zabibu). Je, Serikali ina mpango gani wa kuviimarisha vituo hivyo kwa kuvipatia vitendea kazi vya kutosha. Kilimo cha utafiti cha Hombolo ni muhimu sana. Je, kwa nini vituo hivyo vilifungwa na kuna mpango gani wa kuvifufua vituo hivyo na pia kufufua vituo vya *Oxen Training Centres* ili wakulima wapate mafunzo, kilimo cha majembe ya kukokotwa na ng'ombe.

Mheshimiwa Spika, kilimo cha umwagiliaji ndiyo mkombozi wetu hasa maeneo ya mabonde ya umwagiliaji kama vile Bonde la Lumuma ambalo linahudumia Wilaya ya Kilosa na Mpwapwa. Hivi karibuni wafadhili wamejenga vibanio katika Bonde hilo la Lumuma, je, ni fedha kiasi gani zimetumika kujenga vibanio hivyo na vibanio hivyo vitahudumia ekari ngapi katika bonde la Lumuma na kama bonde hili litalimwa lote litatoa chakula tani ngapi? Je, Bonde hilo la Lumuma likilimwa lote haliwezi kulisha chakula Mkoa wa Morogoro na Dodoma na kupunguza uhaba wa chakula katika Mikoa hiyo. Mheshimiwa Waziri Mkuu Februari, 2003 alitoa maagizo kwamba Bonde hilo lilimwe lote badala ya kuacha mapori je, hilo limetekelezwa?

Mheshimiwa Spika, kwa utafiti wa mazao Kanda ya Kati je, ni lini kituo hicho kitaimarishwa kwa kufanyiwa ukarabati na kupatiwa vitendea kazi vya kutosha kama vile matrekta, *computers,* kuwekea simu ili kuboresha mawasiliano, hivi sasa wana simu ya upepo, hakuna simu ya *TTCL.* Kwa kuwa kituo hiki ni cha zamani mapendekezo yangu ni kwamba kipewe hadhi na kuwa Kituo cha Utafiti wa Kilimo. Mazao Kanda ya Kati badala ya kuwa chini ya Kituo cha Utafiti Kanda ya Kati Mpwapwa ambacho kinashughulikia sekta ya Mifugo zaidi. Kituo cha Utafiti Makutupora (Zabibu) kiimarishwe na kupatiwa vitendea kazi. Zao la zabibu ndiyo mkombozi kwa wananchi wa Mkoa wa Dodoma, tatizo kubwa hakuna soko la zao hili kwa mfano JKT Makutupora wamefanya kazi nzuri sana ya kufufua zao la zabibu, wamelima zaidi ya ekari 65. Je, Wizara ya Kilimo inawasaidije JKT Makutupora baada ya kuvuna zabibu zao watafutiwe soko la kuuza zao hilo. Kuhusu Vituo vya Matrekta, vituo hivi ni muhimu sana, hapo zamani Serikali ilianzisha vituo vya matrekta Vijiji vya Mtanana na Iduo Wilayani Kongwa. Wananchi waliweza kukodi matrekta hayo kwa gharama nafuu.

Kwa kuwa Wilaya ya Mpwapwa inakabiliwa na uhaba wa chakula na pia Mkoa wa Dodoma kwa ujumla unakabiliwa na uhaba mkubwa wa chakula. Je, ni lini Serikali itaanza kusaidia chakula na hata cha kununua kwa maeneo yenye uhaba wa chakula? Wananchi wapo tayari kununua chakula hicho. Uhaba wa chakula umeweza kusababisha mahudhurio mabaya katika shule za msingi Wilaya ya Mpwapwa na Mkoa wa Dodoma kwa ujumla na Mikoa mingine yenye uhaba wa chakula hapa nchini. Naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. JEREMIAH J. MULYAMBATTE:** Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii nyeti sana ya kukupongeza wewe na Naibu Waziri wako, Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo pamoja na Menejimenti yote kwa kuandaa bajeti nzuri ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka huu wa 2003/04. Hongera sana. Hata hivyo napenda kuchangia Wizara hii kwa kutoa taarifa kuwa Wilaya ya Meatu imekumbwa na njaa kutokana na ukame uliodumu kwa muda wa siku tisini bila ya mvua. Hivyo ni njaa sana hasa hasa upande wa Jimbo la Meatu. Hatua za haraka zichukuliwe na Serikali za kupeleka chakula, Serikali isije kushangaa kusikia watu Wilayani Meatu wanakufa njaa.

Mheshimiwa Spika, pili mpango wa Serikali wa kutoa fedha nyingi za utafiti kwa mazao ya biashara nchini ni jambo jema, hasa ikizingatiwa suala zima la mazao yote ya biashara kama vile kahawa, korosho, pamba, chai, pareto na tumbaku. Hii itaweka *balance* kwa nchi nzima. Angalau kama ilivyo sasa hivi inaonyesha waziwazi kuwa, fedha hizo zinakwenda Kanda ya Kaskazini ambako waliko wakubwa tu. Mazao yote ya biashara nchini yapewe fungu la kufanyiwa utafiti kwa Bajeti hii ya 2003/2004. Lakini kama ilivyo kwa sasa italeta hisia na dhana ya upendeleo kwake Waziri wa Kilimo na Chakula.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo na Chakula ndiyo yenye watu wengi na dhamana kubwa kwa Watanzania kwa kutegemea kilimo na ndiyo uti wa mgongo wa uchumi wa Taifa letu la Tanzania. Hata hivyo huko Wilayani, Wizara hii bado imechanganywa na Wizara tatu yaani, Kilimo na Chakula, Ushirika na Masoko na Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, Wilayani Meatu. Wizara hizo tatu zinaongozwa na mtaalam wa mifugo ambaye yuko Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, iweje basi, aongoze na Kilimo pia na Ushirika? Lazima yeye ataegemea upande wake wa Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo. Kilimo Wilayani yafaa kuwa na mtaalam pekee ambaye amebobea kwa suala la kilimo.

Kwa mtindo huu tulio nao hivi sasa, kilimo lazima kitakwama jumla jumla. Kumbe, kama Serikali inapeleka fedha nyingi huko Wilayani pawe na mtaalam basi wa kilimo ambaye atakuwa tayari kusimamia na kusukuma utekelezaji wa kilimo na ambaye atakuwa chini ya Wizara ya Kilimo na sio chini ya Wizara nyingine. Pia utaratibu huu tulio nao watumishi wengi wa Wizara ya Kilimo na Chakula kuchangaywa pamoja na watumishi wa Wizara za Ushirika na Masoko na Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo ni kuwakosesha taratibu za kiutumishi wao na wengine kupoteza kabisa mafao yao ya uzeeni (Pensheni).

Mheshimiwa Spika, tatizo la mbegu la msimu huu wa 2002/03 kuungua ni suala la kuangalia kwa karibu zaidi ili wakulima wa zao la pamba waweze kupata moyo na ari ya kuendelea na kilimo cha zao la pamba. Sana sana wakulima wapewe fidia ya mbegu za kupanda mwaka huu wa 2003/2004. Naomba hili lizingatiwe sana na Serikali. Aidha, kulikuwa na tatizo la ndege wa aina ya *parrots* ambao walikuwa wakishambulia mazao ya chakula ya wakulima msimu huu wa 2003 katika Kata za Nkoma, Mwanjolo na Bukundi. Hivyo basi Serikali ijiandae msimu ujao kuwaangamiza kabisa hao ndege katika Wilaya ya Meatu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii. Ahsante sana.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Spika, salaam kwa *staff* yote ya hapo mbele. Hongera sana na karibuni sana Dodoma, sisi tupo hapa tangu 9/6/2003. Hotuba yenu ni shwari na tulivu ingawa haivutii. Yapo mapungufu ya hapa na pale lakini siyo ya sera bali ya kiutendaji tu. Nawatakia kila la kheri.

**MHE. STEPHEN M. KAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe mchango wangu kwenye Hotuba ya Waziri wa Kilimo na Chakula kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza kwa dhati Waziri wa Kilimo na Chakula, kwa hotuba yake ambayo imejenga hoja nzuri kwenye Bunge lako Tukufu. Kwa namna hiyo hiyo, naomba sana

nimpongeze Naibu Waziri wa Kilimo na Chakula, Katibu Mkuu na pia Makamishna na Wataalam wote wa Wizara hii kwa juhudi zao kwenye hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitachangia mambo machache ambayo naiomba Wizara iyatafutie mtindo wa jibu la kudumu wa namna ya kuyatekeleza Kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ni kuoanisha mipango ya utendaji. Kwenye Bajeti ya mwaka unaomalizika wa 2002/2003, Wizara tuliitegemea kwa namna moja kwa kutumia kiasi cha fedha iliyopewa ingekuwa imepiga hatua angalau za mwanzo kwenye mipango yake ya kilimo cha umwagiliaji, wanyamakazi, vyombo vya kilimo kama vile matrekta na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo haya ya mipango na shughuli za kilimo mnapokuwa Vijijini hayaonekani. Nguvu za Wizara ya Kilimo na Chakula kwenye maeneo ya Vijiji ni kuwa na Mabwana Shamba Wakuu wa Wilaya kukagua kilimo na kadhalika. Haya yote hayapo Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua hizi kama zingechukuliwa mwaka 2002, basi Bajeti ya mwaka huu ingetumika kuendeleza tu. Je, Wizara itatoa uhakika gani mwaka huu kwamba mambo yatabadilika? Je, fedha zinazoombwa zitatumika vizuri? Je, utekelezaji wa mipango ya mwaka huu ukoje? Hatutaki mwaka huu mambo ya mwaka jana yajirudie, kwa mfano, mbegu za pamba zisiote. Hayo yametokea kwa sababu Wizara haikufika Vijijini katika mwaka huu unaoisha wa 2002/2003.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kuna hili suala la kilimo cha mboga, nyanya, vitunguu, matunda, maua na kadhalika *(horticultures)*, ambalo nilitegemea litaongelewa na hata kutolewa mwongozo wa namna ya kuendeleza kilimo hiki Kitaifa, lakini halikujitokeza kwenye Hotuba ya Bajeti. Kilimo cha *horticulture* sasa kinazidi kuendelea na hata kilimo cha maua ambacho sasa kinaleta pato kwenye Taifa letu zikiwemo fedha za kigeni. Kwa vile Wananchi wameanza kuelekeza *resources* zao kwenye eneo hili, ni busara kwa Serikali kupitia Wizara ya Kilimo na Chakula, kuanza kushirikiana nao ili kuwawekea mazingira mazuri ya kilimo hiki. Kuna suala zima la masoko kwenye mazao haya, hivyo, ni lazima sasa iandaliwe Sera ambayo itahusisha Wilaya na Halmashauri zetu kwenye utaratibu wa kuwakutanisha wakulima na wanunuzi wa mazao haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, utaratibu wa pembejeo za kilimo haujakaa vizuri. Kwa vile shughuli za kufufua Ushirika bado zinaendelea, ni vizuri kukawa na utaratibu *effective* kwa muda huu wa kushikilia mpaka hapo Ushirika utakapoimarika. Wakulima hasa wa zao la pamba bado wana matatizo ya kupata pembejeo. *Machinery* ya kugawa pembejeo kwenye zao hili bado si nzuri. Wafanyabiashara wenye tamaa na wajanja wanavuruga utaratibu huu kwa kuchanganya mafuta au maji kwenye dawa za kuua pamba.

Matokeo yake dawa zinashindwa kuua wadudu kwenye zao la pamba. Kwa vile tatizo la pembejeo hasa dawa za kuua wadudu kwenye zao la pamba limekuwa likijitokeza kila mwaka na pia tatizo la mbegu za pamba kutoota, kutomfikia mkulima kwa wakati na kadhalika, Wizara ya Kilimo na Chakula sasa inatoa maelezo gani ya uhakika kwamba, imedhibiti matatizo haya yote kwenye zao la pamba?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya machache haya, naomba kuunga mkono hoja hii.

**MHE. TEMBE K. NYABURI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Napenda kusema kuwa hotuba ni nzuri, lakini nakumbusha kuhusu Wizara kuziagiza Wilaya kuandaa mipango yao kuhusu kilimo cha umwagiliaji. Wilaya ya Bunda tuliandaa kwa kulenga eneo la zamani lililokuwa la umwagiliaji yaani Nyatwali na Tamau kando ya Ziwa Victoria. Mashine za kusukuma maji zipo japo zimechakaa, mabomba yaliyotandazwa yapo tayari na eneo kubwa ambalo Wananchi walikuwa wakilima.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mapendekezo ya Wilaya kwa Wizara, tuliomba mradi huu uhusishwe. Mimi mwenyewe na Mkuu wangu wa Wilaya, Mama Hawa Mchopa, tulikuja Wizarani pamoja na kukabidhi rasimu ya mapendekezo ya Wilaya. Mheshimiwa Waziri, aliahidi kuwa Mradi utajumuishwa, lakini katika hotuba yake Nyatwali na Tamau haikujumuishwa. Matokeo yake mradi uliotajwa kuhusishwa

ni ule wa Nansimo ambao tayari ulishajumuishwa kutekelezwa kupitia *IFAD - MARAFIP* ambayo inasuasua.

Mheshimiwa Naibu Spika, natumaini Mheshimiwa Waziri ana kumbukumbu nzuri hata alipotembelea Bunda alijionea kwa macho na akaahidi kuhusu Mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kuomba mradi huu uingizwe kiutekelezaji mwaka 2003/2004. Wakati anajumuisha aligusie suala hili kikamilifu.

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, pamoja na Wataalam wote wa Wizara, kwa kutayarisha mpango mzuri wa kufufua kilimo. Mpango huu kama utakamilika kikamilifu, naamini kilimo mwaka ujao kitakua kwa asilimia zaidi ya 6, hivyo itaongeza pia mchango wa Sekta ya Kilimo katika Pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mpango ni mzuri, kwa niaba ya Wananchi wangu, naunga mkono Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula kwa asilimia mia moja.

Napenda kumwambia Mheshimiwa Waziri kuwa, kwanza, ili mpango huu uweze kufanikiwa tunahitaji Wataalam wa kutosha kwa ajili ya kuusimamia. Kwa sasa Wilaya ya Mbinga tunao Wataalam 85 na tuna upungufu mkubwa wa Wataalam 166. Upungufu huu ni mkubwa sana ukizingatia Wilaya ya Mbinga sehemu kubwa ni milima, ina Kata 37, Vijiji 179 na Vitongoji vyenye hadhi ya kuwa Vijiji 1,127. Idara ya Kilimo Mbinga iliandika barua kwa Katibu Mkuu, Wizara ya Kilimo na Chakula, lakini bado sijapata majibu. Wataalam tulionao ni wachache sana na inawawia vigumu kutekeleza kazi zao kwa ufanisi mzuri. Tunaomba sana Wataalam.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, Wilaya ya Mbinga kwa muda wa miaka zaidi ya sita tumewahamasisha Wananchi wa Tarafa tatu kulima korosho na kwa hivi sasa kuna korosho zaidi ya miti mikubwa 300,000 na inazaa, kwa sasa tuna matatizo ya aina tatu:-

(a) Tuna Mtaalam mmoja tu wa korosho na wengine hawana utaalam wa zao hili na wanasimamia kwa kubahatisha. Tunaomba sana tuongezewe Wataalam wenye ujuzi wa zao hili. Kama hali ni ngumu, basi Wizara ifanye utaratibu wa kuwaandalia hao wengine kozi fupi fupi.

(b) Ingefaa sana utaratibu wa pekee ukafanyika ili wakulima wasaidiwe *sulphur.*

(c) Kwa kuwa Mbinga kuna Tarafa 3 zinazolima korosho, tunaomba sana Kituo cha Utafiti kilichofungwa Rwanda kifunguliwe ili kiweze kutoa huduma kwa wakulima wa korosho Wilaya ya Mbinga.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, Wananchi wengi wanafuga kuku wa kienyeji, lakini wanarudishwa nyuma na ugonjwa wa mdondo. Tunaomba Wataalam wetu wangefanya kila linalowezekana kuwasaidia Wanavijiji ili waweze kuongeza mapato yao kwa njia ya kufuga kuku wa kienyeji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, wakulima wetu wanapoteza sehemu kubwa ya mazao yao kabla na baada ya kuvuna. Tunaomba Wataalam wetu watafute njia ya kupunguza au kufuta kabisa tatizo hili. Vile vile, Wataalam watoe elimu, watafute njia rahisi na yenye gharama nafuu ili iwasaidie wakulima kuzuia upotevu huu wa mazao. Ahsante sana.

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishukuru Wizara ya Kilimo na Chakula, hasa kwa kazi kubwa iliyofanyika katika Wizara yake kwa kuzingatia ukurasa wa 41 kuhusu Udhibiti Husishi wa Visumbufu vya Mimea katika mwaka 2002/2003. Pia, katika Ibara ya 42 magugumaji katika Ziwa Victoria yamedhibitiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumzia kuhusu maeneo matatu: Eneo la kwanza ni kwamba, kulikuwa na Mradi wa *Tanzania Cotton Authority* katika Wilaya ya Geita, baada ya Mradi huo kwisha waliacha mali zisizohamishika *(assets),* kama nyumba na mashamba. *Assets* hizi zilikabidhiwa kwa Wanaushirika yaani *Nyanza Cooperative Union (NCU),* ambao wamekuwa wamiliki wa mali hizi na wamekaa nazo kwa muda mrefu kiasi ambacho sasa wameishiwa wanataka kuanza kuuza nyumba hizo ili kulipia madeni ya Benki.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasikia, sina uhakika, kuwa hatimiliki ya nyumba na mashamba haya yako chini ya Wizara yako. Je, hili ni kweli? Kama ni kweli ni kwa nini *NCU* wauze hizo nyumba bila ridhaa yenu au mmewaruhusu kutumia mali hii bila kuwashirikisha? Naomba Wizara ya Kilimo na Chakula isitishe zoezi linaloendelea la kuuza nyumba za Mradi wa *Tanzania Cotton Authority* ili muweze kuchukua mali zenu ambazo zinataka kutolewa kinyemela.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ni kuhusu Mradi wa Umwagiliaji Maji kutoka Ziwa Victoria. Itakuwa ni jambo la kushangaza ikiwa tuna maji mengi halafu yanawanufaisha Wananchi wa nchi za mbali kama Misri na sisi hapa tunaogopa Sheria za Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya yetu ya Geita tuna maeneo makubwa ya mbuga, kama tungepata Mradi wa Umwagiliaji Maji, basi eneo hilo lingeweza kwa kiasi kikubwa kupunguza tatizo la njaa hapa nchini mwetu. Namwomba Waziri wa Kilimo na Chakula atume Wataalam wake waje Geita katika maeneo ya Nzera, Rwezera sehemu ya Ziwa ambayo mbuga hii imeanzia na kuenea maeneo ya Wilaya jirani ya Sengerema katika Mbuga za Ibanda na Ngoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, kuna utaratibu wa kupeleka Miradi ya Majaribio katika Mikoa na Wilaya zenye maendeleo na zenye miundombinu yenye kueleweka. Najua katika Wilaya za Majaribio, Wilaya ya Geita haitakuwemo, lakini naomba isiachwe kwa sababu Wananchi wake ni maskini sana ingawa inazalisha Pato la Taifa kwa asilimia kubwa.

**MHE. FAUSTINE K. RWILOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naunga mkono hoja hii. Pia, ninampongeza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula, kwa hotuba nzuri, lakini ninaomba maelezo kwa mambo yafuatayo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri hakueleza wazi wazi ni vipi maji ya Ziwa Victoria yatatumika kwa umwagiliaji, ni maeneo yapi yatahusika na ekari ngapi? Kwa maelezo ya Waziri inaonekana hakuna tendo litakalofanyika kuhusu maeneo yanayozunguka eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuelezwa ni Wilaya zipi zilizochaguliwa katika mradi. Huenda ni zile zile zinazopendelewa mara kwa mara kwa sababu ya kuwa na watetezi wengi Wizarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna *ginnery* ya Bukoli - Geita, ilijengwa kwa fedha nyingi za Serikali (wakulima). Mwekezaji wake alitoroka nadhani na fedha nyingi sana. Serikali ina mpango gani wa *ginnery* hiyo ambayo mitambo yake inaendelea kuoza? Naomba maelezo kuhusu ufumbuzi wa *ginnery* hiyo kuanza kazi

**MHE. TALALA B. MBISE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri wa Kilimo na Chakula, Mheshimiwa Charles Keenja, Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Prof. Pius Mbawala na timu nzima ya Wizara, kwa hotuba nzuri ya Bajeti ya Wizara na yenye matumaini.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia kama ifuatavyo: Kwanza, shamba la Madiira liko Kata ya Seela/Singisi, Jimbo na Arumeru Mashariki km 14 kutoka Arusha Mjini kuelekea Moshi. Kufuatia kilio na ombi la Wananchi wa Arumeru Mashariki kuhusu uhaba wa ardhi ya kuishi na kilimo, Mheshimiwa Rais, Benjamin William Mkapa, alitafuta hatimiliki *(lease)* ya shamba hili, pamoja na mashamba mengine ili yagawiwe kwa Wananchi wa Arumeru, ikiwa ni pamoja na Wananchi wa Seela/Singisi, hiyo ilikuwa takriban miaka 4 - 5 iliyopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapouliza Wizara husika kwa nini shamba la Madiira wasigawiwe Wananchi walengwa, tunaambiwa Wizara ya Kilimo na Chakula imelisimamisha kwa kigezo kwamba, ni mali ya Wizara, yaani Wizara ilishalinunua. Kufuatia swali langu Bungeni mwezi Aprili, 2003, Wizara ya Ardhi na Makazi iliahidi kuonana na Wizara ya Kilimo na Chakula, ili washauriane na kufikia muafaka wa suala la Shamba la Madiira. Wananchi wana dhana kwamba, Wizara ya Kilimo na Chakula ndiyo inayowanyima haki waliyopewa na Rais wao na hawaelewi ni kwa vipi hii inawezekana!

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri ni tamko kuhusu Shamba la Madiira. Kama hiyo haiwezekani sasa, basi atoe ahadi ya kukutana na Wananchi wa Seela/Singisi kuwaeleza hatma ya Shamba la Madiira. Tutamkaribisha kwa moyo mkunjufu na kwa mikono miwili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata za Makiba na Mbuguni zilizopo Tarafa ya Mbuguni ni *grain basket* ya Arumeru Mashariki na labda Arumeru yote. Tatizo kubwa ni kwamba, zinategemea umwagiliaji kwa kutumia maji ya Mto Kikuletwa. Maji ya Mto huo hutegemea kiasi cha mvua za masika na wakati mwingine mvua za vuli. Maji ya mvua ya nyakati hizi ni mengi sana, yakivunwa yataweza kukidhi kwa kiasi kikubwa mahitaji ya umwagiliagi kwenye hizo Kata mbili za Makiba na Mbuguni. *AFGEM* (Mererani) wameonyesha *interest* ya kusaidia kujenga mabwawa ya kuvunia maji ya mvua yanayofuata mikondo ya mito ambayo si *all weather.*

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri ni kutembelea maeneo haya na kutuunga mkono kwenye hoja ya kuomba msaada *AFGEM* wa kujenga mabwawa ya kuvuna maji ya kumwagilia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Kilimo Tengeru kimesahaulika na hali yake inazidi kudorora. Bajeti ya *maintenance* na uendeshaji haitoshi, hadhi yake inaendelea kushuka wakati ambapo wanafunzi na wateja wengine kutoka nje ya nchi wanaongezeka, hasa kutoka nchi za *SADC.*

Mheshimiwa Naibu Spika, yaelekea kuna hali ya kutegeana kati ya Wizara tatu za Kilimo na Chakula, Maji na Mifugo na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Huenda tatizo ni kwamba haifahamiki ni nani mwenye Chuo kati ya Wizara hizo tatu. *All of them are responsible but none is responsible.* Sasa inabidi Serikali itambue ni nani awajibike kutatua matatizo ya Chuo cha Tengeru. Bajeti yao iongezwe, majengo yakarabatiwe, umeme na maji ziwe huduma za uhakika.

**MHE. BAKARI M. MBONDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Waziri wa Kilimo na Chakula, kwa imani kwamba, Sekta ya Kilimo sasa imepewa msukumo mpya. Sote tunafahamu ili tuondokane na umaskini kwa Watanzania walio wengi, matumaini yapo kwenye Kilimo na Ushirika. Kama tutaendelea na kilimo duni na Ushirika ukaparaganyika, basi Watanzania tutaendelea kuwa duni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuipongeza Wizara ya Kilimo na hasa Naibu Waziri, Mheshimiwa Prof. Pius Mbawala, kwa msukumo na jitihada zake binafsi kuhakikisha kwamba, *Tanzania - Japan Food Aid Counterpart Fund* inatupatia mamilioni ya Shilingi kwa ajili ya Kilimo cha Umwagiliaji Segeni, Wilayani Rufiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa ushauri ufuatao: Kwanza, ni kuhusu huduma za ugani. Sikubaliani na ushauri wa Kamati kwamba, Maafisa Kilimo na Maafisa Ugani wasimamiwe moja kwa moja na Wizara. Ni vyema Maafisa hao wakawajibika moja kwa moja kwa Halmashauri kwa vile huduma za ugani kwa wakulima ni muhimu na kwa vile kilimo ni sehemu ya shughuli za maendeleo kwenye Halmashauri. Ni vyema Maafisa hao wakawajibika kwa Halmashauri ili kuwe na usimamizi wa karibu na kuondoa mparaganyiko katika uwajibikaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ni kuhusu matokeo ya utafiti. Utafiti usiwe ni zoezi la kitaaluma *(Academic Exercise)* tu, bali tafiti zisaidie kuinua kilimo na itawezekana hivyo tu kama utafiti utawafikia wakulima. Hii ina maana kwamba, huduma za ugani lazima ziimarishwe. Kwa kuanzia tuwe na utaratibu wa kuwa na Afisa Ugani kwa kila Kata kama siyo Kijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu huduma za matrekta, tunaweza kuongeza uzalishaji kwa kuongeza maeneo ya kilimo au kupanda kitaalam kwa eneo lililopo. Tatizo kubwa sasa hivi ni uhaba wa matrekta na uhaba wa huduma za ugani. Katika Wilaya ya Rufiji tunayo matrekta manne, pia, tunacho Kituo cha Kukodisha Matrekta *(Farm Mechanization Centre)*, lakini kimekufa. Nashauri kituo hicho cha Mkongo Wilayani Rufiji kifufuliwe. Kama tukipata matrekta kumi, ni dhahiri kilimo kitakuwa mkombozi katika Wilaya ya Rufiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Rufiji ina ardhi nzuri inayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji. Wilaya ya Rufiji ni muhimu sana endapo Serikali itawekeza kilimo kwenye Wilaya hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Waziri, Naibu Waziri na Watumishi wote wa Wizara ya Kilimo na Chakula, lakini wajue kwamba kilimo ndiyo uchumi muhimu Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SULEIMAN A. SADDIQ:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, ninampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba nzuri ya matumaini na pia kabla sijachangia naomba kutamka kwamba naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa ushauri kwenye maeneo yafuatayo: Kwanza, ni eneo la umwagiliaji. Eneo hili limechangiwa sana na Waheshimiwa Wabunge wengi na wanaona ndiyo mkombozi katika kilimo. Kwa mtazamo wangu naona siyo sahihi kwani nchi yetu ina hali nzuri ya hewa na tunapata mvua nchi nzima angalau mara moja kwa mwaka. Yapo maeneo mengi ambapo Wataalam wameshirikiana na wakulima, wamejipanga vizuri na wamefanikiwa sana bila ya kutumia umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sipingi kilimo cha umwagiliaji, pia nakubaliana na baadhi ya maeneo kupewa kipaumbele, lakini ushauri wangu ni kwamba, kilimo cha sasa kinachotegemea mvua nacho kipewe kipaumbele. Kwa kuona mifano hai ya mafanikio katika maeneo mengi ya nchi yetu, nashauri Wizara isimamie suala hili kwa kuwatumia Wataalam na pia maeneo ya uhakika yatazamwe kwa macho mawili, kwa maana ya kujua matatizo ya wakulima. Yapo maeneo Serikali ikiweka malengo tutafanikiwa mfano ni Mkoa wa Morogoro, nasikitika Wizara bado haijatoa maelekezo rasmi kwa kila Wilaya ni nini kifanyike.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo nashauri litazamwe ni *Dakawa Rice Farm*. Inasikitisha sana kuona shamba zuri na kubwa kama hili halina faida yoyote kwa Taifa letu. Ni muda mrefu hatuna uamuzi kamili wa Serikali, kuna ngonjera za muda mrefu na uamuzi usio na utekelezaji. Wananchi wa Kijiji cha Dakawa muda mrefu hawana maendeleo na wanazidi kuwa maskini kutokana na Wizara kutosimamia hatma ya shamba hili. Leo kuna kundi la watu wachache wanaotumia ubabe na kufanya shamba ni mali yao na maji ya umwagiliaji ni haki yao na hao ndiyo wanazorotesha juhudi zote za Viongozi na maelekezo yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri twende Dakawa, tupewe shamba kwani Wananchi wamejipanga eneo hili kulima mazao ya biashara na chakula ikiwemo mpunga na miwa. Naomba sana suala hili litolewe kauli katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Ombi langu ni kwamba, tukae na Wanavijiji na wadau wengine, tugawe shamba, tunawapa umaskini Wananchi wa maeneo jirani wakati utajiri upo mbele ya macho yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la mwisho ambalo napenda kuishauri Wizara kuwa makini sana ni Sikukuu ya Wakulima (Nane Nane). Inapofika sikukuu hii wakulima huelekeza macho na masikio yao kwenye eneo hili kwa lengo la kutaka kusikia Wizara inatamka nini na wakulima wameandaliwa nini. Tuna utaratibu mzuri wa kufanya sikukuu hii Kitaifa na Kikanda. Nashauri utaratibu uwe hadi Vijijini na Wataalam wasimamie.

Mheshimiwa Naibu Spika, sherehe hizi mwaka 2002 Kitaifa zilifanyika Morogoro na Viongozi wa Kitaifa waliofika pale walishauri angalau kwa miaka mitatu maonyesho yale yangefanyika katika uwanja ule. Inasikitisha mpaka leo hakuna kauli au tamko rasmi la Wizara kuwa Kitaifa mwaka huu Nane Nane

itakuwa Morogoro. Uongozi wa Kanda hii umeshaanza maandalizi ya awali katika uwanja huo. Hivyo, nashauri Serikali itamke rasmi ili wadau waanze maandalizi yao mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matumaini yangu kuwa hoja zote tatu zitapata majibu muafaka na naunga mkono hoja.

**MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Pili, naomba kutoa pongezi zangu za dhati kwa Waziri wa Kilimo na Chakula, Mheshimiwa Charles Keenja, Naibu Waziri, Mheshimiwa Prof. Pius Mbawala na bila kuwasahau Watendaji wote wa Wizara hii, pamoja na Idara zake zote, kwa umoja wao na kuandaa hotuba hii ambayo *Insha-Allah* Mwenyezi Mungu atayafanikisha yale ambayo yamekusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba hii imezungumza mambo mengi sana, lakini Mheshimiwa Waziri hakuzungumzia hata kidogo kuhusu zao la minazi, ambalo ndilo zao la biashara katika Kanda nzima ya Pwani, pamoja na kuwa kuna Kituo cha Utafiti wa Minazi kilichopo Mikocheni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Mheshimiwa Waziri, azungumzie zao hili ili Wananchi waliopo katika Ukanda huu wa Pwani hasa Mafia, basi wajione kuwa Serikali pia inatambua juhudi za Wananchi na kulitambua zao hili la minazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, hivi sasa minazi kuanzia maeneo ya Wilaya ya Mkuranga hadi Rufiji inakufa, ni kwa sababu gani? Je, maradhi gani yanayoua minazi hiyo? Je, hakuna dawa? Je, haiambukizi? Je, ni tahadhari gani inachukuliwa kudhibiti ugonjwa huo usienee katika maeneo mengine? Je, katika Kisiwa cha Mafia tujikinge vipi na maradhi hayo, maana hayajafika na Mungu atunusuru?

Mheshimiwa Naibu Spika, kule Mafia maeneo ya Tereni kuna nyumba ambazo zipo chini ya Wizara ya Kilimo na Chakula au Kituo cha Utafiti cha Mikocheni *(NGDP)*. Naomba kuchukua fursa hii kuomba nyumba hizo ili tuweze kufanya majengo ya Shule ya Sekondari ya Wasichana na naomba kwa niaba ya Dayosisi ya Pwani (Dar es Salaam) ya Kanisa Katoliki. Wao wana nia ya kufanya hivyo na tayari Muadhama Kardinali *Polycarp* Pengo, nimeshampeleka kwenda kuyaona japokuwa sikuomba ridhaa kutoka kwa wamiliki, naomba msamaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima kubwa tunaomba tena hayo majengo ili tuyaokoe. Baada ya hapo narudia tena kuunga mkono hoja hii na ninawatakia kila la kheri na baraka katika kukiendeleza kilimo katika nchi yetu. Mungu bariki kilimo katika nchi yetu ya Tanzania.

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nitamke kuwa ninaunga mkono hoja hii ya Wizara ya Kilimo na Chakula. Pili, Mkoa wa Morogoro ni mmoja ambao unaweza kujitoa kabisa katika mzunguko wa njaa. Huu ni Mkoa wenye mito ya kudumu mwaka mzima na inatokana na sifa ya kuwa na milima na mabonde. Je, ni kwa nini basi Morogoro hawazalishi chakula cha kutosha?

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima wa Morogoro bado wanalima kizamani, wanategemea Mungu kuleta mvua na kujaza mito ili ifurike na makonde yajae maji. Hawamwagilii kwani utaalam huu hawana na hakuna wataalam wa kufundisha umwagiliaji. Mito mingi iko chini sana na hivyo umwagiliaji ambao unafaa ni wa *pump* za kuvuta maji mtoni na kumwaga kwenye mashamba. Pia, mkulima wa Morogoro sasa hivi anahitaji bei ya uhakika ya mazao. Kutokujua bei ya mazao mkulima hajui alime nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwa teknolojia inahitajika katika Jimbo la Morogoro Kusini, haishindi uhakika wa bei. Naomba rasmi kuwa tunahitaji matrekta ya kukodisha kwenye Kata za Mvuha, Selembala, Bwakira Chini, Mngazi na Kata ya Kisaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata hizi zipo kwenye tambalale na zinaweza kuzalisha chakula cha kulisha Morogoro yote. Mheshimiwa Waziri, ni shahidi kwani alipotembelea hadi Duthami alijionea mwenyewe ardhi nzuri, lakini umaskini wa watu unaonyesha jinsi wasivyoweza kulima kwa kiasi kikubwa.

**MHE. HALIMENSHI K. R. MAYONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba pesa za *STABEX* za kujenga barabara za Vijijini zigawanywe kwa Mikoa ilimayo zao la Kahawa kwa usawa, Mkoa wa Kigoma hulima zao hilo. Pia, pesa za umwagiliaji katika Jimbo langu ninapendekeza sehemu za Pamila, Msimba na Nsamwa, ninaomba sehemu hizo zipatiwe msaada huo.

**MHE. MWADINI ABASS JECHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba nichangie kuhusu soko kwa mazao ya mkulima hususan mazao ya mboga na matunda. Kama tunavyofahamu kwamba, mazao mengi ya mboga na matunda ni ya msimu. Wakulima huchukua jitihada kubwa kuzalisha mazao hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini bahati mbaya msimu wa uzalishaji unaposhamiri, bei ya mzaao hayo hushuka sana na kumletea hasara mkulima. Aidha, nichukue nafasi hii kuwapongeza wale wote ambao wamewekeza katika viwanda vya kusindika mboga na matunda. Kwani kwa kufanya hivyo tunamkomboa mkulima kwa kumpunguzia hasara na kupunguza uharibifu wa mazao. Bidhaa zinazosindikwa huwa zinapatikana katika soko hata kama msimu wa uzalishaji umepita. Kubwa zaidi hali hiyo humshawishi mkulima kuongeza nguvu yote ya uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini uwekezaji katika viwanda vya kusindika mboga na matunda bado ni mdogo haujaweza kukidhi mahitaji. Tunashuhudia wakati wa msimu wa uzalishaji wa mazao hayo, mananasi, maembe, machungwa, nyanya maparachichi na kadhalika, huwa yanazagaa kila pembe kuonyesha kwamba, bado juhudi kubwa inahitajika kutafuta wawekezaji watakaoweza kuitumia mali ghafi yote inayozalishwa na wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kama hii huwa inawakumba wakulima wa Zanzibar. Kule Zanzibar katika misimu ya uzalishaji wa matunda na mboga (machungwa, ndimu, malimao, shokishoki, maembe, mananasi na nyanya), huwa ni mkubwa sana kiasi ambacho soko la ndani linazidiwa. Kwa bahati mbaya Zanzibar hakuna viwanda ya kusindika matunda na mboga, matokeo yake wakulima hupata hasara kubwa. Aidha, hatua zinazochukuliwa na Serikali kuwahimiza wakulima kuzalisha zaidi bila kuangalia wapi watapata soko madhubuti ni kuwatafutia janga wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuepuka hayo ninamwomba Mheshimiwa Waziri, ajaribu kuona umuhimu wa kuandaa utaratibu utakaowawezesha wawekezaji kupata hamu ya kuwekeza katika viwanda vya kusindika mazao ya wakulima. Aidha, kutokana na mashirikiano yaliyopo baina ya Wizara za Serikali ya Muungano na za Serikali za Zanzibar (ambazo si za Muungano) ninamwomba Mheshimiwa Waziri, ashirikiane na Waziri mwenzake mwenye dhamana ya Kilimo Zanzibar, ili Zanzibar nayo inufaike katika hii azma nzima ya kutafuta wawekezaji ambao watawekeza katika viwanda vya kusindika matunda na mboga.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na wataalam wote wa Wizara ya Kilimo na Chakula, chini ya Katibu Mkuu, kwa kuandaa mpango na hotuba nzuri, yenye maelezo marefu na ya kina.

Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia kilimo, zipo aina mbili za kilimo. Kilimo cha mazao ya chakula na kilimo cha mazao ya biashara. Tunapozungumzia kilimo ni lazima tukumbuke kwamba, wanawake ndio wakulima wakubwa (kwa asilimia) wa mazao ya chakula. Wanawake wanafanya kazi hii kwa zana na utaalam duni na hivyo mara nyingi katika maeneo mengi uzalishaji pia huwa duni. Ninashauri na kutegemea kwamba, Wizara katika mpango wake wa *PADEP* itawapa umuhimu wanawake. Wanawake wanahitaji mafunzo juu ya kanuni za kilimo na namna ya kuhifadhi chakula na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia kwako, namwomba Mheshimiwa Waziri, atafute kila njia ya kuusaidia Mradi wa *KAEMP,* yaelekea Mradi huu ulianza *Top - Bottom* badala ya kinyume chake hivyo wananchi hawakuelewa mapema, ilichukua muda mrefu kuuelewa na kushiriki. Sasa wakati mradi unaelekea kumalizika ndipo wananchi wanaanza kuuchangamkia. Tunaomba wafadhili wa mradi huu waendelee kutoa msaada ili wananchi wafaidi maana hapo mwanzo hawakuelewa malengo yake. Kwa ujumla mradi ulikuwa na malengo mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda niunge mkono kwa dhati Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Kilimo na Chakula, kwani imekidhi matarajio ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizi napenda kutoa ushauri ufuatao:-

Moja, kuboresha Miradi ya Umwagiliaji *(PIDP/IFAD),* Wilaya ya Manyoni ni miongoni mwa Wilaya 12 zenye Miradi Shirikishi ya Umwagiliaji. Miradi imeanza vizuri na walengwa wameanza kupata tija. Hata hivyo, itafaa hatua kwa hatua, Wizara iboreshe skimu hizo kwa kuzipatia vianzo vya maji ili walengwa wawezeshwe kulima na kuvuna mara mbili au tatu kwa mwaka. Tunaomba jitihada za makusudi zifanyike kuchimba mabwawa hayo kwa kila mwaka kwa kila Wilaya zenye skimu hizo.

Pili, kuhamasisha kilimo cha plau. Tunapongeza jitihada za Wizara hii za kufufua vituo vya kufundishia maksai hasa katika maeneo yenye mifugo mingi. Hata hivyo, namna moja ya kuhamasisha kilimo cha plau ni kusambaza kwa wingi plau za kukokotwa na maksai kwa kuwakopesha walengwa. Wizara imefanya vizuri kushusha bei ya matrekta madogo na kuyakopesha. Hatua kama hiyo itafaa ifanyike kwa majembe ya kukokotwa na ng'ombe (plau). Hatua hii itaongeza eneo linalolimwa kwa plau kutoka asilimia 20 ya sasa hadi asilimia 50 - 60, hasa katika Wilaya zenye mifugo. Lakini tatizo leo ni mwamko mdogo wa kutumia ng'ombe hao katika kilimo.

Tatu, kilimo cha mbegu za mafuta *(Oil Seed Crops).* Mikoa ya Kanda ya Kati imebobea katika umaskini wa kipato kutokana na kukosa mazao ya uhakika ya biashara. Lakini ukanda huu una uwezo mkubwa sana wa kuzalisha mazao ya mbegu za mafuta kama karanga, alizeti, ufuta na nyonyo. Bahati mbaya sana hatuna mipango kamambe ya kuendeleza mazao haya katika ngazi ya Taifa, Hotuba ya Wizara hii ni shahidi na hata katika ngazi ya Wilaya. Wataalam wa kilimo wa ngazi hizo wapewe changamoto hii, Kanda ya Kati igeuzwe kuwa *Big One* katika kilimo cha mbegu za mafuta. Viwanda vidogo na vya kati vinavyoendelea kufunguliwa ili kusindika mafuta viunganishwe katika mpango wa kilimo hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia kusema kwamba, naunga mkono hoja hii.

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii, kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara, kwa malengo ya kisera yaliyoainishwa katika utekelezaji wa kazi zenu kwa mwaka 2003/2004. Hivyo, ninayo machache ya kuchangia ili kuboresha utekelezaji kwa ajili ya kuinua kilimo chetu.

Moja, huduma za ugani kwa mkulima mmoja mmoja ni duni sana, Serikali iwe na kampeni ya makusudi kuhuisha huduma hii ambayo kwa sasa imekufa kabisa vijijini.

Pili, naipongeza Serikali kwa kuhuisha masoko ya tumbaku kwa msimu uliopita. Lakini nailalamikia Bodi ya Tumbaku kwa ratiba zake za ununuzi zilizofuata baada ya ufunguzi wa masoko. Bodi ilitengeneza ratiba ya soko mara moja kwa mwezi, hali hii ni ya unyanyasaji kwa wakulima. Napongeza jitihada zilizofanywa na wataalam kadhaa waliotumwa kusawazisha kasoro hii. Naiomba Serikali ihakikishe jambo hili halirudiwi tena katika misimu ijayo na ninaiomba Bodi ya Tumbaku kuwa na mawasiliano ya mara kwa mara na viongozi wa maeneo ya wakulima hasa Waheshimiwa Wabunge wanaopata kero za aina mbalimbali za wakulima.

Tatu, tunalo tatizo la uhifadhi wa mazao ya nafaka, kwa mfano, mahindi na kadhalika. Mpaka sasa wananchi wanajitahidi kununua madawa ya kuhifadhia nafaka, lakini yamekuwa hayakidhi haja ya

uhifadhi kwani nafaka zimeendelea kuharibika na kuwaweka wakulima wetu kwenye hatari ya kupata njaa hata kama walikuwa na chakula cha kutosha. Naiomba Serikali itoe tamko juu ya suala hili ili wananchi wetu waweze kupata ukweli wa madawa haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii, nikizingatia kuchukuliwa na kufanyiwa kazi ushauri wangu nilioutoa.

**MHE. MWADINI ABASS JECHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nachukua nafasi hii kushukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia katika hoja hii.

Pili, naomba nimpongeze Waziri wa Kilimo na Chakula, Mheshimiwa Charles Keenja, kwa Hotuba yake nzuri na yenye mwelekeo wa kuleta Mapinduzi ya Kilimo hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda pia niipongeze Kamati ya Bunge ya Kilimo na Ardhi, kwa taarifa yake ambayo inalenga katika kuboresha utekelezaji wa shughuli za kilimo kwa ujumla.

Halikadhalika, ninampongeza Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Msemaji Mkuu wa Upinzani kwa Wizara ya Kilimo na Chakula, kwa kutoa mwelekeo kwa Serikali katika mambo mbalimbali, ambao utaboresha uzalishaji wa chakula nchini. Nianze kuichangia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri na zaidi nitazungumzia suala la utafiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niseme niko tofauti kimtazamo na wale wanaodhani kwamba, shughuli za utafiti wa kilimo kwa sasa hauna umuhimu na kuwa fedha zote zilizotengwa kwa shughuli za utafiti zielekezwe moja kwa moja kwa mkulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima tufahamu kwamba, shughuli yoyote yenye kuelekezwa katika kuleta mabadiliko inahitaji kufanyiwa utafiti wa kina. Madhumuni ya utafiti ni kutuelekeza kujua mwelekeo wa kufuata, namna ya kuutekeleza, faida na hasara itakayopatikana. Ni katika hatua hizo na nyingine, ndio hutufanya kutoa maamuzi muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo ni sayansi, sayansi haiendi au haitekelezwi kwa kubahatisha. Inahitaji kufanyiwa utafiti wa kina na ulio endelevu. Vinginevyo, itakuwa siku zote wakulima wanakosa utaratibu maalum wa uzalishaji mazao na hatimaye ni kupata mavuno kidogo na hafifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, umuhimu wa utafiti unakuja kutokana na sababu kwamba, shughuli za kilimo ili zifanikiwe zinategemea mambo mengi miongoni mwake ni ardhi, maji, hali ya hewa, pembejeo, taaluma na mengine mengine. Yote haya huwa yanabadilika kulingana na hali ya mazingira ilivyo. Kwa namna yoyote ile utafiti katika masuala hayo ni jambo la lazima ili kwenda na badiliko la mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niseme tu kwamba, Serikali imekuwa inatumia fedha nyingi sana katika kugharamia *on station research,* katika vituo mbalimbali (Chuo Kikuu cha Sokoine, Uyole, Kibaha, Ukiriguru, Naliendelee, Selian na kadhalika).

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi matokeo ya tafiti hizi huwa hayamfikii mkulima kabisa kabisa na huishia makabatini kwenye *files* au huchelewa kumfikia na hatimaye huwa kwa wakati ule hauna faida kwa yeye. Haya hutokea pale ambapo hakuna ushirikiano baina ya utafiti, ugani na mkulima, kama ambavyo hali inaonekana hivi sasa hapa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi za dunia ya tatu, ambazo zimepiga hatua katika Mapinduzi ya Kilimo, walielekeza nguvu zao kufanya utafiti mashambani kwa kuwashirikisha wadau wote (watafiti, wagani na wakulima). Utafiti wa aina hii huitwa *On Farm Research.*

Mheshimiwa Naibu Spika, uzuri wa aina hii ya utafiti unajenga mahusiano mazuri baina ya wadau niliowataja hapo awali. Lakini pia mkulima anapata fursa ya kujifunza kwa vitendo jinsi ya kuendesha tafiti ndogo ndogo kulingana na mazingira yanayomzunguka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia hayo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, zile fedha zilizotengwa kwa ajili ya kuendeleza utafiti wa kilimo, basi mkazo zaidi auelekeze kwenye tafiti za mashambani *(On Farm Research)* kwani mkulima ambaye ndiye mlengwa atafaidika zaidi na Mapinduzi ya Kilimo, yatakayopatikana kwa muda mfupi kabisa.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kwa njia ya maandishi, nampongeza Waziri wa Kilimo na Chakula, Mheshimiwa Charles Keenja, Naibu Waziri, Mheshimiwa Prof. Pius Mbawala, Katibu Mkuu, pamoja na watendaji wote walioshiriki kuandaa Bajeti hii yenye mwelekeo wa kuboresha Sekta ya Kilimo na Chakula kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza pia Serikali kwa kuona umuhimu wa kuongeza Bajeti hii. Nadhani sasa tunasubiri utekelezaji kwani Waswahili husema maneno sio matumizi bali matendo. Nimwombe Mheshimiwa Waziri, akumbuke kutoa huduma sawa kwa wakulima wote wanaojishughulisha na kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima wanajitahidi sana kulima mazao mbalimbali ya chakula na biashara bali hawana utaalam wa kutosha ili waweze kulima kilimo cha kisasa kwa kulima eneo dogo kitaalam na kupata mavuno mengi yenye kukomaa barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inatokana na Maafisa Ugani kuwa wachache hasa kwa ngazi ya vijiji, ambao ndio hawa tunawategemea kutoa taaluma hii kwa wakulima. Hata ngazi ya Kata na Tarafa, ambapo ndiyo wangefanya kazi ya kuwatafutia mbegu bora na za kisasa. Vilevile Maafisa hawa hawajishughulishi hata kulima mashamba ya mfano ili wananchi waweze kuiga mfano wao. Naiomba Serikali iweke sheria ya kila Bwana Shamba awe na shamba la mfano kwa ajili ya wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali ihakikishe kila Kijiji, Kata na Tarafa, ina Afisa Ugani ili waweze kusimamia kilimo bora, kilimo cha wakati, upatikanaji wa mbegu bora na madawa ya mimea. Vile vile inaonekana Maafisa hawa taaluma zao zimeshuka kwani wengine walisoma miaka mingi iliyopita. Hivyo, nashauri semina, warsha na kozi fupi zifanyike kwa maafisa hawa kuboresha taaluma zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata utaratibu wa Maafisa Ugani kukaa kituo kimoja kwa miaka mingi unawavunja moyo ama wanalowea na kuanzisha biashara zao badala ya kufanya kazi iliyowapeleka hapo na inayowapa kipato. Utaratibu wa Serikali uheshimiwe wa mtumishi kukaa miaka mitatu hadi mitano halafu ahamishwe.

Naibu Naibu Spika, ni kweli wakulima wanajitahidi kulima na kuvuna mazao ya kutosha bali Serikali haiwasaidii kuwapa madawa ya kuzuia nafaka isipekechwe wanapohifadhi kwa matumizi ya muda mrefu, kwani madawa wanayouziwa madukani yanaonekana hayafai kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti hii imetamka bayana kukopesha pembejeo kwa wakulima. Naiomba Serikali itoe mikopo hii moja kwa moja kwa walengwa kwa muda muafaka ili wasipitwe na msimu wa kilimo kwa kutokuwa na pembejeo na elimu itolewe na taratibu zipi zinafuatwa kupata mikopo hii kwenye Vyama vya Ushirika au benki mbalimbali ambazo zitakuwa zimeandaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati nachangia Bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, niliongelea kilimo cha umwagiliaji na nimeona nirudie tena kwa Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana awakumbuke wakulima wa bustani za mboga wa Singida Mjini wapatiwe ufumbuzi wa maji kwani maji wanayotumia hukauka mapema. Kwa kweli bustani hizo ni mkombozi sana kwao, za maeneo ya Ziwa Singidani na Ziwa Kindai na maeneo mengine mengi kwa Wilaya zote za Mkoa wa Singida.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Singida unalima mazao mengi ya biashara kwa mfano, alizeti, pamba, dengu, vitunguu, ufuta na kadhalika. Pamoja na soko huria, lakini ni bora wakulima wakawa na soko la uhakika kuliko utaratibu wa sasa mkulima anavuna mazao anakuwa na kazi kubwa kuyasafirisha kwa ajili ya kutafuta soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mazao mengine ambayo yanaweza kukamuliwa huko huko vijijini mfano zao la alizeti. Naomba wakulima wenye uwezo wakopeshwe mashine hizo ili waweze kuzijengea huko vijijini kupunguza gharama za kusafirisha mazao kufuata mashine za kukamua mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusema kuwa wanawake hawapo mbali na suala zima la kilimo. Hivyo wapewe kipaumbele kuwakopesha ili wapate nyenzo za kilimo. Natumaini Mheshimiwa Charles Keenja, ni shahidi alijionea mwenyewe katika ziara yake Mkoani Singida aliyoifanya kwa siku 8 alipokuwa anaelezwa kupitia Mpango Shirikishi Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie pia nafasi hii kumpongeza Waziri wa Kilimo na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Prof. Pius Mbawala, kwa msaada wa mbegu za korosho alizotoa kwa Wabunge wote wa Mkoa wa Singida. Sasa mbegu hizo zimekuwa changamoto kubwa kwa wakulima ni matumaini yangu sasa zitaletwa kwa wakulima, wengi wanapenda kulima zao hili la korosho.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kutamka rasmi kuwa naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri, ajibu hoja zangu ili wakulima wa Singida wapate faraja kwa Serikali yao.

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula, kwa hotuba nzuri ambayo inatoa dira ya namna ya kuiendeleza Sekta ya Kilimo na Chakula kama Sekta Kiongozi katika uchumi wa nchi yetu kwa mwaka huu wa 2003/2004. Ili kuboresha zaidi, naomba nitoe ushauri wangu kama mwakilishi wa watu kama ifuatavyo:-

Moja, kuupa nguvu utafiti. Chuo cha Kilimo na Kituo cha Utafiti cha Uyole vipewe nyenzo madhubuti za kufanyia utafiti, bila fedha za kutosha haiwezi kuleta ufumbuzi wa matatizo ya wakulima. Pia watumishi wa Kituo hiki cha Utafiti wanalalamika kutopata *promotion* zao kwa muda mrefu zaidi. Karibu asilimia 50 ya watumishi hawajapata *promotion* zao kwa muda mrefu sasa. Pia rejea barua yangu ya taarifa ya ziara.

Pili, Watumishi waliokuwa chini ya Shirika la Kilimo la Uyole wanadai haki yao kwa kipindi cha miaka 10 ya utumishi wao. Kwanza, wale ambao wamerudishwa Serikalini wanataka kujua haki zao zimepelekwa wapi? Pili, wale ambao walisimamishwa au kupunguzwa kazi mpaka sasa wanadai haki zao. Katika hili naomba Mheshimiwa Waziri, unipatie majibu sahihi kwani wawakilishi wa wafanyakazi hawa wapo hapa kujua hatma ya maisha yao.

Tatu, fedha za *STABEX,* pamoja na dhamira nzuri ya kuboresha utafiti wa kahawa, ingefaa pia fedha kiasi ziende kwa wakulima moja kwa moja pia badala ya kuelekezwa fedha zote Kituo cha Lyamungo, kwa nini fedha hizo zisiende kuimarisha Kituo cha Utafiti cha Uyole na hasa Kituo cha Kahawa Mbimba Mbozi, ambacho kinaelekea kufa sasa, eneo ambalo lilikuwa na mashamba ya mfano.

Nne, kilimo cha pamba, kwa kuwa viwanda vingi kama *Mbeya Textiles, Mbeya Ginneries, Mbeya Industries, Highlands Ginneries,* vyote hivi vimefungwa kwa kukosa malighafi ya pamba. Utafiti uliofanywa unaonyesha wazi kuwa upo uwezo wa kumdhibiti mdudu *red boll, reference* za utafiti ninazo. Nyuzi za pamba za mbegu ni zile ndefu, nzuri. Suala la pamba ni siasa kwetu, hivyo ni vyema Mheshimiwa Waziri, ukatueleza ni lini tutaanza kulima pamba tena. Sisi kama viongozi tupo tayari kuwa na mashamba ya mfano. Suluhisho la tatizo la ajira, malighafi kwa viwanda vyote vya Mbeya ni kuwepo kilimo cha pamba.

Mwisho, ninaunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri, kwa asilimia mia moja.

**MHE. ROBERT J. BUZUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kuipongeza Serikali kupitia kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote. Juhudi dhahiri zimeonekana juu ya kuhifadhi kilimo kuwa nyenzo muhimu katika maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi mipango iliyopo, programu na miradi iliyowekwa inalenga kukiinua kilimo toka katika hali duni ya nyenzo za zamani hadi kuwa kilimo cha kisasa kinacholenga teknolojia mpya na utumiaji wa mabwawa katika kumwagiliaji maji mashambani. Ili kuboresha Bajeti na shughuli za Wizara, napenda kushauri juu ya maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hali ya kilimo nchini inaonyesha kuwa mazao ya pamba, kahawa na chai bei zake zinashuka katika soko la dunia. Napenda kushauri Serikali kuwa katika mpango wa kuboresha kilimo, ni vyema kwenda sambamba na kuhimiza kilimo cha mbogamboga kama mazao ambayo yatatumika kwa chakula na biashara maana ndiyo mazao yenye soko kubwa duniani. Badala ya kuendelea kung'ang'ana na mazao ambayo kiuchumi sasa hayalipi *(Not Viable Economically).*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ni vyema Serikali kwa ushirikiano kati ya Wizara mbili za Ushirika na Masoko, pamoja na Wizara ya Kilimo na Chakula, wakaoanisha mipango yao ili uzalishaji wa mazao ulenge juu ya yale yenye soko na upatikanaji wa masoko huelezwa mapema kabla watu/wananchi hawajaanza uzalishaji ili wafanye shughuli zao kwa uhakika wa masoko ili kuondokana na kilimo cha kubahatisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kilimo chetu kinaelekea kulenga umwagiliaji zaidi, nashauri Serikali pamoja na juhudi zinazofanywa za kuainisha maeneo ambayo yatafaa kwa kilimo cha aina hii, napenda kuiomba Wizara kukamilisha ahadi ya Naibu Waziri, Mheshimiwa Prof. Pius Mbawala, aliyoitoa katika ziara yake Jimboni Solwa hasa Kijiji cha Nduguti ya kujengwa bwawa ambalo litatumika kuhifadhi maji kwa lengo la umwagiliaji wa kilimo cha mpunga. Aidha, ili kukidhi haja hii, nashauri Vijiji vya Butini, Igembya na Nyida pia vitengenezewe au kuchimbiwa mabwawa kwa lengo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Wizara iendelee na utafiti wa kuainisha maeneo yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji. Katika Jimbo ninaloliwakilisha yako maeneo yaliyo kando ya mkondo wa Ziwa Victoria katika Kata za Salawe, Mwakitoryo, Solwa, Iselamagazi na Lyabukande ambavyo nashauri viingizwe kwenye mpango wa kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu tatizo la njaa, naomba Serikali kupitia Wizara hii kwamba ilete chakula mapema katika Wilaya zenye tatizo hili. Hasa nashauri katika Jimbo langu la Solwa chakula kiletwe kipindi hiki cha Julai, 2003, kwa kuwa tayari wananchi wengine hawana chakula kabisa. Aidha, ni vyema kutumia muda huu kwa kuwa wananchi wengi watakuwa wanao uwezo wa kifedha baada ya kuuza mazao yao ya kibiashara na hivyo itawawezesha kununua chakula hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango huo, naomba kuunga mkono hoja hii. Ahsante sana.

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie mawazo yangu machache katika hoja iliyo mbele yetu, hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula. Awali ya yote, naomba niunge mkono hoja hii na kumpongeza Mheshimiwa Charles Keenja, Naibu Waziri, Mheshimiwa Prof. Pius Mbawala, Katibu Mkuu na safu nzima ya wataalam, waliounganisha nguvu na ubunifu wao mpaka ikazaliwa hotuba nzuri iliyowasilishwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishukuru Serikali kwa uamuzi wa kutoa ruzuku ya mbolea kwa Mikoa ya Kusini Nyanda za Juu likiwemo Jimbo langu la Rungwe Magharibi. Bei ya juu ya mbolea ilikuwa imelalamikiwa sana na wakulima Jimboni kwangu. Bei ya mfuko mmoja wa mbolea ya uchumvi kilo 50 ilikuwa shilingi 20,000/=. Katika ziara yangu Jimboni kwangu hivi karibuni, mkulima mmoja alifanya mahesabu na kunieleza kwamba, ilibidi auze kilo 560 za majani ya chai ili apate mfuko mmoja wa mbolea. Nina imani kuwa kumpunguzia mkulima mzigo wa gharama hizi utaongeza ari ya wakulima wa chai, kahawa, viazi, kakao na mazao mengine katika Wilaya yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kitabu cha Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, suala la mbolea na madawa limepewa theluthi ya ukurasa wa 32, tafsiri yake ikiwa kwamba suala hili halipewi kipaumbele na Wizara husika. Ni dhahiri kupunguzwa kwa gharama kutampa mkulima uwezo wa kupata mbolea nyingi zaidi kwa kiasi kile kile alichotumia msimu uliopita, lakini haikuonesha ni hatua gani zimewekwa ili mbolea hiyo ipatikane. Sababu mojawapo iliyotajwa katika hotuba hii ni kuwa katika kipindi kilichoishia leo tarehe 30 Juni, 2003, upungufu ulitokana na baadhi ya Makampuni kutoagiza mbolea kwa wingi. Je, kasoro hii itarekebishwa vipi?

Vilevile suala ninaloongelea mara kwa mara ni kuhusu mbolea ya samadi na majani *(organic),* ikilinganishwa na ile ya kiwandani *(Chemical* au *Inorganic)*. Ni ukweli usiopingika kwamba, *organic manure* ni *more plant and soil friendly* kuliko mbolea ya chumvi. Rutuba ya ardhi haiathiriki, haina madhara ya kiafya kwa binadamu anayetumia mazao yaliyooteshwa na mbolea hiyo na yanapata bei nzuri mara nne au zaidi katika masoko. Ingawa hatujafikia uwezo wa kutengeneza *organic fertilizers* kwa kiwango *commercial*, nilitegemea kwamba, Wizara ingeonesha kwamba inatambua faida ya mbolea ya mboji ukilinganisha na ile ya chumvi, pamoja na kuelezea kuna mipango gani ya kuifanya ipatikane.

Katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ilifahamishwa kwamba, Serikali inaelekeza kwamba kila Wilaya ichague mazao ya kuyaendeleza, moja la chakula na moja la biashara. Napenda kumfahamisha Mheshimiwa Waziri kwamba, kama inawezekana katika Wilaya au Mikoa mingine, katika Wilaya ya Rungwe hii haiwezekani. Tuna kanda tatu zenye hali ya hewa tofauti *(topography, mean annual temperatures, mean annual rainfall)* na kutokana na hilo mazao yanayooteshwa kila kanda ni tofauti. Viazi mviringo na pareto vinalimwa ukanda wa Kaskazini karibu na Mlima wa Rungwe, migomba, mahindi, chai na kahawa Ukanda wa Kati, ambapo mahindi, migomba na kakao vinastawi vizuri Ukanda wa Kusini. Kwa maana hiyo kwa Wilaya ya Rungwe hatuwezi kuwa na zao moja tu la biashara au la chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, narudia kusema naiunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula.

**MHE. ABU T. KIWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ibara ya 22 ya Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula, inaelezea hatua za kuchukuliwa kukabiliana na upungufu wa chakula zipatazo tano. Napendekeza marekebisho yafuatayo kifungu kwa kifungu:-

Kifungu (a) pamoja na kuafiki maneno yote kwenye kifungu hicho, Mheshimiwa Waziri angeongeza maneno yafuatayo: "kwa kuwa taratibu za makusudi kabisa, sehemu zenye upungufu wa chakula mkubwa, usafirishaji wa chakula kati ya sehemu moja ya nchi kwenda kwingine, usafirishaji huu usimamiwe kikamilifu na Watendaji wa Vijiji, Kata na Wilaya ili kuepukana na kuzuka uhaba wa chakula, kunakoweza kuletwa na walanguzi na raia wenye tamaa ya kipato cha haraka bila kujali hali halisi ya chakula, hasa kwenye miezi ya Mei, 2004. Muda ambao sehemu nyingi ni wakati wa maandalizi ya kilimo na mwanzo wa mavuno kwa msimu ujao." Vifungu (b) na (c) hakuna mabadiliko.

Kifungu (d) pamoja na yote, Mheshimiwa Waziri angelichukua pia hatua za makusudi kabisa, kuteua kwa kupitia Watendaji wake wa Wilaya, Mikoa, sehemu maalum kwenye vijiji ambazo zitakuwa ni vituo kwa wananchi kuhudumiwa. Aidha, ununuzi wa chakula hicho toka kwa wafanyabiashara watakaoteuliwa kuuza vyakula hivyo toka *SGR* zetu au Maafisa watakaoshiriki kwenye zoezi zima la kuhudumia raia, usambazaji wa chakula hicho kutoka *SGR*. Kifungu (e) hakina mabadiliko pia.

Kuhusu hali ya chakula Jimboni Kilombero. Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula, kwenye jedwali Na.1 ukurasa wa 9 kwenye hotuba yake, ameelezea kutokuwa na shida ya chakula Wilayani Kilombero, hali halisi ni kama ifuatavyo: Mahitaji ya kawaida ya chakula Jimboni ni tani 100,000, hali halisi ya chakula hivi sasa kutokana na hali ya hewa na ukame ni tani 60,000, upungufu wa chakula Jimboni ni tani 40,000 na upungufu wa chakula hicho Kikata; Kata ya Mlimba tani 10,000, Kata ya Ifakara tani 10,000, Kata ya Kidatu tani 10,000, Kata ya Mang'ula tani 5,000 na Kata ya Mchombe (Mngeta) tani 5,000. Jumla tani 40,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na kuunga mkono hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula, kwa asilimia mia moja.

**MHE. AZIZA SLEYUM ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niunge mkono hoja hii. Kwa kuwa kilimo ndiyo uti wa mgongo hapa kwetu Tanzania na kwa kuwa wapo wananchi wengi wanaojishughulisha na kilimo, nachukua nafasi hii kutoa maoni yangu kwa Wizara ya Kilimo na Chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana wengi hawana ajira hapa nchini na huzurura tu bila ya kazi, je, Wizara haioni umuhimu wa kuanzisha sehemu kama Wilaya ya Kinondoni, Kituo cha Madale, ambapo vijana hujishughulisha na kilimo cha ufugaji, ujenzi wa nyumba bora na kazi za mikono?

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana wengi hupenda kuwa na ajira zao hata kujituma kwa shughuli mbalimbali na nina imani Wizara ya Kilimo na Chakula na JKT, kama zitaandaa utaratibu wa ushirikiano na nina imani vijana wengi na pia nchi yetu itajikwamua na shida ya njaa na pia hata ujenzi wa nchi yetu. Nina imani Wizara ya Kilimo na Chakula, itakuwa ndiyo mkombozi zaidi kwa vijana katika kupata ajira, laiti kama Wizara itaanzisha kila kijiji lazima kuwe na kikundi cha vijana ambao watajiunga na kuchukua eneo kubwa ili walimiliki na kuanzisha kilimo cha ufugaji, ujenzi, nina imani chakula kitakuwepo na hata ujenzi wa nyumba na mambo mengine mengi ambayo ni kwa ajili ya mwamko wa maendeleo yatakuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia kwako naomba kumwomba Mheshimiwa Waziri na Katibu Mkuu, katika mipango yao waweze kuangalia vijana wa nchi hii, kwa kuwasaidia vijana kujikwamua kwa kupata ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja hii.

**MHE. DR. IBRAHIM S. R. MSABAHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu tatizo la njaa na kilimo cha umwagiliaji maji Kibaha. Katika ukurasa wa 9, Jedwali Na.1, juu ya maeneo yaliyoathiriwa zaidi na upungufu wa chakula. Wilaya ya Kibaha imeonekana kama Wilaya inayojitosheleza na yenye ziada. Sijui vigezo vilivyotumika katika kuiorodhesha Kibaha kuwa haina tatizo la upungufu wa chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, mwezi Mei 2003 nilifanya ziara ya Jimbo la Kibaha na nilitembelea kata zote kila nilipokwenda vijijini nililalamikiwa kuwa wananchi walikuwa wanakabiliwa na njaa kiasi kwamba wengi wanalazimika kuishi kwa mlo mmoja kwa siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya ziara hiyo nilimwandikia Mkuu wa Mkoa, kumwelezea tatizo hilo. *RC* alinifahamisha kuwa na yeye alikwishapelekewa tatizo hilo. Mheshimiwa Waziri, kwa vyovyote vile, hali inayoelezwa katika ukurasa wa 9 kuwa Kibaha na hasa Kibaha vijijini, kuna ziada ya chakula, haiendani na hali halisi niliyoikuta vijijini. Nashauri ufanywe uchunguzi upya juu ya hali ya chakula Kibaha ili kuwanusuru wananchi wanaokabiliwa na baa la njaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, juu ya kilimo cha umwagiliaji maji ukurasa wa 27 imeorodheshwa Ruvu na Bagamoyo. Ni matumaini yangu kuwa Ruvu ni pamoja na Ruvu Juu iliyoko Wilaya ya Kibaha, ambako kuna kilimo cha mpunga, mahindi, nyanya, bamia na mbogamboga zingine. Msaada mkubwa unaohitajika katika maeneo ya Kata za Kwala, Ruvu, Mlandizi na Visiga, ambako Mto Ruvu unapita kuelekea Bagamoyo ni vifaa vya umwagiliaji, pembejeo na *tractors.* Naomba nimkaribishe Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula atembelee maeneo haya ajionee mwenyewe baada ya Bunge la Bajeti kuahirishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. JOHN P. MAGUFULI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampa hongera sana Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba nzuri na mipango mizuri ya Wizara yake. Mchango wangu ni mmoja tu. Napenda nishauri fedha za *STABEX dollar* bilioni 10 zitakazotolewa na Wizara ya Kilimo na Chakula, kwa ajili ya barabara zisipelekwe moja kwa moja *TANROADS*. Fedha hizo zipelekwe kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, naye atazipeleka *TANROADS* kwa *Performance Agreement*. Huu ndio uwe utaratibu ili Wizara iweze kudhibiti matumizi ya fedha hizo. Ieleweke *TANROADS* iko chini ya Wizara ya Ujenzi hivyo, sioni mantiki ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo na Chakula, kutomwamini Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, kwa kupeleka fedha moja kwa moja *TANROADS.*

Sheria ya mwaka 98 iliyoanzisha *Road Fund,* inasititiza *TANROADS* watapata fedha kwa *Performance Agreement* na hivyo ndivyo tumekuwa tukifanya katika kuhakikisha fedha zinatumika kama ilivyotarajiwa. Hivyo, fedha za *STABEX* zipelekwe kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi na kama Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi haaminiki, basi zipelekwe kwenye Bodi ya Mfuko wa Barabara *(Road Fund Board),* nao baadaye watazipeleka *TANROADS* kwa *Performance Agreement.*

Naunga mkono hoja hii na ninampongeza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote, kwa kazi nzuri wanazozifanya. Ni kweli Wizara ya Kilimo na Chakula sasa ina mwelekeo mpya.

**MHE. ARCADO D. NTAGAZWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. Mchango wangu ni kama ifuatavyo: Kilimo inabidi kitazamwe pamoja na masuala kama barabara, mawasiliano, umeme, masoko, suala zima la hifadhi ya mazingira kwa upana na urefu wake, bila kusahau upatikanaji wa mikopo midogo midogo kwa wakulima walio wengi. Kwa vyovyote kilimo ni suala mtambuka.

Suala la barabara kuhudumia kilimo nilieleze kwa kutumia Mkoa wa Kigoma, ambao nina uzoefu nao. Mkoa wa Kigoma ambao Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula anaufahamu fika, watu wake ni wachapakazi hodari, Mwenyezi Mungu, katujalia mvua za uhakika na hivyo Taifa halijawahi kuhangaika kuulisha kutokana na ukame au upungufu wa chakula. Mashariki mwa Mkoa wa Kigoma, wenzetu Mikoa ya Shinyanga, Tabora, Mwanza, Singida hadi Dodoma, husumbuliwa na upungufu wa chakula kutokana na ukame. Kutokana na kutokuwepo barabara ya kuunganisha Kigoma, Magharibi mwa nchi na Mikoa ya Mashariki bila ya ulazima wa kuzunguka sana, chakula kinacholimwa Mkoani Kigoma hakiwafikii majirani zetu katika Mikoa iliyotajwa kama ambavyo ingetegemewa.

Katika hali hiyo hoja ya kiuchumi ya gharama ya kufikisha chakula kutoka nje ya nchi, ikilinganishwa na chakula kinacholimwa nchini mwetu, kama vile Mkoa wa Kigoma nilioutolea mfano, huonekana rahisi kwa kuzingatia suala la gharama peke yake. Pamoja na ukweli wa takwimu au tarakimu za mlinganisho wa gharama, *(Unit Cost)*, hali hiyo huchangia kudumaza maendeleo ya kilimo chenyewe pamoja na upatikanaji wa huduma nyinginezo kama nilivyotangulia kusema. Hali hiyo haiharakishi kukua kwa uchumi wetu kwa jumla. Aidha, hali hiyo haitoi mchango utakiwao katika mapambano dhidi ya adui umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, huo ndio mchango wangu katika kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wale wote ambao waliomba kuchangia hoja hii wamepata nafasi na wamemalizika. Kwa muda uliobaki hatuwezi kumpa mtu mwingine achangie. Kwa sababu mliyoyasema ni mazito, nafikiri ni vizuri upande wa Serikali wakaenda kuyachambua vizuri. Kwa hiyo, nasitisha Shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni, watakapopata nafasi ya kujibu.

*(Saa 6.10 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*
*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alikalia Kiti*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge, wenzangu kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula. Kwanza napenda kumpongeza sana kwa hotuba yake nzuri. Moja kwa moja naiunga mkono hoja hiyo kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Aidha, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ambao wametupongeza sisi wasaidizi wa Waziri wa Kilimo na Chakula kwa kumsaidia Mheshimiwa Waziri kwenye maandalizi ya hotuba yake hiyo.

Pili, kwa niaba ya wapiga kura wa Jimbo la Namtumbo na mimi mwenyewe, niungane na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula, kuwapongeza sana Waheshimiwa Wabunge wote 19 wapya walioshinda katika uchaguzi mdogo wa tarehe 18 Mei, 2003 na hatimaye kuingia katika Bunge hili Tukufu, hongereni sana wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mchango wangu wa kusaidia kujibu baadhi ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge, naanza kwa kusema kuwa, tumefarijika sana na kunufaika na michango mizuri mno kutoka kwenu Waheshimiwa Wabunge wote mliochangia kwa maandishi na kwa kauli. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siyo rahisi kujibu michango yote kwa sababu ya ufinyu wa muda. Kwa hiyo, nitajaribu kufanya hivyo kwa maeneo sita yafuatayo: La kwanza, kuhusu umwagiliaji maji mashambani, ya pili ubinafsishaji wa mashamba, tatu vituo vya kukodisha matrekta na wanyamakazi, nne huduma za ugani, tano, utafiti na mwisho usindikaji mazao.

(a) Mheshimiwa Spika, kuhusu umwagiliaji maji mashambani, Waheshimiwa Wabunge 27 walizungumzia hoja hiyo. Nakubaliana na hoja za Waheshimiwa hao na kusema kuwa Serikali itashirikiana na Serikali ya Malawi kwa kutayarisha mpango wa kuendeleza Bonde la Songwe.

(b) *PIDP* ina skimu za hekta 1,149 katika Bonde la Mto Bubu.

(c) Serikali na Benki ya Dunia inaendeleza miradi 15 ya hekta 5,059 katika Mabonde ya Mto Pangani.

(d) Katika mwaka huu wa fedha wa 2003/2004, Serikali imeainisha mabwawa kumi ya kuvuna maji ya mvua kwa ajili ya umwagiliaji maji mashambani.

(e) Serikali itazingatia ushauri wa kutumia visima vifupi kumwagilia zabibu.

(f) Mwisho Wizara ya Kilimo itashirikiana na Wizara ya Ardhi kuainisha maeneo ya wawekezaji wakubwa wa mashamba ya umwagiliaji maji nchini.

Hoja ya pili, ilikuwa ubinafsishaji mashamba kwa wakulima wadogo. Waheshimiwa Wabunge watano walizungumzia hili.

(a) Wakulima wadogo watamilikishwa mashamba kwa kuyanunua eka 4 tu kwa mkulima kwa shamba la Mbalali.

(b) Wakulima wadogo waliomilikishwa mashamba hayo watasimamia mashamba, mifereji ya kuingiza maji mashambani.

(c) Mifereji mikuu mabanio na mitambo ya mashine ya kukobolea mpunga vitakuwa chini ya usimamizi wa watalaam wa kilimo na chakula.

Mheshimiwa Spika, hoja ya tatu, vituo vya kukodisha matrekta na wanyamakazi. Waheshimiwa Wabunge 9 walizungumzia suala hilo.

(a) Wizara itahamasisha sekta binafsi kuanzisha vituo na kukodisha zana za kilimo.

(b) Wizara imeanza kufufua vituo vya maksai.

(c) Kupitia Mfuko wa Pembejeo Wizara itatoa mikopo kwa wakulima kununua matrekta mapya na kukarabati mabovu.

Mheshimiwa Spika, eneo la nne, Huduma za Ugani. Waheshimiwa wabunge 15 walizungumzia hoja hii.

(a) Wizara inakubaliana na Waheshimiwa Wabunge kuwa upo udhaifu katika utoaji huduma za ugani. Tutarekebisha kwa mbinu zifuatazo:-

(i) Kuhimiza matumizi ya mbinu shirikishi kwa watumishi 4,725 wanaohudumia vijiji 10,740; *(Makofi)*

(ii) Tutaomba kibali kuajiri watumishi wapya kulingana na uwezo wa Serikali kifedha; na *(Makofi)*

(iii) Watumishi wasiotekeleza wajibu itabidi Halmashauri husika iwaadhibu. Mtakumbuka Waheshimiwa Wabunge kuwa, watumishi wote hawa 4,725 wako chini ya mamlaka ya Halmashauri za Wilaya, Miji na Jiji;

(b) Watumishi watapata mafunzo rejea na tutaanza na watumishi 750 mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, eneo la tano lilikuwa utafiti. Waheshimiwa Wabunge 33 walichangia suala hili.

(a) Serikali itaviimarisha vituo vya utafiti kwa kuvipa vitendea kazi na kuvikarabati.

(b) Itaajiri watumishi wengine 20 mwaka huu na 20 walishaajiriwa mwaka uliopita. *(Makofi)*

(c) Serikali itagharamia mafunzo ya watafiti 48 kwa kiwango cha *Masters* na *Ph.D. degrees*.

Eneo la mwisho ni usindikaji mazao. Waheshimiwa Wabunge 7 walizungumzia hoja hii. Ili kuboresha mazao na kupata bei nzuri kabla ya kuuza mambo yafuatayo yatafanyika:-

(a) Tutazidi kuhamasisha usindikaji wa mazao yote kabla ya kuuzwa ili kumwongezea pato mkulima ikijumuisha usindikaji wa mbegu za mafuta. Kama wengi walivyozungumza mawese, ufuta na kadha wa kadha.

(b) Tunampongeza Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga, kwa kufufua zao la korosho mwambao mwa Ziwa Nyasa. *(Makofi)*

(c) Mawasiliano yanaendelea kuwapata wawekezaji katika kusindika pareto huko Arusha. Vile vile jitihada zinaendelea kupata soko kwa wakulima wa pareto wa Nyanda za Juu Kusini.

(d) Serikali itakazia ubanguaji wa korosho katika viwanda vidogo vidogo. Aidha, jitihada za kukodisha au kubinafsisha viwanda vikubwa vyote 12 vya korosho zinaendelea.

(e) Serikali imo mbioni kuunda bodi ya mazao mchanganyiko. *(Makofi)*

(f) Wakulima wahusishwe katika kuchagua zao la biashara huko Wilayani. Hata hivyo, uteuzi huu hauna maana kuwa mazao mengine yasiendelezwe. Haya ni baadhi ya majibu kwa kifupi.

Mheshimiwa Spika, mwisho ingawa siyo kwa umuhimu naomba na mimi nisisitize umuhimu wa kilimo cha Mihogo nchini. Historia ya ukame na njaa nchini mwetu ameonyesha Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula kuwa imeanza tangu miaka ya 1800 na kitu na imekuwa ikisababisha nchi yetu kukumbwa na njaa kwa mzunguko wa miaka 10 aliyoiainisha yeye hasa ile inayoishia na namba 4. Mfano Profesa Peter Rigby, katika kitabu chake *"Cattle and kinship among the Gogo",* kilichochapwa na *Cornell University Press,* ukurasa wa 21, ambapo ameorodhesha pia matukio ya ukame na njaa kuanzia katikati ya karne ya 19 enzi za njaa za Konyamagulu hadi katikati ya karne ya 20. Naomba ninukuu matukio haya ya majanga ya ukame katika eneo la Ugogoni kama ifuatavyo:-

"Mwaka 1894 hapa hapa tulipo Dodoma kulikuwa na njaa inaitwa Nzije, halafu kuna njaa ya Sabatele iliyotokea mwaka 1914 Ugogoni, halafu kuna njaa ya Nzala Dodo au Ndele iliyotokea mwaka 1924, Njaa ya John au Masaje iliyotokea mwaka 1934, Njaa ya Makambi iliyotokea mwaka 1944, halafu Njaa ya Maumau iliyotokea mwaka 1954 na kuendelea."

Mheshimiwa Waziri ameainisha vizuri katika hotuba yake ya kauli. Hii ni dhahiri kuwa njaa imekuwa nasi siyo tu kwa sababu ya uharibifu wa mazingira, lakini inaonekana kuna *circle* ya miaka 10 njaa inatokea. Kwa hiyo, Wizara ya Kilimo na Chakula ya mwaka 2004 wakae chonjo njaa yaja. Pamoja na uharibifu wa binadamu lakini inaonekana kuna *circle* ya aina hiyo.

Aidha, mtaalam mwingine Profesa John Eliffe katika kitabu chake *"A Modern History of Tanganyika"* kilichochapwa na *Cambridge University Press,* ukurasa wa 315, naye amenukuu matukio mbalimbali ya ukame na njaa katika Ugogo na Uzigua na kusema: *"The chief reason in both areas was drought"* halafu akaendelea kusema, yaani maana yake kuwa sababu kubwa ilikuwa ni ukame na mengine yapo. Lakini vile vile akaongezea *"unwillingness to cultivate maniac"* na mazao mengine ambayo ni *drought resistant*. Hii ina maana kuwa hata wakoloni nao waliona kuwa tulikuwa na mazoea ya kutokupenda mazao ambayo yanahimili ukame, mathalani kilimo cha muhogo. Wizara ya Kilimo na Chakula kwa kutambua umuhimu wa zao hili ambalo naweza kusema kwa kiasi fulani haliliwi sana na nzige, maana wakila majani baadaye itachipua, halihitaji ghala, angalau linaweza likaota likakaa kwa mwaka mzima kwenye shamba na hata upotevu wa mazao baada ya mavuno unakuwa mchache zaidi kuliko mazao ya aina ya mahindi au mtama. Vile vile halishambuliwi kwa urahisi na viwavi jeshi na kadhalika.

Kwa kutambua hilo Wizara imetenga maeneo matatu ya vituo au mashamba ya utafiti ya kilimo. Kwa upande wa Ukanda wa Pwani kuna Kibaha, Ukanda huu wa Kati kuna Hombolo siyo mbali kutoka hapa na Ukanda wa Ziwa kuna Shamba Ukiriguru. Huko kunapatikana mbegu bora ambazo zinaweza kuota kwa muda mfupi na muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, sasa ombi langu kwa Waheshimiwa Wabunge kwa maelezo haya naomba niwaombe mjaribu kwa kiasi kikubwa kuhimiza kilimo cha mihogo katika Majimbo yenu. Kila palipo na mihogo hakuna njaa. Hata hawa Waheshimiwa wanaolalamika sasa hivi kuwa kuna njaa huku kwetu, ukiangalia maeneo mengi yatakuwa hayana muhogo. Kwa hiyo, dawa ya kupambana na tatizo hili kama alivyosema Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake, ni kukazia kilimo cha muhogo. Kwa hiyo, tafadhali mpeleke ujumbe huo kwa sababu kupitia sisi Wabunge utafika kila mahali siyo tu hapa Ugogoni hata Namtumbo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa baada ya kusema hayo, ninapenda nimuahidi Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula kuwa, nitaendelea kumsaidia kwa uwezo wangu wote na kwa ubunifu, nikishirikiana na Katibu Mkuu na Watalaam wote katika sekta ya kilimo katika kufanikisha majukumu ya Wizara yetu.

Napenda kurudia tena kusema kuwa naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kujibu baadhi ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge hapa Bungeni na nikupongeze kwa kazi nzuri sana unayofanya ya kuongoza Bunge hili na utakayofanya kesho ya kuwakaribisha Marais wawili hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna Waheshimiwa Wabunge 29 waliochangia kwa kutoa hoja na kwa ruhusa naomba niwataje. Wabunge hao ni Mheshimiwa Abdula Lutavi, Mheshimiwa Abu T. Kiwanga, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, Mheshimiwa Benito Malangalila, Mheshimiwa Chegeni R. Masunga, Mheshimiwa Chrisant M. Mzindakaya, Mheshimiwa Christopher Wegga, Mheshimiwa Cynthia Ngoye, Mheshimiwa Dr. Suleiman Juma Omar, Mheshimiwa Edson M. Halinga, Mheshimiwa Edward Nziriye Ndeka, Mheshimiwa Eliachim Simpasa, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Felix Mrema, Mheshimiwa Gwassa A. Sebabili, Mheshimiwa Ireneus N. Ngwatura, Mheshimiwa Mathew Taki Ole- Timan, Mheshimiwa Musa Lupatu, Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mheshimiwa Omar Said Chubi, Mheshimiwa Paschal C. Degera, Mheshimiwa Edward Ntwina, Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Talala B. Mbise, Mheshimiwa Yete Mwalyego na Mheshimiwa Paul Makolo. *(Makofi)*

Waliochangia kwa maandishi ni wengi, wameonyesha kabisa umahiri wao wa kuandika wako 76. Naomba nao niwataje. Mheshimiwa Mwanne I. Mchemba, Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatib, Mheshimiwa Musa Lupatu, Mheshimiwa Towagale Kiwanga, Mheshimiwa Alhaj Shaweji Abdallah, Mheshimiwa Arcado D. Ntagazwa, Mheshimiwa Aridi Uledi, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali,

Mheshimiwa Beatus Magayane, Mheshimiwa Bakari Mbonde, Mheshimiwa Dr. Batilda Burian, Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, Mheshimiwa Benson Mpesya, Mheshimiwa Chrisant Mzindakaya, Mheshimiwa Damas Nakei, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga, Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, Mheshimiwa Edson Halinga, Mheshimiwa Edward Ndeka na Mheshimiwa Gwassa Sebabili.

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Ernest Mabina, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Fatma S. Ali, Mheshimiwa Faustine Rwilomba, Mheshimiwa Feteh Saad Mgeni, Mheshimiwa Frank Mussati, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Halimenshi K. Mayonga, Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Mheshimiwa Hassan Kigwalilo, Mheshimiwa Cynthia Ngoye, Mheshimiwa Ireneus Ngwatura, Mheshimiwa John Mwakipesile, Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, Mheshimiwa Joel Bendera, Mheshimiwa John Singo, Mheshimiwa John Magufuli, Mheshimiwa Juma S. Kidunda, Mheshimiwa Talala Mbise, Mheshimiwa Karim Said Othman, Mheshimiwa Khalid Suru, Mheshimiwa Lephy Gembe, Mheshimiwa Major Jesse Makundi, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud, Mheshimiwa Njelu Kasaka, Mheshimiwa Paul Makolo, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Paschal Degera na Mheshimiwa Paul Ntwina.

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Philip Marmo, Mheshimiwa David Mwakyusa, Mheshimiwa Juma Mikidadi, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Robert Jacob Buzuka, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Suleiman A. Sadiq, Mheshimiwa Said Nkumba, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Stephen Kazi, Mheshimiwa Benson Mpesya, Mheshimiwa Tembe Nyaburi, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa William Lukuvi, Mheshimiwa Yete Mwalyego, Mheshimiwa Henry Shekiffu, Mheshimiwa Leonard Derefa, Mheshimiwa Remidius Kissassi, Mheshimiwa Capt. John Chiligati, Mheshimiwa Mwadini Abass Jecha na Mheshimiwa Elizabeth Batenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wapo pia waliochangia wakati wa Hotuba ya Waziri Mkuu, ambao ni Mheshimiwa George Mlawa, Mheshimiwa Dr. James Msekela, Mheshimiwa Edward Nziriye Ndeka, Mheshimiwa Parseko Kone, Mheshimiwa Leonard Derefa, Mheshimiwa Mohamed H. Missanga, Mheshimiwa Stanley Kolimba, Mheshimiwa Khalid Suru, Mheshimiwa Ramadhani H. Khalfan na Mheshimiwa George Lubeleje. *(Makofi)*

Wakati wa Hotuba ya Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango, waliochangia ni Mheshimiwa Anne Makinda, Mheshimiwa Suleiman Sadiq, Mheshimiwa John Mwakipesile, Mheshimiwa Philip Marmo, Mheshimiwa Charles Kagonji, Mheshimiwa Capt. Theodos Kasapira, Mheshimiwa Aisha Kigoda, Mheshimiwa Mariam Mfaki, Mheshimiwa Christopher Wegga, Mheshimiwa Benson Mpesya, Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Joel Bendera, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Benito Malangalila, Mheshimiwa Aridi Uledi, Mheshimiwa Musa Lupatu, Mheshimiwa John Singo, Mheshimiwa Philip Marmo na Mheshimiwa Maria Watondoha, bila kumsahau Mheshimiwa Profesa Pius Mbawala, Naibu Waziri wa Kilimo na Chakula, kwa mchango wake alioutoa dakika chache zilizopita. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge wote nawashukuru sana kwa michango yenu mizuri sana. Mengi mliyotoa ni mapendekezo tutayazingatia katika utendaji wetu wa kazi na kwa hiyo, nitakalofanya kwa kweli ni kujaribu kutoa maelezo mafupi kadri ninavyoweza, juu ya baadhi ya hoja mlizotoa. Kama kutatokea hoja yoyote ambayo haitapata maelezo ya kutosha, naomba tuwasiliane ili tuwape nyongeza ya maelezo. Naomba nianze na masuala mawili ya ujumla.

Mheshimiwa Spika, sisi wote Wabunge, hususan wale tunaotoka kwenye Majimbo tungetaka kila kitu kifanyike leo kwa kiasi kikubwa sana. Lakini ninachoomba tukumbuke kwamba, miaka michache iliyopita hali yetu ya mapato ya Serikali ilikuwa mbaya sana. Kutokana na umahiri wa Rais wa kusimamia uchumi, mapato yamekuwa yakiongezeka kidogo kidogo kila mwaka kufikia hapa tulipofikia. *(Makofi)*

Kutokana na umahiri wake wa kusimamia masuala mbalimbali ya uchumi pia, tukafikia mahali tukasamehewa baadhi ya madeni kwa hiyo, baadhi ya fedha tulizokuwa tunalipia madeni zikabaki humu nchini. Kwa hiyo, hali yetu bado si imara sana, si imara kiasi ambacho tunaweza kwa mfano kumwagilia

hii nchi yote maji, tukalima hekta 29.4 milioni. Kwa hiyo, ambacho kimekuwa kikitokea na Serikali kuongeza *allocation* yake kwa kilimo kadri uwezo wake unavyoongezeka. Mwaka 2002 tuliongezewa kwa asilimia 32, mwaka huu bajeti yetu iko juu ya mwaka 2002 kwa shilingi bilioni 20. Mimi naishukuru sana Serikali kwa hizi jitihada ambazo inafanya za dhati kabisa za kuwekeza katika kilimo ili kuhakikisha kwamba, hiki kilimo kinakua, lakini umaskini vijijini unapungua na Pato la Yaifa linaongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ningekuwa nimewaelewa vizuri sana Wabunge, kama wangekuwa wametoa hoja hapa Bungeni kwamba, Mheshimiwa Rais wetu, ama apewe nishani au tuzo fulani ya kukubali umahiri wake katika kuongoza uchumi na nchi kwa ujumla. Mimi nina hakika katika hili kama Mheshimiwa Thomas Ngawaiya na Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi na Wapinzani wanakubaliana na mimi.

Mheshimiwa Spika, suala la pili, katika mazungumzo hapa Bungeni imejitokeza mara nyingi kidogo kwamba, sasa haya yaliyoandikwa katika hotuba yanaelekea kuwa ni mazuri. Lakini wakauliza hivi kweli hii Wizara ina mwelekeo wa tunakokwenda na kwamba tutabaki tukielekea huko huko tunakokwenda? Je, haya yaliyomo kwenye kitabu hiki yatatekelezwa? Mimi nikafikiri tumesahau maana mwaka 2002 tuliwagawia mkakati wa kuendeleza sekta ya kilimo, ambao ulionyesha kabisa nini tunachotaka kufanya. Naomba wale ambao hamjausoma muusome maana unasomeka vizuri sana. Bodi na Asasi zote zilizoko chini ya Wizara ya Kilimo zimeandaa mikakati na programu za kutekeleza mikakati hiyo ya kuendeleza maeneo wanayosimamia. Kwa hiyo, nafikiri tumejaribu kuainisha vizuri ni wapi tunakotaka kwenda na tuna hakika kwamba, huko tunakoelekea tutafika. Katika fedha mlizotupa mwaka 2002 tulizitumia zote. Tulichopewa tulitumia kikamilifu kabisa kuishia jana tarehe 30 Juni, 2003. Sasa tulifanya vizuri mwaka uliopita nawaomba pia msiwe na wasiwasi tutafanya vizuri pia mwaka huu. *(Makofi)*

Jambo muhimu ni kutambua, mimi nilikuwa nawaambia wenzangu jana kwamba, jana na leo ni siku za wakulima na Wabunge walioko Bungeni wengi, karibu asilimia 99 aidha ni wakulima ama wana uhusiano wa karibu na wakulima. Kwa hiyo, naomba basi sisi wakulima tulioko humu Bungeni tujitahidi sana kuhakikisha kwamba, haya tunayoyapitisha hapa tunayasimamia ili yatekelezwe kikamilifu ili tupate haya manufaa ambayo Bunge hili lingetaka tupate. *(Makofi)*

Viongozi Wakuu kama nilivyowaeleza, wanakienzi sana kilimo na ndiyo maana wamekiongezea fedha. Ukimwangalia hata Mheshimiwa Spika, amevaa tangu korosho mpaka mahindi nakadhalika kwenye joho lake. Ni dalili za kukienzi kilimo. Kwa hiyo, naomba tukisimamie kwa ukaribu kabisa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, baadhi ya mambo yaliyochangiwa ni pamoja na hali ya chakula. Wabunge kumi na wawili walichangia hoja hii. Wabunge hao ni Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Paschal Degera, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Abu Kiwanga, Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Felix Mrema, Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha na Mheshimiwa Benito Malangalila.

Waheshimiwa Wabunge, walizungumzia juu ya hali ya chakula. Hali yetu ya chakula mwaka huu si nzuri kama ilivyokuwa mwaka 2002. Tuna upungufu wa takribani tani 350,000 za chakula. Tumeshazungumza na wafanyabiashara na ahadi tulizopata za kuagiza chakula kutoka nje zinazidi upungufu tulionao. Kwa hiyo, tuna hakika kwamba, kitaagizwa chakula kutoka nje cha kutosheleza kujaza pengo lililopo. Tuna chakula kwenye *SGR* pale Shinyanga zaidi ya tani 8000, hapa Dodoma tuna tani zaidi ya 11,000, Arusha tuna tani karibu 20,000 na tuna viwango vingine vidogo huko Songea, Makambako na Sumbawanga.

Mheshimiwa Spika, tumetoa maagizo kwamba, Wakuu wa Mikoa sasa wawaagize wafanyabiashara wanunue chakula kutoka *SGR* lakini wasimamie kuhakikisha kwamba, kinakwenda kwenye maeneo yenye upungufu. Kile chakula ukiruhusu kinunuliwe bila kukielekeza sehemu za kupelekwa, kinaweza kikavushwa kikaenda nchi za jirani, kazi ambayo kwa kweli tumeisimamisha kwa wakati huu kwa sababu hali yetu siyo nzuri sana. Kwa hiyo, tuna hakika kwamba, chakula tulichonacho

katika *store,* chakula kilichopo nchini na chakula ambacho tumeahidiwa kwamba kitaagizwa, kitasaidia kujaza hili pengo. Tumekwishaanza kufanya mazungumzo na baadhi ya wahisani na baadhi wameahidi kutusaidia. Kwa mfano, Serikali ya India na Japan zimeahidi kwamba watatusaidia chakula kiasi cha kutusaidia kujaza hili pengo. Kwa hiyo, tuna hakika kwamba hatua zinazochukuliwa na Serikali zitatusaidia kuhakikisha kwamba, kuna chakula cha kutosha.

Lakini tunaomba chakula kitunzwe, wale wanaotumia nafaka kunywea pombe, wapunguze kidogo wanywe bia ama wanywe kitu kingine. Lakini ile pombe ya komoni tunaomba kwa mwaka huu tupunguze kidogo mpaka hali itakapobadilika na kuwa nzuri zaidi, tukiwa tena na neema kama ilivyokuwa msimu uliopita ndipo turudie. Tumekwisha kuomba kwamba vizuizi visiwekwe mahali popote. Chakula kiruhusiwe ku-*flow* nchini kwa uhuru kabisa ili chakula kitoke kwenye maeneo yenye ziada kwenda kwenye maeneo yenye upungufu. Tumepeleka timu za wataalam mara tatu mikoani, kubaini ni maeneo gani yenye upungufu na tunafahamu mpaka ni Kata ipi yenye upungufu na kiasi gani. Kwa hiyo, tupo katika nafasi nzuri ya kuweza kuelekeza chakula hiki kwenda huko ambako kinatakiwa kiende. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, naomba ushirikiano wenu katika suala hili kwa sababu wakati kuna upungufu wa chakula, Taifa lina tatizo, wakati watu wameshiba tatizo si kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, suala la pili liliulizwa na Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, juu ya watu wanaodaiwa kwa chakula kilichoingizwa humu nchini. Ni kweli kwamba, kutokana na chakula tunachopewa cha msaada ambacho kinaingia kwenye *Food Aid Counterpart Fund,* fedha zake zinaingia *Food Aid Counterpart Fund.* Kuna watu waliouziwa chakula na ambao hawakukilipia kikamilifu, watu hao ni mchanganyiko wa mashirika ya umma yakiwemo kwa mfano kampuni za Mikoa na watu binafsi waliuziwa chakula kile. Ni mchanganyiko pia wa watu ambao muda wa kulipa umeshapita na wengine ambao bado muda upo wa kulipia. Kwa hiyo, wanaendelea kulipia.

Sasa orodha yenyewe ni ndefu kidogo, ina majina kama 14 na kama Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, angependa kuwajua ni kina nani hao, nitakuwa tayari kabisa kumpa orodha hiyo huenda atanisaidia kudai ili walipe madai hayo. *(Makofi)*

Tumeteua makampuni ya kutusaidia kufuatilia madeni haya kwa sababu kwa kweli mtu yeyote ambaye anachukua deni kutoka Serikalini ni kwamba, anaukopa umma wa Tanzania na ni lazima alipe. Uwezekano wa kukopa halafu akaondoka hivi hivi bila kulipa haupo na kwa hiyo tutafuatilia kuhakikisha kwamba wanalipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nafika kwenye lile suala muhimu linaloitwa *STABEX* wengine wanaita *STABEC* ina majina mbalimbali. Hoja juu ya suala hili ilikuwa inaongozwa na ndugu yangu Ngawaiya, naona amestaafu akamwachia Mheshimiwa Mutungerehi na Mzee wa mifereji anaitwa Mheshimiwa Mwanri. Nitajitahidi kutoa maelezo na ninaomba nikubaliane na maelezo haya. Waliozungumzia juu ya *STABEX* walikuwa wanane wakiongozwa na Mheshimiwa Mutungirehi, Mheshimiwa Alhaj Shaweji Abdallah, Mheshimiwa Mayonga, Mheshimiwa Mpesya, Mheshimiwa Ntwina, Mheshimiwa Magufuli na Mheshimiwa Mwanri.

Mheshimiwa Spika, tunakubaliana kuwa utaratibu uliokuwepo zamani ulikuwa ni kwamba, *EU* chini ya *Lome Convention* walikuwa wanatoa fedha za kumfidia mkulima pale bei za dunia zinapokuwa sio nzuri sana na utaratibu huu umeendelea kwa miaka kama minne hivi. Mwaka 2000 wakatujulisha kwamba, zilikuwepo fedha za *STABEX* ambazo tulielewa kwamba zilikuwa ni kwa ajili ile ile tuliyozoea ya kulipa fidia kwa wakulima. Zilikuwepo *Euro* kama milioni 26 hivi. Kwa hiyo, tukakaa Wizara ya Fedha, Wizara ya Kilimo na Chakula, Wizara ya Ushirika na Masoko, tukaandaa mapendekezo ambayo pamoja na mambo mengine, tulipendekeza *Euro* milioni 17 zitumike kuwalipa wakulima fidia. Tukapendekeza kiasi kingine kitumike kwa ajili ya barabara, kiasi kingine kwa ajili ya utafiti, kiasi kingine kuimarisha ubora wa kahawa, kuimarisha Vyama vya Kuweka na Kukopa na kadhalika. Nilipokwenda *EU*, wakajibu wakasema tunakubaliana na hayo mengine yote isipokuwa lile la kwanza la fedha za kuwagawia wakulima hatukubaliani nalo na wakatoa sababu tatu za kutokubaliana.

Ya kwanza, walisema hakuna tena utaratibu wa uhakika wa kujua ni nani aliuza kahawa kiasi gani. Pili, kutokana na tatizo hilo la takwimu ambazo hazina uhakika, kuna uwezekano wa watu wasiohusika wakafaidika na fedha hizo. Tatu walikwishafidia hawa wakulima mara tatu mwaka wa 1993, 1994, 1995 na 1997. Kwa hiyo, wakasema hilo hawakubaliani nalo.

Mheshimiwa Waziri wa Fedha na bahati nzuri yuko hapa, akaenda *Brussels* akakutana na Kamishna Nelson, akamwambia Mheshimiwa Kamishna tunaomba uruhusu tutumie sehemu ya fedha tuwalipe wakulima moja kwa moja. Kamishna akamwambia haiwezekani na haiwezekani kwa sababu uamuzi huu umefanywa na Bunge la Ulaya. *(Makofi)*

Kwa hiyo, si tu kwamba haiwezekani kuzungumza nao hapa, haiwezekani hata kuzungumza nao Makao Makuu kwa sababu suala hili lilipitishwa na Bunge lao. Sasa sisi tunataka maamuzi yanayofanywa na Bunge hili yaheshimiwe na wao maamuzi yanayofanywa na Bunge lao wanataka yaheshimiwe. Kwa hiyo, uwezekano huo haupo.

Mheshimiwa Spika, kilichofuata tulikaa tukashauriana tena na *EU* jinsi ya kutumia fedha hizi na tukafikia makubaliano kama ifuatavyo:-

Utekelezaji wa mkakati wa kilimo yaani *ASDP Euro* milioni 18, kuendeleza barabara za Wilaya kwenye maeneo ya kahawa, *Euro* milioni 10 na kuna maneno yanaelezwa hapa ambayo sikubaliani nayo hata kidogo kwamba, wananchi eti hawataki barabara zao zitengenezwe. Si kweli, mimi nilikwenda Hai nikawaeleza wananchi juu ya haya matumizi ya fedha za *STABEX* kwamba, hawatapata fedha za kununua pombe hata kidogo bali watapata fedha za kutengeneza barabara, wakanipigia makofi. Kwa sababu ni kweli barabara katika maeneo mengi hazipitiki. *(Makofi)*

Nimekwenda Rorya kwa Mzee Sarungi, simwoni hapa, nikamweleza juu ya hizi fedha za *STABEX* kutumika kutengeneza barabara na shughuli nyingine, walipiga makofi, wanataka barabara zao zitengenezwe. Wengine wanasema fedha za kutengeneza barabara ziko nyingi lakini si kweli. Kuna barabara nyingi sana na Mheshimiwa Magufuli, anaposimama hapa kila wakati kutueleza juu ya mipango yake ya barabara, lakini anaacha nyingi tu bila kutaja. Sasa mimi nafikiri ni vizuri tukatumia hizi *Euro* milioni kumi tukatengeneza barabara kule kwa Mheshimiwa Mutungirehi na kule kwa Mheshimiwa wa mifereji ili wananchi waweze kupita kwa urahisi zaidi kwenda kwenye shughuli zao na kusafirisha mazao yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utatifi wa zao la kahawa ulitengewa *Euro* milioni tisa na nilipokuwa Arumeru juzi, Mheshimiwa Mbise nafikiri ni shahidi, labda kama hakuwepo lakini anaweza akaenda kuuliza. Waliniambia wanataka wapate miche inayostahimili ukungu na inayostahimili *leaf rust* kwa sababu ile inawapunguzia sana gharama. Nikawaambia nitakwenda kujitahidi. Sasa pesa yenyewe ya kuwasaidia miche hiyo ndio hii hapa ambayo itatolewa *TACRI* ili *TACRI* wazalishe ile miche isambazwe na itasaidia sana kupunguza gharama. Halafu imebakia *Euro* milioni 1.4 ambazo zitatumika kwa shughuli za usimamizi, ukaguzi, uratibu na kadhalika.

Sasa naomba nisisitize kwamba, sasa kuna makubaliano yaliyotiliwa saini tarehe 12 Desemba, 2002 na *Chief Authorized Officer* ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha. Yule Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha ana majina mengi sana na moja ni hilo la *Authorized Officer.* Alitia saini kwa niaba ya Serikali kukubaliana na huu mgawanyo wa hizi fedha. Tunaloweza kufanya ni kuangalia chini ya vifungu hivi tutumie vipi hizi pesa. Hilo lina nafasi ya kuzungumza, lakini kwamba sasa tuvuruge utaratibu huu tuweke utaratibu mwingine, hizi fedha ni za *EU* na hivyo ndivyo tulivyokubaliana kuzitumia. Sasa Mheshimiwa Mutungirehi, alisema hajaridhika. Sasa naomba baada ya maelezo haya aridhike, lakini asiporidhika vile vile haimsaidii. *(Kicheko)*

Asiporidhika vile vile haimsaidii kwa sababu utaratibu uliopo sasa ndio huu na utaratibu huu uko katika mkataba na ninao hapa, akitaka nitampa asome. Sasa haya ni makubaliano kati ya nchi yetu na *European Union.* Sasa kama bado haridhiki, basi ananipa tu matatizo ya jinsi ya kukubaliana naye. Lakini nina uhakika Mheshimiwa Mutungirehi, ameelewa hata kama hakubali. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kulikuwepo na suala la mashamba makubwa na baadhi ya Wabunge waliniona nje ya Ukumbi huu wakaniambia wangependa sana nitoe kauli inayoeleweka juu ya baadhi ya haya mashamba. Kwanza yako mashamba ya mkonge ambayo hayashughulikiwi ipasavyo. Baadhi tumekuwa tukiyashughulikia, lakini kufuatana na utaratibu wa sheria tulifika mahali tukakwama, tunamngojea *Attorney General* ili tushirikiane, tuchukue hatua inayofuata kwa sababu uamuzi wa Serikali ulikwishafanywa. Lengo letu ni kuhakikisha kwamba, mashamba yote yanayoweza kufufuliwa yanafufuliwa na yale ambayo hayawezi kufufuliwa, basi yawekwe katika matumizi mengine kwa kuwagawia wananchi au kwa kuendeshwa na wananchi. Sasa naomba watu wote ambao wana mashamba haya waanze kuyashughulikia kabla sisi hatujawashughulikia. *(Kicheko/ Makofi)*

La pili, ni mashamba ya *NAFCO*. Yapo mashamba ya *NAFCO* yaliyokuwa yanalimwa mpunga kama vile Ruvu, Dakawa, Mbarali na Kapunga. Uamuzi wa Serikali ni kwamba, mashamba haya yauzwe kwa wananchi kwa utaratibu utakaowekwa. Kwa hiyo, wale waliotaka nitoe tamko, basi natoa tamko hilo kwamba, mashamba hayo yatauzwa kwa wananchi, wakulima wadogo wadogo ambao sasa watayalima na kuzalisha na kwa utaratibu tutakaowekeana. Utaratibu huo unaandaliwa, zimeshaundwa Kamati katika kila Wilaya za kushughulikia suala hili. Nitakwenda kuhakikisha kwamba, Kamati hizo zinafanya kazi zake haraka iwezekanavyo. Kwa hiyo, huo ndio utaratibu. Mheshimiwa Estherina Kilasi simwoni hapa, Mheshimiwa Saddiq namwona, nategemea nimejibu hiyo hoja. Kwa hiyo, haya mashamba tunataka yalimwe.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la sukari ambalo alilizungumza Mwenyekiti wa Kamati yangu kwamba, alipokwenda kule Kilombero alikuta kuna malalamiko kwamba, kuna sukari inayoagizwa nchini kama *industrial sugar*. Tulikubaliana, tuliweka utaratibu mzuri kabisa kwamba, wale watumiaji wakubwa wa *industrial sugar*, watengenezaji wa pombe na watengenezaji wa soda, waruhusiwe kuagiza sukari yao moja kwa moja kutoka nje kwa ajili ya matumizi yao na Waziri wa Fedha kwa kutumia *instrument* za kisheria alizonazo, aliruhusu hilo. Kuna wengine waliokuja huku nyuma wakatumia utaratibu wa Mahakama wakataka waruhusiwe kuagiza sukari. Kwa kweli sheria iliyopitishwa hapa Bungeni inakataa kutambua mtu anayetengeneza sukari kwa kuchukua sukari na kuiongeza kwenye sukari na kuzalisha sukari. Kwani sheria inasema, *that is not manufacturing process*. Kwa hiyo, ni *process* ambayo kwa kweli itafika mahali itakwisha, haitaendelea kukwepo. Lakini kuna tatizo la Mikoa mitatu ya Kusini. Mkoa wa Iringa hasa Ludewa, Mkoa wa Mbeya na Mkoa wa Rukwa. Hii Mikoa mitatu imekuwa ikilalamika kwamba haipati *allocation* ya sukari kutoka kwenye mashamba yetu na kwa hiyo imekuwa ikiomba iruhusiwe kuchukua sukari kutoka Zambia na Malawi. Tunazungumza na viwanda tukaomba wahakikishe kwamba, Mikoa hii nayo inapelekewa sukari ya kutosha mahitaji yao ili waweze kuitumia na tupunguze uagizaji wa sukari kutoka nje. *(Makofi)*

Suala lingine ambalo linajitokeza hapa ni suala la kilimo cha pamba katika Mikoa ya Kusini. Suala hili limekuwa na sisi tangu niingie katika Wizara hii. Mimi naomba niseme tu kwa ufupi. Tatizo letu si kwamba mdudu huyu *American Red Boll Worm* hawezekani kuuliwa, hapana hilo sio tatizo. Tatizo ni kwamba, unamuua kwa gharama gani? Ndio *problem* kwamba, ukimwachia huyu mdudu akaenda aka-*cover* Ukanda wote wa Pamba, gharama zako zitakuwa kiasi gani? Je, tukiruhusu akapita kutoka huko aliko Zambia, Malawi na Msumbiji na Afrika Kusini akaenda Ukanda wa Kaskazini, kwa hiyo akaenda kwenye *Eastern Cotton Growing Area,* je, bado tutaweza kuendelea ku-*afford* kulima pamba hasa kwa kuzingatia kwamba, bei za pamba katika Soko la Dunia zimekuwa chini sana katika miaka mingi? Mwaka huu kidogo tuna unafuu, tunamshukuru sana Mwenyezi Mungu na Bodi imetangaza bei ambayo ni karibu mara mbili ya mwaka 2002.

Lakini kwa kawaida bei ya pamba katika Soko la Dunia sio kubwa sana. Sasa ukiruhusu kuingiza mdudu ambaye ataongeza gharama za kulima pamba; je, tunaweza kuendelea kulima pamba? Hilo ndio swali tu ambalo tunajiuliza. Kama jibu ni ndio, *then* mruhusu huyo mdudu aenee halafu tuongeze mnyunyizio wa dawa. Kama jibu ni hapana usimruhusu kwa sababu ataua *the cotton industry* katika nchi hii.

Wakulima wa pamba katika hizi nchi za jirani, wakulima wanaonyunyizia mashamba yao kwa ndege na walio na nidhamu ya kuondoa masalia ya pamba shambani mara baada ya kuvuna, katika maeneo

yetu mengi ukienda baada ya kuvuna unakuta yale masalia bado yapo, yanabeba wadudu kutoka msimu mmoja kupeleka katika msimu wa pili. Wao wananyunyizia mara 12, sisi tunanyunyizia pamba mara sita. Sasa hivi kwa kutumia hizi mbinu bora za ku-*control* wadudu, tunaweza kunyunyizia mara mbili mpaka mara tatu. Kwa hiyo, mkulima anabaki na fedha zaidi kidogo.

Tija yetu katika pamba bado iko chini sana. Ni kilo 250 mpaka kilo 300 badala ya kilo 1,400. Kwa hiyo, uki-*tip* hii *balance* kidogo tu, mkulima ataacha kulima hiyo pamba kwa sababu haitamlipa tena na kwa nini unataka umpelekee huyu mkulima wako mdudu ambaye hakuwa naye? Ndio zawadi ya *Christmas? (Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, tuna Kamati ya Kilimo na Ardhi, Mwenyekiti wetu ni Mheshimiwa Simpasa, kwa hiyo, mimi naomba suala hili tulishughulikie kwenye ile Kamati ya Kilimo na Ardhi halafu tutarudi tena hapa Bungeni kuja kueleza ni nini tulichoona na ni nini tunachopendekeza katika nchi hii. Tutashirikiana na watafiti wetu na wataalam wetu na wale Wabunge ambao wangependa kwenda nchi za jirani kwenda kuona pamba inavyolimwa, tutawafanyia mipango waweze kwenda huko ili kwenda kuona hali ikoje. Ni suala ambalo kwa kweli ni kuchukua *facts* zilizopo na kukaa na kuziweka mezani kuzi-*discuss* na kukubaliana. Hakuna jambo la mtu hapa. Mimi ningependa nchi nzima ilime pamba, ningezalisha pamba nyingi sana mpaka ningeonekana kwamba ni mtu, ndio ile miamvuli ingefunguka sawasawa. Lakini matatizo ndio hayo na ninaomba tukubaliane kwamba tufanye utaratibu huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo lilijitokeza sana na lililozungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengi sana ni suala la pembejeo. Kwanza kutokana na hii hali nzuri ambayo imeanza kuboreka, mwaka huu, Serikali imeweza kutenga fedha kwa ajili ya kusaidia kupunguza gharama za pembejeo kwa kulipa sehemu ya gharama za usafirishaji. Tunaishukuru sana Serikali kwa kazi hii nzuri na Mheshimiwa Mramba, nafikiri anafanya kazi nzuri kuweka hesabu hizi vizuri. Fedha hizi bado ziko Hazina na zitatumika wakati utakapofika. Kwa hiyo, pamoja na zile shilingi bilioni 54 tulizopata, kuna shilingi hizo kwa ajili ya usafirishaji wa pembejeo na kuna pesa nyingine kwa ajili ya kusaidia masuala mengine yanayohusiana na kilimo pia.

Kwa hiyo, tunatarajia kwamba hali ya pembejeo nchini mwaka huu itakuwa nzuri zaidi. Tumeshazungumza na wafanyabiashara, kuwahimiza walete mbolea nchini kwa wingi, Waziri wa Fedha ametiliana saini na Balozi wa Japan kwamba, watusaidie tena mbolea kiasi na tunaangalia uwezekano wa kutumia uwezo wetu wenyewe kuagiza baadhi ya mbolea kutoka nje. Lakini jambo lililoleta mgogoro mkubwa hapa ni Mfuko wa Pembejeo. Sasa naomba nieleze kwamba, huu Mfuko wa Pembejeo haumkopeshi mkulima mdogo. Haukuanzishwa kwa ajili ya kukopesha pembejeo kwa mkulima mdogo, ulianzishwa kwa ajili ya kukopesha wasambazaji wa pembejeo. *Stockist* wanaita, ndio nia ya huu mfuko. Huyu *stockist* ni lazima aonyeshe kwamba akikopa ana uwezo wa kulipa ndio maana ya kuwa na *collateral*. Huwezi kwenda pale Benki ukasema nipe tu pesa niende nyumbani nitakwenda kusambaza pembejeo. Tulijaribu kufanya hivyo, wakati tulipokuwa tunagawa wenyewe, watu walishachukua fedha na wengine wako humu ndani, wakaenda wakaanzisha *Dispensary,* wakanunua daladala na waliofanya vizuri zaidi wakaoa wake wa ziada. *(Kicheko/Makofi)*

Kwa hiyo, ndio maana tukaamua kwenda Benki ili Benki zikopeshe kwa misingi ya Benki. Kuna mzee mmoja alikuja Ofisini kwangu akaniambia anataka sehemu ya mkopo iliyobaki. Nikamwuliza mzee unalima wapi? Akaniambia shamba lake lilipo. Nikamwuliza maji utapata wapi? Akasema bomba linalokwenda Mjini linapita shambani kwangu, kwa hiyo nitachukua maji kutoka kwenye bomba hilo. *Is it possible* ukachukua maji ya Mjini ukamwagilia? Haya maji yanayokuja Dodoma tulikuwa tunamwagilia zabibu zamani, lakini hiyo wamekataza na wakikuwekea mita huwezi kulipa hayo maji. Kwa hiyo, zile tulipokuwa tunazitoa wenyewe zilitufikisha hapo, ndio tukaenda Benki ili Benki watumie taratibu za kibenki kukopesha.

Mheshimiwa Spika, lakini katika mwaka unaokuja, tunapanua wigo. Tulitafuta mabenki ya kukopesha, tukapata mawili tu, *Exim Bank* ambao walikuwa na mazoea ya kukopesha fedha za kilimo kwa kuwa walikuwa wanashughulikia fedha za *STABEX* na Benki ya Ushirika ya Kilimanjaro. Tumeshazungumza na Benki ya Wakulima wa Kagera, tumeshazungumza na Benki ya Wakulima ya Mufindi na tumezungumza na Umoja wa Vyama vya Kuweka na Kukopa, ili tupitishe fedha hizi kwenye vyama hivyo na vyama hivyo sasa vinaweza kumkopesha mkulima mmoja mmoja kwa sababu sasa

itakuwa rahisi zaidi na wanafahamiana, kwa hiyo, hata pengine hakuna haja ya *collateral.* Lakini sheria mliyopitisha hapa, mfuko huu unaruhusiwa kuwakopesha wasambazaji wa pembejeo pekee.

Lakini tumekuwa tukipanua mfuko huu kwa sababu hatuna chombo kingine. Kuanzia mwaka huu wa fedha ulioanza leo tarehe 1 Julai, 2003 watakuwa wanakopesha fedha kwa ajili ya kununulia matrekta. Sasa hapa tutakuwa tuna-*deal* na mtu mmoja mmoja, maana huwezi kukopesha trekta kwa maana ya kupitia kwenye Vyama vya Ushirika. Kwa hiyo, huyu mtu atakwenda katika hiyo Taasisi inayokopesha, akiiridhisha itampa fedha atakwenda kununua trekta.

Tumesema vile vile tutumie hizi fedha kutengeneza matrekta yaliyoko nchini. Yako matrekta 6,000 mabovu ambayo mengine ni matairi yamekwisha, mengine yameharibika labda yanataka injini, mengine yanahitaji *pump and so on and so forth.* Kwa hiyo, tukasema hizi fedha ziwe *available* kwa mtu anayetaka kukopa ili trekta lake lirudi shambani. Watu wakatuambia kwamba, ooh, unajua hii ya kukopesha kutengeneza matrekta mabovu hapana, nunua mapya tu. Lakini haya mapya yakiwa mabovu yasimame yaongeze idadi tu? Kwa hiyo, afadhali tufufue tuliyonayo na tununue mapya tuongezee ili matrekta yaweze kuwa mengi zaidi hapa nchini. Naomba tukubaliane na wale mnaopiga makofi nafikiri mnakubaliana na sisi. *(Makofi)*

Kwa upande wa pamba mwaka 2002 tulipata tatizo kidogo la mbegu kutokuota, nyingine zile za Bariadi hazikuota kwa sababu mvua hazikunyesha japokuwa hatukukubaliana juu ya hilo. Katika mwaka huu tutaacha kabisa kuondoa masalia ya nyuzi kwenye mbegu kwa kutumia tindikali. Kwanza ile tindikali inaharibu mazingira na haitupi uhakika wa mbegu kuota. Tumekwishatoa maagizo kwamba, mbegu zitakazosambazwa ni zile tu zitakazoondolewa masalia ya nyuzi kwa kutumia mashine na tumegundua kwamba, tuna *capacity* ya kutosha kabisa kupata mbegu zilizoondolewa nyuzi kwa kutumia mashine kwa sababu kuondoa nyuzi ni moja ya hatua katika kuandaa mbegu kwa ajili ya kutengeneza mafuta. Aidha, tumewaagiza ile Taasisi yetu ya mbegu kwamba, ni lazima wasimamie na kuthibitisha ubora wa mbegu kabla mbegu hizo hazijagawiwa kwa wakulima. Kwa hiyo, hatutarajii tena kupata tatizo la mbegu kutoota kwa sababu ya utaratibu wa kuziandaa. Lakini mbegu zinaweza zisiote kwa sababu ya ukame na shughuli nyingine.

Suala lingine ambalo tuliulizwa ni juu ya mbolea ya Japan. Naambiwa miaka iliyopita kuliwekwa utaratibu wa kugawa tu hii mbolea halafu ule utaratibu ukaleta migogoro kwa sababu haukuwa wa uwazi na vile vile ulikuwa na dalili za upendeleo. Kwa hiyo, baadaye Serikali ikazungumza na Wajapani, yakafikiwa makubaliano kwamba, hii mbolea iuzwe kwa utaratibu wa tenda. Huu utaratibu wa tenda umetupa matatizo sana mwaka huu. Umetupa matatizo kwa mchele, umetupa matatizo kwa mbolea ukachelewesha mchele ukakaa bandarini miezi karibu mitatu, minne, mbolea ikakaa Bandarini kwa muda mrefu.

Kwa hiyo, suala hili tutaliangalia upya na kuweka utaratibu mpya wa jinsi ya kushughulikia hii mbolea inayoletwa nchini na kuhakikisha kwamba, inakwenda kwa mkulima na kwa bei nzuri kwa sababu utaratibu ambao tumekuwa tukitumia hautupi uwezo wa kuhakikisha kwamba, mkulima anaipata kwa bei nzuri. Kwa hiyo, tutaweka utaratibu wa kuhakikisha hivyo.

Suala lingine lililozungumziwa ni *PADEP,* ule mradi wa uwezeshaji ambao Mheshimiwa Maghembe ameuzungumzia sana na Mheshimiwa Mrema na Mheshimiwa Lupatu kwamba, utaratibu huu unakwenda kwenye Wilaya 28 tu na mapesa yanayohusika ni mengi sana. Kwa hiyo, wakauliza hivi kwa nini huu mpango usiende kwenye eneo pana zaidi?

Mheshimiwa Spika, hizi fedha za mkopo aliziomba Mheshimiwa Waziri Mkuu binafsi na alipotembelea Marekani ni moja ya mambo aliyofuatilia kuhakikisha kwamba, huu mpango unakamilika. Nashukuru sana kwa kunipigia Makofi kwa kazi nzuri hiyo. *(Makofi)*

Lengo la mpango huu lilikuwa ni kuhakikisha kwamba, wakulima wanapata pembejeo za kutosha ili kuinua ukuaji wa kilimo na tulitarajia kwamba, huu mkopo ungepatikana mapema zaidi. Sasa urasimu wa Benki ya Dunia umeendelea mpaka sasa tunakuja kuishia na Wilaya 28. Nimewaambia wenzangu kwamba, itabidi tukae tulitazame suala hili upya hata kama inabidi tu-*negotiate* makubaliano na *World*

*Bank* kwa sababu huu ni mkopo, wala sio fedha za zawadi. Kwa hiyo, tutalitazama upya na kwa kupitia kwenye Kamati yetu ya Kilimo na Ardhi, tutaripoti *back* hapa Bungeni kwamba, ni nini tulichofanya. Nawashukuru sana kwa *concern* zenu na kwa kutaka kwenu kwamba hili suala lipanuliwe ili Wilaya nyingi zaidi zifaidike na mkopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala linalofuata ni suala linalohusu Shamba la Madira alilozungumzia Mheshimiwa Talala Bana Mbise. Hili shamba lilikuwa la Wagiriki wanaitwa *MASIS*. Huyu aliyekuwa na hili shamba alikufa lakini kabla ya kufa aliacha wosia kwamba, angetaka hilo shamba litumike kwa manufaa ya watu wengi. Mke wake akabaki akaenda kwa Rais wa Awamu ya Kwanza, Marehemu Mwalimu Nyerere, akamwambia angetaka ali-*handover* hili shamba na akaomba alipwe chochote. Mwalimu akaiagiza Wizara ya Kilimo na Mifugo wakati ule inunue hili shamba kwa Shilingi milioni 7.7 sawasawa na Dola za Kimarekani laki nne. Wizara ikalipa hizo fedha ikanunua hilo shamba na kuna maandishi hapa ya ku-*transfer* hati za hilo shamba kulipeleka Kilimo. Sasa kule Arumeru kuna tatizo kubwa sana la ardhi. Mheshimiwa Talala Mbise, anafahamu tatizo hilo na Mheshimiwa Aggrey Mwanri pia analifahamu sana tatizo hilo kwamba, kuna tatizo kubwa sana la ardhi.

Kwa hiyo, ardhi yoyote wanayoona imekaa kaa haina mwenyewe, wanataka wagawane vihamba kila mtu apate hapo kipande. Mimi nataka kusema, utaratibu huo ni kujaribu kutatua tatizo la kudumu kwa utaratibu wa muda mfupi. Wala haitusaidii hata kidogo.

Mkichukua mashamba makubwa mkayagawa sehemu za kuzikana, haitatusaidia katika kilimo hata kidogo na baada ya miaka miwili, mitatu, tatizo lile liko pale pale. Sasa naomba tukae tutafute majawabu ya kudumu kwa matatizo ya kudumu tuliyonayo na haya mashamba ya Serikali tuyaache Serikalini ili yasaidie umma wote wa Tanzania. Lile shamba ndilo linafanya tafiti za migomba, tafiti za mboga za majani, *TPRA* ndio wanatumia lile shamba kujaribu madawa yao na kadhalika.

Ukiliondoa ukawagawia watu vihamba utatatua tatizo leo, lakini baada ya miaka miwili, mitatu, tuko pale pale. Tutakuwa tumejenga vibanda vyetu pale, tumechimba makaburi ya kuzikana na makaburi ya siku hizi yanajengewa, si shamba na hivyo shamba lote limepotea?

Naomba tukubaliane kwamba, litabaki ni shamba la Serikali lakini nimewauliza watu wa Arumeru, hivi mkitaka kujenga Chuo Kikuu mnajenga wapi? Pale pana Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Mifugo, pana Kituo cha *Horticulture*, kuna Chuo cha Maendeleo ya Jamii na kuna lile eneo ambalo mkichukua mkayaunganisha yote haya mnaweza mkaweka Chuo Kikuu pale kikashughulikia kilimo, hata sayansi za kwenda anga za mbali. Nafikiri mfikirie huko mbele tunakokwenda badala ya kufikiria kutatua tatizo tu la sasa hivi. *(Makofi)*

Naomba Mheshimiwa Mbise, kama linakupa matatizo kwenda kueleza, mimi niko tayari kwenda Arumeru kulielezea hili kwamba, Waheshimiwa shamba halipatikani na kama tatizo la ardhi linaendelea, hameni mwende katika maeneo mengine, maana Katiba yetu inatoa uhuru kuhamia mahali popote ilimradi huvunji sheria. Kuna Mheshimiwa Mbunge wa Biharamulo amekukaribisha upeleke baadhi ya watu wako kule. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya ningeomba tu nirudie kusisitiza yale aliyozungumza Naibu Waziri wa Kilimo na Chakula, Mheshimiwa Profesa Mbawala kwamba, dalili zilizopo zinaonyesha kwamba, kuna uwezekano mkubwa wa kuwa na njaa mwakani, kwa kuangalia hizo kumbukumbu zote za karne zilizopita, karibu karne mbili sasa. Maana tunaanza *nineteenth century*, tunakuja *twenties century*. Kila mwaka unaoishia na nne tulikuwa na ukame na tulikuwa na njaa.

Kila mwaka ulioishia na nne! Mwaka unaokuja ambao tumebakiza miezi kama sita tu kuufikia unaishia na nne. Sasa naomba tutakaporudi nyumbani tukahimize kilimo cha mazao yatakayostahimili ukame ili tuwe na chakula mwaka kesho.

Naomba tutilie mkazo sana hili zao la muhogo kwa sababu kila nilikokwenda ambapo wamelima muhogo hawakuwa na wasiwasi wa njaa hata kidogo na muhogo unaota karibu nchi nzima. Wanaoogopa kula muhogo ni Wapare tu kama Mheshimiwa Maghembe pale, wanafikiri inaua. Lakini muhogo ni chakula kizuri sana na kikiandaliwa vizuri wala hutajua kama ni muhogo mpaka uambiwe. Kwa hiyo, tunaomba sana tuchukue tahadhari tusije tukajikuta katika matatizo mwakani wakati tuna muda. *(Kicheko)*

Kwa upande wa Serikali tutahakikisha mashamba yote ambayo yanaweza kulimwa yanalimwa na tumeweka Mameneja wa kusimamia kuhakikisha yanalimwa kikamilifu. Lakini yale mashamba hayatoshi kulisha nchi nzima.

Kwa hiyo, *I appeal to everybody* kwa kweli kila kiongozi na kila mwananchi achukue kila hatua inayowezekana kuhakikisha anazalisha chakula chake na wale watakaopata chakula cha kutosha mwaka huu wajiwekee akiba mpaka watakapokuwa na uhakika wa mavuno ya mwaka kesho.

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza haya, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**VOTE 43 - WIZARA YA KILIMO**

| | | |
|---|---|---|
| *Programme 10 - Administration .. ... ... ...* | Sh. | 1,024,672,000/= |
| *Programme 20 - Crop Development ... ... ...* | Sh. | 3,603,637,300/= |
| *Programme 30 - Research Development ... ...* | Sh. | 3,338,993,400/= |
| *Programme 40 - Cooperative Development ...* | | - |
| *Programme 50 - Food Security ... ... ...* | .Sh. | 3,119,311,800/= |
| *Programme 60 - Livestock Development ... ...* | | - |
| ***Total of Vote ... ... ... ... ... ...*** | **Sh.** | **22,628,841,900/=** |

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa nachangia kwenye Hotuba ya Waziri Mkuu, niliomba maelezo kwa nini ndege haikupelekwa kwenda kuangamiza ndege waharibifu Singida kuanzia Januari mpaka Mei, kiasi kwamba ilipokwenda mazao yote yalikuwa yameathirika na hapakuwa tena na mantiki ya kupeleka ile ndege. Hiyo moja.

Lakini pili, mpaka naondoka Jimboni, ilikuwa bado hakijatolewa kibali cha kuwaangamiza ndege kasuku na kwa ajili hiyo, taswira kuhusu upungufu wa mazao ulikuwa mkubwa sana. Ningependa kupata maelezo kwa sababu sikupata maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haya maelezo ambayo anayatoa Mheshimiwa Missanga, yanatushangaza kidogo kwa sababu tulifanya mipango ya kupata ndege mapema sana mwaka huu na ndege mbili zilikuja kutoka Shirika la Nzige wa Jangwani na tulizitumia kuua nzige na zilikuwa *stationed* Manyoni, Singida na baadhi ya maeneo ya Arusha.

Kwa hiyo, ndege zilikuwepo zikipambana na kwelea kwelea muda wote mpaka Mbaradi, Dodoma, kila mahali walipotokea. Sasa kama kulitokea ucheleweshaji ni kwamba, *capacity* yetu haikutosha ku-*deal* na kila mahali palipokuwa na *out-break.* Lakini mwaka huu tulikuwa *efficient* sana katika kushughulikia hawa ndege. Juu ya kasuku tulikuwa na *problem* ya ndege kasuku.

Ndege kasuku ni ndege ambao wanahifadhiwa na Wizara ya Maliasili na Utalii. Kwa hiyo, hairuhusiwi kwenda kuwaua tu ovyo. Zamani walikuwa wanakamatwa wanauzwa nje, wakapungua sana. Kwa hiyo, ni ndege ambao wako *protected*. Kwa hiyo, ilibidi tuzungumze na Wizara ya Maliasili na Utalii, tukubaliane ndipo baada ya kukubaliana tulikwenda kuwanyunyizia dawa na tukawapunguza sana.

Kwa hiyo, tunafikiri tutamshauri Waziri wa Maliasili na Utalii, awaruhusu tena wale vijana waliokuwa wanauza ndege nje waendelee kuwakamata kamata ili kuwapunguza wasije wakawa wengi sana. Lakini nafikiri Mheshimiwa Msindai, Mheshimiwa Kilasi na Wabunge wengine watakubaliana na mimi kwamba, tulijitahidi kwa kweli kuwa *very efficient* katika kushughulikia suala hili. *(Makofi)*

**MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siridhiki na maelezo ya Mheshimiwa Waziri, kwa sababu analichukulia suala hili *very light*. Wakulima kule wanasema mnatuhimiza tulime, tumelima, ndege wanakula mazao ya biashara na mazao ya chakula, tunawaambia tusaidieni ndege ije kuwaangamiza, hamleti; sasa kwa nini tuendelee kulima? Sasa anavyolielezea, analielezea *very lightly* kiasi kwamba, haoni kama ni jambo la muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado sijaridhika na maelezo hayo. Hilo moja. Pili, niliuliza siku ile, kama kasuku kwa maana ya ndege, basi Serikali iseme kama raslimali ndege ni bora kuliko raslimali watu. Sasa nataka nijue hapa na wananchi wanataka kujua je, raslimali ndege ni bora zaidi kuliko raslimali watu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sijui Waziri aeleze nini zaidi ya hapo. Ngoja Mheshimiwa Waziri Mkuu, atoe maelezo ya nyongeza.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu kuthibitisha maelezo ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo. Ndege zilikuwa Singida, ninalikumbuka sana hilo kwa sababu Singida ni majirani sana na Wilaya ya Hanang. Wilaya ya Hanang walikuwa na shida na hao ndege kwelea kwelea. Kwa kweli ndege hizo wakati zilikuwa zinatafutwa zilikuwa Singida. Zimefanya kazi ya kunyunyizia Singida ndiyo baadaye zikaenda Hanang na sehemu za Mbulu, Haidom. Kwa hiyo, ndege zilikuwa Singida na haikuwa wala mwezi wa tano, ilikuwa mapema zaidi. Ndege ziliwahi sana Singida.

La pili, hili la kasuku. Ndugu Mwenyekiti, ni kweli kasuku tunawafahamu sana, ni ambao wamepungua sana. Lakini tusisahau pia utaratibu wetu wa kiasili wa kufukuza wanyama waharibifu na ndege waharibifu. Kwa sababu hawa kasuku si wengi kama kwelea kwelea. Kwa hiyo, tunao utaratibu ambao wa kawaida tu tunaweza tukaokoa mazao lakini tukifikiria kwamba, kila mahali ambapo kutakuwa na ndege wa aina fulani, ndege ije ya kunyunyizia, kwa kweli haiwezekani.

Kwa hiyo, nataka tu kuthibitisha maneno aliyoyasema Waziri yalifanyika, kwa kweli Wizara imekuwa ikisimamia sana suala hili la kupambana na ndege waharibifu. Kwa hiyo, halikuchukuliwa kimzaha mzaha kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

**MHE. EDSON M. HALINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilizungumzia kuhusu tatizo tulilonalo huko kwa wakulima wa kahawa juu ya fedha za *STABEX* na Waziri amekiri kabisa kwamba, Serikali ilipangia hela hizo bila kuwashirikisha wakulima hawa wa vijijini. Je, tuseme kuanguka kwa zao hili Serikali itakubali kubeba lawama hiyo kwa kuwa imepanga hela na matumizi yasiyolingana na haja ya watu? *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejaribu kueleza kwa kirefu sana nini kilichotokea kwamba, hata Serikali ilikuwa inafikiri kwamba sehemu ya fedha hizi ingetumika kulipa wakulima kwa kuwalipa moja kwa moja. Lakini anayetoa fedha, *EU* ikakataa, ikasema hakuna utaratibu wa uhakika wa kubaini ni nani aliyeuza kahawa kiasi gani na Mheshimiwa Halinga, atakubaliana na mimi kwamba, kwa utaratibu wa soko huria si rahisi kujua ni nani aliyeuza kahawa kiasi gani na hata tulipolizungumza na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, walisema tukahesabu miti.

Lakini ni kweli kwamba, sio miti yote kwenye shamba inayozaa katika mwaka. Kwa hiyo, kuhesabu miti si jawabu. Mwenye fedha akikataa, akisema fedha zangu zisitumike kumgawia mkulima mmoja mmoja, kwa hiyo, tukakaa tuka-*negotiate* utaratibu mwingine wa kutumia fedha zile, ama sivyo tungelipoteza. Sasa Serikali ikubali kwamba, kuanguka kwa kahawa ni kosa lake, itakuwa ni kosa la kutokutekeleza mambo mengine yanayohusiana na kilimo cha kahawa na wala siyo kosa la Serikali.

**MWENYEKITI:** Nadhani maelezo yanaridhisha Mheshimiwa Halinga.

**MHE. EDSON M. HALINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Kilimo ilikwisha hesabu miti yote ya wakulima kule kwetu. Sasa uamuzi huo umeishia wapi na wananchi bado wanangojea kwa kujua kuwa miche yote au miti yote waliyonayo ya kahawa imehesabiwa. Sasa tegemeo hili litakuwa vipi?

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshaeleza kwamba huwezi kutumia miti kama njia ya kusema ni kiasi gani kilichozalishwa. Hili la kwanza. Lakini la pili naomba nirudie, mwenye fedha hizi alikataa zisitumike kuwagawia mkulima mmoja mmoja na huyu ndiye mwenye fedha, mwenye chake muungwana, akasema hawezi, pesa hizi zisitumike kumlipa mkulima mmoja mmoja, tulizungumza na mwakilishi wa *EU* hapa, akasema ndiyo maagizo yake. Waziri wa Fedha akaenda Brussels akazungumza na Makamishna wanaohusika, akamwambia kwamba maagizo haya ni ya Bunge la Ulaya. Kwa hiyo, hayawezekani kutenguliwa. Kwa hiyo, uwezekano wa kupata fedha hizi kwa ajili ya kugawia wakulima haupo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Maelezo yanaridhisha.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuthibitisha aliyoyasema Mheshimiwa Waziri wa Kilimo kwamba, fedha hizo haziwezi kupatikana kwa utaratibu wa kugawa fedha kwa kila mkulima wa kahawa. Hii haiwezekani kabisa na mimi nimekwenda mpaka Brussels, mwaka 2002 kwenye mwezi Machi hivi. Nimekutana na wahusika wakuu na jambo hili kule na jibu lilikuwa ni kwamba, heshimu uamuzi wa Bunge la Ulaya *(European Parliament)*. Ndiyo imeamua hilo na hilo Bunge la Ulaya ndiyo linaloamua misaada mingine yote inayokuja Tanzania na nchi nyingine zinazoendelea.

Kwa hiyo, uamuzi wa Serikali ukawa tufanye kile ambacho kinatakiwa, sisi tutakubaliana na ndivyo alivyoeleza Waziri wa Kilimo na ndivyo nilivyoeleza mimi juzi wakati nikijumuisha majadiliano ya Bajeti na ndivyo tutakavyotekeleza hizo fedha na hata mimi nasikitika kwa sababu mimi ni Mbunge wa kahawa na watu wangu wanataka hizo fedha. Lakini nimeenda kuwaambia hivyo kwamba mwenye hela hataki tutumie hivyo. Kwa hiyo, tunatafuta utaratibu mwingine.

La pili, ambalo Waziri wa Kilimo pengine angelisisitiza kwamba kuanguka kwa zao la kahawa hakuna uhusiano kabisa na fedha za *STABEX*, zao la kahawa likaanguka. Jibu la zao la kahawa ni kushughulikia ubora wa kahawa yenyewe, kwa njia tulizozoea au kwa njia kama alivyosema Waziri wa Kilimo, ushahidi ni nini. Nimekwenda mwenyewe New York, mwezi Mei, kwenye Mkutano wa matajiri wakubwa wa kahawa duniani. Nikatoa hotuba pale ya kuomba jamani tusaidieni sisi maskini, ongezeni bei ya kahawa. Wakasema kuna kitu kinachoitwa *Niche Markets,* kwamba ni uchochoro soko la kahawa leo sio pana tena kama zamani. Kuna vichochoro, ukienda kichochoro hiki, bei Sh. 1,200/= kwa kilo. Ukienda kichochoro hiki Sh. 2,000/= kwa kilo. Ukienda kichochoro hiki chini zaidi.

Mimi nimerudi Tanzania, nimewaandikia Wakuu wote wa Mikoa ya kahawa na juzi walipokuwa hapa wiki iliyopita, wamenithibitishia kupata barua zangu na mmoja yuko hapa, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro. Nimewaandikia na wameshawaandikia *DCs* wao kwamba, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro yuko hapa sasa hini na ndiyo shahidi kwamba, kilimo kwa sasa hivi wale wanaovuna, watumie mbinu zilizoko kutoa kahawa yenye ubora wa *triple A, double A,* hii ni bora kabisa, inaitwa spesheli kwa lugha za kienyeji huko tunakotoka sisi. *(Kicheko)*

Kwa njia hiyo, watapata kwa kilo shilingi 900/=, 1,000/= mpaka 2,000/= na huo ndiyo mpango na utaratibu wa kuinua ubora wa kahawa na pato kwa mkulima. Kwa hiyo, ningependa ndugu yangu Halinga, ambaye ni Mwana-Mbozi mwenzangu, akubali maelezo haya kwa sababu ni ya kweli na tumeyashughulikia kwa kila njia na hakuna namna nyingine. *(Makofi)*

**MHE. BENEDICT K. LOSURUTIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti na mimi napenda nipate maelezo kwa mambo mawili. La kwanza, umesitisha vibali ya kuuza mazao nje ya nchi lakini umeruhusu kwa upande mwingine wa Jamhuri sehemu ya Kusini wanauza Malawi. Sasa hivi gunia moja la maharage kule ni shilingi 22,000/= na mwaka 2002 watu kutoka Kusini, Rukwa wamekuja kununua mahindi mpaka Kiteto na Dodoma hapa. Sasa sikuelewa hivyo vibali ni kwa mikoa ipi? *(Kicheko)*

Ili tuweze kuelewa sasa na wakati mmeruhusu *movement* ya chakula izunguke katika nchi nzima, sasa sikuelewa mipaka yako kwamba ni mikoa ipi, ambayo hairuhusiwi kuuza chakula nje, ili tuweze kuelewa ili tuweze kuwaelekeza wakulima wetu kwamba sehemu fulani ni nafuu. La kwanza hilo ambalo naomba maelekezo.

La pili, ni suala la mikopo ya matrekta, sisi tumejaribu sana, lakini naomba kitu kimoja, tunapokopa lazima kuwe na *grace period*. Unakopa trekta mwaka huu unaambiwa lipa mwaka huu huu. Sasa tunaomba kwa sababu tunataka kuinua maisha ya wakulima tupe maelezo kama inawezekana tupate ka-*grace period* ukikopa trekta angalau mwaka mmoja uangalie, mwaka wa pili uanze kulipia na kama ni wakulima hasa tunataka kuwainua, tupe miaka mitano ndiyo tunalipa sawasawa. Naomba maelezo hapa kama inawezekana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na swali la pili. Mimi ninachoomba basi ni kwamba, muidhishe haya makisio yaliyopo hapa Bungeni, maana mkishaidhinisha sasa tutakuwa na fedha za kukopesha, hapa nilipo sasa hivi sina hata senti tano. Niko mweupe kabisa. *(Kicheko)*

Kwa hiyo, mkishaniidhinishia basi njooni tuzungumze masharti ya kukopesha. Pesa sina sasa tunazungumzia masharti tunaanzia wapi. Ni kweli kwamba, mikopo ya matrekta ni lazima tofauti na mikopo ya pembejeo. Kwa sababu trekta ni kifaa kitakachodumu kwa muda mrefu zaidi na bei yake ni kubwa zaidi. Hii ya pembejeo anachukua mtu anakwenda kuuza anatakiwa arudishe zile fedha katika msimu, asiporudisha hatarudisha tena kwa sababu atakuwa amezitumia kwa shughuli nyingine. Lakini kwa upande wa trekta tulichompa akaja akatumia kwa muda mrefu. Tunategemea kwamba, tutakuwa na muda mrefu zaidi. *(Makofi)*

Mimi naomba tukubaliane kwamba, tuna upungufu wa chakula nchini sasa hivi na moja ya Mikoa yenye upungufu wa chakula ni Mkoa wa Manyara. Sasa turuhusu watu wachukue kile chakula kwenye Mkoa wa Manyara wapeleke kwenye nchi jirani, wakauze huko, ama tuweke utaratibu ili kisaidie wale wananchi walioko katika Mkoa wa Manyara na kwa kuwa kuna upungufu wa chakula bei lazima itakuwa nzuri. Kwa hiyo, tunashauri tuuze chakula humu humu nchini na kusiwe na kizuizi kabisa cha mtu kuhamisha chakula kutoka eneo moja la nchi kwenda eneo lingine.

Sasa kwa upande wa Rukwa, tuna *problem* na kama haikuwepo nayao tungeiweka katika kundi. Kuchukua gunia la mahindi kutoka Rukwa kulileta mpaka Morogoro, litachukua shilingi karibu 7,500/= haliuziki. Sasa ni afadhali tukamruhusu huyu mtu wa Rukwa akauze lile gunia lake *across the boarder* kama atapata bei nzuri. Nimeeleza katika *statement* yangu hapa Bungeni kwamba, nchi ya Zambia na Malawi hawana shida ya mahindi mwaka huu, tena Malawi tunaambiwa walipata misaada zaidi ya mahitaji yao. Kwa hiyo, wana *surplus* kutokana na misaada peke yake kabla hata ya mavuno yao mazuri ya mwaka huu.

Nchi zenye matatizo ni Congo na Burundi. Kwa hiyo, tunatarajia Rukwa watatumia soko la Congo na kwa hiyo, wataondoka na tatizo hilo. Lakini tujipende wenyewe kwanza, tule, tushibe, ndipo tufikirie watu wengine. Nashukuru Mwenyekiti. *(Makofi)*

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka niwe *positive*. Lakini nilikuwa nataka ufafanuzi kwa sababu nimepigiwa simu kutoka huko huko kwenye mashamba ya kahawa kuhusu pesa hizi. Kwa sababu Wizara ya Afya, huwa wanatuandikia kwamba Wabunge wafuatilie fedha hizi kila baada ya miezi miwili na Wizara ya Ujenzi vile vile, hata leo nimepata barua ya namna hiyo kwamba kuna fedha zimekwenda kule kwako na zitafanya kazi hii, kwa hiyo fuatilia. Je, Waziri ataweza kutupa ufafanuzi namna ya hizo pesa na sisi Wabunge tuweze kupata maelekezo hayo tukawaeleze watu wetu?

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sina hakika kama nimemwelewa vizuri Mheshimiwa Mbunge, lakini mwaka huu tuna fedha kwa ajili ya *District Development Plans* na baada ya kukubaliana zinakwenda wapi, basi tutafuata utaratibu wanaofuata wenzetu wa Wizara ya Afya na Ujenzi, kuwajulisha Wabunge juu ya utekelezaji wake. *(Makofi)*

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninazugumzia juu ya *STABEX* na sitaridhika hapa mpaka watu wa *EU* huko watakapotujibu kwa sababu nitatafuta utaratibu. Maana yake ni kwamba, *when is the question of money everybody is of the same religion.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani tumeelewana. Nadhani tunaruhusiwa sisi Wabunge kusema ukweli ndani ya Bunge. Mimi ninachotaka kusema kwamba sijaridhika na maelezo kwamba, *EU* wao ndiyo walitoa mapendekezo kwamba Serikali ya Tanzania isiwalipe wakulima wa kahawa moja kwa moja. Nina barua hapa ya Mheshimiwa Mramba, ikienda kwa Kiongozi wa Upinzani na anasema katika kipengele (d), ni barua ya tarehe 8 mwezi Februari, 2002. Anasema, tulikuwa tumemwuliza maswali kama *EU* ndiyo imezuia: *"As to whether the EU Commission as directed that the STABEX funds should not be paid direct to the farmers, I wish to assure you that, this has not been the case."* Anaendelea, "*While compensation to tea growers started in June, 2002 and expected to be concluded at the end of September, 2002"*.

Wale chai wamepata na tunaishukuru Serikali kwa sababu hatuoni wivu. Sasa katika kitu kama hiki, mimi sidhani kwamba *EU* wakae Bunge waseme msiwape wakulima, kwa sababu hii *STAB*EX inatoka kwa chai, katani na vitu vingine kwamba, wa chai muwape, hawa wengine msiwape! Hizi hoja za kwamba kulikuwa na soko huria, wao ndio wana-*place* nchi za Ulaya, kwa sababu masharti ya *STABEX* yote yanachosema ni pamoja na demokrasia, ushirikishaji wa umma, pamoja na uwazi na katika hili mimi nitawashangaa wale kama wamebadilisha Sera zao za kusema kwamba wasitushirikishe sisi, wananchi na wawakilishi wao katika kuamua hizi hela ziende wapi! *(Makofi)*

Kwa sababu katika mambo ya msingi wanasema tena uwape wakulima hata wakitaka kuzitumia tu, *according to their habits*, hata kama wanataka kuolea. Wana *principle* zao hizo. Mimi siwezi kuliambia Bunge lako uwongo Mheshimiwa Mwenyekiti. Kwa hiyo, ninachokisema ni kwamba, kama bado hatukubaliani na sisi sote ni wananchi, acha mambo ya Upinzani, tukianza barua ya sisi Wabunge tulioko humu tunaolima kahawa kwamba hatukubaliani na ninyi tunataka maelezo zaidi kama Serikali ya Tanzania, ni kweli au si kweli, huenda ikaleta vurugu hata hizo hela kusimama. Sasa tukubaliane hapa tuambizane ukweli kama kuna tatizo tulitanzue.

Kwa sababu siamini kama wao wana *principle* zao. Tunazo takwimu hapa, tumekwisha chukua yote nzima ilikuwa inahusu nini. Kwa hiyo, ndicho ninachotaka kumwambia kwamba, Mheshimiwa Waziri anapotujibu hapa, tunataka kumhakikishia kwamba, kwanza ajibu kimsingi. Naona Mheshimiwa Waziri wa Fedha, anataka kujibu. Ni kwa nini wale wa chai mliwapa, wakati mmezuiliwa kwamba, msiwape kama ndiyo hivyo? *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wowote kuanzia kesho, niko tayari kumlipa Mheshimiwa Mbunge, nauli aende Dar es Salaam, aende Brussels, kuthibitisha hili jambo nililolisema hapa. Lakini ikitokea kwamba, atapata jibu hilo hilo, itabidi arudishe nauli. *(Makofi)*

Ndiyo, itabidi a-*refund* nauli Serikalini. Mimi nasema mwezi Machi, 2002 nilikwenda Brussels, nilifanya kikao kamili siyo kikao cha kichochoroni, ni kikao rasmi kabisa na yule mtu alihusika. Mashahidi wangu ni Profesa Mbilinyi. Maana huyo mtu ni rafiki wa Profesa Mbilinyi, alinituma salamu kwa Profesa na nimeziwasilisha na Ofisa huyo ndiye kanipa jibu hilo. Lakini pale Dar es Salaam yuko Balozi, huyo huyo wa mwaka 2002 ndiyo huyo huyo aliyeko mpaka sasa hivi. Balozi wa *EU.* Niko tayari kumpeleka Mheshimiwa Mbunge kwa Balozi wa *EU,* akakae naye siku moja, siku mbili, kwa gharama za *Treasury*. Akileta jibu tofauti na hilo nililotoa hapa, alete hapa. *(Makofi)*

Mimi sina matatizo kama nilivyosema, mimi mwenyewe ni mdau kwenye suala hili. Yeye na mimi tuna tatizo hilo hilo. Wapiga kura wetu wanatuuliza, tupe hela. Hela hamna. Kwa hiyo, mimi ningemwomba tu Mheshimiwa Mutungirehi, aamini kwamba siyo Serikali ya Tanzania imezua kwamba, eti tusipewe fedha. Siyo Serikali ya Tanzaania ni wao. Tutamwonyesha na *minutes* kule *Treasury* za vikao ambavyo vimefanywa ngazi ya Maofisa na watu wengi, kwa hiyo, hakuna jipya kabisa.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimesoma barua nikisema ni ya Mheshimiwa Mramba, ya tarehe 8 Julai, 2002. Yeye anasema amekwenda kule

Machi, 2002 labda kama nimemsikia vibaya. Kwa hiyo, hajaikanusha na kama akiikanusha akasema siyo ya kwake basi mimi ni mwongo nalidanganya Bunge na napoteza muda wa Kamati yako.

La pili, nikasema katika hayo, mwezi wa sita ambako yeye alikwenda mwezi wa tatu wakamzuia, waliwapa watu wa chai mpaka mwezi wa kumi na moja. Mbona katika hilo hataki kujibu? *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri tuzungumzie *STABEX* ya kahawa, ndiyo inayohusika hapa, siyo chai. Maana mnaweza kwenda mkakokota mizoga yote mkaleta tu hapa. Tunazungumzia kahawa. *(Kicheko/Makofi)*

Hiyo ndiyo yenye *problem* hapa. Wenye fedha walikataa tusilipe mkulima mmoja mmoja. Waziri wa Fedha ameeleza. Nimejaribu kueleza mpaka mate yamekauka. Sasa ukweli inategemea unaweza kukutana nao usiutambue na mimi nafikiri ndiyo *problem* tuliyo nayo hapa. Kwa upande wa chai hakuna *problem* ya ku-*identify* ni nani aliyeuza chai kwa sababu wanauza kwenye viwanda na wanakuwa *recorded*, hakuna tatizo la ku-*identify* nani aliyeuza chai kiasi gani na ndiyo maana wakaruhusu walipwe na wao ilikuwa imebakia pesa kidogo tu ya kumalizia wakalipwa kwa hiyo ikamalizika. Sasa tuendelee na hili la kahawa. Mimi nakuomba ukubaliane na Waziri wa Fedha, akulipie gharama uende ukacheki ili upate ukweli pengine utautambua. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Nafikiri maelezo yanaridhisha, ndiyo yanaridhisha.

*(Fungu lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**FUNGU 43 - WIZARA YA KILIMO NA CHAKULA**

Fungu 43 - Wizara ya Kilimo na Chakula .... .... Sh.31,517,964,200/=

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu hilo la 43 - Wizara ya Kilimo na Chakula, *Sub-Vote 3001- Research Development,* ukurasa wa 72, *Project 6263 Tanzania Tea Research.* Nilitaka ufafanuzi tu kwa sababu nilipoangalia hapo nimeona fungu lililotengwa hapo ni kwa ajili ya *Employment Allowances.* Sasa sioni *Development* itakwenda kwendaje, labda kuna fedha mahali pengine?

Kwa sababu katika kumwandikia Waziri, nilitoa maombi kwamba, *Research* imefanyika zaidi Rungwe na Njombe, huko *Western Usambara* hakujafanyika chochote. Kwa hiyo, chai pale inahitaji ifanyiwe *research* iweze kuimarika zaidi.

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kama inavyoelezwa kwenye fungu hili kwamba, fedha ambazo zimetengwa hapa ni kwa ajili ya kulipa *allowances* za ajira za watu mbalimbali watakaoajiriwa na hizi fedha zinatoka Serikali ya Ireland. Lakini tuna *sources* nyingine za fedha ambazo zinatusaidia kugharamia vituo hivi.

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianzie kwenye hilo lililoishia. Mheshimiwa Waziri, amesema kwamba, fedha zilizoonyeshwa hapa kwa ajili ya *Employment Allowances* ni fedha za Serikali ya Ireland. Lakini ningependa kuendelea kwamba, katika taarifa zilizotolewa hapo awali, mimi ningependa kurudi nyuma zaidi na kuonyesha *record* tulizonazo, ninayo hapa taarifa ambayo imesainiwa mwaka 2002 na Mheshimwia Ngumbullu, pamoja na Mheshimiwa William Hannah, ambayo ni *Joint Annual Report Tanzania/EU Co-operation.*

Sasa kadri ya taarifa hizi, Serikali ya Tanzania ndiyo iliyoomba kwa kupitia *National Indicative Programme,* kwa hiyo, siyo *condition* iliyowekwa kutoka *EU,* lakini sisi ndiyo tuliyoweka na mapendekezo kwamba, tungependa kuzitumia namna hii. Labda niki-*stick* hapo niseme kwamba, kwa bahati nzuri wewe mwenyewe uliniteua mwaka 1995 nikawa Mwakilishi wa Bunge lako katika *Joint EU/SP Assembly,* kwa

miaka yote mitano. Toka 1997 mpaka mwaka 2000 nilikuwa Mjumbe kwenye Kamati ya Utendaji inaitwa *Bureau* ya *Joint Assmbley* hiyo. Kwa kweli wakati ule Mheshimiwa Waziri, nafikiri atakumbuka hasa wakati ule alikuwa Mheshimiwa Mbilinyi kwamba, *STABEX* ilikuwa inafutwa, lakini Wajumbe tulikazana isifutwe na *conditions* zikaendelea kuwekwa.

*STABEX* inaongozwa kwa ngazi tatu. Ngazi ya kwanza ni ya *Council of Ministers,* ambayo na sisi kwa bahati nzuri tunawakilishwa na Mheshimiwa Waziri wetu wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Ngazi ya pili ni ya *Joint Assembly,* ambayo ni kama Bunge na ngazi ya tatu ni ya Mabalozi. Katika ngazi zote hizo *conditions* zilizowekwa ni kwamba, *STABEX* imsaidie mkulima wa chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa la kwanza ambalo mimi naliona ni tatizo, ni usemi wa Mheshimiwa Waziri kwamba, wale wa *EU* waliona hatuwezi kulipa kwa kahawa kwa sababu hatumjui mkulima mmoja mmoja. Sasa ni tatizo la nani kama mkulima mmoja mmoja hajulikani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za mwaka 1991/1992, zimelipwa mwaka 1997 na zilipolipwa wakalipwa wakulima wadogo wadogo shilingi laki nne na hamsini, taarifa zote zipo katika *Joint Report*. Sasa tunajiuliza, je, ni vipi Mheshimiwa Waziri leo anatuambia kwamba haiwezekani kuwalipa wakati wa chai tumewalipa kwa sababu tuna *record*, kwa nini kwenye kahawa tumeshindwa? Ni vema Mheshimiwa Waziri akatueleza taarifa sahihi ni kitu gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafikiri kwa kuwa muda wangu utaisha, kuna *record* vile vile ambayo inaonyesha na Mheshimiwa Waziri amejaribu kujibu kiubabe kidogo hapa, naomba samahani nitumie neno hilo lakini nisingelipenda, lakini kwa kweli tusingependa alivyojibu. *Record* zinaonyesha hapa kwamba, hata *STABEX* ya nyuma haikulipwa. Hii ni taarifa iliyotoka kwenye *EU* yenyewe na ambayo Mheshimiwa Waziri, angetakiwa kutufafanulia. Kwa mfano, hapa tuna *Project* ya *STABEX* ya mwaka 1991/1992 mpaka 2002 ilipolipwa, imelipwa asilimia nane tu. Sasa ni kitu gani kimetokea? Tungependa kufahamu hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *STABEX* ya pamba ambayo ilitakiwa vile vile ilipwe, haikulipwa mpaka sasa kiasi chote kinachotakiwa kwa ajili ya *research* ya pamba na mwaka 2002 tunajua wakulima wa Mwanza na Shinyanga walipelekewa mbegu mbovu. Sasa tunataka hayo maelezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafikiri kwa kumalizia ningependa kujua Mheshimiwa Waziri aniambie, je, yuko tayari sasa kwamba suala hili la *STABEX* liwasilishwe kwenye Kamati yetu ili lifanyiwe uchambuzi wa kina? *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haikuwa lengo langu kujibu kibabe, maana nimejaribu kujieleza, nikaeleza mpaka sauti ikakauka.

Lakini napenda niseme kwamba, mambo ya mwaka 1995 na mwaka 2000 ni tofauti, watu hubadilisha nia. Sisi maelezo tuliyonayo ndiyo haya tuliyoyatoa hapa kwamba, tulitaka tupate fedha kwa ajili ya kuwagawia wakulima lakini *EU* wakasema hapana, hakuna pesa kwa ajili ya kuwagawia wakulima. Kwa hiyo, ikabidi tukae tu-*renegotiate*, tukakubaliana kwamba, hizi fedha zitumike kwa ajili ya barabara, *Agricultural Sector Development Program* na kadhalika na ndipo tukawekeana sahihi mkataba na wao.

Fedha za pamba kwa ajili ya *research* tumeendelea kuzitumia. Ukienda Ukiliguru sasa hivi kile kituo kipo *beautiful equipped* na *new equipment* ambazo zimenunuliwa kutokana na fedha za *STABEX*. Kwa hiyo, wameendelea ku-*dispatch* na kwa upande wa chai hivyo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa napenda niseme vile vile kwamba, kumbukumbu alizonazo kama angekuwa amenipa mapema ningezifanyia kazi, lakini amezikumbatia anazo mwenyewe, mimi sina, kwa hiyo siwezi kuzifanyia kazi na kuthibitisha *or sensation* yake. Kwa hiyo, akinipa baada ya hiki kikao nitazifanyia kazi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, isitoshe kama alivyosema mwenyewe, tuna Kamati ya Kilimo na Ardhi. Mimi nakubali kabisa kwamba, tukae na Kamati yetu tulifuatilie suala hili mpaka tulielewe kwa utaratibu unaoeleweka. Nashukuru. *(Makofi)*

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na maelezo mazuri katika ukurasa wa 62, *Project 4458, STABEX Coffee.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo mazuri yanayotolewa, bado ninahisi kwa wapiga kura wangu hayawezi kueleweka kwa hiyo, ni vizuri nikaondoka na maelezo ya uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *loan for renegotiated 1998, confirmed by court of agreement,* jambo mojawapo linalosisitizwa kati ya *EC* na *ACP* ni *Local Participation* kwamba, maamuzi yote yatakayofanyika yawe na baraka za *Local Participation*, iko kwenye *agreement*. Sasa ningependa kujua Mheshimiwa Waziri, alipokwenda huko Brussels alipata maoni ya *Local Stakeholders* ikiwemo wakulima wenyewe wa kahawa, aliwauliza walau kwamba wangependa nini maana ina msisitizo, ni sehemu ya mkataba?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *agreement* niliyopata, uzuri siku hizi hakuna siri kwa sababu kila kitu kiko kwenye mtandao. Ukienda kwenye kompyuta unapata habari zote, kwa hiyo, hakuna siri tunamshukuru Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika vipengele vilivyoainishwa kwenye *agreement* hiyo hiyo ni vitatu. Kwanza, ni *ASDP eighteen billion shillings* ziende kwa wakulima moja kwa moja, lakini mchanganuo unaonyesha *eighteen billion shillings* zote hazitakwenda kwa wakulima. Sasa ningependa atuhakikishie hapa kwamba eighteen billion zote zitakwenda kwa wakulima moja kwa moja kwenye *district level?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini siyo hiyo tu, *Tanzania Coffee Research* haikutajwa ni shilingi ngapi. Sasa ningependa kujua wapi walikaa wakaamua iwe *nine billion* kwa sababu kule kwenye *agreement* haikutajwa moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, *Rehabilitation of Priority Regional Roads Program, ten billion shillings*. Sasa tuliweke vizuri maana ukisema *region* unaweza ukakuta zile barabara za Vijijini hazitengenezeki kabisa. Ningependa atuhakikishie kwamba, anaposema *region* ni barabara kwenye Mkoa au zinaweza zikawa hata za Vijijini? Hili ni suala la *interpretation.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini zile bilioni moja na kitu zinazobaki, ambazo kwenye makubaliano yao zinaonekana kutotajwa kule kulingana na vyanzo vyetu vingine vya habari, basi na zenyewe zipelekwe kwa mkulima moja kwa moja, zisipelekwe tena kwenye utafiti na mambo mengine kwa sababu *nine billion shillings* zinatosha, ambazo tayari zimetengwa kwa utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, kwa sababu jambo hili linaonekana kuleta utata na kutoaminiana, basi Kamati mojawapo ya Bunge ipelekewe, ilitazame upya ili tuondoe giza hili la kutoelewana na kuzua hisia zisizo za lazima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa, Mheshimiwa Waziri atamke kwamba, kama huko mbele ya safari itabainika ...

**SPIKA:** *Time* yako imekwisha.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naona hili jambo la *STABEX* bado lina maneno mengi. Lakini mimi nataka niwaeleze kweli kwamba, hayo yanayozungumzwa na Mheshimiwa Waziri, ndivyo mambo yalivyokuwa. *STABEX* kwa utaratibu wake ni kweli hiyo ya kufanya watu wa-*participate* kutoka zile nchi zinazohusika ni kweli. Miaka yote tumekuwa tukipata fedha za *STABEX* zikiwa zinagawanywa na sehemu kubwa ilikuwa inakwenda kwa wakulima. Lakini pia fedha za *STABEX* zilikuwa

haziji mwaka ule ule au mwaka unaofuata ndiyo maana Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, anazungumza habari ya mwaka 1991/1992 zilikuja mwaka 1997/1998. Kwa hiyo, zimekuwa zikichelewa hivyo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini za mwaka 1991/1992, wakati ule ununuzi wa kahawa haukuwa katika utaratibu wa sasa. Sasa hizi fedha zilipokuja na kama tutakumbuka ni za muda mrefu kidogo kwa sababu tumekuwa tukishauriana sana na *EU,* mashauriano yamechukua muda mrefu sana kwa sababu na Serikali tulikuwa tunapata tatizo kwamba, wakulima wamezoea kulipwa fedha. Kwa hiyo, wasipolipwa fedha kutakuwa na manung'uniko sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *particularly* watu wa Kagera hili wangelikuwa wanalijua zaidi kwa sababu katika fedha ambazo zililipwa kwa kuokoa *KCU* lengo lilikuwa ni kwamba, fedha zile zingelitokana na *STABEX* lakini na zenyewe zilikuja zikashindikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nini kilitokea? Wakati sasa tunafanya mashaurino ni namna gani tutawalipa wakulima, *EU* wakasema kwa sababu hakuna *records* za mkulima mmoja mmoja ameuza kiasi gani, hatuwezi tukalipa fedha hizo kwa wakulima, ni mpaka tuwe na utaratibu ambao utatuonyesha kwa sababu kama mnavyosema hivyo hivyo kwamba, fedha hizo zinatakiwa zimnufaishe yule mkulima mdogo. Kwa hiyo, ni mpaka tuwe na *records* hizo kwa sababu tulikwishaingia kwenye ununuzi ambapo magulio yamekuwa kila mahali, kila mtu anauza kahawa wakati wowote, *records* za kahawa unazipata kwa wale wanunuzi wenyewe lakini siyo kwa mkulima. Kwa hiyo, ndiyo wakasema kwamba, *in the absence of the records* ambazo zinakwenda kwa *individual farmers,* haiwezekani fedha hizo zikalipwa. Kwa hiyo, ndiyo ukatafutwa utaratibu mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii ya Serikali kwamba iliwaandikia, ni baada ya mvutano huo kwamba sasa tusije tukakosa hizo fedha, kama tunaona sasa lazima tuzitumie kwa kunufaisha zao la kahawa, ndiyo sasa tukaona kwamba, basi ni afadhali ziende kusaidia maeneo hayo kwa sababu kama utasaidia *research*, kama utasaidia barabara na kama utasaidia shughuli nyingine zozote za kahawa, ukweli ni kwamba, unamsaidia mkulima yule mdogo ili aweze kuboresha uzalishaji wa zao hilo. Kwa hiyo, ndicho kilichotokea. Kama Waheshimiwa Wabunge wanataka, tunaweza kuleta taarifa kamili ya jambo hili ndani ya Bunge lako hili Tukufu. Kwa hiyo, hakuna kitu chochote kinachofichwa wala chenye utata. Nashukuru. *(Makofi)*

**MHE. NJELU E. M. KASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi suala langu liko kwenye upande wa *Research and Development.* Kwenye kifungu cha utafiti nilikuwa nimependa kufahamu hatma ya Kituo cha Utafiti cha Tumbi, kwa sababu kituo hiki hivi karibuni kulikuwa na mazungumzo kwamba kitaendeshwa na Vyama vya Ushirika ama kitaendeshwa na wanunuzi, pamoja na wakulima na mpaka tukaona *Tobacco Apex,* ambayo ni ya Ushirika, inashughulikia kituo hicho, lakini ninavyoelewa mimi kituo kile ni kikubwa hakiwezi kuendeshwa na wanachama wa Vyama vya Ushirika wala wakulima wenyewe. Tulikuwa tumezungumza toka mwaka 2002 na Mheshimiwa Waziri na mwaka huu, wakati ule Mheshimiwa Waziri alionyesha kwamba, kwa kweli lazima utafiti uendeshwe na Serikali. Kwa hiyo, sasa hivi nilikuwa nataka kupata maelezo kama kweli Serikali ndiyo inayoendesha kile kituo au bado?

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Njelu Kasaka, maana kama alivyosema, mwaka 2002 yeye alikuwa Mkuu wa Mkoa kule Tabora na alikuwa anayafahamu mazingira yale vizuri kwa hiyo, akanijulisha ya kwamba, kulikuwepo na hilo tatizo na tumelifanyia kazi. Kile Kituo cha Tumbi kitaendelea kuwa ni Kituo cha Utafiti na Makao Makuu ya Kanda yetu ya Utafiti ya Magharibi kwa sababu kuna Mheshimiwa Mbunge kutoka Kigoma aliuliza juu ya suala hilo. Kwa hiyo, kile kituo kitabaki mikononi mwa Serikali na kitakuwa ndiyo Makao Makuu ya Kanda yetu ya Magharibi. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Mimi niko hapa hapa kwenye *Vote Book* kwamba, hapa tunaona 4458, *STABEX Coffee.*

**SPIKA:** Nadhani *agenda* ya *STABEX* sasa imefungwa kwa maana ya Kamati hii, Mheshimiwa Waziri Mkuu, amesema itatoka *statement* ya Serikali. Kwa hiyo, siruhusu tena maswali ya *STABEX* katika

Kamati hii kwa leo kwa sababu yatakuja maelezo marefu ya Serikali ambayo mnaweza kuyatumia katika Majimbo yenu ili kuwaelezea wakulima. *STABEX* imefungwa kama una lingine endelea. *(Makofi)*

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka kuuliza kuhusu fedha.

**SPIKA:** Fuata amri ya Kiti.

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niko kwenye kifungu cha 6261, ukurasa wa 70, *Agriculture Research Project.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu huu mpya tuliouanza tungependa tupate ufafanuzi wa kina. Katika kifungu hiki chote cha *research* karibu fedha zote zilizopo hapa ni mikopo na ni mikopo karibu zote kutoka Benki ya Dunia, shilingi bilioni nne. Lakini katika shilingi bilioni nne kazi inayofanywa na kifungu hiki ni *feasibility study* na *renovation* na sehemu nyingine zote zinaishia kwenye vifungu ambavyo ni *recurrent expenditure,* kwa utaratibu tuliouzoea kule nyuma. Sasa ni vipi tunaanza kuchukua mikopo na kuanza kulipa *Employment Allowances* na kuanza kulipa *hospitality* na kulipa taratibu za *stationary* na kadhalika, kwa fedha za mkopo wakati hawa watu wanaofanya kazi hizi, ni watu ambao tayari tunao kwenye Taasisi ,ambazo tayari zina ajira. Mimi nafikiri hapa tunaingia kwenye matatizo makubwa na utaratibu huu umeingia kwenye Kitabu hiki cha Nne katika Wizara karibu zote. Mimi nafikiri hapa tunaanza kuruhusu kitu kipya ambacho si kwa maslahi ya Taifa letu.

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba tukumbuke hali mbaya sana tuliyokuwa nayo kwenye vituo vyetu vya utafiti. Mwaka 2000 nilitembelea vituo vya utafiti na hakuna hata kimoja nilichoona ambacho hakikunisikitisha. Kutokana na fedha hizo za *PAP II,* vituo karibu vyote vimefanyiwa *renovation* na sasa hivi ukienda kwenye vituo vile utakubali kwamba, ni vituo vya mahali panapoweza kufanyiwa kazi ya kisayansi na inayoridhisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wame-*equip* hivi vituo vyote na cha mwisho ambacho kinashughulikiwa sasa ni Kituo cha Mlingano kilichoko Tanga, vimenunuliwa *equipment* pia. Wakati ule ilibidi tufanye hivi kwa sababu hatukuwa na fedha za Serikali za kuwekeza katika utafiti na ndiyo suala la msingi lililosababisha tuombe huu mkopo kutoka *World Bank.* Lakini kadri tunavyoendelea, tumekuwa tukibuni njia nyingine mbalimbali za kutuwezesha kuendesha vituo vya utafiti kwa maana hii mikopo haiwezi kuwa endelevu, itabidi tufike siku tuendeshe hivi vituo wenyewe. Tatizo lililotupata ni kukosa *resources* za kuongeza kwenye hivi vituo tukakopa ili tuweze kuviendesha na sasa viko katika hali nzuri sana na ninaipongeza sana kazi hii ambayo imefanyika. *(Makofi)*

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya Mheshimiwa Waziri, ninayakubali kwamba, hali ya vituo vyetu ilikuwa mbaya, mimi pia ninakubali na *research* ni lazima tuifanye. Lakini lengo letu lilikuwa kusisitiza fedha zote za mikopo ziende moja kwa moja kwenye shughuli za utafiti na utafiti huo uweze kufikishwa kwa wananchi. Tulitegemea kwamba, watu wale wana mishahara, watu wale wana *Employment Allowances,* kwa maana ya hela za *overtime* na pia watu wale tayari wanazo zile *budget* za kawaida za uendeshaji lakini fedha zote ziende. Sasa unapotazama hapa katika shilingi bilioni nne unakuta ni karibu shilingi bilioni moja tu ndiyo inakwenda kwenye *research,* mimi nafikiri tunatumia fedha vibaya. Naomba ufafanuzi wa kina. *(Makofi)*

**SPIKA:** Utaupata.

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ninayopata ni kwamba, fedha za mishahara zinalipwa na Serikali ya Tanzania na siyo mkopo. *(Makofi)*

*(Fungu lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**TAARIFA**

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Matumizi ya Bunge nzima imepitia Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Kilimo na Chakula ya mwaka 2003/2004 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko. Kwa hiyo, naomba Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Kilimo na Chakula kwa mwaka wa fedha 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Wizara ya Kilimo na Chakula kwa Mwaka 2003/2004 yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ratiba ya kesho ni kwamba, tutaanza na Kikao Saa Tatu Asubuhi kama kawaida, tukimaliza maswali mtoa hoja wa Wizara inayofuata, Wizara ya Ujenzi atawasilisha hoja yake, Msemaji wa Kamati atatoa maoni ya Kamati na Msemaji wa Upinzani pia atatoa maoni, ikifika hapo tutasitisha shughuli za Bunge ili kumpokea mgeni halafu jioni Saa 11.00 tutaendelea kama kawaida.

Baada ya maelezo hayo, sasa naahirisha Bunge hadi kesho Saa Tatu Asubuhi.

*(Saa 12.50 jioni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatano Tarehe 2 Julai, 2003 Saa Tatu Asubuhi)*